

31 MEI, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 31 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAIBU SPIKA: Ahsante.

31 MEI, 2022

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa kutokana na matatizo ya mtandao, *Order Paper* zenu kidogo hazijakaa vizuri lakini zinarekebishwa kwenye vishikwambi vyenu.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Swalle kwa niaba ya Mheshimiwa Nyamoga.

Na. 294

Hitaji la Vituo vya Afya – Lupembe

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. EDWIN E. SWALLE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika Jimbo la Lupembe ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka na imekwishaanza kutekeleza mpango wa kujenga vituo vya huduma za afya katika Jimbo la Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya katika Jimbo la Lupembe. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2022 imekwishapeleka shilingi bilioni 1.5 ambapo shilingi milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya lkondo na Kitiwa; shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu za lhang'ana, Maduma na Lyalalo; na shilingi milioni 800 kwa ajili ukarabati wa miundombinu ya Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nyamoga.

31 MEI, 2022

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 Waziri wa TAMISEMI aliahidi kujenga kituo cha afya katika Kata ya Ikuna; je, Serikali ni lini itatimiza ahadi hiyo? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Wilaya ya Kilolo, Kata ya Ukumbi, wananchi wamejenga jingo la kituo cha afya kwa nguvu zao wenyewe na OPD imekamilika; je, Serikali iko tayari kuelekeza fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika Kata ya Ukumbi ili majengo yale ya vituo vya afya yaweze kukamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo kwa niaba ya Mheshimiwa Enosy Swalle Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali tunatambua tuna *commitment* ya kupeleka fedha kujenga kituo cha afya cha Kata ya Ikuna, na Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe, Mheshimiwa Edwin Swalle, amekuwa akifuatilia mara kwa mara kwa bidii sana kuhusiana na miradi ya maendeleo kwa ujumla, lakini Kituo cha Afya cha Ikuna. Nimhakikishie kwamba Serikali tayari tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga Kituo cha Afya cha Ikuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kilolo ambacho wananchi wamejenga niwapongeze sana wananchi wa Kilolo kwa kutoa nguvu zao na niwahakikishie kwamba Serikali imeweka mpango wa kuchangia nguvu za wananchi kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya na tutafanya hivyo, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nani? Wewe hapo, Mheshimiwa Hasunga. (Makofi)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Ihanda na Msia, wametenga maeneo na wametayarisha matofali na mawe kwa ajili ya vituo vya afya.

Je, upi mkakati wa Serikali katika kuwaunga wananchi hao kuhakikisha vituo vya afya hivyo vinajengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

31 MEI, 2022

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasunga Mbunge wa Jimbo la Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango, kwa mwaka ujao wa fedha wa kukamilisha vituo vya afya, zahanati na hospitali za halmashauri, lakini kununua vifaa tiba kwa ajili ya kuhakikisha vituo vile vinaanza kutoa huduma na baada ya hapo sasa tuaendelea na ukamilishaji wa vituo vya afya, vikiwemo vituo vya afya vya Jimbo la Vwawa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali, je ni lini Serikali itaanza ukarabati wa Kituo cha Afya cha Mwika, kwa kuongeza jingo la wodi ya watoto pamoja na jengo la upasuaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kimei, amefuatilia sana suala la ukarabati wa Kituo cha Afya cha Mwika, na sisi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, tulishamhakikishia kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga wodi ya watoto, wodi ya upasuaji lakini pamoja na ukarabati wa kituo kile na tutafanya hivyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kujua Kituo cha Afya Honyali, tulikipelekea shilingi milioni 250 wajenge na baada ya hapo wataongeza milioni 250 kukimalizia. Wananchi wamejitahidi kwa kupitia Halmashauri ya Bunda na wako katika hatua nzuri. Ni lini sasa hela ya pili itaenda shilingi milioni 250 ili wamalizie kituo chao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tulipeleka shilingi milioni 250 na kazi ya Ujenzi wa Kituo cha Afya inakwenda lakini masharti ni kwamba baada

31 MEI, 2022

ya kukamilisha ujenzi wa shilingi milioni 250 ndipo shilingi milioni 250 nyingine zitapelekwa. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutapeleka mara baada ya kukamilisha matumizi ya shilingi milioni 250 ya kwanza. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, hospitali ya Mji wa Mafinga inahudumia zaidi ya halmashauri tano na pia iko kando kando ya barabara kuu ya kwenda Zambia mpaka *South Africa*. Kutokana na sababu hiyo imekuwa na msongamano mkubwa sana wa wagonjwa katika kutoa huduma.

Je, Serikali iko tayari kupitia *basket fund*, kuongeza bajeti katika Hospitali hii ya Mafinga ambayo inahudumia halmashauri zaidi ya tano?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Hospitali ya Mji wa Mafinga iko barabara inahudumia wananchi wengi kutoka pia kwenye kata na halmashauri za jirani, na utaratibu wa fedha za *basket fund* utaendelea kutolewa kulingana na *population* iliyoko ndani ya halmashauri husika na ndicho kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la msingi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan inajenga vituo vya afya katika kata zote za kimkakati na hospitali za halmashauri katika halmashauri ambazo hazina hospitali. Kwa hiyo, *automatically* tutapunguza wagonjwa ambao wengi wanakwenda hospitali ya Mji wa Mafinga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ninatambua mchango wa Mbunge wa Jimbo la Rungwe katika kuchangia Zahanati ya Kiwira, Serikali mtatuongezea lini fedha ili aweze kumalizia jengo hilo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

31 MEI, 2022

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba wananchi wamechangia nguvu zao na kujenga Zahanati ya Kiwira na nimhakikishie Serikali imeweka mkakati ambao kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha tunafanya tathmini na kuongezea fedha na kukamilisha majengo hayo na tunafanya pia tathmini katika Zahanati hii ya Kiwira. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tundaendelea, Mheshimiwa Dkt. Musukuma Joseph, Mbunge wa Geita.

Na. 295

Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara – Halmashauri ya Geita

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa barabara ya kilometa tatu kwa kuanzia katika Halmashauri ya Geita?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kashoku, Mbunge wa Jimbo la Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Lami nyepesi kilometa moja katika eneo la Nzera.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliopo ni kuendelea kuweka kwenye mipango na bajeti ya kila mwaka ili kuweza kukamilisha ujenzi wa kilometa tatu ifikapo mwaka 2025.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri, lakini mwaka 2020 wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliposimama pale katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Geita aliahidi kilometa tatu na mwaka 2021/2022 TAMISEMI, ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa moja, lakini

31 MEI, 2022

mpaka leo tunaenda mwaka wa Serikali kumalizika hatujawahi kuiona hiyo kilomita moja.

Je, kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba sasa mtatekeleza kilomita mbili na sio kilometa moja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kasheku Musukuma, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama fedha hizi zipo katika bajeti ambazo zimetengwa, nitalifuatilia na nimelipokea ili kuhakikisha kwamba linatekelezeka kama ambavyo limeainishwa katika bajeti, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha kutokana na tozo mbalimbali; ni lini sasa itaweka vipaumbele kwenye majimbo ambayo yana changamoto kubwa sana za barabara ikiwemo Jimbo la Nyamagana Jijini Mwanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanlaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inazingatia vipaumbele kulingana na mahitaji ya kila jimbo ikiwemo Jimbo la Nyamagana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kituo cha Afya cha Upugi kiko kilometa nne kutoka barabara kubwa ya Tabora - Nzega. Mheshimiwa Rais alipopita pale wananchi walimuomba awawekee barabara ya lami kwa sababu wagonjwa wakizidiwa kutoka kituo

31 MEI, 2022

cha afya kwenda mjini inakuwa taabu sana. Je, Serikali iko tayari kuanza kujenga barabara hiyo ya kilometa nne?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kwa ajili ya kutekeleza maeneo yote yenye utata wa barabara ikiwemo eneo ambalo amelianisha Mheshimiwa Mbunge, isipokuwa kwa sasa tunatafuta fedha ili tuzitenge katika bajeti ili tuanze utekelezaji. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kuniona kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Liwale ni mji unaokua kwa kasi sana na ni miaka 42 sasa umri wa mji ule, lakini una kilometa 1.8 tu za lami pale mjini. Je, Serikali iko tayari kutuongezea mtandao wa barabara ya lami kwenye mwaka huu wa bajeti?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuambie tu kwamba Serikali iko tayari na tumetenga fedha na ninaamini eneo la Liwale ni sehemu ambayo tumewaanishia katika bajeti ya mwaka huu 2022/2023.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga.

Na. 296

Serikali Kuajiri Watumishi wa Kada za Afya na Elimu

MHE. JONAS W. MBUNDA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri watumishi wa kutosha katika kada za afya na elimu nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mkakati wa kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya na elimu kwa awamu kwa kutenga vibali vya ajira katika bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuajiri watumishi wa kada ya afya na elimu kwa awamu na katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepanga kuajiri watumishi 7,612 wa kada ya afya na watumishi 9,800 wa kada ya ualimu katika halmashauri zote nchini. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunda.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mbinga Mjini mahitaji ya walimu kwenye shule za sekondari ni idadi ya 370 lakini waliopo ni 279 kuna upungufu wa walimu 91 hasa kwenye masomo ya sayansi na hesabu. Shule za msingi mahitaji ni 1,026 waliopo ni 605 upungufu 421 na ikama ya wafanyakazi katika afya wanaohitajika ni 725 waliopo ni 294 upungufu ni 431. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu huu mkubwa na kwa sababu Serikali imeahidi kwamba inafanya ajira, nilitaka nijue, je, Naibu Waziri ananihakikishia kwamba katika mgao huo wa watumishi, jimbo langu litapata watumishi wa kutosha ili kuweza kuziba hilo pengo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika maelezo ya Serikali na mkakati uliopo ni kujenga vituo vingi vya afya nchini. Lakini Serikali haijaonesha kwamba kuna mkakati gani wa dharura wa kuajiri watumishi ili kuhakikisha kwamba tunaziba hili pengo la wafanyakazi? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na upungufu wa watumishi wa sekta zote, sekta ya elimu na sekta ya afya naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka mikakati ya dhati na inatekelezwa ya kuajiri watumishi wa elimu na watumishi wa afya na ndiyo maana hivi sasa tunapoongea tunaajira ambazo zinaendelea kuchakatwa za maombi ya watumishi ambao watapelekwa kwenye vituo vyetu vya afya lakini pia kwenye elimu na tutaendelea kufanya hivyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Oliver.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkenge – Misenyi tunaishukuru Serikali kutujenge vituo vya afya vya Kanyigo, Kakunyu na Kabyaile. Je, ni lini Serikali itatupelekea watumishi wa afya katika vituo hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Semuguruka amekuwa akifuatilia sana suala la watumishi katika vituo hivyo na nimhakikishie kwamba Serikali kama ilivyoanza kuajiri sasa tutahakikisha tutaendelea kuajiri, lakini pia kupeleka watumishi katika vituo hivyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kapinga.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, shida iliyopo Mbinga Mjini inalingana sawasawa na Mbinga Vijijini kwa wahudumu wa afya tulitakiwa kuwa nawatumishi 751 waliopo ni 210 tu tuna upungufu zaidi ya asilimia 80. Je, Serikali ipo tayari angalau kupunguza upungufu wa watumishi huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Kapinga nimhakikishie kwamba tunafahamu kuna upungufu wa watumishi wa afya lakini pia wa elimu katika Halmashauri ya Mbinga Vijijini na mkakati ni kwamba kufuatia tathimini yetu halmashauri zile zenye upungufu mkubwa zaidi kama Mbinga Vijijini tutaleta watumishi wa kutosha zaidi, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Taska Mbogo.

Na. 297

Hitaji la Maji Safi na Salama - Katavi

MH. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata maji safi na salama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Katavi ni wastani wa asilimia 71 kwa vijijini na asilimia 60 kwa mijini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji 42 katika Wilaya zote za Mkoa wa Katavi lengo likiwa ni kuhakikisha Wananchi wanapata maji safi na salama. Miradi hii ni pamoja na mradi wa maji Karema kwa kutumia Ziwa Tanganyika katika Wilaya ya Tanganyika unaotarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2022. Vilevile Mji wa Mpanda utanufaika na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaajiri Mtaalamu Mshauri wa kufanya usanifu kwa kutumia vyanzo vya Ziwa Tanganyika ili kuwapatia maji wananchi wa Wilaya za Tanganyika, Mlele, Mpanda na maeneo ya karibu na kufikia lengo la asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini ifikapo mwaka 2025.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, wananchi wa Mkoa wa Katavi hususani Wilaya ya Mpanda Kata za Majengo, Kashaulili, Mpanda Hotel wamekuwa na mgao wa maji hawapati maji kila siku, lakini lipo Bwana la Milala ambalo lilikuwa ni chanzo cha maji sasa hivi bwawa hilo halitumiki kwa sababu limechafuka. Je, Serikali ina mkakati gani wa kusafisha bwawa hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Ziwa Tanganyika ndiyo chanzo kikuu cha kutoa matatizo ya maji kwenye Mkoa wa Katavi; Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha upembuzi yakinifu ili maji yaweze kutoka Ziwa Tanganyika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Mbogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali yayote napokea pongezi, lakini vilevile napenda kurudi kwenye jibu langu la msingi eneo la Mpanda linakwenda kunufaika hivi punde na ule mradi wetu mzuri ambao tumeusubiri kwa muda mrefu na Mheshimiwa Rais hivi punde anakwenda kufanya yake na maji yanakwenda kuanza kutekelezwa kupitia mradi wa miji 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na bwawa kuchafuka, tutaangalia uwezekano wataalamu watakwenda kuangalia uwezekano wa kuona kama bwawa hili litatufaa au litatupotezea fedha, kama litakuwa linahitaji fedha nyingi ambayo haina tija sana kwenye matokeo tutaendelea na mikakati mingine, lakini suala la msingi ni kuhakikisha wananchi wanakwenda kupata maji safi na salama bombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matumizi ya Ziwa Tanganyika ni moja ya mikakati ya wizara nimekuwa jibu hili mara kadhaa tutakwenda kutumia Ziwa Tanganyika kwasababu hakuna asiyefahamu kwamba ni chanzo ambacho kitatuletea tija kubwa sana na miradi itabaki kuwa endelevu kwa vizazi na vizazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Minza.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio kikubwa sana kwa wakazi wa Mkoa wa Simiyu hususani Wilaya za Busega, Itilima na Meatu; je, ni lini akina mama wa mkoa huo watafaidika na maji safi na salama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu unakwenda kunufaika na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria mradi ambao ni mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira na tunatarajia maeneo hayo yote aliyoyataja yanakwenda kunufaika, Meatu ipo katika mpango huo na tayari wananchi wameanza kulipwa fidia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza niipongeze Serikali na Wizara yake ya Maji kwa kuzidi kutukamilishia mradi wetu wa maji na maji yameshaingia maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Nyang'hwale, lakini wananchi wanalalamika bei ya maji ni kubwa ukilinganisha na mjini. Nyang'hwale tunalipa shilingi 2500 kwa *unit* moja wakati Mji wa Geita na Mwanza wanalipa 1,350.

Je ni lini Serikali itatoa kauli kwa Wilaya ya Nyang'hwale kupunguza bei ya maji? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Nyang'hwale pamoja na maeneo mengine kama Karatu tunafahamu bei bado si rafiki sana kwa wananchi na hii ilisababishwa na utekelezaji wa mradi, lakini kama Wizara tunaendelea kufanya mapitio ili kuona kwamba bei zinakwenda kuwa bei rafiki kwa wananchi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru; mradi wa maji wa Nansio Jimboni Ukerewe ulishakamilika na kuanza kutoa huduma, lakini bado maji hayajaweza kuwafikia wananchi wote zinahitajika bomba takribani kilometa kama 67 ili kuweza ku-cover eneo lote na maji yawafikie wananchi.

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari sasa kusaidia mamlaka hii ya maji bomba hizi ili huduma ya maji iweze kuwafikia wananchi wote kwenye Mji wa Nansio? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema mradi umekamilika tunahitaji kuona maji bombani, hivyo kama tumeshakamilisha mradi wa fedha nyingi hili suala la usambaji wa mabomba kuwafikia wananchi ndiyo jukumu letu kubwa. Hivyo nipende kukutoa hofu Mheshimiwa Mbunge tutafika na tutafanya kwa pamoja na wananchi wanakwenda kunufaika na maji bombani.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Juliana Shonza.

Na. 298

Changamoto ya Uhaba wa Maji Mji wa Mlowo

MHE. JULIANA D. SHONZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatua ndoo kichwani wanawake wa Mji wa Mlowo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa maji inaboreshwa nchi nzima. Hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Mlowo ni wastani wa asilimia 44.5. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imekamilisha mradi wa maji wa Selewa - Mlowo ambapo mradi wa maji wa Mahenje - Mlowo utakamilika mwezi Juni, 2022. Miradi hii itaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itatekeleza mradi kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Bupigu ulioko Wilayani Ileje. Aidha, mpango wa muda mrefu ni kujenga miundombinu ya

kuchukua maji kutoka mradi mkubwa wa Mto Kiwira ambao utahudumia Jiji la Mbeya na maeneo jirani ikiwemo Mji wa Mlowo na maeneo ya pembezoni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shonza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwa kuwa nimekuwa nikifuatilia mradi huu kwa muda mrefu sana na majibu ya Serikali yamebaki kuwa haya haya.

Sasa naomba kupata *commitment* ya Serikali inawahakikishiaje wanawake wa Mlowo, wanawake wa Vwawa na Tunduma kwamba ni kweli kwa mwaka wa fedha ujao watatuletea mradi huu wa kutoa maji lleje na kuweza kuyasambaza kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba hatuwezi kumaliza tatizo la maji kwa kujenga miradi midogo midogo; sasa naomba kufahamu tunaye mkandarasi ambaye anatatumia miradi ya maji katika Kata ya Mkwajuni pamoja na Galula kule Songwe, lakini mpaka sasa hivi hajamaliziwa fedha na huo mradi umeanza mwaka 2019.

Je, ni lini sasa Serikali itammaliza fedha mkandarasi huyo ili kuweza kuwapunguzia adha ya maji wanawake wa Wilaya ya Songwe? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shonza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha maji yanapatikana maeneo yote nchini na hili tumeona jitihada za dhati kabisa Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi zaidi ya asilimia 95 mpaka sasa, mpaka tumalize mwaka huu wa fedha itakuwa zaidi ya hapo. Hivyo, Serikali tutafika maeneo yote na kuhakikisha miradi ambayo haikuteteleza inakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkandarasi kulipwa Mkwajuni – Songwe wakandarasi wanaendelea kulipwa kulingana na walivyofanyakazi walivyo *raise certificates* na kuna sababu mbalimbali zinazopelekea hawa baadhi ya wakandarasi malipo yao kuchelewa hivyo niwatake wakandarasi wote wafanyakazi kadri ya mikataba nakwa ambaye hajalipwa basi aweze kufuata taratibu ili malipo yake yaweze kufanyika mara moja.

NAIBU WAZIRI: Ahsante tunaendelea Mheshimiwa Ally Kassinge.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka jana wakati akijibu swali langu la msingi kwenye swali la nyongeza alinihidi kunipatia fedha kwa ajili ya kuchimba kisima kimoja cha maji katika Kijiji cha Nainokwe.

Je, lini fedha hizi zitakwenda ili wana Nainokwe wakafarijike kutokana na adha ya maji wanayoipata?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika tulifanya pamoja ziara na kisima hiki ni lazima kichimbwe. Mheshimiwa Mbunge tafadhali baada ya session hii ya leo tukutane ili tuweze kufuatilia pamoja hii fedha itoke. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; Tarafa ya Murongo imepatakana na Mto Kagera ambako ni chanzo kikubwa cha maji, lakini hizo kata hazina maji.

Nataka kujua nini mkakati wa Serikali katika kuwatua kina mama ndoo kusaidia upatikanaji Kata ya Kibingo, Bugomora, Murongo, Kibale, Kimuli, Bugara na Businde? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarafa hiyo ya Murongo aliyoitajwa ni moja ya maeneo tunaendelea kuyafanyikazi na kwasababu ipo karibu na chanzo cha uhakika naomba nitoe wito kwa wananchi tuendelee kuvumilia, tunakotoka ni mbali tunakokwenda ni karibu, hizi kata zote zinakwenda kupata huduma ya maji na salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ighondo.

Kuboresha Miundombinu ya Vituo vya Polisi – Singida Kaskazini

MHE. ABEID R. IGHONDO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya vituo vya polisi vya Ilongero, Ngamu, Ngimu, Msange na Mtinko katika Jimbo la Singida Kaskazini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Abeid Ramadhan Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uchakavu wa vituo vya polisi vya Ilongero, Mtinko na Ngamu. Tathmini iliyofanyika imebaini kuwa kiasi cha fedha shilingi 46,480,000 zinahitajika ili kugharamia ukarabati wa vituo hivyo. Katika maeneo ya Ngimu na Msange hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya vituo vya polisi. Napenda kutumia fursa hii kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Singida itenge maeneo yenye ukubwa stahiki pamoja na kutoa hatimiliki ili kuwezesha Serikali kupanga na kutelekeza kazi ya ujenzi wa vituo vya polisi kwenye maeneo hayo kwa kushirikiana na wadau. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ighondo.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi, pamoja na majibu yao ya Serikali lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; ni lini sasa fedha hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri zitaletwa kwaajili ya kuboresha miundombinu ya vituo hivi vya polisi vya Mtinko na Ngamu pamoja na kujenga vile vingine vya Msange na Ngimu maana yake tayari maeneo yapo?

Swali la pili nataka nijue, Serikali sasa inamkakati gani wa kujenga kituo cha polisi cha hadhi ya Wilaya katika Mji wa Ilongero ambao unakuwa kwa kasi unawatu wengi, lakini pia na kwa sasa ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya kwa hiyo, unahitaji usalama, huduma na pamoja na kwamba kituo hicho sasa eneo hilo linanyumba za polisi? Naomba kuwasilisha. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

31 MEI, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili nyongeza ya Mheshimiwa Ighondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja lini fedha? Bahati nzuri tumeshafanya tathimini tumepata shilingi milioni 46.4 zinahitajika kwaajili ya kukamilisha ukarabati huo, lakini katika mwaka huu wa fedha kama tulivyosema tutaendelea kutoa fedha kwa awamu kulingana na upatikanaji wake. Niombe kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mwaka ujao tunachukua *commitment* ya kuweka fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkakati wa kujenga kituo cha polisi cha hadhi ya Wilaya niseme tu kwamba Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla kuhakikisha tunajenga kituo chenye hadhi ya wilaya kwenye Makao Makuu ya Wilaya sasa hii ni Wilaya ya Singida ambayo OCD anaofisi yake lakini tutakachoweza kufanya ni kuimarisha vituo vya polisi ngazi ya kata na tarafa ili viweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi badala ya kila jimbo kuliwekea kituo cha polisi chenye hadhi ya Wilaya. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Zaytun.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii; kutokana na ongezeko la uhalifu katika machimbo ya Rubi yaliyopo Mandala na Longido Mbunge wa Jimbo akishirikiana na wananchi wa pale kwa juhudi zao binafsi wamejenga kituo cha polisi mpaka ngazi ya lenta.

Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi hawa ili kumailizia kituo hiki cha polisi? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Sanga.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Wizara kwamba pale ambapo wananchi watakuwa wamefanya juhudi na kujenga kufika kiwango chochote Serikali inaweza ikatoa fedha kukamilisha. Niombe tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na Mheshimiwa Zaytun wakati wa ziara yetu katika mkoa huo tuweze kuona kiwango kilichofikiwa ili kupitia Mfuko wetu wa Tuzo na Tozo tuone kiwango cha fedha tunachoweza kutoa ili kukamilisha kituo hicho kama njia ya kuunga mkono juhudi za wananchi. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Sanga jiandae Mheshimiwa .

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ongezeko ni kubwa sana la uhalifu katika Mji wa Makambako na kwa sababu Makambako kipolisi ni Wilaya na tunakituo kimoja. Ni lini Serikali sasa itaondoa adha hii kwa kujenga kituo kingine pale Majengo, pale Idofi, pale Maguvani ili kuwaondolea adha wananchi waishi kwa amani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Mji wa Makambako umekuwa kwa kasi, kuna ongezeko kubwa la watu na shughuli za kiuchumi ambako ni kivutio kwa wahalifu pia. Nimuahidi tu kama kituo kilichopo kwa sasa hakikidhi haja, tutafanya tathmini kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya na kuona namna gani tutahitaji kufanya kwa maana ya kupanua huduma za polisi katika eneo lake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Kaboyoka, ajiandae Mheshimiwa Shomar.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; Tarafa ya Gonja yenye kata nne na Tarafa ya Mambavunja yeye kata tano zote hizi zimekuwa hazina kituo cha polisi na kwa muda mrefu tumeomba mpaka wananchi wameweka nafasi za kwamba polisi wanaweza kuanzia pale na kuna sehemu za kujenga vituo vya polisi.

NAIBU SPIKA: Swali Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, je, lini Serikali itatusaidia kujenga vituo hivyo? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyoka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua uwepo wa baadhi ya tarafa na kata zisizokuwa na vituo vya polisi na polisi wetu tunaowapanga mpaka kwenye ngazi ya kata wanatumia majengo ambayo huamuliwa na mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Nimuombe Mheshimiwa Kaboyoka kuwa na subira, tunavyoanza kutekeleza mkakati wetu wa kujenga vituo vya polisi

31 MEI, 2022

mahala ambako hakuna kabisa vituo, zikiwemo tarafa alizozitaja huko Gonja. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fakharia.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuuliza swali moja la nyongeza ambalo dogo tu.

Je, ni lini Serikali itaweka uzio katika Kituo cha Polisi cha Ng'ambo, Wilaya ya Mjini Unguja? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba uzio upo katika baadhi ya vituo vya polisi. Lakini niseme kwa kuwa baadhi ya maeneo hayana kabisa vituo vya polisi, kipaumbele hakiwezi kuwekwa kwenye uzio, kipaumbele cha Wizara ni kuweka vituo mahala ambako hakuna vituo kabisa na nyumba za makazi kwa ajili ya askari wetu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa atuvumilie tumalize vipaumbele *then* haya mambo mengine ya uzio yafuate. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa George Ngassa.

Na. 300

Ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Igunga

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Igunga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Igunga lilianza kujengwa mwaka 2004 na lilifunguliwa rasmi mwaka 2006. Hadi sasa mabweni mawili ya

31 MEI, 2022

wanaume yenye uwezo wa kulala wafungwa 51 kila moja yamekamilika na ujenzi wa jengo la utawala sambamba na nyumba za askari unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za kukamilisha ujenzi wa Gereza hili zinaendelea na fedha kiasi cha shilingi 77,694,000 zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la utawala. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngassa.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; cha kwanza nataka nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri anavyosema kwamba mabweni mawili yamekamilika si kweli kwa sababu yale mabweni hayajakamilika. Mpaka sasa wameziba kwa mabanzi na mbao chakavu kwa ajili ya kuwa-*accommodate* wale wafungwa, jambo ambalo ni kinyume cha haki za binadamu na utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake walifanyie kazi waweze kulikamilisha gereza hili ili liweze kutoa huduma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili,, kwa sasa Serikali inapata hasara kwa kuwa mabweni ya wanawake hayapo, inasababisha kama kuna mfungwa ambaye ana kesi mbili au kesi inaendelea anachukuliwa anatolewa Igunga anapelekwa Nzega na inapoitwa kesi mahakamani inabidi arudishwe. Jambo ambalo linaingiza Serikari hasara.

Je, haoni kuendelea kuingiza Serikali hasara wasipomaliza ujenzi wa hili gereza? Ahsante.

NAISU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ngassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili ambalo ameniambia kwamba majengo hayajakamilika na ni machakavu kwangu pia ni jipya. Nachukua dhima ya kuongozana na wataalam wetu baada ya Bunge hili kwenda Igunga kujiridhisha, kuona ukweli wa hiki ambacho kinasemwa na kwa kweli kama tutakuwa iko tofauti tutachukua hatua stahiki kwa hawa waliotupa majibu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la mabweni ya wanawake kutokuwepo Igunga tunatambua, lakini kama nilivyokwishasema tunajenga kulingana na upatikanaji wa bajeti. Kwa vile hatujapata fedha akubali tu Mheshimiwa hawa wafungwa wa kike waendeleo kupelekwa katika gereza

la jirani. Lakini mipango ya Wizara ni kuendelea kujenga mabweni hitajika, na kwa sababu angalau mwaka huu tuna bajeti tuweze kuona jinsi ambavyo tutaweza kuwa-*accommodate* akinamama ambao wanakuwa wanasafirishwa kwenda gereza la mbali. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mama Salma.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na samahani sauti yangu imekuwa mbaya leo.

Kwa kuwa kuona ni kuamini, je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini tutafuatana mimi na wewe kwenda Kingurungundwa ambako kuna gereza la miaka mingi na gereza hili ni la mabati na hali yake ni mbaya sana? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, swali zito hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kuona ni kuamini na niko tayari kuongozana naye wakati wowote baada ya shughuli za Bunge ili pamoja na mambo mengine kuangalia uchakavu wa gereza hili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa kukubali. Mheshimiwa Aysharose.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa gereza la Wilaya ya Manyoni limejengwa miaka 52 iliyopita hali inayopelekea miundombinu yake kuwa ni chakavu sana. Je, ni lini Serikali itakarabati na kufanya upanuzi wa gereza hili ili kupunguza msongamano katika gereza hili? Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aysharose Mattembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali baadhi ya magereza ikiwemo la Manyoni ni la muda mrefu na lina uchakavu na ndiyo maana tumeanza mkakati wa kukarabati magereza chakavu kama tulivyokwishafanya Liwale na maeneo mengine. Nachukua ahadi kwamba tutaendelea kukarabati magereza haya kulingana na upatikanaji wa fedha. Nashukuru.

31 MEI, 2022

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Dkt. Thea Ntara.

Na. 301

Uwanja wa michezo wa Nelson Mandela University

MHE. DKT. THEA M. NTARA aliuliza:-

Je, nani anahusika kukamilisha ujenzi wa viwanja vya michezo Nelson Mandela University ili shughuli za michezo ziendelee?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanja vya michezo katika Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia umefanywa na Mkandarasi *Elerai Construction Company Ltd.* chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Ardhi. Hata hivyo, wakati ujenzi unaendelea kulijitokeza dosari na hivyo ujenzi haukukamilika na kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ndiyo inayohusika na ukamilishaji wa ujenzi huo. Hivyo mwezi Machi, 2021 Wizara iliitisha kikao cha wahusika wote wa mradi huo ambao ni Wizara ya Fedha na Mipango, *Pension Property Ltd.*, Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia, Mshauri Elekezi na Mkandarasi kujadili suala hili. Katika kikao hicho ilikubalika kuwa Chuo Kikuu cha Ardhi kiendelee kumsimamia mkandarasi Elerai na kuhakikisha anakamilisha kazi ya ujenzi wa viwanja hivyo. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujenzi wa kiwanja hicho umechukua miaka saba, kama kuna hilo tatizo, sijui mgogoro inanishangaza.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa ku-review mkataba huo ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika na kiwanja kinatumika mara moja? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

31 MEI, 2022

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu wa suala hili. Kabla hajaliuliza hapa bahati nzuri aliwahi kufika ofisini na tulilijadili kwa kina.

Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge katika kikao hiki cha tarehe 4 Machi, 2021 pamoja na mambo mengine kilijadili vilevile kufanya *review* ya mkataba lakini vilevile kufanya *review* ya *design* ya viwanja vile. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi, *review* imeshafanyika na mchakato sasa mwingine unaendelea katika kuhakikisha kwamba tunafanya *review* ya thamani au gharama za ujenzi ili kazi hii iweze kukamilika kwa haraka. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, baadhi ya vyuo nchini vinakabiliwa na ukosefu wa viwanja vya michezo.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka Wizara kupita kwenye Wilaya zote na Mikoa kuona viwanja vilivyopo na namna ya kushirikiana na wadau? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Issaay kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukakubali kwamba kuna changamoto ya viwanja kwenye maeneo yetu ya vyuo, tunaomba tubebe/tuchukue ushauri huu wa Mheshimiwa Issaay ili tuweze kwenda kufanya tathmini namna gani tunaweza kushirikiana na wadau wengine kuweka kufanya maendeleo ya viwanja kwenye vyuo vyetu. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 302

Kuvuja kwa mitihani inayosimamiwa na Vyuo vya Afya

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza: -

31 MEI, 2022

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kuvuja kwa mitihani inayosimamiwa na vyuo vya afya mwaka 2021?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri kutokea kwa changamoto ya kuvuja kwa mitihani inayosimamiwa na vyuo vya afya mwezi Agosti, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha kuwa tatizo hili halijitokezi tena kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza; ni kuboresha mfumo wa utungaji, uchapishaji na ufungaji wa mitihani kwa kushirikiana na Mpiga Chapa wa Serikali.

Jambo la pili ni kufanya mapitio ya Mwongozo wa Mitihani iliyo chini ya Wizara ya Afya ili kuendana na mahitaji ya kiulinzi na kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuongeza kasi ya kuanzishwa Mamlaka itakayosimamia mafunzo ya vyuo vya afya ngazi ya kati pamoja na uendeshaji wa mitihani.

Jambo la nne ni kushirikisha vyombo vya ulinzi na usalama kwenye ulinzi wa mitihani katika hatua zote kuanzia utungaji, usambazaji hadi utoaji wa matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Husna.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, na kwa kuwa Serikali imeshakiri kwamba tatizo lipo na kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa, sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mulugo

MHE PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni nyeti sana, mimi ni mtu wa elimu. Suala hili limeulizwa leo ni mara ya pili; mimi kama mlezi wa TAMOSCO, elimu upande wa vyuo na elimu msingi na

sekondari napata shida sana pale ambapo kwenye shule za msingi, kwenye shule za sekondari *O-level* na *A-level* mitihani ikivuja na hasa kwenye shule za *private* Serikali inachukua hatua haraka na kuwapeleka mahakamani na kuwapa adhabu na ikiwezekana kufunga shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala hili limejitokeza Wizara ya Afya kwa *NACTE* ambao ni watu wa Serikali, liko kimya, ni kimya kimya wanafunzi wamerudia mitihani, wameenda wamefanya kimya kimya na wazazi wamepata adha ya kurudia mtihani na kulipia zile ada mara ya pili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mulugo uliza swali. Swali, swali.

MHE PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Serikali kuwapa adhabu Maafisa wote wa Serikali Wizara ya Afya waliohusika na uvujaji wa mitihani? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa hoja yake muhimu ambayo mara nyingi sana na yeye huwaga tunashirikiana na anakuja ofisini mara nyingi. Mheshimiwa Mbunge nikutoe wasiwasi, tunakwenda kuhakikisha kwamba maeneo haya tunakwenda kuyasimamia vizuri kwa mujibu wa kanuni, sheria, taratibu na miongozo iliyopo. Na nikuondoe wasiwasi kwamba jambo lile tayari limeshachukuliwa hatua na liko kwenye hatua za mwisho kabisa kuhakikisha kwamba adhabu inatolewa kwa wale wote waliohusika kwenye jambo hili. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mitihani hii imevuja na inasimamiwa na Wizara ya Afya. Nataka kujua wajibu wa *NACTE* katika kusimamia mitihani hii ni nini? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Sima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa *NACTE* kwenye uratibu wa zoezi zima la mafunzo katika vyuo vyetu vyetu vya kati ni pamoja na mitihani hii. Lakini kwa upande wa mitihani ile ya muhula wa kwanza, mara nyingi sana inafanyika na kusimamiwa na kuratibiwa na Wizara ya Afya.

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimezungumza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tunakwenda kuanzisha chombo maalum kitakachokuwa kinaratibu masuala haya ya mitihani katika Wizara ya Afya kwa ujumla wake ambayo itashirikiana sasa na NACTE kwa ukaribu. Kwa hiyo, matatizo haya tunakwenda kuyamaliza na kuyaondoa kabisa. Nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge wakati mabanda ya Wizara ya Nishati, wewe nenda tu. Mabanda ya Wizara ya Nishati, Waziri na timu yake waliweza kukidhi majibu ya karibuni Wabunge wote kuhusu matatizo ya umeme. *(Makofi)*

Sasa kwa bahati mbaya wengine walikuwa na dharura, walikuwa na shughuli muhimu na ajenda muhimu kama mwenzetu Mheshimiwa Mwambe. Kwa hiyo, sasa Mheshimiwa Cecil Mwambe. *(Makofi)*

Haya inatosha, Mheshimiwa Mwambe. *(Makofi)*

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana. Nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa namna ambavyo mlíchukulia jambo letu mimi na Rose kuwa ni la muhimu sana kwa sisi Wabunge wote humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee sana niwashukuru pia na Waheshimiwa Wabunge kwa kutupa pongezi, tumezipokea, muendeleo kutuomba ili Mungu atulinde. *(Makofi)*

Na. 303

Vijiji vilivyopitiwa na Msongo wa Umeme 33KV unaoelekea Masasi

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaviunganishia umeme vijiji vya Jimbo la Ndanda vilivyopitiwa na nguzo za umeme wa msongo wa 33KV kuelekea Masasi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ndanda lina jumla ya kata 16 na vijiji 69, vijiji 33 vina umeme na 36 bado havijapata umeme vikiwemo vijiji vya Mkungu, Chipite, Mkang'u, Mumburu B, Muongozo, Mdenga na Mbemba

vinavyopitiwa na njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Mahumbika kuelekea Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote 36 ambavyo havina umeme katika Jimbo la Ndanda vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA III mzunguko wa pili unaotekelezwa na Mkandarasi *M/s Namis Corporate Engineers and Contractors*. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kazi ya usambazaji umeme kwenye vijiji ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amevitaja unaendelea, lakini hata hivyo kazi hii bado inafanyika kizamani, kwa maana ya kwamba inafanyika tu sehemu kubwa ya makao makuu ya kata. Lakini inasababisha sasa kwa mfano Kijiji cha Mumburu A na B kwenye vitongoji vya Chalinze na Mtakuja. Lakini pia Chipite, Mkang'u, Mwongozo na Nganga A Shule ya Msingi, Mbemba pamoja na Namali kazi ya kuweka umeme inafanyika kwenye maeneo madogo sana, kwa maana ya scope.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara haioni kuna haja maeneo mapya wanapoweka umeme wakafanya kazi kubwa tofauti na ilivyokuwa zamani wanapeleka nguzo 20 tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwenye Wilaya yetu ya Masasi kumekuwa na tatizo kubwa sana la kukatika katika kwa umeme na Serikali hii ilituahidi kwamba itatengeneza *line* ya pekee kutoka Maumbika mpaka Masasi kwa bajeti ya shilingi bilioni 10. Nataka nifahamu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kazi hiyo inakusudiwa kuanza lini? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye swali la kuongeza wigo wa upelekaji wa umeme kwenye vitongoji, nikiri kwamba kweli bado tunavyo vitongoji vingi ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme, lakini Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imejitahidi kwa kuanzia na mradi wa *REA III round two* kwa kupeleka umeme kwenye vitongoji vya kuanzia katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeshasema hapa mara kadhaa, Serikali inatafuta pesa ya kutosha kabisa kuweza kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini vilivyobakia takribani trilioni sita zinahitajika kwa

ajili ya kukamilisha kazi hii na hatua za kuendelea kutafuta pesa hiyo zinaendelea na tunaamini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tutafanikiwa kwa jambo hilo katika muda mfupi unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, ni kweli Serikali iliahidi kujenga njia ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Maumbika kuja mpaka Masasi na tayari upembuzi umeshafanyika na pesa imeshapatikana na katika bajeti ambayo tunaisoma hapa kesho kipande hicho ni kimoja wapo katika ambavyo tunaviahidi kuvitekeleza katika mwaka wa fedha unaofuata. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nusrat.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru; ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji vya Jimbo la Singida Magharibi ikiwemo Kintataa, Irisia na Mwasutianga? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maalum Singida, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vijiji ambavyo havikuwa vimefikiwa na miundombinu ya umeme lakini Mradi Kabambe wa Upelekaji wa Umeme Vijijini, Mzunguko wa Tatu, Awamu ya Pili, utakamilisha vijiji vyote kufikia Desemba mwaka huu kwa mikataba tuliyokuwa nayo. Kwa hiyo na vijiji alivyovitaja Mheshimiwa vimo katika mpango huo na vitapelekewa umeme.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; nina vijiji 27, vitongoji zaidi ya 300 katika Jimbo la Tarime Vijijini vikiwepo Magoma, Kitenga, Masurura, Gibaso, Nyabitocho, Kebweye, Korotambe, Kegonga, Mosege, Kihongera na Soroneta. Wananchi hawa waliahidiwa kwamba mwaka jana mwezi Desemba umeme ungeweza kuwaka mpaka sasa haujawaka. Mheshimiwa Naibu Waziri ana kauli gani katika maeneo haya ya kupata umeme? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yetu ya kupeleka umeme vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili inaendelea katika vijiji vyote nchini ambavyo havikuwa vimefikwa na miundombinu ya umeme na tunatarajia kuanza Desemba tutaanza kukamilisha miradi hii, na upelekaji wa umeme katika vijiji na vitongoji upo katika hatua mbalimbali.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Waitara kwamba vijiji hivyo viko katika taratibu za kupelekewa umeme na kufikia Desemba tunaamini tutakuwa tumekamilisha mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji hivi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Florence, ajiandae Mheshimiwa Tarimba.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi; je, ni lini Serikali itaunganisha Mkoa wa Kigoma na Gridi ya Taifa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma ni mmoja wapo kati ya mikoa michache iliyokuwa imebakia bila kuunganishwa na Gridi ya Taifa, na nimpe taarifa na habari njema ya Serikali ya Awamu ya Sita kwamba kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu Gridi ya Taifa itakuwa imeanza kufika Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tutapeleka Gridi ya Taifa Mkoa wa Kigoma kwa njia nyingi, naomba uniruhusu nizataje kwa haraka haraka; tunaanza na njia ya msongo wa Kv33 kutoka katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Nyakanazi kwenda Kakonko – Kibondo – Kasulu mpaka Kigoma Mjini, na hiyo itakamilika mwezi Agosti. Kuna njia ya msongo wa Kv 400 ambayo inajengwa kutoka Nyakanazi kwenda mpaka Kigoma, mkandarasi wa TATA yuko site; lakini kuna njia ya msongo wa kv 400 inayotoka Sumbawanga kuja kuingia mpaka Kigoma, na yenyewe itapeleka pia umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema zaidi ni kwamba tunajenga mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Malagarasi (megawati 49.5), kufikia mwaka 2025 utakuwa na wenyewe umefikisha umeme.

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri, ameshakuelewa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tarimba, halafu Mheshimiwa Manyinyi.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo ya kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Kinondoni na mara nyingi sana bila hata taarifa kutoka TANESCO.

Ni nini kauli ya Serikali katika kuondoa tatizo hili ili wananchi wa Kinondoni waweze kuishi kwa amani na kupata huduma hii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kabisa jitihada kubwa zimefanyika katika siku chache zilizopita na imepunguza sana kukatikakatika kwa umeme katika maeneo mengi sana nchi. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti inayokuja, Serikali imetenga pesa ya kutosha kwa ajili ya kurekebisha vituo vya kupoza umeme, kuongeza ukubwa wa transfoma tulizonazo, kurekebisha miundombinu ya umeme kama nyaya na nguzo na hivyo tuna uhakika kwamba kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha ujao matatizo ya kukatika kwa umeme yatakuwa kama siyo kuisha, yamepungua kwa asilimia kubwa kabisa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tarimba ulikuwa na ratiba nzito wiki iliyopita, tulishatangaza Bungeni Rais ametoa shilingi bilioni 500 kwa nchi nzima kurekebisha *stabilization* ya umeme nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Manyinyi.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Musoma Mjini, Mitaa kama Bukoba, Songambele, Zanzibar na kule Bukanga mwaka mmoja nyuma ilikuwa inapata umeme wa shilingi 27,000 kwa sababu ni mitaa ya pembezoni. Lakini kwa sasa hivi tayari mambo yamegeuka, wanalipa zaidi ya shilingi 300,000 ambapo wananchi wengi hawana uwezo.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kuendelea kuwaruhusu waendeleo kulipia umeme kwa bei ya shilingi 27,000 kama ilivyokuwa awali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mathayo Manyinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto ya tafsiri na utekelezaji wa gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi, na kwa haraka haraka kuna watu wako maeneo ya mijini na wanaonekana wako mijini lakini hali zao za kiuchumi hazawezi kukidhi malipo ya gharama kubwa ya kuunganisha umeme. Lakini vilevile kuna watu wanaonekana wako maeneo ya vijijini, lakini hali zao za kiuchumi ni kubwa na wanaweza wakalipa zile gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuonekana kuna changamoto hiyo tumepata maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, na tayari imeundwa timu ambayo inapita kila eneo na kubaini namna gani nzuri ya kuweza kupeleka umeme na gharama nafuu katika maeneo hayo. Na katika bajeti tunayosoma kesho hilo ni eneo mojawapo ambalo tutalieleza na kutoa ahadi njema ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 304

Serikali Kuwasaidia Wakulima wa Parachichi – Iringa

MHE. DKT. RITTA E. KABATI aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa parachichi Iringa ili waweze kulima kilimo chenye tija?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwawezesha wakulima wa parachichi Mkoani Iringa na kwa nchi nzima, Serikali inachukua hatua zifuatazo: -

- (i) Kuzalisha miche milioni 20 kwa kushirikiana na sekta binafsi na kuziua kwa njia ya ruzuku;
- (ii) Kufanya utaratibu wa usajili wa wazalishaji wa miche;

- (iii) Kuandaa mwongozo wa kusimamia soko la parachichi na kuandaa mfumo wa madaraja;
- (iv) Serikali kujenga vituo vya kuhifadhi parachichi la kuchakata na kuhifadhi (*common use facility*) katika mikoa mitatu kwa maana ya Dar es Salaam, Kilimanjaro - Wilaya ya Hai na Iringa - Wilaya ya Mufindi, Kijiji cha Nyororo).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tarehe 8 Agosti huwa ni siku ya wakulima nchini, na siku hiyo wakulima wengi hupata fursa ya kukutana kuonesha maonesho na kujifunza, na kwa kuwa Serikali imesimamisha haya maonesho karibu mwaka mmoja na nusu sasa.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kusimamishwa Maonesho haya ya Nanenane nchini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa kumekuwana vikwazo vingi sana barabarani kwa magari yanayosafirisha bidhaa hizi za mazao yanayoharibika kama nyanya, parachichi na kadhalika na kusababisha hasara kubwa sana kwa wakulima.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa vibali maalum kwa ajili ya magari yanayosafirisha mazao haya kwa saa 24, kwa sababu kuna magari makubwa ambayo yanazuiwa, saa 12 yanaambiwa yasisafirisha mazao kupeleka hata nje ya nchi kama *South Africa*? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, zao la parachichi na mfumo mzima wa parachichi katika nchi yetu haukuwa na mwongozo. Kwa hiyo Serikali sasa hivi iko kwenye hatua za mwisho na tutazindua mwongozo wa kusimamia zao la parachichi kuanzia shambani mpaka sokoni na utaratibu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kupitia Bunge lako tukufu wakati tunafanya mawasiliano ndani ya Serikali kati ya Wizara ya Kilimo, TRA na

watu wa TANROADS kwa maana ya Wizara ya Miundombinu ili ku-develop stika maalum ambazo zitasimamia mazao ya *horticulture*, magari yote yanayobeba mazao ya *horticulture* yatakuwa na stika maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nipitie Bunge lako tukufu kuziomba Mamlaka za Serikali za Mitaa kwamba mazao ya *parachichi* na mazao ya *mbogamboga* ni *perishable*, ni vizuri kutokuweka vikwazo visivyokuwa na ulazima barabarani kwa kipindi hiki ambacho tunaandaa mwongozo ambao utasimamiwa ndani ya Serikali katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo huu utaratibu wa kuwazuia kusafiri usiku nadhani siyo sahihi na ninapenda kupitia Bunge lako tukufu kuwaomba viongozi wa mikoa wa-*facilitate transportation* ya mazao ya kilimo hata kama ni usiku namna gani. Kama mtu anasafiri aendelee na kusafirisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kipengele cha pili kuhusu Nanenane; ni kweli Serikali ilisimamisha Nanenane kwa muda, na ninataka kupitia Bunge lako tukufu kuwatangazia Watanzania na wakulima kwamba Nanenane tunarudisha na mwaka huu Kitaifa itafanyika Mkoa wa Mbeya. Serikali iko kwenye kufanya *total reform* ya mfumo wa Nanenane. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ningepitia Bunge lako tukufu kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa; shughuli za Nanenane zitasimamiwa na Wizara ya Kilimo na sekretarieti za mikoa. Taasisi iliyokuwa inaitwa *TASO* ambayo ilikuwa imejamilikisha kusimamia Nanenane haitahusika na wala haihusiki na masuala ya Nanenane na viwanja vya Nanenane. Suala hili litasimamiwa na Serikali, Wizara ya Kilimo na Mamlaka za Mikoa kwa maana ya mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa hivi tuko kwenye hatua za mwisho za kuandaa mfumo mpya wa shughuli za Nanenane, na Tanzania tutakuwa na kitu tunaitwa *Tanzania International Agricultural Trade Show* ambapo tutakuwa na eneo moja ambalo nchi nzima kila mwaka kimataifa litakuwa linafanyika hapo na mikoa itakuwa inafanya shughuli za kikanda. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Deo Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni kumekuwa na taarifa ambazo zimekuwa zikitapakaa kwenye mitandao pamoja na picha zikionesha kwamba *parachichi* ya Tanzania haikidhi viwango, jambo ambalo siyo kweli. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Watanzania na niwahakikishie wateja wote wanaonunua parachichi za Tanzania kuwa parachichi za Tanzania zinakidhi vigezo vya kimataifa na ndiyo maana tumekuwa sasa hivi tukifungua masoko mapya na hivi karibuni tumefungua soko la India, na ni Tanzania pekee ambayo imepata *import duty exemption* ya parachichi yake katika soko la India, hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; tunazo *international certification institutions* ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, parachichi yetu inapotoka nje ya mipaka inakuwa na *certifications* za kimataifa zote ambazo zinakubalika katika soko la dunia. Kumekuwa na tatizo la *competitors* wetu na mimi nataka niwaombe *exporters* wa Tanzania wahakikishe wanapo-export parachichi ya Tanzania inaondoka na *trademark* iliyoandika *Produce of Tanzania* ili kuweza kui-protect *image* ya parachichi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindani upo, watu watataka ku-*distort image* yetu. Niwaombe Watanzania, yeyote anayepata taarifa yenye mashaka kuhusu *product* ya Tanzania awasiliane na Wizara ya Kilimo na sisi tutakuwa tayari kui-protect bidhaa yetu popote pale.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni 127 wa Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni viongozi na watendaji wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo wakiongozwa na Mheshimiwa Balozi Joseph Sokoine, Katibu Mkuu; karibu sana na Mheshimiwa Balozi Fatma Rajab, Naibu Katibu Mkuu. (Makofi)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Balozi Mulamula ni wawakilishi wa Jumuiya za Kimataifa kutoka ofisi za kibalozi na mashirika ya kimataifa yaliyopo nchini, nitawatambua; H.E. Ahamada El Badaoui Mohamed, Dean of Diplomatic Corps and Ambassador, welcome to the Parliament. (Makofi)

H.E. Andrew Kumwenda, High Commissioner of Malawi, welcome to the Parliament. (Makofi)

H.E. Ricardo Ambrosio Sampaio Mtumbuida, High Commissioner of Mozambique, muito obrigado, karibu sana. (Makofi)

H.E. Lebbius Tangeni Tobias, High Commissioner of Namibia. (Makofi)

31 MEI, 2022

H.E. Zakaria El Goumiri, Ambassador of the Kingdom of Morocco. (Makofi)

H.E. Tri Yogo Jatmiko, Ambassador of Indonesia. (Makofi)

H.E. Mahayub Buyema, Ambassador of Saharawi. (Makofi)

H.E. Chen Mingjian, Ambassador of China. (Makofi)

H.E. (Rtd.) A.N. Sanyatwe, Ambassador of Zimbabwe. (Makofi)

Hon. Dr. Peter Mutuku Mathuki, Secretary General of EAC. (Makofi)

Hon. Eng. Steven D.M. Mlote, Deputy Secretary General of the EAC. (Makofi)

Hon. Ngoga Martin, Speaker East Africa Legislative Assembly; ahsanteni. Spika Ngoga ni familia ya Bunge la Tanzania, karibu sana Spika Ngoga. (Makofi)

Ms. Sarah Gordon Gibson, Country Director and Representative World Food Programme. (Makofi)

Hon. Judge Amani Daouf Aboud, President African Court. (Makofi)

Mr. Lahoucine Rahmoni, Deputy Ambassador of the Kingdom of Morocco. (Makofi)

Mr. Yang Zhiyu, Counsellor, Chinese Embassy. (Makofi)

Ms. Liu Xiaoyi, Attachee Chinese Embassy. (Makofi)

Ms. Melissa Yuanita Repi, Head of Protocol and Consular Affairs, Indonesia Embassy. (Makofi)

Mr. Jealous Chirove, In charge ILO. (Makofi)

Mr. Faraja Msangi, OIC – UNESCO. (Makofi)

Ms. Sinead Collins, Second Secretary, Ireland Embassy. (Makofi)

Mrs. Pham Thi Nguyet, Second Secretary of Vietnam Embassy. (Makofi)

Mr. Chris Msocha, Counsellor of Zimbabwe Embassy. (Makofi)

Ms. Edna Maria Dos Santos, Third Secretary, Angola Embassy. (Makofi)

31 MEI, 2022

Mr. Tomoyoshi Tabuchi, Representative, Embassy of Japan. (Makofi)

Mr. Christopher Denis Ntyangiri, Grants Assistance Grass Roots Human Security Project, Embassy of Japan. (Makofi)

Mr. Richard Shaba, Liaison Officer – Embassy of The Federal Republic of Germany. (Makofi)

Wote karibuni sana kwenye Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge, wasimame kwa pamoja. Wageni wote wa Wabunge, simameni kwa pamoja, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 100 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 31 Mei, 2022 saa 7.00 mchana kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wote katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina itahusu migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Semina hiyo itaendeshwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo ambayo ni muhimu saa 7.00 mchana.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilisha leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na pia lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda nitawasilisha hotuba yangu kwa muhtasari hivyo naomba hotuba yangu ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023 isomeke na kuchukuliwa yote kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza mwaka mmoja wa kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo mawili, kwanza kabisa kwa uongozi wake makini, nyota yake angavu akiwa mwanadiplomasia namba moja uliyotuwezesha kuipaisha nchi yetu kwenye medali ya diplomasia kama nchi ya kimkakati na ya kutumainiwa. Kwa hakiki amefanya kazi yangu kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwa laini na nyepesi. Hakuna mlango alioungonga ambao haukufunguka, mialiko kwake imekuwa mingi, muda unakuwa mchache. Pili nimshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kuniamini kuingoza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na mwanadiplomasia namba moja nchini kwa hatua anazozichukua katika kuitangaza Tanzania Kimataifa. Kwa namna ya kipekee nimpongeze kwa hatua zake za ubunifu kupitia filamu ya Tanzania *The Royal Tour* ambayo inaendelea kuitangaza Tanzania na kuirajamu kwa fursa zake hususan katika utalii, utamaduni, uwekezaji na biashara. Katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Mheshimiwa Rais Wizara imeweka filamu hiyo kwenye tovuti za Balozi za Tanzania na kila Ubalozi umejipanga vyema kuitangaza ipasavyo kama wanavyosema wataitangaza *far and wide* kwa lugha zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Phillip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namshukuru kwa uongozi wake kwenye kusimamia masuala ya Muungano na masuala ya Mazingira. Uongozi wake umekuwa msaada mkubwa kwetu katika diplomasia, mabadiliko ya tabia nchi yaani *climate change diplomacy* ambayo imeshika kasi kwa sasa duniani. *(Makofi)*

Namshukuru pia kwa kuiwakilisha nchi yetu kwenye mikutano mikubwa ya Kimataifa anayemwakilisha Mheshimiwa Rais *ikiwemo World Economic Forum* uliyomalizika hivi karibuni tarehe 26 Mei, 2022 huko Davos Uswizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu ni Wizara ya Muungano, hivyo mafanikio yetu katika kulinda na kuendeleza maslahi ya Taifa hayawezi kupatikana bila mchango mahsusi na muhimu wa Zanzibar. Kwa namna ya kipekee nimshukuru Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na kupitia kwake niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano wanaotupatia. *(Makofi)*

Nimepata fursa ya kukutana na Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa mara kadhaa katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kupata miongozo yake kwa yale mahsusi ya utekelezaji wa sera yetu ya mambo ya nje. Nimshukuru pia Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiwakilisha nchi yetu na Rais wetu vizuri kwenye mikutano ya wakuu wa nchi wa SADC kuhusu masuala ya amani, ulinzi na usalama na kwenye makongamano ya uchumi, biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Kassim Majaaliwa Majaaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake shupavu na ufuatiliaji wake wa karibu wa masuala yanayohusu yanayohusu utendaji wa Wizara yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa hotuba yake nzuri aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na muongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Namshukuru pia kwa kuiwakilisha vyema nchi yetu na kumuwakilisha Mheshimiwa Rais kwenye mikutano na shughuli mbalimbali nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa na Bunge hili kwa asilimia 100 kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wingi wa kura za Wabunge ni kauli thabiti kuwa tuna imani na wewe Mheshimiwa Spika na kwamba umeenea na kutosha katika kiti hicho. Naamini uko humu ndani unanisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze pia kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakushukuru kwa uongozi wako mahiri wakati ukiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Nje ya Ulinzi na Usalama. Aidha, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge; dada yangu Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge maarufu kwa kuendelea na majukumu yao ya kukusaidia kutekeleza kikamilifu majukumu ya kuliongoza Bunge letu tukufu. *(Makofi)*

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, ninawapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushauri mzuri na ulezi wao kwa Wizara yetu. Naomba nikiri kuwa Kamati inatupatia ushirikiano mzuri sana na daima michango yao imejielekeza katika kutujenga na kutuimarisha. Wanatutia moyo na kutupa ari kubwa ya kuendelea kupambania maslahi ya nchi yetu huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na waliyonitangulia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na kuchaguliwa kuwa wawakilishi wa wananchi kwenye Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Aidha, naomba kwa masikitiko kutoa pole kwako na kwa Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mheshimiwa Elias Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa Marehemu William Tate Ole-Nasha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Marehemu Mheshimiwa Irene Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa.

Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa salamu za rambirambi kufuatiwa kuondokea kwa Balozi wetu Edwin Rutageruka aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Diplomasia ya Uchumi Wizarani. Mwenyezi Mungu aziweke roho za wapendwa wetu mahali pema peponi na azitie nguvu na kuzipa faraja familia zao.

Mheshimiwa Spika, niruhusu kipekee nimshukuru mume wangu mpendwa Mhandisi Dkt. George Steven Mulamula kwa kuwa msada na nguzo yangu imara toka ujanani hadi sasa. Nawashukuru watoto wangu Taya na Alvin na familia zao, pamoja na familia yangu kwa ujumla wao ambao wengi wao wako hapa kwa uvumilivu wao na kuendelea kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ambayo mara nyingi yanani lazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu. Wao ndiyo utu na utulivu wangu kama wasemavyo vijana wa mjini, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ingawa si mwisho kwa umuhimu, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na taasisi zake ambayo nasema ni majembe yangu kwa lugha isiyo rasmi kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kulinda na kutetea maslahi ya nchi yetu ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Kwa namna ya pekee, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, namshukuru Balozi Joseph Edward Sokoine, Katibu Mkuu, namshukuru Balozi Fatma Mohammed Rajab, Naibu Katibu Mkuu,

nawashukuru Waheshimiwa Mabalazi wa Tanzania walioko nje, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi, kwa ufanisi, kwa moyo wa uzalendo na kujitoa kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu sasa nizungumzie kwa ufupi Tanzania na Uhusiano wa Kimataifa. Dunia imebadilika, changamoto mpya zimezaa mazingira mapya, leo hii janga la UVIKO-19 limefanya pia suala la majanga ya afya kuwa sehemu ya diplomasia duniani yaani *Global Health Diplomacy*. Halikadhalika hali ya mabadiliko ya tabia nchi linatishia uhai wa dunia, mahitaji ya dunia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na mahitaji ya nishati mbadala nayo yamebadilisha mawanda ya diplomasia. Sasa tuna diplomasia ya tabia nchi yaani *climate change diplomacy*. Wakati huohuo hususan Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imezaa diplomasia ya umma yaani *public diplomacy* inayotaka sera ya mambo ya nje iwajibike kwa umma na tutumie teknolojia na mitandao kuishawishi na kupanua maslahi yetu nje. Sera yetu ya mambo ya nje nayo haina budi kubadilika kuendana na nawakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo halitabadilika ni misingi ya sera yetu, Sera yetu ya Mambo ya Nje ambayo imetuvusha salama katika majira yote na kutuheshimiwa duniani kama nchi huru na yenye kutumainiwa. Misingi hiyo ni kutounga mkono vitendo vya uonevu na ukandamizaji popote pale duniani, lakini pia kulinda uhuru wetu, kulinda mipaka ya nchi yetu, kutetea haki, kuimarisha ujirani mwema, kutekeleza sera ya kutofungamana na upande wowote na kutambua dhima ya Umoja wa Mataifa katika utatuzi wa migogoro na ushirikiano wa Kimataifa katika kutatua changamoto za dunia yaani *multilateralism*, katika haya Tanzania itabaki ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekamilisha mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 na kuandaa rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje ambayo kwa sasa ipo katika ngazi ya maamuzi Serikalini. Sera inayopendekezwa imezingatia maeneo mapya yenye maslahi mapana kwa Taifa ikiwemo msisitizo wa ushiriki wa sekta binafsi, ushirikishwaji wa *diaspora* katika kuchangia maendeleo ya nchi, uchumi wa kidijitali, masuala ya uchumi wa bluu, uhifadhi wa mazingira na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na kukuza matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nizungumzie kwa kifupi kuhusu hali ya siasa, ulinzi na usalama duniani; mafanikio ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023 na kufikiwa kwa malengo ya Serikali na Taifa kwa ujumla kama yalivyofafanuliwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na bajeti zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri yatategemea sana na

mwenendo wa hali ya dunia kisiasa, kiusalama na kiuchumi. Kutokana na uhalisia huo tumeanisha taarifa kuhusu mienendo hiyo katika aya ya 18 hadi aya ya 32 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu tu kwa uchache hata hivyo kugusia kidogo kuhusu hali ilivyo. Tunaona mambo mawili yakiendelea kuathiri mwenendo wa dunia kwa mwaka 2022/2023; kwanza kabisa dunia ingali inajitutumua kuamka kutoka kwenye athari za janga la UVIKO-19, bado mnyororo wa uzalishaji duniani yaani *supply change* haujatengamaa, gharama za usafirishaji nazo zimebaki juu na muda wa usafirishaji umekuwa mrefu kutokana na uchache wa meli. Hali hii imesababisha kuibuka kwa mtikisiko wa biashara duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, vita kali inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambayo kwa kweli hatma yake badi haijajulikana. Vita hii imechangia kupanda kwa bei za mafuta na bei ya ngano duniani. Mafuta na ngano ni bidhaa muhimu pia katika uzalishaji viwandani. Matokeo yake bei ya bidhaa nyingi zimepanda, tunaomba Mwenyezi Mungu lisitokee tena janga lingine la afya au vita.

Aidha, Tanzania inaunga mkono jitihada za Kimataifa za kutatua vita na migogoro inayoendelea duniani kwa njia za amani na njia za kidiplomasia na tunaunga pia jitihada za Kimataifa za kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotufaraji na kututia moyo kwa upande wetu ni uongozi imara na Madhubuti wa Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kutokana na haiba yake na kukubalika duniani tumeweza kudhibiti kwa kiasi kikubwa athari hizi. Kuaminiwa kakwe kumutuwezesha kupata chanjo na mikopo nafuu ya kukabiliana athari za kiuchumi za UVIKO-19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, misingi ya sera na hali ya dunia, ninaomba sasa uniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki yameanishwa katika Muundo wa Wizara katika Toleo la tarehe 4 Februari, 2022 na katika aya ya 34 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulizingatia pamoja na masuala mengine llani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya mwaka 2020 hadi 2025, imezingatia Mpango wa Tatu wa Taifa wa

Maendeleo wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026. Pia imezingatia Sera yetu ya Mambo ya Nje na maagizo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na viongozi wa Kitaifa. Pia imezingatia maazimio ya Bunge lako tukufu, imezingatia pia maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu sasa nipitie Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa upande wa mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kukusanya shilingi 2,550,879,000. Kati ya kiasi hicho, shilingi 47,240,000 ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na shilingi 2,503,636,000 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania nje. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na uthibitisho wa nyaraka, pamoja na pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya zabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 854,335,192 sawasawa na asilimia 33 ya lengo letu. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi zetu. Hali hii imesababishwa na janga la UVIKO-19 uliosababisha biashara nyingi katika nchi mbalimbali kufungwa na utaratibu wa biashara hizo kufanyia kazi majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha shilingi 192,265,438,000 kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 178,765,438,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 13,500,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwezi Aprili, 2022 Wizara imepokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi 174,640,751,565. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 90.8 ya fedha zote za bajeti katika mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022, Wizara ilitumia kiasi cha shilingi 174,640,751,568 kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa. Maelezo zaidi kuhusu mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yameainishwa kwenye aya 37 hadi 41 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutaja majukumu ya Wizara, miongozo mbalimbali iliyozingatiwa katika utekelezaji wa majukumu pamoja na taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ninaomba nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi husika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi za Afrika, Asia na Austrasia, nchi za Mashariki ya Kati na nchi za Ulaya na America katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya Kimataifa ya Dubai (*Dubai Expo-2020*) yaliyofanyika kuanzia mwezi Oktoba, 2021 hadi Machi, 2022 Dubai Umoja wa Falme za Kiarabu na ambayo yaliyashirikisha nchi 192. Nchi yetu ilipewa heshima ya kuwa na siku maalum ya Tanzania katika maonesho hayo yaliyoadhimishwa tarehe 26 Februari, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa mgeni rasmi katika siku hiyo maalum ambapo alihutubia viongozi wa Serikali, wafanyabiashara, wawekezaji na washiriki wengine wa maonesho hayo. Hotuba hiyo ilirushwa mbashara na kutazamwa na nchi nyingi duniani na hivyo kutoa nafasi kwa nchi yetu kujitangaza vyema katika Jumuiya ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Jijini New York, Marekani ambako ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mkutano huo, Mheshimiwa Rais alielezea Jumuiya ya Kimataifa kuhusu juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukabiliana na athari za kiafya, kijamii na kiuchumi zilizosababishwa na mlipuko wa UVIKO-19 duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Tanzania ilisisitiza umuhimu wa Jumuiya ya Kimataifa kutumia majukwaa ya diplomasia majumui kukabiliana na matatizo yanayoikabili dunia. Maelezo zaidi kuhusu ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi za Afrika, nchi za Asia na Austrasia nchi za Mashariki ya Kati, nchi za Ulaya na Mashirika ya Kimataifa naomba nielekeze katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia aya ya 43 hadi 106 ambayo imechukua nafasi kubwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ili kunufaika na fursa zinazopatikana katika Jumuiya hizo kama ifuatavyo:- Naomba nianze na Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Leo umeona kwamba kuna uwakilishi mkubwa kutoka Jumuiya ya Sekretarieti ya Afrika Mashariki pamoja na Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za mtangamano za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia masuala mapana ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2022 Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi

Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Mkutano huo nchi wanachama ziliridhia ombi la Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) kujiunga na Jumuiya, hatua itakayoifanya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na wanachama saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Aprili, 2022 Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mwenyekiti wa Jumuiya kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki alisaini, pamoja na Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Shilombo Rais wa DRC mkataba wa kuiwezesha nchi hiyo kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa DRC inaendelea na taratibu za ndani za kikatiba za kuridhia mkataba huo na inatarajiwa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya, hati ya kuridhia kujiunga kabla ya tarehe 29 Septemba, 2022 yaani mwaka huu ili kuwa mwanachama kamili. Kujiunga kwa nchi hiyo ni kiashiria cha kuendelea kukua kwa Jumuiya na kuongezeka kwa fursa za kiuchumi na kijamii katika Jumuiya. Taarifa ya kina ya namna Wizara ilivyoratibu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama nilivyoeleza katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia aya ya 107 hadi aya ya 136 ya kitabu cha hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kwa kifupi kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC); Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambapo katika kipindi hiki Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa kituo cha SADC cha kupambana na ugaidi chenye makao makuu yake Jijini Dar es Salaam. Kituo hiki kilichoinduliwa rasmi tarehe 28 Februari, 2022 kitasaidia kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Taasisi za Kikanda na za Kimataifa zinazoratibu mapambano dhidi ya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuanzia mwezi Agosti, 2021 hadi Agosti, 2022 Tanzania imeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Rasilimali Watu na Utawala ya SADC na kutokana na Uenyekiti huo Tanzania imechangia kuboresha Sera za Ajira katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Wazee la SADC la Usuluhishi wa Migogoro kwa kipindi cha miaka minne yaani kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2025. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika Bi. Hellen Rwegasira aliyewahi kuwa mtumishi wa Wizara ameteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa timu ya upatanishi ya SADC kwa kipindi cha miaka minne yaani mwaka 2021 hadi mwaka 2025. Kuteuliwa kwa viongozi hawa ni ishara ya Tanzania kuendelea kuaminiwa katika usuluhishi wa migogoro na kutafuta amani katika kanda

yetu. Maelezo ya kina ni kama nilivyoyaelezea katika kitabu changu cha hotuba kuanzia aya ya 137 hadi aya 144. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nizungumzie kwa kifupi kuhusu ushirikiano wetu katika Umoja wa Afrika; mwezi Februari, 2021 Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango Makamu wa Rais alimuwakilisha Mheshimiwa Rais katika mkutano huo. Pamoja na masuala mengine mkutano uliridhia pendekezo la Tanzania la Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika. Aidha, katika mkutano huo Tanzania iliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Aprili, 2022 hadi Aprili, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata heshima ya kumuwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa 16 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, uliofanyika hivi karibuni kuanzia tarehe 27 - 28 Mei, 2022 Jijini Malabo, Equatorial Guinea. Mkutano huu ulijadili masuala ya majanga na huduma za kibinadamu pamoja na masuala ya ugaidi, siasa na itikadi kali na mabadiliko ya Serikali yasiyozingatia misingi ya kikatiba (*Unconstitutional Changes of Governments*). Nilihutubia mkutano huo kwa lugha ya Kiswahili na viongozi wote walifurahia kusikia lafudhi ya lugha ya Kiswahili ikitumika katika mkutano huo kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika jitihada za kukuza lugha yetu ya Kiswahili katika safu ya Kimataifa tarehe 23 Novemba, 2021 nchi wanachama wa Shirika la UNESCO walipitisha kwa kauli moja, tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku ya lugha ya Kiswahili duniani (*World Kiswahili Language Day*). Kutambuliwa lugha ya Kiswahili katika Umoja wa Afrika na UNESCO ni mafanikio ambayo Wizara yangu inajivunia kupitia Balozi zetu katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niongelee kwa kifupi kuhusu Mkataba wa Eneo la Biashara la Bara la Afrika; mwezi Septemba, 2021 kupitia Bunge lako tukufu Tanzania iliridhia Mkataba wa Kuanzisha Eneo Huru la biashara la Bara la Afrika. Kuridhiwa kwa Mkataba huu kunaongeza wigo wa fursa za kukuza soko la bidhaa na huduma za Tanzania katika soko la Afrika. Hatua hii pia itajibu kiu ya wafanyakazi wa Tanzania kutaka kunufaika na fursa za masoko ya nchi nyingine za Afrika ambayo sio wanachama wa Jumuiya ya SADC na *East African Community*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2022 Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia ulielekeza nchi wanachama kufungua soko kwa asilimia 87.7 kati ya 90 zilizokubalika na kuendelea na majadiliano ya asilimia zilizobaki. Hadi sasa

nchi 29 kati ya nchi 44 ikiwemo Tanzania zimewasilisha orodha ya bidhaa zitakazofunguliwa zinazokidhi vigezo vya mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushirikiano wa Kimataifa mwezi Mei, 2022 Wizara iliratibu na kufanikisha uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2022/2027 wa ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Mataifa nchini uliozinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mwakilishi wa Umoja wa Mataifa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo unachukua nafasi ya Mpango wa Pili unaofikia tamati mwezi Juni, 2022. Kupitia mpango huu Tanzania na Umoja wa Mataifa zitashirikiana kutekeleza maeneo ya vipaumbele ya Ajenda 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Mei, 2022 wakati wa Mkutano wa mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) uliofanyika Accra, Ghana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alipokea tuzo ijulikanayo kama *2020 Super Prize Great Bidder Trophy* inayofadhiliwa na *African Development Bank* na kutolewa na *Africa Builders*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutunukiwa tuzo hii inayotambua mchango wake kwenye mafanikio ya ujenzi na mtandao wa barabara na reli hapa nchini, pamoja na uongozi wake kwenye usimamizi wa fedha nyingi zilizoingia kwenye ujenzi wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio la Bunge lako tukufu la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kupokea tuzo hiyo. Maelezo ya kina kuhusu ushirikiano wa Kimataifa yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba kuanzia aya ya 145 hadi aya ya 161.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nieleze kwa kifupi kuhusu kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na hati za makubaliano za ushirikiano. Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mikataba na hati za makubaliano ya ushirikiano zinazolenga kuimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi nyingine na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa hati na mikataba hiyo iliyosimamiwa na Wizara, taasisi na sekta binafsi kulingana na maudhui yake ili kuhakikisha nchi inanufaika. Orodha ya mikataba na hati hizo imeambatishwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kwenye ukurasa wa 115 hadi 121. Wizara imeendelea kuratibu masuala ya

haki na kinga kwa Jumuiya ya wanadiplomasia hapa nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hiki Wizara imeratibu uwasilishaji wa hati za utambulisho kwa Mabalazi kutoka nchi za Australia, Belarus, Chile, China, Colombia, India, Indonesia, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Korea, Malawi, Morocco, Saudi Arabia, Ufaransa na Uholanzi. Aidha, binafsi hivi karibuni nimepokea nakala za hati za utambulisho kwa Mabalazi wa nchi za Ethiopia, Cuba na Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuimarisha uhusiano na Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini, Wizara imejiwekea utaratibu wa kukutana nao na kutoa taarifa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa, Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kushirikiana nami katika kutoa taarifa hizo kwa manufaa ya nchi yetu na mahusiano na nchi nyingine. Serikali imeendelea kuongeza wigo wa uwakilishi nje ya nchi kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Katika kipindi hiki Serikali imefungua Ubalozi na uwakilishi wa kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa Vienna, Austria. Tumefungua Ubalozi wa Tanzania Jakarta, Indonesia na Konseli Kuu mbili katika Jiji la Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Jiji la Guangzhou, China zimefunguliwa katika kipindi hiki. Hatua hiyo inaifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 45 duniani na Konseli Kuu tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za viongozi wakuu wa kitaifa katika nchi mbalimbali na ziara za viongozi wa Serikali na mashirika ya kimataifa hapa nchini, kama nilivyoeleza kuanzia aya ya 162 hadi aya ya 165 ya kitabu cha hotuba yangu. Ziara hizo zinaendelea kuifungua Tanzania kimataifa katika azma yake ya kukuza na kutekeleza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kwa kifupi kuhusu utaratibu wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi yaani wana-*diaspora*; Wizara inaendelea kuhamasisha *diaspora* kuchangia maendeleo nchini. Kutokana na jitihada hizo, mchango wa *diaspora* umeendelea kuongezeka ambapo kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Kuu ya Tanzania fedha zilizotumwa na *diaspora* nchini (*remittances*) zimeongezeka kutoka dola za Marekani takribani milioni 400 mwaka 2020 hadi kufikia dola za Marekani 569,300,000 mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, *diaspora* pia wamewekeza kiasi cha shilingi bilioni 3.9 katika mfumo wa UTT AMIS na kununua nyumba zenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 za Shirika la Nyumba la Taifa na mradi wa *Hamidu City Park* uliopo Kigamboni, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha mikutano baina ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *diaspora* wakati wa ziara zake nchini Kenya, Burundi, Ufaransa, Ubelgiji, Umoja wa Falme za Kiarabu na Marekani. Aidha, iliratibu na kufanikisha mkutano kati ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *diaspora* waliopo Singapore. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishiriki mkutano wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na *diaspora* wanaoishi katika nchi mbalimbali uliofanyika kwa njia ya mtandao. Vilevile kwa nyakati tofauti nilikutana na kufanya mazungumzo na *diaspora* wanaoishi nchini Kenya, Italia, Saudi Arabia, Jamhuri ya Korea na Marekani. Mikutano hiyo ilitoa fursa kwa *diaspora* kupata taarifa za uwekezaji, ufafanuzi wa sera na mipango mbalimbali ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kutoa shukrani kwa *diaspora* na jumuiya zao kwa kuendelea kuchangia maendeleo ya uchumi nchini. Maelezo zaidi kuhusu ushiriki wa wana-*diaspora*, uratibu na Watanzania wanaoishi nje ya nchi yapo katika aya ya 170 hadi aya ya 177 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nieleze utawala na maendeleo ya watumishi; Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kufanikisha malengo ya utekelezaji wa dhamana na majukumu yake. Katika kutekeleza hilo watumishi 138 wa kada na vyeo mbalimbali walipelekwa balozini katika mwaka wa fedha 2021/2022 ili kuimarisha utendaji katika Balozzi za Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi 19 kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Austria, Brazil, Comoros, Ethiopia, India, Indonesia, Italia, Israel, Kuwait, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Japan, Malawi, Marekani, Misri, Qatar Rwanda, Sweden na Urusi. Vilevile Mheshimiwa Rais amewateuwa mabalozi saba kuwa wakurugenzi wa idara na vitengo na Wizara imewathibitisha wakurugenzi watatu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2020/2021, Wizara imeendelea na jukumu la kusimamia matumizi ya fedha na mali za Serikali. niseme ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara na Balozzi zake imepata Hati Safi za Ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo, 2019/2020 na 2020/2021. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako kuwa Wizara inaendelea kuboresha matumizi, mifumo na usimamizi wa fedha na utunzaji wa mali za

Serikali kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Maelezo zaidi yako kwenye hotuba yangu aya 139 hadi 138. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara umeendelea vizuri. Wizara ilitengewa bajeti ya maendeleo ya shilingi 13,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Wizara imekamilisha taratibu za ununuzi kupata wakandarasi watakaotekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati kwenye Balozi zetu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri muda wako umekwisha omba pesa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
...Nairobi, Kinshasa, Muscat na Washington DC.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu sasa niweze kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,559,879,000; mapato haya yatatokana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania ambavyo ni pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na kuthibitisha nyaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023; Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha shilingi 208,366,964,000; kati ya fedha hizo shilingi 203,666,964,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinazojumuisha shilingi 188,937,219,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 14,729,745,000 kwa ajili ya mishahara. shilingi 4,700,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara, shilingi 500,000,000 ni kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini (APRM); shilingi 1,000,000,000 ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia; shilingi 1,243,661,150 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; na shilingi 170,000,000 ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 2,833,778,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi 4,700,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi 4,000,000,000 ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyopo jijini Arusha na shilingi 700,000,000 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho. Ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 208,366,964,000 na kati ya fedha hizo shilingi 203,666,964,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,700,000,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Unatakiwa Mheshimiwa Waziri kutoa hoja. Wewe toa hoja, toa hoja wenzio ndio wasimame.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Eeh?

NAIBU SPIKA: Umeunga mkono? Umetoa hoja?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (MB.), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na pia lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

3. Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja wa kuiongoza nchi yetu. Ninawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wao mahiri na wa kizalendo.

4. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kimaendeleo katika Taifa letu ikiwemo kuimarika kwa diplomasia na uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa. Ninaungana na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuendelea kuwaomba viongozi wetu Wakuu kwa Mwenyezi Mungu aendeleo kuwapa nguvu, ulinzi, afya na kila lililo la heri katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Taifa ikiwemo kukuza na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia. **Kazi lendelee!**

5. Mheshimiwa Spika, ninakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza pia Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Aidha, ninawapongeza Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) kwa kuendelea kukusaidia kutekeleza kikamilifu majukumu ya kuliongoza Bunge letu tukufu.

6. Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, ninawapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya kuishauri Wizara na Serikali kwa ujumla. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ninawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati nyingine za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mhe. Emmanuel Peter Cherehani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea

kuniamini na viongozi wenzangu, Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri; Balozi Joseph Edward Sokoine, Katibu Mkuu; na Balozi Fatma Mohammed Rajab Naibu Katibu Mkuu, kuiongoza Wizara hii. Naomba pia niwapongeze watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa mchango wao katika kufanikisha majukumu ya Wizara. Tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa weledi na utumishi uliotukuka ili kuleta maendeleo katika Taifa letu.

9. Mheshimiwa Spika, kipekee ninapenda kumshukuru mume wangu mpendwa Mhandisi Dkt. George Steven Mulamula; watoto wangu pamoja na familia yangu kwa uvumilivu wao, na kuendelea kunipa moyo katika kutekeleza majukumu yangu ambayo mara nyingi yanatilazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu. Mungu awabariki sana.

10. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba zao katika Bunge hili la Bajeti.

11. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako na Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mhe. Elias Kwandikwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mhe. William Tate Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); na Mhe. Irene Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Nitoe pia pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wetu.

12. Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa salamu za rambirambi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Serikali, Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini na Washirika wa Maendeleo kufuatia kifo cha Balozi Edwin Rutageruka aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Diplomasia ya Uchumi Wizarani. Tunatambua na kuthamini upendo na faraja katika kipindi hicho kigumu.

13. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya, familia na Wakenya wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Emilio Mwai Kibaki aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu aliyefariki tarehe 22 Aprili 2022. Aidha, ninatoa salamu za pole kwa Mtukufu Sheikh Mohammed bin Zayed Al Nahyan, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), familia na wananchi wote wa Umoja huo kwa kuondokewa na Mtukufu Sheikh Khalifa bin Zayed bin Sultan Al Nahyan aliyekuwa Rais wa Pili wa UAE aliyefariki tarehe 13 Mei 2022. Kadhalika, ninatoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni Rais wa Jamhuri ya Uganda, Spika wa Bunge la nchi hiyo, familia,

ndugu na jamaa kwa kuondokewa Mhe. Jacob L' Okori Oulanyah aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Uganda. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema, Amina.

2.0 TANZANIA NA UHUSIANO WA KIMATAIFA

14. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa na ushawishi katika Jumuiya ya Kimataifa na kusimamia misingi madhubuti iliyowekwa na Waasisi wa Taifa letu katika uhusiano wa kimataifa ambayo inapinga na kulaani vitendo vya uonevu na ukandamizaji popote duniani, kulinda uhuru na kujiamulia mambo yetu wenyewe; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza sera ya kutofungamana na upande wowote kama dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa.

15. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Wizara imekamilisha mapendekezo ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2022 ambayo ipo katika hatua za kuridhiwa ndani ya Serikali. Mapendekezo ya Sera hiyo yamezingatia maslahi mapana ya Taifa ikiwa ni pamoja na misingi ya Taifa letu, ujirani mwema, diplomasia ya uchumi, uchumi wa buluu, masuala ya Diaspora, mabadiliko ya tabianchi na kubidhaisha Kiswahili. Mapendekezo ya Sera hii, yataendelea kuimarisha uchumi kupitia uhusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa.

16. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa kipaumbele cha kujumuisha masuala ya Diaspora kwenye Sera mpya, na kwa kutambua ombi la Diaspora la muda mrefu la kutaka uraia pacha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa Andiko lenye mapendekezo yanayohusisha maoni mahsusi ya Diaspora. Andiko hilo litatoa mwongozo wa masuala ya Diaspora ikiwemo Hadhi Maalum.

3.0 HALI YA SIASA, ULINZI NA USALAMA

17. Msheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama imeendelea kuimarika katika maeneo mengi duniani. Licha ya changamoto ya vita baina ya Urusi na Ukraine iliyosababisha mtikisiko wa uchumi duniani. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, nchi mbalimbali zilifanya chaguzi kwa utulivu, uhuru na amani. Tunawapongeza viongozi waliochaguliwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali zao.

18. Msheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya siasa, ulinzi na usalama kama ifuatavyo:

3.1 Afrika

19. Mheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama imeendelea kuimarika barani Afrika, isipokuwa katika baadhi ya nchi zenye changamoto za kisiasa na kiusalama zilizosababishwa na uwepo wa makundi ya waasi, mashambulizi ya kigaidi na mapinduzi ya kijeshi. Baadhi ya nchi hizo ni:

Ethiopia

20. Mheshimiwa Spika, mapigano ya wenyewe kwa wenyewe nchini Ethiopia yameendelea kuzorotesha hali ya usalama nchini humo, ambapo vikosi vya Serikali ya Shirikisho la Ethiopia vilikabiliwa na vikosi vya jeshi la Jimbo la Tigray. Tanzania inaunga mkono juhudi za jumuiya ya kimataifa katika kusitisha mapigano kwa njia ya mazungumzo ya amani kurejesha amani nchini humo.

Jamhuri ya Afrika ya Kati

21. Mheshimiwa Spika, kikundi cha waasi cha Seleka kimeendelea kufanya mashambulizi dhidi ya majeshi ya Serikali ya Jamhuri ya Afrika ya Kati hasa katika miji ya Bangui na Bassangoa. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na jumuiya ya kimataifa katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo ikiwemo kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hiyo kwa kuchangia vikosi vya kijeshi kwenye Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani ya Afrika ya Kati (MINUSCA).

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)

22. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini DRC imeendelea kuwa tulivu katika maeneo mengi isipokuwa katika majimbo ya Kivu Kaskazini, Ituri na Kivu Kusini yaliyopo mashariki mwa nchi hiyo. Vikundi vya waasi vikiwemo M23, Cooperative for Development of Congo (CODECO) na Allied Democratic Forces (ADF) viliendelea kufanya mashambulizi ya kutumia silaha dhidi ya wananchi, majeshi ya Serikali na vikosi vya walinda amani. Tanzania inaendelea kuungana na jumuiya ya kimataifa katika kusaidiana kuleta amani nchini DRC kupitia SADC na kwa kuchangia vikosi vya kijeshi kwenye Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani DRC (MONUSCO).

Msumbiji

23. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Msumbiji imeendelea kuwa tulivu katika maeneo mengi isipokuwa katika Jimbo la Cabo Delgado lililopo kaskazini mwa nchi hiyo. Jimbo hilo limeendelea kukabiliwa na changamoto ya kiusalama zinaosababishwa na mashambulizi ya kigaidi yanayofanywa na kikundi cha Ansaar Al- Sunna wal Jamaa. Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi nyingine wanachama wa SADC kurejesha hali ya usalama na amani nchini Msumbiji kwa kuchangia vikosi vya walinda amani katika Misheni ya SADC nchini Msumbiji (SAMIM).

24. Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Agosti 2021 Zambia ilifanya Uchaguzi Mkuu uliomba ushindi Mheshimiwa Hakainde Hichilema wa Chama cha United Party for National Development. Ninatumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hichilema kwa ushindi alioupata pamoja na wananchi wa Zambia kwa kufanya uchaguzi huo kwa amani na utulivu. Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali yake katika kudumisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili.

3.2 Mashariki ya Kati

25. Mheshimiwa Spika, eneo la mashariki ya kati limeendelea kukabiliwa na migogoro ya kisiasa na mapigano katika baadhi ya mataifa hali ambayo imeendelea kudhoofisha usalama wa eneo hilo kama ifuatavyo:

Yemen

26. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Yemen haijatengamaa kutokana na mapigano yanayoendelea kati ya jeshi la Serikali na kundi la wanamgambo wa Houthi. Tunapongeza usitishwaji wa mapigano katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhan, na ni matumaini yetu kuwa hatua hii itakuwa chachu ya kufikia amani ya kudumu kwa taifa hilo. Tanzania inaendelea kuunga mkono msimamo wa Umoja wa Mataifa unaozitaka pande zote zinazohasimiana kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano.

Lebanon

27. Mheshimiwa Spika, Lebanon imeendelea kukabiliwa na changamoto za kisiasa, mdororo wa kiuchumi, ulinzi na usalama ambazo zimesababisha machafuko ya mara kwa mara nchini humo. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za jumuiya ya kimataifa katika kuleta amani na usalama Lebanon, ikiwemo kuchangia vikosi vya kijeshi katika misheni ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa nchini humo (UNIFIL).

Israel na Palestina

28. Mheshimiwa Spika, mgogoro kati ya Israel na Palestina umedumu kwa miongo mingi, ambapo mataifa hayo yameendelea kuwa na mapigano ya mara kwa mara yanayochangia kudhoofisha hali ya usalama katika eneo hilo. Tanzania inaendelea kuunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika yanayozitaka pande husika kuheshimu makubaliano ya kuwepo kwa nchi mbili katika eneo hilo ambazo ni Palestina huru na Israel salama.

3.3 Ulaya na Amerika

29. Mheshimiwa Spika, kiumjama hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Ulaya na Amerika imeendelea kuwa ya utulivu na amani isipokuwa vita kati ya Shirikisho la Urusi na Jamhuri ya Ukraine iliyoanza mwezi Februari 2022. Hatua hiyo imechangia kuzorota kwa hali ya usalama katika eneo la mashariki ya Ulaya. Vita hiyo imesababisha athari hasi katika uchumi wa dunia, ambapo nchi nyingi ikiwemo Tanzania zimeshuhudia kuongezeka kwa bei za bidhaa mbalimbali hususan bidhaa za nafaka, nishati ya mafuta na gesi. Hali hiyo, inatokana na nchi hizo kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa hizo duniani.

30. Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za jumuiya ya kimataifa za kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano baina ya pande mbili zinazohasimiana kwa lengo la kurejesha amani na usalama.

31. Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili 2022, Ufaransa ilifanya Uchaguzi Mkuu uliomba ushindi Mheshimiwa Emmanuel Macron kutoka Chama cha La République en Marche na kuendelea kushika kiti cha Urais kwa muhula wa pili. Ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Macron kwa ushindi alioupata pamoja na wananchi wa Ufaransa kwa kufanya uchaguzi huo kwa amani na utulivu. Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali yake katika kudumisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili.

3.4 Asia na Australasia

32. Mheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Asia na Australasia iliendelea kuwa salama na tulivu licha ya uwepo wa mivutano ya kisiasa baina ya mataifa ya Pakistan na India; na Jamhuri ya Korea na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea. Tanzania inaendelea kuzisihii pande zinazohasimiana kutafuta suluu ya migogoro hiyo kwa njia ya amani.

33. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, misingi ya sera na hali ya dunia, ninaomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

34. Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba nitaje majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama

yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara Toleo la tarehe 4 Februari, 2022 kama ifuatavyo:-

- i. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje;
- ii. Kusimamia na kuratibu masuala ya uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine;
- iii. Kusimamia na kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa;
- iv. Kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za wanadiplomasia waliopo nchini;
- v. Kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki na uwakilishi;
- vi. Kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli;
- vii. Kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
- viii. Kuratibu na kusimamia masuala ya wataanzania wanaoishi ughaibuni;
- ix. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- x. Kuratibu biashara ya kimataifa na diplomasia uchumi;
- xi. Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Wizara; na
- xii. Kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani na katika Balozi za Tanzania.

35. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulizingatia sera, sheria na miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001; Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; Ajenda ya 2030 ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 na Itifaki zake; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 1992 na Itifaki zake; Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 2017/2018 - 2021/2022; na Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo wa SADC 2020 – 2030.

36. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ulizingatia pia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026; na maagizo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

4.1 **Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

4.1.1 **Mapato**

37. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi 2,550,879,000. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 47,240,000 ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na Shilingi 2,503,639,000 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania nje. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na uthibitisho wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya zabuni.

38. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 854,335,191.66 sawa na asilimia 33 ya lengo lililopangwa kwa mwaka 2021/2022. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi. Hali hii imesababishwa na uwepo wa janga la UVIKO-19 uliosababisha biashara nyingi katika nchi mbalimbali kufungwa. Fedha zote za maduhuli zilizokusanywa na wizara ziliingizwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama taratibu zinavyoelekeza.

4.1.2 **Fedha Zilizoidhinishwa**

39. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha Shilingi 192,265,438,000 kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 178,765,438,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 13,500,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida, Shilingi 167,937,219,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 10,828,219,000 ni kwa ajili ya mishahara.

4.1.3 **Matumizi**

40. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Wizara imepokea kutoka HAZINA kiasi cha Shilingi 174,640,751,594.47. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 90.8 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, Shilingi 163,186,284,122.63 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 97.2 na Shilingi 11,454,467,471.84 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 105.8.

41. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara ilitumia kiasi cha Shilingi 174,640,751,594.47. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 163,186,284,122.63 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 11,454,467,471.84 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 105.8. Ongezeko hilo linatokana na watumishi waliohamishiwa Wizarani kutoka Wizara na taasisi nyingine za Serikali pamoja na kupandishwa vyeo kwa watumishi.

42. Mheshimiwa Spika, baada ya kutaja majukumu ya Wizara, miongozo mbalimbali iliyozingatiwa katika utekelezaji wa majukumu pamoja na taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ninaomba nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi husika kama ifuatavyo:

4.2 Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Uhusiano Baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi Nyingine

43. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii kama ifuatavyo:

4.2.1 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika

44. Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara rasmi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda kwa mwaliko wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda. Wakati wa ziara hiyo nchi hizi mbili zilisaini hati mbili za makubaliano ya ushirikiano kuhusu ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme wa kV 400 kutoka Masaka hadi Mwanza na masuala ya ulinzi na usalama. Vilevile, Tanzania na Uganda zilikubaliana kushirikiana katika uzalishaji wa chanjo na dawa za binadamu na mifugo.

45. Mheshimiwa Spika, makubaliano mengine ni kufunguliwa upya kwa njia ya usafirishaji wa mizigo kutoka Mwanza hadi Port Bell Uganda kupitia ziwa Victoria ambayo itapunguza gharama za kufanya biashara ambapo idadi ya siku za kusafirisha mizigo itapungua kutoka wastani wa siku 9 hadi 4. Kupitia makubaliano hayo Tanzania itaanza kununua dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (ARV) na Uganda imeahidi kutuma tani 10,000 za sukari ili kufidia upungufu wa bidhaa hiyo nchini. Wizara itaendelea kufuatilia utekelezaji wa hati hizo.

46. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Umoja wa Ulaya uliofanyika jijini Brussels, Ubelgiji. Katika mkutano huo, Umoja wa Ulaya uliahidi kutenga fedha kiasi cha Euro bilioni 150 kwa ajili ya kufadhili utekelezaji wa miradi ya maendeleo barani Afrika hususan sekta za nishati ya umeme, TEHAMA na uchukuzi ili kuchochea maendeleo ya bara hilo. Aidha, ufadhili huo unalenga kuchagiza utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA). Wizara inaendelea kufuatilia hatua zaidi za utekelezaji wa ahadi hiyo ya Umoja wa Ulaya.

47. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2022 Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa Nne wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda uliofanyika jijini Kampala, Uganda. Katika mkutano huo, Hati sita za Makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ya habari; huduma za jamii, utamaduni na sanaa; mifugo na uvuvi; menejimenti ya utumishi wa umma; elimu na michezo; na afya zilijadiliwa. Majadiliano ya kukamilisha kusainiwa kwa hati hizo yanaendelea.

48. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano ya ushirikiano baina ya Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kati ya Uvinza – Musongati – Gitega – Kindu. Utekelezaji wa mradi huo utainufaisha nchi yetu kiuchumi kwa kuzingatia kuwa nchi za Burundi na DRC zinatumia Bandari ya Dar es Salaam kusafirisha sehemu kubwa ya shehena za mizigo. Ujenzi wa reli hiyo utarahisisha huduma ya uchukuzi na kukuza uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo.

49. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya hapa nchini kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara. Aidha, kupitia ziara hiyo, nchi hizi mbili zimeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

50. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda hapa nchini. Wakati wa ziara hiyo, nchi hizi mbili zilikubaliana kushirikiana katika kukuza na kuimarisha biashara na uwekezaji; kutengeneza chanjo ya kudhibiti UVIKO - 19; kukamilisha utekelezaji wa miradi ya pamoja katika sekta ya nishati na ujenzi wa miundombinu; na masuala ya ulinzi na usalama. Vilevile, Mheshimiwa Marais walishiriki katika kongamano la biashara kati ya Tanzania na Uganda lililowakutanisha wafanyabiashara kutoka nchi hizi mbili. Kadhalika, akiwa hapa nchini, Mheshimiwa Rais Yoweri Museveni alikabidhi Serikali shule ya awali na msingi iliyojengwa wilayani Chato, Geita kwa ufadhili wake.

51. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri. Kupitia ziara hiyo, nchi hizi mbili zilisaini Hati za Makubaliano ya Ushirikiano katika elimu na michezo. Aidha, wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alifanya mazungumzo na wafanyabiashara wakubwa nchini Misri kwa lengo la kuwahamasisha kuwekeza Tanzania. Ninapenda kuliarifufu Bunge lako tukufu kuwa, kufuatia ziara hiyo, mnamo mwezi Desemba 2021 ujumbe wa wafanyabiashara 100 kutoka Misri

ulitembelea nchini na kushiriki ufunguzi wa kiwanda cha kutengeneza vifaa vya umeme kinachoitwa El-Sewedy Electric Company chenye thamani ya Dola za Marekani milioni 35 kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam. Kiwanda hicho kitachangia kukuza ajira, mauzo ya nje na kuongeza mapato ya Serikali.

52. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa Nne wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Kupitia mkutano huo, nchi hizi mbili zilisaini Hati tatu za Makubaliano za Ushirikiano katika maeneo ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia; mashauriano ya kisiasa na kidiplomasia; na uhakiki wa mipaka kati ya Tanzania na Kenya.

53. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda. Ziara hiyo imechangia kuimarisha ujirani mwema kati ya nchi hizi mbili. Aidha, makubaliano yalifikwa kuhusu kuimarisha ushirikiano katika sekta ya uchukuzi hususan uendelezaji wa miundombinu ya ushoroba wa kati kupitia ujenzi wa reli kutoka Isaka – Rusumo, Tanzania hadi Kigali, Rwanda. Vilevile, nchi hizo zilikubaliana kushirikiana katika kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kuongeza fursa za ajira na biashara.

54. Mheshimiwa Spika, vilevile, mwezi Agosti 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa 15 wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda uliofanyika jijini Dar es Salaam. Kupitia mkutano huo, nchi hizi mbili zilisaini Hati nne za Makubaliano ya Ushirikiano katika maeneo ya habari na TEHAMA; elimu; uhamiaji; na udhibiti wa vifaa tiba.

55. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Burundi. Katika ziara hiyo, Marais wa Tanzania na Burundi walifanya mazungumzo na kushuhudia kusainiwa kwa Hati nane za Makubaliano za Ushirikiano kwenye maeneo ya mashauriano ya kisiasa na kidiplomasia, nishati, madini, uvuvi, ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Burundi na Kifaransa nchini Tanzania, kubadilishana wafungwa, kilimo na afya.

56. Mheshimiwa Spika, sanjari na hayo, nchi hizi mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika uendelezaji wa miundombinu ya usafiri na uchukuzi ikiwemo ujenzi wa reli kutoka Uvinza, Kigoma kwenda Musongati - Gitega, Burundi. Aidha, ilikubalika kuharakisha utekelezaji wa mradi wa umeme wa Rusumo wa Megawatt 80 unaotekelezwa na Tanzania, Burundi na Rwanda. Vilevile, nchi hizo zilikubaliana kushirikiana katika sekta ya

mawasiliano hasa baada ya Burundi kuunganishwa na mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye uwezo wa Gigabaiti 100.

4.2.2 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Asia na Australasia

57. Mheshimiwa Spika, ninapenda kukufahamisha kuwa mwezi Aprili, 2022 nilifanya ziara ya kikazi nchini Jamhuri ya Korea kufuatia mwaliko rasmi wa Mhe. Chung Eui – Yong, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Korea. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuadhimisha miaka 30 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Korea ambao ulianzishwa rasmi tarehe 29 Aprili, 1992. Wakati wa ziara hiyo nilifanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Korea pamoja na viongozi wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA) na benki ya Exim ya Korea. Kufuatia mazungumzo hayo Serikali ya Korea imeahidi kuendelea kutoa misaada yake kwa Tanzania kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati.

58. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Tanzania na Japan wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Yen za Japan bilioni 24.31 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Barabara ya Arusha-Holili; mkataba kati ya Tanzania na Japan wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Yen za Japan bilioni 10.864 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Mjini Zanzibar; na mkataba kati ya Tanzania na Japan wa msaada wenye thamani ya Yen za Japan bilioni 2.726 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ukarabati wa Bandari ya Kigoma. Utekelezaji wa miradi hiyo utachochea maendeleo ya maeneo husika na kusogeza huduma kwa wananchi.

59. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa fedha za ujenzi wa Shule ya Uongozi ya Julius Nyerere iliyopo Kibaha, Pwani. Shule hiyo iliyojengwa kwa ufadhili wa Chama cha Kikomunisti cha China kwa gharama ya Shilingi 101,000,000,000 ilifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari 2022. Shule hiyo itatoa elimu ya uongozi kwa makada wa Chama cha Mapinduzi na vyama rafiki kutoka ukanda wa kusini mwa Afrika ikiwemo FRELIMO (Msumbiji), ANC (Afrika Kusini), SWAPO (Namibia), ZANU PF (Zimbabwe) na MPLA (Angola).

60. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali ya Tian Tan na Chama cha Madaktari China (CMA). Kupitia ushirikiano huo, MOI itanufaika na uhawilishaji wa maarifa na uzoefu katika masuala ya tiba kwa njia ya TEHAMA na uchunguzi wa magonjwa. Hatua hiyo itaongeza uwezo wa Tanzania wa kitabibu na kuipunguzia Serikali na wataanzania kwa ujumla

gharama za matibabu nje ya nchi. Aidha, kuimarika kwa huduma za kitabibu nchini ni kichocheo cha kukua kwa utalii wa tiba kwa kuwa raia kutoka nchi nyingine hususan nchi za jirani watakuja kupata huduma za tiba nchini.

61. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha uwekezaji wa Kampuni ya Huaxin Cement kutoka nchini China katika kiwanda cha saruji cha Maweni Limestone Limited kilichopo mkoani Tanga. Kampuni ya Huaxin Cement ilinunua kiwanda hicho kutoka kampuni ya Arthi River Mining Group ya Kenya iliyokuwa ikizalisha saruji ya Rhino Cement. Uwekezaji huo umetoa ajira kwa watazania, kuongeza uzalishaji wa saruji na mauzo ya nje pamoja na kupunguza nakisi ya bidhaa hiyo katika soko la ndani.

62. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) uliofanyika Dakar, Senegal. Katika mkutano huo, China na Afrika kwa pamoja ziliandaa Dira ya Ushirikiano ya 2035, ambapo katika miaka mitatu ya mwanzo ya utekelezaji wa Dira hiyo, China itashirikiana na nchi za Afrika kutekeleza programu tisa ambazo ni, programu ya afya na utabibu; programu ya kupunguza umaskini na kuendeleza kilimo; programu ya kukuza biashara; programu ya kukuza uwekezaji; programu ya uvumbuzi wa kidijitali; programu ya mapinduzi ya kijani; programu ya kujenga uwezo; programu ya utamaduni na muingiliano wa watu; na programu ya ulinzi na usalama.

63. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulieleza Bunge lako tukufu kuwa, Wizara imeratibu na kufanikisha uwasilishaji wa mapendekezo ya awali ya miradi ya Tanzania kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kupata ufadhili. Miradi iliyowasilishwa ni mradi wa kufua umeme wa Ruhudji na njia za kusafirishia umeme; mradi wa kufua umeme wa Rumakali na njia za kusafirishia umeme; mradi wa ujenzi wa vyuo saba vya ufundi katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Pwani, Mtwara, Tabora na Arusha; na mradi wa upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

64. Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji; mradi wa ujenzi wa hospitali mkoani Dodoma; mradi wa ujenzi Geopark Ngorongoro – Lengai; na mradi wa uzalishaji wa malisho ya mifugo kwa kutumia teknolojia ya Juncao Tanzania Bara. Miradi mingine iliyowasilishwa ni mradi wa ujenzi wa Hospital ya Rufaa ya Binguni; mradi wa ujenzi wa kituo cha biashara, maonesho na mikutano; mradi wa ujenzi wa maeneo maalumu ya viwanda pamoja na ujenzi wa barabara zenye jumla ya kilometa 110.2 Zanzibar.

65. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, pembezoni mwa Mkutano wa Mawaziri wa FOCAC, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China iliahidi kutoa msaada wa Yuan milioni 100 kwa ajili ya kutekeleza miradi

mbalimbali ya maendeleo nchini. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo.

66. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mkataba wa kutangaza bidhaa za Tanzania kwenye mtandao wa JD.COM wa China ambao hutembelewa na watu takriban milioni 700 kwa siku. Hatua hiyo, itasaidia kutangaza bidhaa za Tanzania katika soko la China na nchi nyingine ambazo wananchi wake wanautumia zaidi mtandao huo kufanya manunuzi ya bidhaa. Hadi sasa kampuni 57 kutoka Tanzania zimejisajili kwenye mtandao huo.

67. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2021, Wizara iliratibu na kushiriki katika mkutano wa majadiliano ya kisera kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea uliofanyika jijini Dar es Salaam. Kupitia mkutano huo, Serikali ya Jamhuri ya Korea iliahidi kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani bilioni 1.3 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi 14 ya maendeleo nchini kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021 hadi 2025.

68. Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa makao makuu ya NIDA na ofisi 13 za mikoa za NIDA; mradi wa kuimarisha mipango ya ardhi kwa njia ya kidigitali; mradi wa maji safi na maji taka katika mkoa wa Iringa; mradi wa ujenzi wa chuo cha mafunzo ya reli; na mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufaa Binguni na kituo cha mafunzo ya utabibu Zanzibar.

69. Mheshimiwa Spika, sanjari na hayo, ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa, Wizara imeratibu na kufanikisha majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China kuhusu kurejeshwa kwa safari za moja kwa moja za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kutoka Dar es Salaam hadi Guangzhou, China. Ninayo furaha kukufahamisha kuwa Serikali ya China imeridhia kurejeshwa kwa safari hizo ambapo ndege za ATCL zitaanza kufanya safari mara moja kwa wiki kati ya Dar es Salaam na Guangzhou.

4.2.3 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati

70. Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu. Kupitia mkutano huo, nchi hizi mbili zilikubaliana kukuza ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama, mashauriano ya kidiplomasia, misaada ya kibinadamu na maendeleo, biashara, nishati na madini, mawasiliano, uchukuzi, fedha na kilimo na chakula. Taratibu za kukamilisha Hati za Makubaliano katika maeneo ya ushirikiano zinaendelea.

71. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Kimataifa ya Dubai (Dubai Expo 2020), yaliyofanyika kuanzia mwezi Oktoba 2021 hadi Machi 2022 Dubai, Umoja wa

Falme za Kiarabu (UAE), na ambayo yalishirikisha nchi 192. Kauli mbiu ya nchi yetu katika maonesho hayo ilikuwa *“Tanzania is ready for take off”*, ambayo ililenga kuhamasisha uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na mataifa mengine hususan katika biashara, uwekezaji, utalii na TEHAMA.

72. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, nchi yetu ilipewa heshima ya kuwa na siku maalum ya Tanzania katika maonesho hayo iliyoadhimishwa tarehe 26 Februari, 2022. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa mgeni rasmi katika siku hiyo maalum, ambapo alihutubia viongozi wa serikali, wafanyabiashara, wawekezaji na washiriki wengine wa maonesho hayo. Hotuba hiyo ilirushwa mubashara na kutazamwa na nchi nyingi duniani na hivyo kutoa nafasi kwa nchi yetu kujitangaza vema katika jumuiya ya kimataifa.

73. Mheshimiwa Spika, sanjari na maonesho hayo, Wizara iliratibu na kufanikisha kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Kongamano hilo lilikutanisha kampuni kutoka sekta binafsi za nchi hizi mbili. Aidha, jumla ya Hati 37 za Makubaliano ya ushirikiano kati ya Tanzania na UAE zenye thamani ya Shilingi trilioni 18.5 zilisainiwa, ambazo utekelezaji wake utazalisha ajira zipatazo 246,785 katika sekta mbalimbali zikiwemo nishati (mafuta na gesi), kilimo, uzalishaji viwandani, uchukuzi, huduma, mawasiliano na utalii. Hati hizo za makubaliano zilizosainiwa zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

74. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mhe. Badr Bin Hamad Bin Hamood Al Busaidi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman na Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Mtukufu Sultan Haitham Bin Tarik, Mfalme wa Oman. Akiwa nchini Mjumbe huyo alikutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kufuatia mazungumzo hayo, nchi hizi mbili zimekubaliana kufanya Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kudumu kati ya Tanzania na Oman kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha.

75. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa kibali cha kuuza nyama na bidhaa za nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo kutoka Tanzania katika soko la Saudi Arabia. Hadi sasa kampuni ya *Tanchoice* ndiyo imekidhi vigezo na kupata ithibati ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Saudi Arabia (SFDA) kuuza nyama na bidhaa za nyama nchini humo. Kampuni hiyo pia imepata ithibati ya kuuza nyama na bidhaa za nyama katika nchi ya Jordan. Aidha, kampuni ya Eliya Food inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya SFDA ili nayo iweze kupata ithibati. Hatua hiyo inatarajiwa kukuza mauzo ya nchi yetu nje, kuongeza mapato ya Serikali na kuinua kipato cha wafugaji nchini. Kadhalika, Saudi

Arabia imeonesha nia ya kushiriki katika Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam mwezi Julai 2022.

76. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022 nilifanya ziara ya kikazi nchini Saudi Arabia kwa mwaliko wa Mwana Mfalme Mtukufu Faisal bin Farhan Al Saud, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo. Ziara hiyo ililenga kukuza na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Saudi Arabia. Katika ziara hiyo niliambatana na Mhe. Mashimba Ndaki (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mhe. Dkt. Damas Ndumbo (Mb), wakati huo akiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Tukiwa nchini humo, tulifanya mikutano na Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Biashara na Naibu Waziri wa Kilimo pamoja na viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wenye Viwanda Saudi Arabia na kuelezea fursa za biashara na uwekezaji zilizopo nchini katika sekta za mifugo, uvuvi, kilimo, utalii na usafiri wa anga. Aidha, tuliwahamasisha wafanyabiashara wa Jumuiya hiyo kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayofanyika mwezi Julai kila mwaka.

77. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha kikao cha pamoja kati ya Tanzania na Qatar kujadili utekelezaji wa mkataba wa ushirikiano kati ya nchi hizi mbili kuhusu ajira kwa watanzania nchini Qatar uliosainiwa mwaka 2014 kilichofanyika jijini Dar es Salaam. Kupitia kikao hicho, Tanzania na Qatar zilikubaliana kutatua changamoto zilizokuwa zinakwamisha utekelezaji wa mkataba huo zikiwemo masuala ya viza na usajili wa mawakala binafsi wa ajira.

78. Mheshimiwa Spika, makubaliano hayo yamewezesha mawakala binafsi wa ajira kutoka Tanzania kwenda Qatar kufanya mazungumzo na mawakala binafsi wa ajira katika nchi hiyo kuhusu fursa za ajira kwa watanzania nchini Qatar hususan wakati huo ambapo nchi hiyo itakuwa mwenyeji wa mashindano ya kombe la dunia la mpira wa miguu yatakayofanyika mwezi Novemba na Desemba 2022. Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa watanzania kupata fursa za ajira nje ya nchi na kuhakikisha kuwa ajira hizo zinakuwa rasmi na zenye staha ili kulinda maslahi yao.

79. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2022, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika ziara hiyo Mheshimiwa Dkt. Mwinyi alishuhudia kusainiwa kwa makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kampuni ya Eagle Hills Regional Properties ya Umoja wa Falme za Kiarabu kuhusu ujenzi wa hoteli ya nyota tano eneo la Kizingo, Zanzibar. Uwekezaji huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu inayolenga kukuza uchumi na kuinua kipato kwa wananchi.

80. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe wa madaktari bingwa 27 wa moyo kutoka nchini

Saudi Arabia waliotembelea nchini kwa lengo la kutoa huduma za upasuaji wa moyo kwa katika Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam. Kufuatia ziara hiyo watoto wapatao 100 walifanyiwa vipimo vya maradhi ya moyo na watoto 34 kati yao walifanyiwa upasuaji.

81. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Dkt. Sidi Ould Tah, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA) hapa nchini. Kupitia ziara hiyo, BADEA iliidhinisha nyongeza ya mkopo wa masharti nafuu kiasi cha Dola za Marekani milioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa kilomita 22.1; upanuzi na ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja; na ujenzi wa shule tatu za sekondari za ufundi. Kwa hatua hiyo, jumla ya mkopo uliotolewa na Benki hiyo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar umefikia Dola za Marekani milioni 21.4.

82. Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu na kufanikisha upatikanaji wa ajira 600 kwa vijana wa kitanzania katika Bandari ya Dubai (DP World) ambapo hadi sasa vijana 90 wamefaulu usaili na kuwasili Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ajili ya kuanza kazi. Vilevile, Wizara iliratibu na kufanikisha vijana 80 kwenda kushiriki mafunzo ya utarajali wa kilimo na mifugo nchini Israel. Vijana hao wanatarajiwa kukamilisha mafunzo hayo na kurejea nchini mwezi Septemba 2022.

83. Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Agosti 2021 hadi Aprili, 2022 Wizara iliratibu na kufanikisha ujio wa watalii 4,500 kutoka Israel. Ujio wa watalii hao ni matokeo ya juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa utalii wa kutoka Israel na hapa nchini.

4.2.4 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika

84. Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Marekani. Akiwa nchini humo, Mheshimiwa Rais alizindua filamu maalum ya kutangaza utalii wa Tanzania iliyopewa jina la “*Royal Tour*” ambayo yeye mwenyewe alishiriki katika uandaaji wake. Tanzania inakuwa nchi ya tisa duniani na ya pili Afrika kuandaa filamu kama hiyo. Aidha, filamu hiyo inatarajiwa kuwa chachu katika kuvutia wawekezaji na watalii wengi zaidi kutoka sehemu mbalimbali duniani.

85. Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara hiyo, Wizara iliratibu na kufanikisha mazungumzo baina ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani yaliyofanyika katika Ikulu ya Marekani. Viongozi hawa wakuu walikubaliana kuendelea kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili uliodumu kwa miaka 60.

86. Mheshimiwa Spika, vilevile, wakati wa ziara hiyo, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa hati za makubaliano saba ya uwekezaji yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 5.04. Utekelezaji wa mikataba hiyo unatarajiwa kuzalisha ajira zipatazo 301,110 hapa nchini katika sekta mbalimbali zikiwemo sekta za kilimo, utalii na biashara. Mikataba iliyosainiwa ni kama ifuatavyo: Mkataba kati ya Kampuni ya Taifa Group na Kampuni ya Northern Feed ya Marekani kukuza kilimo cha umwagiliaji cha mazao ya soya, alizeti na miwa; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania na Corporate Council on Africa kukuza ushirikiano wa kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati.

87. Mheshimiwa Spika, Mikataba mingine ni kati ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Kampuni ya Daaya Group Ltd kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa sekta ya utalii; Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania na Chama cha Wafanyabiashara cha Marekani kuimarisha biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani; Tanzania Mercantile Exchange (TMX) na STONEX Financial Inc. kwa kushirikiana na Kampuni ya SJS Ltd na Tanzania Electronic Market Exchange kuimarisha uwezo wa TMX; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na FE Jordan & Associates kuendeleza maeneo maalum ya uzalishaji; na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Kampuni ya WABI International Ltd kuendeleza uwekezaji katika sekta ya nyumba na huduma za malazi.

88. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa. Akiwa nchini humo, Mheshimiwa Rais alishiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Bahari Kuu (One Ocean Summit) uliofanyika nchini Ufaransa. Mheshimiwa Rais Samia pia alifanya mazungumzo na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Ufaransa (MEDEF) kwa lengo la kuwahamasisha kuwekeza hapa nchini katika sekta mbalimbali na kuitangaza vema Tanzania nchini mwao. Aidha, Tanzania na Ufaransa zilisaini tamko la pamoja la dhamira kuhusu kushirikiana katika eneo la uchumi wa buluu na usalama wa bahari.

89. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulifahamisha Bunge hili Tukufu kuwa, kufuatia ziara hiyo ya Mheshimiwa Rais, ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji kutoka kampuni zipatazo 41 wanachama wa Jumuiya MEDEF na Business France ulifanya ziara nchini mwezi Mei 2022. Ziara hiyo ililenga kuangalia fursa za biashara na uwekezaji katika sekta za ujenzi, kilimo, afya, maji; nishati; TEHAMA na uchukuzi. Ninamshukuru kwa dhati Mhe. Rais Samia kwa kutenga muda wake na kukutana na ujumbe huo. Pia, ninapenda kuwashukuru Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Fedha na Mipango, Mhe. Ashatu K. Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Mudrick Soragha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mhe. Dkt. Khalid S. Mohamed, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhe. Suleiman Masoud Makame, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na

Uchukuzi kwa kukutana na kufanya mazungumzo na ujumbe huo wa wafanyabiashara na wawekezaji wa MEDEF na Business France.

90. Mheshimiwa Spika, vilevile, kufuatia ziara hiyo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Serikali ya Ufaransa zilisaini Mkataba wa Ushirikiano ambapo TADB itapata Euro 80,000,000 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo pamoja na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima. Serikali ya Ufaransa pia imeahidi kutoa fedha kiasi cha Euro milioni 178 kwa ajili ya utekelezaji wa Awamu ya 5 ya Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Kasi (*Bus Rapid Transit Phase 5 – BRT*) jijini Dar es Salaam. Kadhalika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kampuni ya Kimataifa ya *Bouygues Bâtiment* (BBI) zilisaini Hati ya Makubaliano ya ukarabati wa Jengo la Pili la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

91. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha majadiliano kati ya Serikali ya Ufaransa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu kuendeleza ushirikiano katika sekta ya uchumi wa buluu. Serikali ya Ufaransa imeahidi kutoa msaada wa kitaalamu na fedhakwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuimarisha doria na uvuvi katika bahari kuu. Ushirikiano huo ni chachu ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu ambayo inalenga kukuza kipato cha wananchi na kupunguza umaskini.

92. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ubelgiji na Makao Makuu ya Umoja wa Ulaya. Kufuatia ziara hiyo, Umoja wa Ulaya uliahidi kuipatia Tanzania kiasi cha Euro milioni 425 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya imeahidi kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Euro milioni 50 kwa ajili kuboresha viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Sumbawanga. Benki hiyo pia imeahidi kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali na wakulima wadogo wa Tanzania kupitia benki za biashara nchini. Vilevile, Serikali ya Ubelgiji imeahidi kutoa nyongeza ya kiasi cha Euro milioni 25 kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Ubelgiji kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2023 hadi 2027. Programu hiyo inatarajiwa kuendeleza sekta ya elimu, maendeleo ya jinsia na kukuza ujasiriamali kwa watanzania.

93. Mheshimiwa Spika, vilevile katika ziara hiyo, Wizara iliratibu na kufanikisha Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Ubelgiji lililohudhuriwa na wafanyabiashara 150 kutoka nchi hizi mbili. Kupitia kongamano hilo, kampuni nne za Ubelgiji na kampuni Dar-Lyon Investments Ltd ya Tanzania zilisaini makubaliano ya kibiashara, ambayo yataiwezesha kampuni hiyo ya Tanzania kuingiza nchini Ubelgiji bidhaa za dagaa, samaki, viungo, mchele, maharage ya njano na pilipili. Aidha, Chama cha Biashara,

Viwanda na Kilimo Tanzania na Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo cha Ubelgiji na Luxembourg vilisaini Hati ya Makubaliano ya kuanzisha ushirikiano wa kibiashara.

94. Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Wizara imefanikisha upatikanaji wa soko la bidhaa za Tanzania hususan dagaa, samaki na mchele nchini Ubelgiji na Umoja wa Ulaya kufuatia jitihada za kutafuta masoko ya bidhaa tunazozalisha nchini. Hadi sasa, tani 4 za dagaa kutoka Kigoma na tani 25 za mchele kutoka Mbeya zimeuzwa nchini humo. Aidha, wastani wa tani 50 za minofu ya samaki kutoka Ziwa Victoria huuzwa kila wiki nchini Ubelgiji.

95. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulieleza Bunge lako tukufu kuwa, Wizara ilifanikisha Tanzania kuchaguliwa kuwa miongoni mwa nchi nne za Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS) zitakazonufaika na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Madini inayotekelezwa kwa ubia kati ya OACPS na Umoja wa Ulaya. Programu hiyo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022 hadi 2024 kwa ufadhili wa Euro milioni 11.1 kutoka Umoja wa Ulaya. Kupitia programu hiyo, sekta ya madini hapa nchini itanufaika na miradi ya kuendeleza wachimbaji wadogo hususan vijana na wanawake hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo. Nchi nyingine zitakazonufaika na programu hiyo ni Suriname, Burkina Faso na DRC.

96. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani wa ushirikiano wa maendeleo katika sekta za afya, maji na michezo. Katika utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano huo, mwezi Aprili 2022 Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) iliipatia Zanzibar Euro 660,000 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya maji Zanzibar. Aidha, Ujerumani imeahidi kuipatia Zanzibar Euro milioni 1,000,000 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya michezo.

97. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha Jukwaa la Biashara kati ya Tanzania na Italia lililofanyika jijini Rome, Italia na kuwakutanisha wafanyabiashara 250 kutoka katika sekta za utalii, madini, anga, kilimo na ujenzi. Kupitia jukwaa hilo Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) lilisaini mkataba wa makubaliano ya awali na kampuni ya SUNESS Limited ya Italia kwa ajili kuendeleza mradi wa kuchimba madini ya shaba mkoani Kilimanjaro.

98. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha Kongamano la kwanza la Biashara kati ya Tanzania na Uingereza lililofanyika jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki 1,100 kutoka sekta za umma na binafsi ambao walijadili na kuweka mikakati endelevu ya kukuza biashara kati ya Tanzania na Uingereza hususan kwenye

uwekezaji na miradi ya maendeleo. Aidha, nchi hizi mbili zilisaini mpango kazi wa kutekeleza maeneo ya ushirikiano kwenye sekta ya biashara na uwekezaji.

99. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha majadiliano ya ushirikiano wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Kufuatia majadiliano hayo, Serikali ya Ujerumani imeridhia kutoa msaada wenye thamani ya Euro milioni 71 kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya maliasili na utalii hususan uhifadhi wa mbuga za taifa; sekta ya maji; utawala bora; na afya ya mama na mtoto.

100. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha majadiliano ya kisiasa kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Majadiliano hayo yalilenga kuimarisha uhusiano wa muda mrefu na kukuza ushirikiano kwenye maeneo ya biashara na uwekezaji, miradi ya maendeleo, masuala ya kikanda na kimataifa. Aidha, mara baada ya kukamilika kwa majadiliano hayo, pande mbili zilisaini Tamko la Pamoja kuthibitisha utayari wa kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa.

101. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iliratibu na kufanikisha majadiliano kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya ambapo Umoja huo uliahidi kuipatia Tanzania Euro milioni 703 kwa kipindi cha miaka 7 kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022. Utekelezaji wa makubaliano hayo umeanza ambapo mwezi Machi 2022 Tanzania na Umoja wa Ulaya zilisaini mikataba mitatu ya ufadhili wa miradi yenye thamani ya Euro milioni 180 ambazo zitatolewa katika maeneo ya maendeleo ya jinsia, TEHAMA na maendeleo ya miji. Upatikanaji wa fedha hizo utachangia katika juhudi za Serikali za kuleta maendeleo na kusogeza huduma karibu na wananchi.

102. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kuanza kwa safari za moja kwa moja za shirika la ndege la Eurowings kutoka Frankfurt, Ujerumani hadi Zanzibar. Majadiliano kuhusu shirika hilo kuanzisha safari za moja kwa moja kwenda Kilimanjaro yanaendelea. Kadhalika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kuanzishwa kwa safari za moja kwa moja za Shirika la Ndege la Ufaransa (Air France) kutoka Paris, Ufaransa hadi Zanzibar.

103. Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inaendelea kuratibu majadiliano ya kurejesha safari za moja kwa moja za kampuni ya *TUI Fly* ya Ubelgiji kutoka Brussels kwenda Zanzibar na pia kuanzisha safari za kwenda Kilimanjaro. Kuanza kwa safari hizo kutapunguza gharama za usafiri kwa watalii na wafanyabiashara kutoka barani Ulaya na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii na biashara nchini.

104. Mheshimiwa Spika, ninapenda kukujulisha kuwa, Wizara iliratibu kwa mafanikio zoezi la kuwaondoa wataanzania 289 kati yao 273 ni wanafunzi waliokuwa Ukraine kufuatia vita kati ya Urusi nchini hiyo. Hadi kufikia mwezi Mei 2022, wanafunzi 219 wamesharejea nchini na wengine wapo kwenye nchi mbalimbali walizofikia zikiwemo Poland (11), Hungary (02), Ujerumani (23), Uholanzi (03) wakiendelea kutafuta nafasi ya kuendeleza masomo katika vyuo kwenye nchi hizo. Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoa ushauri na miongozo kuhusu hatma ya masomo ya wanafunzi hao baada ya kurejea nchini. Halikadhalika, Balozzi zetu katika nchi za Sweden, Urusi na Ujerumani zinaendelea kuratibu upatikanaji wa nafasi za masomo katika vyuo vya nchi za jirani na Ukraine na kuwashauri wanafunzi waliobaki katika nchi hizo ipasavyo. Wizara pia imeratibu na kufanikisha kuondolewa kwa watalii wapatao 1,000 kutoka Ukraine waliokwama Zanzibar kufuatia vita hiyo kwenda nchini Poland.

Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 kupitia Ushirikiano wa Kimataifa

105. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa msaada wa chanjo dhidi ya UVIKO-19, ambapo Tanzania imepokea msaada wa dozi 4,900,000 za chanjo kutoka Marekani; dozi 2,300,000 kutoka China; dozi 115,200 kutoka Ubelgiji; dozi 1,000,000 kutoka Uturuki; na dozi 150,000 kutoka Mauritius na dozi 1,024,564 kutoka Rwanda. Aidha, mwezi Februari na Mei 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa vifaa tiba kutoka nchi za Ufaransa na Austria mtawalia kwa ajili ya kukabiliana na UVIKO-19.

106. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha mkutano kati ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bi. Kristalina Georgieva, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Kufuatia mkutano huo, IMF imeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wenye thamani Dola za Marekani milioni 567.25 sawa na Shilingi trilion 1.3 kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zilizosababishwa na UVIKO-19. Sekta zilionufaika na mkopo huo ni afya, elimu, utalii, maji, pamoja na makundi maalum ikiwemo kaya maskini, vijana, wanawake na wenye ulemavu.

4.3 Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

4.3.1 Jumuiya ya Afrika Mashariki

107. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za mtangamano za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa kama ifuatavyo:

Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

108. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mkutano huo, nchi wanachama ziliridhia ombi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kujiunga na Jumuiya, hatua inayoifanya Jumuiya kuwa na wanachama saba. Tarehe 08 Aprili, 2022 Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mwenyekiti wa Jumuiya kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki alisaini pamoja na Mheshimiwa Félix-Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa DRC mkataba wa kuiwezesha nchi hiyo kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

109. Mheshimiwa Spika, hivi sasa DRC inaendelea na taratibu za ndani za kikatiba za kuridhia mkataba huo na inatarajiwa kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya hati ya kuridhia kujiunga ifikapo tarehe 29 Septemba, 2022 ili kuwa mwanachama kamili. Kujiunga kwa nchi hiyo ni kiashiria cha kuendelea kukua kwa Jumuiya na kuongezeka kwa fursa za kiuchumi na kijamii katika Jumuiya.

Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki

110. Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki inayolenga kukuza biashara ya bidhaa na uwekezaji ndani ya Jumuiya. Uchambuzi wa mwenendo wa biashara kwa mujibu wa Taarifa ya Biashara na Uwekezaji ya EAC mwaka 2020, unaonesha kuwa thamani ya mauzo ya bidhaa miongoni mwa nchi wanachama ilipungua kwa asilimia 7.37 kutoka Dola za Marekani Milioni 3,162.80 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 2,929.6 mwaka 2020. Aidha, thamani ya manunuzi ya bidhaa miongoni mwa nchi wanachama ilishuka kwa asilimia 3.71 kutoka Dola za Marekani Milioni 3,175.80 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani Milioni 3,058 mwaka 2020. Kushuka kwa biashara katika mwaka 2020 kulitokana na kuendelea kuwepo kwa vikwazo vya kibiashara baina ya nchi wanachama na athari za UVIKO-19.

111. Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuka kwa biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 674.4 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani milioni 812.5 mwaka 2020 na thamani ya manunuzi ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya ilipungua kutoka Dola za Marekani milioni 329.2 mwaka 2019 hadi Dola za Marekani milioni 324.3 mwaka 2020. Taarifa za awali zinaonesha kuwa mauzo ya Tanzania katika nchi nyingine wanachama yalikuwa Dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 na manunuzi ya Tanzania kutoka nchi nyingine wanachama yalikuwa Dola za Marekani milioni 525.4 mwaka 2021. Kukua kwa biashara na thamani ya mauzo kwa nchi yetu katika kipindi hicho kumetokana na juhudi za Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

112. Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ambao unalenga kupunguza gharama za ufanyaji biashara ndani ya Jumuiya. Mfumo huo umeweka utaratibu wa mizigo kulipiwa kodi kabla ya kuondoka kituo cha kwanza cha forodha mzigo huo ulipoingilia (bandarini, kiwanja cha ndege au mpakani) kusafirishwa kwenda nchi husika. Utekelezaji wa mfumo wa himaya moja ya forodha umepunguza gharama na muda wa kusafirisha shehena za mizigo ndani ya Jumuiya. Mathalan, muda wa kusafirisha mzigo toka bandari ya Dar es Salaam kwenda Kigali, Bujumbura na Kampala umepungua kutoka wastani wa zaidi ya siku 8 mwaka 2013 hadi kufikia siku 4 mwaka 2019. Hata hivyo, kutokana na athari za UVIKO-19 muda huo umeongezeka hadi kufikia wastani wa siku 6. Mafanikio hayo pia yametokana na Tanzania kupunguza idadi ya vituo vya kupima uzito wa magari yanayosafirisha mizigo kwenda nje na matumizi ya vituo vya kutoa huduma pamoja mpakani (OSBP).

113. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu uondoaji wa vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia kamati ya Kitaifa na Kikanda ya ufuatiliaji wa vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha, kuanzia mwaka 2007 hadi Oktoba, 2021 jumla ya vikwazo 232 viliondolewa na nchi wanachama.

114. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu mikutano ya uwili kati ya Tanzania na Kenya iliyofanyika katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022. Kupitia mikutano hiyo vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha 56 kati ya 70 viliondolewa. Vikwazo 14 vilivyosalia vipo katika hatua mbalimbali za majadiliano ya kuviondoa. Miongoni mwa vikwazo visivyo vya kiforodha vilivyopatiwa ufumbuzi ni pamoja na ucheleweshaji wa kupitisha mizigo kutokana na utaratibu uliokuwepo wa matumizi ya mashine ya ukaguzi; ucheleweshaji wa kutoa vibali vya kuingiza bidhaa zitokanazo na maziwa kwa ajili ya kuuza nje; usumbufu wa taratibu za kiforodha uliokuwa unafanywa na Mamlaka ya Mapato Kenya; changamoto ambazo Taifa Gas Tanzania ilikuwa ikizipata ili kuweza kuwekeza Mombasa, Kenya; changamoto ya upatikanaji wa vibali vya kazi kwa wataalam wa Tanzania ili kuweza kufanya kazi Kenya; na watanzania kutakiwa kuwa na cheti cha chanjo ya UVIKO-19 wanaposafiri kwenda Kenya kwa njia ya anga.

115. Mheshimiwa Spika, hatua ya kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha imepunguza gharama za kufanya biashara ndani ya Jumuiya.

Utekelezaji wa Programu za Jumuiya katika Sekta za Uzalishaji

Sekta ya Kilimo

116. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2021, Tanzania iliridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Wanyama na usalama wa Chakula ya mwaka 2013. Kuridhiwa kwa Itifaki hiyo kutaiwezesha Tanzania kuuza bidhaa zitokanazo na mimea, wanyama na samaki ndani ya Jumuiya bila vikwazo ikizingatiwa kuwa nchi yetu inaongoza kwa uzalishaji wa bidhaa za kilimo na mifugo katika Jumuiya. Utekelezaji wa itifaki hii, utakuwa pia kichocheo cha kukuza biashara ya mimea, wanyama na samaki baina ya nchi wanachama wa Jumuiya na nchi nyingine nje ya Jumuiya.

Sekta ya Viwanda

117. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2021 Wizara iliratibu na kufanikisha Maonesho ya 21 ya Nguvu Kazi Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza. Katika maonesho hayo wajasiriamali 1,089 kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walishiriki. Kati ya hao, wajasiriamali 419 walitokea Tanzania Bara na 50 walitokea Zanzibar. Kufuatia maonesho hayo, wafanyabiashara wetu walifanikiwa kupata fursa ya kutangaza bidhaa zao, kubadilishana uzoefu, teknolojia pamoja na taarifa za kibiashara.

Sekta ya Utalii

118. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kufanyika kwa Maonesho ya Kwanza ya Utalii ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Arusha. Maonesho hayo yalishirikisha kampuni za utalii 157, wanunuzi wa kimataifa wa bidhaa za utalii 41, vyombo vya habari kutoka ndani na nje ya Jumuiya ikiwemo Aljazeera na Shirika la Habari la China. Hatua hii ilitoa fursa ya kutangaza utalii wa Tanzania na hivyo kuchangia katika jitihada za serikali kukuza shughuli za kitalii zilizokuwa zimeathirika na UVIKO-19.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia balozi zetu inaendelea kuwahamasisha wanunuzi wa kimataifa wa bidhaa za utalii walioshiriki katika Maonesho hayo, ambao walipata fursa ya kutembelea vivutio vya nchi yetu ili kushirikiana nao katika kuhamashisha watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vya utalii vya Tanzania.

Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki

120. Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki ilisainiwa na nchi wanachama mwaka 2013 na kuanza kutumika mwaka 2014. Itifaki hiyo imeweka misingi ya kufikia umoja wa sarafu ndani ya miaka 10, ambapo nchi wanachama zitatumia sarafu moja ya Afrika Mashariki. Ili kutekeleza azma hiyo, Jumuiya imeendelea kuratibu uanzishwaji

wa taasisi zitakazosimamia utekelezaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki.

121. Mheshimiwa Spika, Mkutano wa 41 wa Baraza la Mawaziri uliofanyika mwezi Novemba 2021 ulipitisha Muswada wa Sheria ya kuanzisha Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki na Muswada wa Sheria ya kuazisha Kamisheni ya Usimamizi, Udhhibiti na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Umoja wa Fedha. Muswada hiyo imewasilishwa katika Bunge la Afrika Mashariki kwa ajili ya kutunga sheria ya kuanzisha taasisi hizo.

Utekelezaji wa Miradi na Programu za Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii

122. Mheshimiwa Spika, katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zilikubaliana kutekeleza programu na miradi katika sekta mbalimbali ili kufikia malengo ya mtangamano. Katika kipindi hiki Wizara imeratibu kwa mafanikio ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kikanda na utekelezaji wa programu na miradi ya Jumuiya kama ifuatavyo:

Sekta ya Barabara

123. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha uwasilishwaji wa mapendekezo ya Tanzania kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Lusahunga – Rusumo / Kayonza - Kigali (km 162) ambao unatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Mitandao ya Barabara kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kati ya Tanzania na Rwanda. Mradi huo umepata ufadhili wa Benki ya Dunia wa Dola za Marekani milioni 72, na kukamilika kwake kutachochea ukuaji wa biashara kwa kuwa barabara hii ni kiungo muhimu kati ya Tanzania na nchi nyingine za Burundi, Rwanda na DRC.

124. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya mradi wa Barabara ya Tanga – Bagamoyo/Malindi - Lunga Lungu (km 400) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kwa upande wa Tanzania, mradi unahusisha ujenzi wa barabara ya Tanga - Pangani - Makurunge yenye urefu wa kilometa 244, ambayo imegawanywa katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ni kipande cha barabara ya Pangani - Tangani (km 50) ambayo inajengwa kwa kutumia fedha za ndani. Sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa kipande cha barabara ya Pangani -Tungamaa (km 14.3); Daraja la Pangani (mita 525); *Ushongo Spur* (km 5.9); na *Pangani Access* (km 5.4). Sehemu ya tatu inahusisha kipande cha barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Mkange (km 95.2) na Sehemu ya nne inahusisha kipande cha barabara ya Makurunge - Mkange (km 73.5).

125. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) mwezi Agosti 2021 zimesaini Mkataba wa wa Dola za Marekani milioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Tatu ya mradi huo ambayo inahusisha kipande cha barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Mkange (km 95.2). Mkandarasi yupo katika hatua ya maandalizi ya kuanza ujenzi.

Sekta ya Reli

126. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Reli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliopitishwa mwaka 2009 na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia Mpango huo, Tanzania inatekeleza mradi wa kujenga reli ya kisasa (SGR) yenye urefu wa km 2,561. Reli hiyo itaunganisha miko ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Kigoma na nchi jirani za Rwanda, Burundi na DRC. Ujenzi wa reli hiyo nchini ina mtandao wa km 1,219 za njia kuu na utekelezaji wake umegawanyika katika Awamu Tano. Awamu zote tano ambazo ni Dar es Salaam – Morogoro (km 300), Morogoro – Makutupora (km 422), Makutupora – Tabora (km 294), Tabora – Isaka (km 130), na Isaka – Mwanza – (km 249) tayari zimepata fedha za ujenzi na wakandarasi wanaendelea na kazi. Reli hii pia, itaiunganisha nchi ya Rwanda kupitia Isaka kwenda Kigali ambapo kwa upande wa Rwanda (Isaka – Kigali; km 532) tayari kazi za usanifu wa kina na upembuzi yakinifu pamoja na matayarisho ya eneo itakapopita reli hiyo yamekamilika.

Vituo vya Huduma kwa Pamoja Mpakani

127. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Manyovu/Mugina kilichopo katika mpaka wa Tanzania na Burundi kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 24 kutoka AfDB. Fedha hizo, ni sehemu ya mkopo wa Dola za Marekani milioni 256.2 zilizotolewa na Benki hiyo kwa ajili ya Mradi wa Barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kabingo – Kasulu – Manyovu/ Rumonge – Gitaza. Kituo hiki kinatarajiwa kuwa cha mfano (*standard model design*) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sekta ya Nishati

128. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu Mradi wa Kikanda wa Kufua Umeme wa Murongo/Kikagati unaotekelezwa kwa pamoja kati ya Tanzania na Uganda. Mradi huu unazalisha jumla ya Megawati 14 ambapo kutokana na Mkataba wa Mradi huo, Tanzania inapata Megawati saba kama ilivyo kwa upande wa Uganda. Mradi huo ulianza uzalishaji mwezi Februari 2022. Umeme huo tayari umesambazwa

katika Wilaya za Kyerwa na Karagwe mkoani Kagera ambapo awali zilikuwa zinatumia umeme kutoka gridi ya Uganda.

129. Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu majadiliano ya utekelezaji wa Mradi wa Kikanda wa Kufua Umeme wa Nsongezi ambao utajengwa katika Mto Kagera kwa ushirikiano baina ya Tanzania, Uganda na Rwanda. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha umeme wa Megawati 39 utakapokamilika ambazo zitagawanywa kwa nchi husika.

Sekta ya Afya

130. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2021 Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 21 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Zanzibar. Kupitia mkutano huo, nchi wanachama zilikubaliana kuimarisha mikakati ya pamoja ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 ikiwemo kuandaa Hati ya Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Health Common Pass*) itakayotumika kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji ndani ya Jumuiya. Aidha, Nchi Wanachama zilikubaliana kufanya uhakiki wa maabara zinazotumika kufanya vipimo vya UVIKO-19 kwa lengo la kuwezesha hati inayotolewa na nchi moja kutambuliwa kutumika katika nchi nyingine wanachama.

Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria

131. Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu na kufanikisha upatikanaji wa Euro milioni 5.3 kupitia Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria inayoratibiwa na kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ya Afrika Mashariki. Fedha hizi zitaiwezesha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza kukarabati na kupanua mtandao wake wa majitaka kwa kilomita 14.4, kuunganisha kaya 1,600 kwenye mtandao huo na kununua vifaa.

132. Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni Sanaa na Michezo uliofanyika jijini Dar es salaam. Mkutano ulipitisha maazimio yanayohusu masuala ya elimu ikiwa ni pamoja na mashindano ya uandishi wa insha kwa shule za sekondari za Jumuiya kwa mwaka 2021 ambapo mwanafunzi wa Tanzania Godson Chrispin Obaga kutoka Shule ya Sekondari Nyerere iliyopo Mwanaga, Kilimanjaro alikuwa mshindi wa kwanza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Washindi sita wa mwanzo mmoja kutoka kila nchi watazawadiwa na mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sekta ya Utamaduni na Michezo

133. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kampuni ya *Camp Fire Logs Guilds* ya nchini Uganda iliratibu Ziara ya Nne ya Waendesha Baiskeli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzia jijini Dar es Salaam mwezi Agosti 2021 na kuhitimishwa jijini Arusha mwezi Septemba 2021. Tukio hilo lililenga kutoa elimu kwa umma kuhusu Jumuiya na fursa zilizopo; kuhamasisha utalii wa ndani na kutoa elimu ya mazingira. Waendesha baiskeli hao walipita katika mikoa ya Pwani, Tanga, Kigoma, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Arusha nchini Tanzania na majiji ya Nairobi, Kampala, Kigali na Bujumbura.

Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama

134. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika kuandaa mpango kazi wa namna ya kushirikisha Wanawake, Asasi za Kiraia na Vijana katika shughuli za amani na usalama za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Mpango Kazi huo, ni kuimarisha ushiriki wa wanawake katika kuzuia na kutatua migogoro pamoja na kujenga amani na usalama endelevu ndani ya Jumuiya. Mpango kazi huo utaimarisha ushiriki wa makundi haya katika kutekeleza mfumo wa utatuzi wa Migogoro wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Bunge la Afrika Mashariki

135. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki, ambalo ni chombo cha kutunga sheria za Jumuiya. Katika kipindi hiki, Bunge hilo lilipitisha muswada wa Sheria wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2019. Madhumuni ya Muswada huu ni kusimamia uadilifu na maadili katika vyombo na taasisi za Jumuiya; kuimarisha mfumo wa kisheria kwa ajili ya kuzuia na kupambana na rushwa katika Jumuiya na kutoa ushirikiano kupitia wakala wa kitaifa katika kupambana na vitendo vya rushwa.

Ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

136. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliratibu na kusimamia kikamilifu mchakato wa ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kuanzia mwezi Oktoba 2021 hadi Aprili 2022. Katika mchakato huo, Tanzania ilifanikiwa kupata nafasi 10 kati ya 37 zilizotangazwa kwa nchi wanachama sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara inaendelea kuratibu fursa za ajira katika jumuiya za kikanda na Mashirika ya Kimataifa.

4.3.2 Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

137. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, ambapo katika kipindi hiki Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Kituo cha SADC cha Kupambana na Ugaidi chenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam. Kituo hiki kilichozinduliwa rasmi tarehe 28 Februari 2022, kitasaidia kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Taasisi za Kikanda na Kimataifa zinazoratibu mapambano dhidi ya ugaidi. Aidha, kuanzia mwezi Agosti 2021 hadi Agosti 2022, Tanzania imeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala ya SADC na kutokana na uenyekiti huo, Tanzania imechangia kuboresha Sera za ajira katika Jumuiya.

138. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika jijini Lilongwe, Malawi. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo, nchi wanachama ziliridhia ombi la Tanzania kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ngazi ya kamati za kisekta za mawaziri za Jumuiya. Nchi wanachama pia ziliridhia kiasi cha Dola za Marekani 73,518.20 kutumika kugharamia mchakato wa kutafsiri nyaraka muhimu za SADC kwa lugha ya Kiswahili zikiwemo Mkataba wa uanzishwaji wa SADC, itifaki na nyaraka za kisera.

139. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Tanzania imeendelea kushiriki katika juhudi za SADC za kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika ukanda wa kusini mwa Afrika, hususan Msumbiji ambayo inakabiliwa na mapigano kati ya majeshi ya Serikali na vikundi vya kigaidi katika eneo la kaskazini mwa nchi hiyo. Ninapenda kulifahamisha bunge lako tukufu kuwa Tanzania imeshiriki kwa kuchangia askari katika Misheni ya SADC nchini Msumbiji (SAMIM) na bajeti ya uendeshaji wa SAMIM kwa mwaka 2021/2022.

140. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha bunge lako tukufu kuwa, Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Makao Makuu ya Kituo hicho kilichozinduliwa rasmi tarehe 28 Februari 2022 yapo jijini Dar es Salaam. Uwepo wa kituo hicho hapa nchini utasaidia kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa zinazoratibu mapambano dhidi ya ugaidi ikiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu na Kituo cha Stadi na Utafiti cha Masuala ya Ugaidi cha Umoja wa Afrika. Vilevile, Tanzania inanufaika kupitia kubadilishana ujuzi, mafunzo, teknolojia na nafasi za ajira.

141. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika jijini Lilongwe, Malawi. Katika mkutano huo, Baraza liliidhinisha jumla ya Dola za Marekani 455,006 kwa ajili ya kutasfiri

machapisho tisa ya Hashim Mbita katika lugha ya Kiswahili na kutengeneza makala za video.

142. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu bunge lako tukufu kuwa, kampuni ya Tanzania iitwayo Epitome Architects ilishinda zabuni ya ujenzi wa sanamu ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo itawekwa katika Jengo la Usalama lililopo Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Addis Ababa, Ethiopia. Mkataba kati ya Sekretarieti na kampuni hiyo unatarajiwa kusainiwa kabla ya kufika mwisho wa mwaka huu wa fedha.

143. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, mwaka 2018 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Hati ya Makubaliano na Sekretarieti ya SADC kwa ajili ya ununuzi wa pamoja wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa nchi wanachama wa SADC. Tangu kusainiwa kwa mpango huo Bohari ya Dawa (MSD) imefanikiwa kununua dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa niaba ya nchi za Comoro na Shelisheli na kuokoa gharama za manunuzi kwa zaidi ya asilimia 55. Nchi ambazo zimeonesha nia ya kuutumia mpango huo ni pamoja na Botswana, Malawi, na Msumbiji. Hata hivyo, mpango huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mwamko mdogo wa kuutumia mpango huo na tofauti ya taratibu za manunuzi. Hivyo, Mkutano wa Baraza la Mawaziri uliofanyika mwezi Machi 2022 uliagiza Sekretarieti ya SADC kushirikiana na Bohari ya Dawa ya Tanzania kushughulikia changamoto hizo ili kuhakikisha Nchi Wanachama zinanufaika na mpango huo.

144. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Wazee la SADC la Usuluhishi wa Migogoro kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025). Kadhalika, Bi. Hellen Lwegasira ameteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Timu ya Upatanishi ya SADC kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025). Kuteuliwa kwa viongozi hawa ni ishara ya Tanzania kuendelea kuaminiwa katika usuluhishi wa migogoro.

4.3.3 Umoja wa Afrika

145. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Pamoja na masuala mengine, Mkutano uliridhia pendekezo la Tanzania la Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kazi ya Umoja huo. Aidha, katika mkutano huo Tanzania iliteuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Aprili 2022 hadi Aprili 2024.

146. Mheshimiwa Spika, nilimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa 16 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa

Afrika uliofanyika tarehe 27-28 Mei 2022 jijini Malabo, Equatorial Guinea. Mkutano huo ulijadili masuala ya Majanga na Huduma za Kibinadamu; na Ugaidi, Siasa na Itikadi Kali na Mabadiliko ya Serikali yasiyozingatia misingi ya katiba.

147. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo pamoja na masuala mengine, ulikubaliana yafuatayo: Kuunda Jeshi la Afrika (African Standby Force) na Brigedi za Kikanda; Kuimarisha ushirikiano na mshikamano; Kujenga uwezo wa nchi zetu kukabiliana na majanga mbalimbali ya asili na kushughulikia changamoto za katika ulinzi na usalama; Kuheshimu katiba na demokrasia; na Mpango wa Kujitathmini kwenye Masuala ya Utawala Bora (APRM).

Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA)

148. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2021, Tanzania iliridhia Mkataba wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Kuridhiwa kwa Mkataba huu kunaongeza wigo wa fursa za kukuza soko la bidhaa na huduma za Tanzania katika soko la Afrika. Hatua hii pia itajibu kiu ya wafanyabiashara wa Tanzania kutaka kunufaika na fursa za masoko ya nchi nyingine za Afrika ambazo siyo wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

149. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia ulielekeza nchi wanachama kufungua soko kwa asilimia 87.7 kati ya 90 zilizokubalika na kuendelea na majadiliano ya asilimia zilizobaki. Hadi sasa, nchi 29 kati ya 44 ikiwemo Tanzania zimewasilisha orodha ya bidhaa zitakazofunguliwa zinazokidhi vigezo vya mkataba huo.

4.3.4 Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR)

150. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi na Serikali zinazotekeleza Mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) uliofanyika jijini Kinshasa, DRC. Mkutano huo ulijadili utekelezaji wa mpango wa kusitisha mapigano mashariki mwa DRC na maeneo mengine kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu ili kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika ukanda huo.

4.3.5 Ushirikiano wa Kimataifa

151. Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2022 - 2027 wa ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Mataifa nchini. Mpango huo, unachukua nafasi ya Mpango wa Pili unaofikia tamati mwezi

Juni 2022. Kupitia Mpango huo, Tanzania na Umoja wa Mataifa zitashirikiana kutekeleza maeneo ya vipaumbele ya Ajenda 2030.

152. tarehe 25, Mei 2022 wakati wa Mkutano wa 48 wa mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) uliofanyika Accra, Ghana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alipokea nishani ijulikanayo kama 2022 Super Prize Great Builder – Trophée Boubacar Ndiaye inayofadhiliwa na AfDB na kutolewa na Africa Road Builders (ARB). Tuzo hii ni kutambua mchango wa Mhe. Rais kwenye mafanikio ya ujenzi wa mtandao wa barabara na reli hapa nchini pamoja na uongozi wake kwenye usimamizi wa fedha nyingi zilizoingia kwenye ujenzi wa miundombinu.

153. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha mkutano wa ngazi ya juu kati ya Serikali na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wakimbizi (UNHCR) uliofanyika jijini Dar es salaam. Mkutano huo ulikuwa na lengo kujadili masuala mbalimbali kuhusu uendeshaji wa shughuli za wakimbizi nchini, uratibu wa zoezi la kuwarudisha wakimbizi nchini mwao kwa hiari pamoja na haki na kinga za kidiplomasia wanazopata watumishi wa Shirika hilo nchini. Wakati wa mkutano huo, pande mbili zilisaini andiko la makubaliano na mapendekezo ya pamoja ya kuongeza ushirikiano, uwazi na mawasiliano ya mara kwa mara katika utekelezaji wa majukumu ya UNHCR hapa nchini.

154. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) uliofanyika jijini New York, Marekani ambapo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mkutano huo, Mheshimiwa Rais aliieleza jumuiya ya kimataifa kuhusu juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukabiliana na athari za kiafya, kijamii na kiuchumi zilizosababishwa na mlipuko wa UVIKO-19 duniani. Aidha, Tanzania ilisisitiza umuhimu wa jumuiya ya kimataifa kutumia majukwaa ya diplomasia majumui kukabiliana na matatizo yanayoikabili dunia.

155. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama za Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP26) uliofanyika jijini Glasgow, Scotland. Katika Mkutano huo, Tanzania ilieleza dhamira yake ya kupunguza kiwango cha uzalishaji wa hewa ukaa kwa asilimia 30 hadi 35 ifikapo mwaka 2030. Vilevile, Tanzania ilieleza namna inavyotekeleza sera, mikakati na programu za uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo upandaji miti takriban milioni 270 kila mwaka kwa lengo la kupunguza athari za hewa ukaa inayozalishwa kutokana na shughuli za kijamii na kiuchumi. Tanzania ilizihimiza nchi zilizoendelea kutimiza ahadi ya kuchangia kiasi cha Dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea kwa ajili ya kuziwezesha

kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyokubaliwa katika Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris wa mwaka 2015.

156. Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, katika Mkutano Mkuu wa 41 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) uliofanyika jijini Paris, Ufaransa mwezi Novemba 2021 Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Shirika hilo kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025). Vilevile, katika Mkutano huo tarehe 7 Julai ilitangazwa kuwa Siku ya Kiswahili Duniani. Kwa hatua hiyo lugha ya Kiswahili inakuwa ya kwanza Afrika na ya nane duniani kuwa na siku maalum ya kuadhimishwa. Lugha nyingine zenye siku maalum za kuadhimishwa ni: Kiarabu (18 Desemba); Kichina (20 Aprili); Kiingereza (23 Aprili); Kifaransa (20 Machi); Kirusi (06 Juni); Kihispania (23 Aprili); na Kireno (5 Mei). Wizara kupitia Balozi zetu inaendelea na Mikakati ya kuadhimisha siku hii kwa lengo la kukibidhahisha Kiswahili.

157. Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mkutano Mkuu wa 27 wa UPU uliofanyika Abidjan, Côte d'Ivoire mwezi Agosti 2021 Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Utawala (CA) na Baraza la Uendeshaji (POC) la Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025).

158. Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Januari 2022 Tanzania imekua ni miongoni wa wajumbe 54 wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa. Tanzania itashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu (2022-2024). Baraza hilo ndilo chombo muhimu kinachoratibu shughuli za kijamii na kiuchumi za Umoja wa Mataifa na mashirika yake yote. Vilevile, chombo hicho husimamia ajenda za maendeleo endelevu na miradi yote ya Umoja wa Mataifa kupitia mashirika yake kama vile UNDP, UNFPA na UNHCR.

159. Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mjumbe kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi vya mashirika ya kimataifa ni ishara ya ukomavu wa diplomasia ya nchi yetu kimataifa. Aidha, ni fursa ya kusaidia kuwaongezea uwezo wa kiutendaji wataalam wetu watakaoshiriki katika shughuli za Mashirika hayo.

160. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa lililofanyika Paris, Ufaransa. Jukwaa hilo lilifanyika mahsus kujiadili tathmini ya miaka 25 ya utekelezaji wa *Beijing Declaration and Platform for Action 1995* na kuweka mikakati ya kuimarisha utekelezaji wake. Katika jukwaa hilo, Tanzania ilikasimiwa jukumu la kutekeleza eneo la Usawa wa Kiuchumi na Haki ambalo ni kati ya maeneo sita yaliyoainishwa katika mpango wa miaka mitano (2021-2026).

161. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuarifu kuwa Wizara iliratibu ushiriki wa nchi kwenye Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa

ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika jijini New York, Marekani mwezi Machi 2022. Mkutano huo ulipitisha makubaliano ya pamoja yanayolenga kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

4.4 Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Hati za Makubaliano za Ushirikiano

162. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mikataba na Hati za Makubaliano ya Ushirikiano zinazolenga kuimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa Hati na Mikataba hiyo inayosimamiwa na Wizara, Taasisi na sekta binafsi kulingana na maudhui yake ili kuhakikisha nchi inanufaika. Orodha ya Mikataba na Hati hizo imeambatishwa kwenye kitabu cha Hotuba yangu.

4.5 Kuratibu Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli

163. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu masuala ya haki na kinga kwa Jumuiya Wanadiplomasia hapa nchini kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa hususan Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 na Waraka Na. 2 wa Rais wa mwaka 1964 kuhusu Mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na Jumuiya Wanadiplomasia.

164. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imeratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa mabalozi wa nchi za Australia, Belarus, Chile, China, Colombia, India, Indonesia, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Korea, Malawi, Morocco, Saudi Arabia, Ufaransa na Uholanzi. Aidha, katika kuimarisha uhusiano na Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini, Wizara imeimarisha utaratibu wa mashauriano kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya maendeleo.

165. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza wigo wa uwakilishi nje ya nchi kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Katika kipindi hiki, Ubalozi na Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa Vienna, Austria; Ubalozi wa Tanzania Jakarta, Indonesia na Konseli Kuu mbili katika jiji la Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na jiji la Guangzhou, China zimefunguliwa. Hatua hiyo inaifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 45 na Konseli Kuu tano.

166. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za kiitifaki na kikonseli ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, viongozi wa vyama vya siasa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Wizara imeendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania nje ya nchi kwa kushirikiana na

wadau wengine na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

167. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za kikazi na kitaifa za viongozi wakuu wa kitaifa katika nchi mbalimbali kama ifuatavyo:

- i. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ghana mwezi Mei 2022 kwenye Mkutano 48 wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB);
- ii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda kwa mwaliko wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, mwezi Mei 2022;
- iii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Marekani kuzindua filamu maalum ya Tanzania Royal Tour, mwezi Aprili 2022;
- iv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu kushiriki Maonesho Kimataifa ya Dubai (Dubai Expo 2020), mwezi Februari 2022;
- v. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ubelgiji kushiriki Mkutano wa Sita wa Ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na Afrika, mwezi Februari 2022;
- vi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Bahari Kuu, mwezi Februari 2022;
- vii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Scotland kushiriki Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama za Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, mwezi Novemba 2021;
- viii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri kwa mwaliko wa Mheshimiwa Abdel Fattah el-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, mwezi Novemba 2021;

31 MEI, 2022

- ix. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Marekani kushiriki Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, mwezi Septemba 2021;
- x. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda kwa mwaliko wa Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, mwezi Agosti 2021;
- xi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Malawi kushiriki Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC mwezi Agosti 2021;
- xii. Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia kushiriki sherehe ya uapisho wa Mheshimiwa Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia, mwezi Agosti 2021;
- xiii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Burundi kwa mwaliko wa Mheshimiwa Gen. Évariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, mwezi Julai 2021;
- xiv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ethiopia kushiriki Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwezi Februari 2022, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- xv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Malawi kushiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Asasi ya Ushirikiano katika Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya SADC mwezi Januari 2022, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- xvi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Singapore kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Majadiliano ya Kiuchumi mwezi Novemba 2021, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- xvii. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa kushiriki Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa mwezi Julai 2021, akimwakilisha

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

- xviii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Januari 2022;
- xix. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Afrika Kusini kushiriki Mkutano wa Ufunguzi wa Maonesho ya Kimataifa ya Biashara kwa Nchi za Afrika mwezi Novemba 2021;
- xx. Ziara za kikazi za Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Qatar na Jordan mwezi Machi 2022, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- xxi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kushiriki Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi wa Serikali zinazotekeleza Mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano nchini DRC na kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu mwezi Julai 2021, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- xxii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Morocco mwezi Julai 2021; na
- xxiii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Burundi kushiriki sherehe za maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo mwezi Julai 2021, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

168. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za viongozi wa Serikali na mashirika ya kimataifa hapa nchini kama ifuatavyo:

- i. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya mwezi Desemba 2021;
- ii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda mwezi Desemba 2021;

31 MEI, 2022

- iii. Ziara ya Mjumbe Maalum Mhe. Ahmed Bin Abudlaziz Kattan, Mshauri wa Mahakama ya Kifalme kutoka kwa Mtukufu Salman Bin Abdulaziz Al Saud, Mfalme wa Saudi Arabia na Msimamizi wa Misikiti miwili Mitukufu;
- iv. Ziara ya kikazi ya Mhe. Lord John Walney, Mjumbe Maalum wa Mhe. Boris Johnson, Waziri Mkuu wa Uingereza katika masuala ya biashara mwezi Novemba 2021;
- v. Ziara ya kikazi ya Mhe. Patricia Scotland, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola mwezi Mei 2022;
- vi. Ziara ya kikazi ya Mhe. Kamina Smith, Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara wa Jamaica mwezi Mei 2022;
- vii. Ziara ya kikazi ya Mhe. Katja Keul, Waziri wa Nchi kwenye Wizara ya Mambo ya Nje ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani mwezi Aprili 2022;
- viii. Ziara ya Kikazi ya Mhe. Dominique Hasler, Waziri wa mambo ya Nje wa Liechtenstein mwezi Machi, 2022;
- ix. Ziara ya Dkt. Akinwumi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) mwezi Februari 2022;
- x. Ziara ya kikazi ya Dkt Sidi Ould Tah, Mkurugezi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (BADEA) mwezi Oktoba 2021;
- xi. Ziara ya kikazi ya Amina J. Mohammed, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Septemba 2021;
- xii. Ziara ya kikazi ya Dkt. Hafez Ghanem, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia mwezi Septemba 2021;
- xiii. Ziara ya Mheshimiwa Sheikh Shakboot Nahyan Al- Nahyan, Mjumbe Maalumu wa Mrithi wa Ufalme wa Abu Dhabi na Naibu Kamanda Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Umoja Falme za Kiarabu mwezi Julai 2021;
- xiv. Ziara ya kikazi ya Mhe. Balozi Victoria Nuland, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani anayeshughulikia masuala ya siasa mwezi Agosti 2021; na
- xv. Ziara ya kikazi ya Mhe. Jakub Kulhanek, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Czech mwezi Oktoba 2021.

169. Mheshimiwa Spika, ziara hizo zinaendelea kuifungua Tanzania kimataifa katika azma ya kukuza na kutekeleza diplomasia ya uchumi.

4.6 Uratibu wa Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora)

170. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha Diaspora kuchangia maendeleo nchini. Kutokana na jitihada hizo, mchango wa Diaspora umeendelea kuongezeka, ambapo kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Kuu ya Tanzania fedha zilizotumwa na Diaspora nchini (remittances) ziliongezeka kutoka Dola za Marekani takribani milioni 400 mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 569.3 mwaka 2021. Diaspora pia wamewekeza kiasi cha Shilingi bilioni 3.9 katika mfuko wa UTT AMIS na kununua nyumba zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.3 za Shirika la Nyumba la Taifa na mradi wa Hamidu City Park uliopo Kigamboni, Dar es Salaam.

171. Mheshimiwa Spika, kadhalika, Diaspora wameendelea kutoa michango ya kijamii ambapo mwezi Machi 2022 jumuiya inayowaunganisha pamoja watanzania waliopo katika sekta ya afya nchini Uingereza (Tanzania – UK Healthcare Diaspora Association-TUHEDA) ilitoa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi milioni 100 kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. TUHEDA imekuwa chachu ya kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Uingereza, ambapo kwa sasa majadiliano yanaendelea kuhusu kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano baina ya nchi hizi mbili yatakayoivezesha Tanzania kunufaika na ubadilishanaji wa ujuzi, upatikanaji wa vifaa tiba na mafunzo kwa wauguzi na madaktari. Vilevile, jumuiya ya watanzania wanaoishi Marekani (Tanzania Diaspora Hub) imepanga kuwekeza nchini takribani Shilingi milioni 400 katika sekta ya uvuvi na kilimo mikoa ya Tanga, Njombe na Singida.

172. Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Diaspora mwekezaji anayeishi nchini Canada ambaye amepanga kuwekeza nchini Dola za Marekani milioni 15 katika ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia ya 'geopolymer', ambayo inatumia mabaki ya migodini na viwandani, hususan viwanda vinavyotengeneza alumina na vioo. Teknolojia hiyo ni mbadala wa matumizi ya saruji katika ujenzi wa barabara hapa nchini. Ninapenda kutambua michango ya Diaspora wengine ambayo iliekezwa katika sekta nyingine za kijamii na kiuchumi ambayo imesaidia kuleta maendeleo nchini.

173. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha mikutano baina ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Diaspora wakati wa ziara nchini Kenya, Burundi, Ufaransa, Ubelgiji, Umoja wa Falme za Kiarabu na Marekani. Aidha, iliratibu na kufanikisha mkutano kati ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Diaspora waliopo Singapore.

174. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki mkutano wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

na Diaspora wanaoishi katika nchi mbalimbali uliofanyika kwa njia ya mtandao. Vilevile, kwa nyakati tofauti nilikutana na kufanya mazungumzo na Diaspora wanaoishi nchini Kenya, Italia, Saudi Arabia, Jamhuri ya Korea na Marekani.

175. Mheshimiwa Spika, mikutano hiyo ilitoa fursa kwa Diaspora kupata taarifa za uwekezaji, ufafanuzi wa sera na mipango mbalimbali ya maendeleo nchini.

176. Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo ya Sera ya Mambo ya Nje kuzingatia tamko la kisera kwa masuala ya Diaspora, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau ndani na nje ya Serikali ikiwemo Diaspora wenyewe inakamilisha Andiko Mahsusili litakalotoa mwongozo wa kisera kwa masuala yanayowahusu Diaspora. Ni matumaini yangu kuwa Andiko hili Mahsusili litatoa suluhisho la mambo mengine ya kisera na kisheria yanayohusu hadhi ya Diaspora ambayo yamekuwa kikwazo katika kuwahusisha Diaspora kuchangia Uchumi wa Taifa lao.

177. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kutoa shukrani kwa Diaspora na jumuiya zao kwa kuendelea kuchangia maendeleo ya uchumi nchini.

4.7 Elimu kwa Umma

178. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi vikiwemo televisheni, redio na magazeti. Vilevile, kupitia majarida na vipeperushi; maonesho ya ndani na nje ya nchi mathalan maonesho ya sabasaba; na tovuti na mitandao rasmi ya kijamii ya wizara. Kupitia njia hizo wananchi wamefahamishwa kuhusu matokeo ya ziara za viongozi, fursa za masoko, ajira, uwekezaji na nafasi za masomo nje ya nchi.

179. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuliarifu Bunge hili kuwa, kwa miaka mitano Wizara imekuwa ikichapisha jarida maalum lenye kuelezea utekelezaji wa diplomasia ya uchumi katika Balozi zetu. Kupitia matoleo ya jarida hilo, Wizara imeelezea pamoja na mambo mengine namna ambavyo Waheshimiwa Mabalizi wanavyo tafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini, kuvutia uwekezaji kutoka nje kutangaza utalii wa Tanzania katika maeneo yao ya uwakilishi. Pia, Wizara iliandaa makala maalum ya televisheni (documentary) kuhusu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Serikali ya Awamu ya Sita na kuirusha katika vyombo vya habari nchini na mitandao ya kijamii.

180. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa vijana wa vyuo vikuu vya Tanzania kwenye Mdahalo wa Saba wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Lengo la mdahalo huo lilikuwa ni kupata washindi wawili kutoka kila nchi wanachama wa Jumuiya ambao wanapewa ubalozi wa vijana katika nchi zao na kukasimiwa majukumu ya kuelimisha vijana kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

181. Mheshimiwa Spika, katika Mdahalo huo, Bw. Eben Mnzava na Bi. Bernadette Massawe kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walishinda nafasi za Balozi na Naibu Balozi mtawalia. Wizara itashirikiana na vijana hawa katika kutoa elimu kwa vijana ili waweze kunufaika na fursa zinazopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

182. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya kikanda na kimataifa kwa makundi mbalimbali ambapo mwezi Septemba 2021 Wizara iliendesha mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu diplomasia na ushirikiano wa kimataifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Vilevile, mwezi Februari 2022 Wizara iliandaa semina kuhusu masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zake kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari ya Jamhuri na Al-Hijra zilizopo mkoani Dodoma. Aidha, Wizara imefanya mikutano minne ya kidiplomasia (diplomatic briefings) na mabalozi na wakuu wa mashirika ya kikanda na kimataifa waliopo nchini kwa lengo la kutoa elimu na ufafanuzi kwa jumuiya hiyo ya kibalozi kuhusu utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya kitaifa ambapo katika kipindi hiki.

4.8 Utawala na Maendeleo ya Watumishi

183. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kufanikisha malengo ya utekelezaji wa dhamana na majukumu yake. Hivi sasa, Wizara ina jumla ya watumishi 530 wa kada mbalimbali, ambapo watumishi 216 wapo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi na 314 wapo Makao Makuu ya Wizara. Kati ya watumishi waliopo balozini, watumishi 138 wa kada na vyeo mbalimbali walipelekwa balozini katika mwaka wa fedha 2021/2022 ili kuimarisha utendaji katika Balozi za Tanzania nje ya nchi. Watumishi 62 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo.

184. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi 19 kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Austria, Brazil, Comoros, Ethiopia, India, Indonesia, Italia, Israel, Kuwait, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Japan, Malawi, Marekani, Misri, Qatar Rwanda, Sweden na Urusi. Vilevile, Wizara

imewathibitisha kwenye vyeo wakuu wa Idara sita na kuwateua wakurugenzi wasaidizi nane.

185. Mheshimiwa Spika, Wizara imeajiri watumishi wapya 11, kati yao 10 ni Maafisa Mambo ya Nje Daraja la Pili na mtumishi mmoja ni Katibu Muhtasi Daraja la Tatu. Aidha, watumishi 70 walihamishiwa wizarani kutoka katika wizara na taasisi nyingine za Serikali, watumishi 170 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo na watumishi tisa walibadilishwa kada baada ya kujiendeleza kielimu katika fani mbalimbali.

186. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, ili kuboresha utekelezaji wa majukumu na malengo yake, Wizara imehuisha muundo wake kwa kuanzisha Idara mpya ya Diplomasia ya Uchumi. Aidha, Wizara imenunua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari mapya 20 kwa ajili ya Makao Makuu na 37 kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

187. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Wizara imeendelea na jukumu la kusimamia matumizi ya fedha na mali za Serikali. Matokeo ya usimamizi huu yanaonekana katika taarifa za kaguzi mbalimbali zinazofanywa na Wizara kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Mdhibili wa Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Udhibili wa Ununuzi wa Umma, na vyombo vingine vya Serikali vya usimamizi. Kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, katika kipindi husika jumla ya balozi 16 Idara na Vitengo ndani ya Wizara zilikaguliwa. Kaguzi hizi zimesaidia sana kurekebisha kasoro mbalimbali za kiutendaji na hivyo kuhakikisha kunakuwepo na matumizi yenye kuzingatia thamani.

Usimamizi wa Rasilimali Fedha

188. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara na Balozi zake imepata Hati Safi za ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo (2019/20 na 2020/21). Ninapenda kulihakikishia Bunge lako kuwa, Wizara inaendelea kuboresha mifumo yake ya fedha na utunzaji wa mali za Serikali kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni.

4.9 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara

189. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilitengewa bajeti ya maendeleo ya Shilingi 13,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imekamilisha taratibu za ununuzi za kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza miradi ya ujenzi na

ukarabati kwenye Balozi zetu nje ya nchi. Miradi hiyo ni Ujenzi wa jengo la Ubalozi na Kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi - mkandarasi aliyepatikana ni CRJE (East Africa) Limited; ujenzi wa jengo la ubalozi na kitega uchumi katika ubalozi wa Tanzania Kinshasa, mkandarasi ni China Railways Construction Engineering Group Limited (CRCEG); ujenzi wa makazi ya jengo la ubalozi na makazi ya Balozi katika ubalozi wa Tanzania Muscat – Mkandarasi aliyepatikana ni Arab Contractors (Osman Ahmed Osman and Co); ujenzi wa jengo la ubalozi na kitega uchumi katika ubalozi wa Tanzania Comoro – mkandarasi aliyepatika ni SUMAJKT Construction Co. Limited; mradi wa ukarabati wa Jengo la zamani la ubalozi (R-street) katika ubalozi wa Tanzania Washington; usanifu wa ujenzi wa makazi ya Balozi katika Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa; na ujenzi wa vyumba vya mihadhara Miradi hii iko katika hatua ya mikataba na utekelezaji wake utanza kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2021/22.

190. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya miradi hiyo yaliyohusisha kazi ya usanifu na uandaaji wa michoro ya ujenzi yamefanyika kwa kutumia fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 na kutunzwa katika akaunti ya amana ya Wizara. Fedha hizo zinazofikia shilingi bilioni 4.1 zimetumika pia kusanifu na kuandaa michoro kwa miradi idadi. itakayotekelezwa miaka ijayo kwa kufuata Mpango wa Wizara wa Uendelezaji wa viwanja na majengo Balozini. Miradi iliyosanifiwa na kuandaliwa michoro kwa utekelezaji miaka ijayo ni: Ujenzi ya Jengo la Ubalozi na Makazi ya Balozi katika Ubalozi wa Tanzania Riyadh; Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Maputo; Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Lilongwe; Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi na Makazi ya Watumishi katika ubalozi wa Tanzania Kigali; Ujenzi wa Jengo la Ubalozi na Makazi ya Balozi katika Ubalozi wa Tanzania Kigali; Ujenzi ya Jengo la Kitega Uchumi na Makazi ya Watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Bujumbura; na Ukarabati wa Makazi ya Balozi katika Ubalozi wa Tanzania Harare.

191. Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza pia kutumia fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2020/21 kukarabati majengo matano (5) ya makazi ya watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Lusaka (Zambia) uligharimu shilingi Milioni 600. Hatua hii imewezesha watumishi wote wa ubalozi katika ubalozi huo kukaa katika nyumba za serikali na kuiokolea serikali fedha za pango. Aidha, Wizara imeweza kutumia kiasi cha shilingi 341,941,115.00 kukarabati jengo la ofisi za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Zanzibar.

192. Mheshimiwa Spika, vilevile, ipo miradi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake uliendelea katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kutumia fedha zilizotengwa miaka iliyopita na zilizokuwa kwenye akaunti za amana za balozi husika. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden);

kuendelea na ukarabati wa makazi ya balozi na nyumba moja ya afisa katika Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden); kuendelea na ukarabati wa majengo matatu (3) ya Ubalozi wa Tanzania Kampala (Uganda); kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji); na kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania Khartoum (Sudan).

193. Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inaendelea na majadiliano na Benki ya CRDB kuhusu kushirikiana na katika ujenzi wa majengo ya ofisi, vitega uchumi na makazi ya watumishi balozini. Aidha, Wizara itaendelea kufanya majadiliano na taasisi nyingine za fedha ili kufanikisha azma hiyo ikiwa ni utkelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa wakati wa uzinduzi wa jengo la makao makuu ya CRDB jijini Dar es Salaam tarehe 05 Machi, 2022.

4.10 Taasisi Zilizochini ya Wizara

194. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi zilizochini yake ambazo ni: Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC); Chuo cha Diplomasia (CFR); na Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:

4.11 Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)

195. Mheshimiwa Spika, majukumu ya AICC ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba na ofisi. Aidha, kituo kinatoa huduma ya afya kupitia hospitali yake.

196. Mheshimiwa Spika, Kituo kinatekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Mpango Mkakati wa miaka mitano (2022/23-2026/2027), unaoainisha dira na dhima ya kuitangaza nchi yetu katika nyanja ya utalii wa mikutano na matukio ambayo inajulikana kama "MICE" (Meetings, Incentive travel, Conferences, Exhibition/Events).

197. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Kituo kilipanga kukusanya mapato ya **shilingi 16,202,606,216**. Hadi mwezi Aprili 2022 Kituo kilikusanya mapato ya **shilingi 10,351,041,115.15** sawa na **asilimia 64** ya malengo. Lengo la makusanyo halikufikiwa kutokana na shughuli za kituo kuendelea kuathirika na UVIKO-19 ambao umechangia kupungua kwa idadi ya mikutano.

198. Mheshimiwa Spika, mapato hayo yalitokana na;

- i. Huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) - **shilingi 4,242,707,034** kati ya lengo la **shilingi 4,634,077,500**;
- ii. Upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi - **shilingi 2,938,029,855** kati ya lengo la **shilingi 3,634,506,432**; na
- iii. Huduma za hospitali - **shilingi 3,170,304,225** kati ya lengo la **shilingi 3,883,370,730**.

199. Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi hicho, kituo kilitekeleza yafuatayo:

- i. Kuhudumia mikutano 239 ya kitaifa na 12 ya kimataifa ambayo ilileta washiriki 52,072 wa kitaifa na kimataifa. Aidha, Kituo kilifanikisha uzinduzi wa filamu maalum ya kutangaza utalii wa Tanzania ya *The Royal Tour* uliofanyika tarehe 28 Aprili, 2022 ukumbi wa AICC jijini Arusha na tarehe 8 Mei, 2022 jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa JNICC;
- ii. Kukamilisha tathmini ya mazingira ikiwa ni utekelezaji wa hatua za awali za mradi wa Ujenzi wa Mount Kilimanjaro International Convention Centre;
- iii. Kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wagonjwa wa nje 71,220 na waliolazwa 1,300;
- iv. Kuandaa na kuratibu kongamano la Asasi za wataalam wa hapa nchini kwa lengo la kuibua na kuvutia mikutano ya kimataifa kufanyika hapa nchini;
- v. Kufanya maboresho ya mifumo ya menejimenti ya usimamizi wa taarifa katika nyanja za rasilimali watu, miliki na uendeshaji wa hospitali;
- vi. Kufanya ukarabati wa nyumba za makazi na ofisi za kituo zilizopo Arusha; na
- vii. Kukamilisha mpango wa mafunzo na kukamilisha zoezi la kuhuisha muundo wa utumishi.

200. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 kituo kilitoa **Shilingi 100,000,000** ikiwa ni gawio la awali kwa Serikali.

4.11.1 Chuo cha Diplomasia

201. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo ya uhusiano wa kimataifa, diplomasia, utatuzi wa migogoro na kuimarisha amani, stratejia, ulinzi na usalama na lugha za kigeni.

202. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Chuo kilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi 7,960,040,070**. Kati ya hizo, **shilingi 4,300,640,000** ni ruzuku kutoka Serikali kuu na **shilingi 3,659,400,070** ni mapato kutoka vyanzo vya ndani. Katika fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu, **shilingi 2,300,640,000** ni ruzuku ya mishahara, **shilingi 1,000,000,000** ni ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na **shilingi 1,000,000,000** ni ruzuku ya matumizi mengineyo.

203. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Chuo kimepokea jumla ya **shilingi 5,937,257,608.00** ambayo ni sawa **asilimia 74.5** ya lengo. Katika fedha hizo, **shilingi 2,794,099,075.00** ni kutoka vyanzo vya ndani, **shilingi 2,162,390,130.00** ni ruzuku ya mishahara na **shilingi 833,333,333.00** ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu.

204. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Chuo kimetumia jumla **shilingi 5,783,383,323.00** sawa na **asilimia 97.4** Kati ya fedha hizo, **shilingi 2,941,534,145.00** ni kutoka vyanzo vya ndani, **shilingi 2,162,390,130.00** ni ruzuku ya mishahara kutoka Serikali Kuu na **shilingi 679,459,048.00** ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu.

205. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2022, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,617 katika ngazi mbalimbali za astashahada, stashahada, shahada na stashahada ya uzamili. Kati ya wanafunzi hao wanawake ni 790 na wanaume ni 827. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa wizara mbalimbali, taasisi na mashirika ya umma, taasisi binafsi, waambata na mabalozi walioteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali. Ninapenda kulifahamisha kBunge hili kuwa Chuo kwa kushirikiana na Wizara kilitoa mafunzo kwa waheshimiwa wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama yaliyofanyika mwezi Septemba 2021 jijini Dar es Salaam.

206. Mheshimiwa Spika, chuo kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundisha na kujifunzia kwa kukarabati miundombinu iliyoharibika na ununuzi wa vifaa na vitendea kazi. Kadhalika chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kitaaluma ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 watumishi 25 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao watumishi 2 wamehitimu masomo ya ngazi ya Shahada ya Uzamili na watumishi 23 wanaendelea na mafunzo.

4.11.2 Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora

207. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) ni Wakala Maalum

wa Umoja wa Afrika ulioanzishwa mwaka 2003. Lengo la Mpango huo ni kufanya tathmini za mara kwa mara za utawala bora zenye nia ya kuimarisha maeneo ambayo nchi inafanya vizuri, kuibua changamoto za utawala bora na kutoa mapendekezo ya namna ya kuzitafutia ufumbuzi. Aidha, Mpango huo unawezesha nchi wanachama wa APRM kwa pamoja kubadilishana uzoefu katika masuala ya demokrasia na utawala bora.

208. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, APRM Tanzania ilitekeleza majukumu yake kulingana na malengo makuu yaliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa APRM Tanzania (2017 - 2022) unaohuishwa kila mwaka, na kwa kuzingatia Mpango kazi na bajeti ya mwaka 2021/2022. Malengo yaliyotekelezwa kwa kipindi hiki ni kama ifuatavyo:

- i. Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM Tanzania;
- ii. Kuimarisha uhamasishaji na mawasiliano kwa umma; na
- iii. Kuhakikisha kuwa shughuli za APRM Tanzania zinakuwa endelevu.

209. Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za APRM Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni **shilingi 800,000,000**. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, APRM Tanzania ilipokea jumla ya **shilingi 492,503,239.85**. Hadi kufikia mwezi Machi 2022 APRM Tanzania ilitumia kiasi cha **shilingi 392,976,554.13** sawa na **asilimia 95.3** ya fedha ilizopokea.

210. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki APRM Tanzania imekamilisha rasimu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM. Rasimu hiyo inahusu hatua zilizochukuliwa katika kutatua changamoto za utawala bora zilizobainishwa katika tathmini iliyofanyika mwaka 2020 ambayo imeangazia maeneo manne ya tathmini: siasa na demokrasia, usimamizi wa uchumi, utendaji wa mashirika ya biashara na maendeleo ya jamii. Taarifa hiyo ina maelezo yaliyofanyiwa utafiti kwa kipindi cha mwaka 2014 hadi 2019.

211. Mheshimiwa Spika, tathmini imeonesha kuwa Tanzania imepata mafanikio katika eneo la siasa na demokrasia kutokana na hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto katika eneo hili. Baadhi ya mafanikio yaliyoainishwa ni utatuzi wa migogoro; kufanyiwa kazi kwa maeneo sita ya muungano; mageuzi katika utumishi wa umma; na uimarishaji wa taasisi za kuzuia na kupambana na rushwa. Aidha, haki za makundi ya wanawake, watoto, vijana na wakimbizi zimeendelea kulindwa kwa kuwekewa sera rafiki zinazosimamia maslahi ya makundi haya.

212. Mheshimiwa Spika, katika eneo la usimamizi wa uchumi, tathmini imeonesha Tanzania imeendelea kutekeleza sera za uchumi mpana zinazolenga kupata maendeleo endelevu. Pia, katika eneo la usimamizi wa mashirika ya biashara, Serikali imeimarisha mfumo wa udhibiti wa mashirika

ya biashara ili kuinua mchango wa mashirika hayo katika maendeleo ya Taifa. Vilevile, katika eneo la maendeleo ya jamii, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha ukusanyaji wa kodi kwa lengo la kuwa na uwezo wa kujitegemea na kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali za jamii.

213. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022, APRM Tanzania ilishiriki katika mkutano wa Wakuu wa Nchi zilizojiunga na Mpango wa APRM. Katika mkutano huo, Tanzania ilieleza dhamira yake ya kuendelea kutekeleza Mpango huo kwa kuwa unatoa nafasi kwa Serikali kujitathmini na kuendelea kuimarisha na kuboresha maeneo yenye upungufu.

214. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki APRM Tanzania iliandaa Mwongozo wa Udhhibiti wa Vihatarishi kama rejea mojawapo ya kuwezesha kuimarisha utawala bora ndani ya Taasisi na kutoa mchango wa kufikia malengo yake. Mwongozo huu ni dira ya kuzingatia katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Taasisi, kufanya maamuzi mbalimbali, mifumo, taratibu na kanuni ili kupata ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

215. Mheshimiwa Spika, pia katika kipindi hiki Taasisi ilihusha Mpango Mkakati wake wa mwaka 2016/2017 – 2021 utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano ambayo ni 2021/2022 – 2025/2026. Mpango ulihushwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa APRM na pia umezingatia mahitaji ya Taasisi katika Awamu ya Pili ya tathmini pamoja na mabadiliko mengine yanayotazamiwa katika nyanja za uchumi, demokrasia, siasa na maendeleo kwa ujumla.

5.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

216. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo mafanikio ya kiutendaji katika kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilikabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi ikilinganishwa na wingi wa majukumu. Wizara imeendelea kuwasiliana na mamlaka ya ajira kwa ajili ya kupata vibali vya ajira mpya na ajira mbadala.

6.0 SHUKRANI

217. Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali yetu chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imeendelea kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa wadau mbalimbali na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi za kikanda na kimataifa.

218. Mheshimiwa Spika, kwa mkatadha huu, ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Australia, Austria, Bangladesh, Brazil, Botswana, Burundi, Canada, China, Comoros, Cuba,

Denmark, Ethiopia, Eswatini, Finland, Hispania, Hungary, Italia, Iran, Ireland, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Japan, Kenya, Kuwait, Lesotho, Madagascar, Malawi, Malaysia, Marekani, Mauritius, Mexico, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Rwanda, Singapore, Sri Lanka, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Zambia, Zimbabwe, Uganda, Saudi Arabia, Shelisheli, Sudan, Sudani ya Kusini, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Ukraine, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno , Urusi, Uswisi, Uturuki, na Vietnam.

219. Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba kutoa shukrani kwa *African Capacity Building Foundation (ACBF)*; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia; *Investment Climate Facility for Africa*; Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID); Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA); Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (OPCW); Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Israel (MASHAV); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Misaada la Marekani (USAID); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA); na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO).

220. Mheshimiwa Spika, mashirika mengine ni Shirika la Umoja Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UNWOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC); Umoja wa Ulaya (EU); Shirika la Afya Duniani (WHO); na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Vilevile, napenda kuwashukuru Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ); *Global Fund*; *International Committee of the Red Cross*; *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*; Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola; *Khalifa Fund for Enterprise Development* (Khalifa Fund); *Medecins Sans Frontieres*; Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori (WWF); *The Association of European Parliamentarians with Africa*; *The Bill and Melinda Gates Foundation*; *TradeMark East Africa (TMEA)*; Umoja wa Posta Duniani (UPU);

Umoja wa Posta Afrika (PAPU) pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada. Ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara, na Serikali kwa ujumla.

221. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee, ninapenda kumshukuru Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Joseph Edward Sokoine, Katibu Mkuu; Balozi Fatma Mohammed Rajab, Naibu Katibu Mkuu; Waheshimiwa Mabalazi wa Tanzania; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi, ufanisi, moyo wa uzalendo na kujitoa kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

7.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

222. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imeweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendelea kulinda na kutetea misingi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi;
- ii. Kuendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kuwezesha Balozi zetu kuwa kiungo muhimu katika kuvutia uwekezaji; kutafuta masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu; na kutafuta fursa za ajira na masomo kwa wataanzania nje ya nchi;
- iii. Kuendelea kuimarisha uhusiano na nchi nyingine na jumuiya ya kimataifa;
- iv. Kuendelea kutangaza na kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili nje ya nchi;
- v. Kuendelea kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje katika kuchangia maendeleo ya nchi;
- vi. Kuendelea kushiriki katika juhudi za kulinda na kuimarisha amani duniani na maendeleo kupitia Umoja wa Mataifa;

- vii. Kuendela kushiriki kikamilifu katika kuimarisha mtangamamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;
- viii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, masuala ya uhusiano wa kimataifa na mtangamano wa kikanda;
- ix. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizopo chini ya Wizara;
- x. Kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya Balozzi zetu ili kupunguza gharama na kuchangia mapato ya Serikali;
- xi. Kuendelea kubaini maeneo mapya kimkakati kwa lengo la kunufaika na fursa zilizopo kwa maslahi mapana ya Taifa; na
- xii. Kuendelea kusimamia rasilimaliwatu na fedha makao makuu ya wizara na balozini.

8.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)

223. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kituo kimepanga kukusanya mapato ya **shilingi 16,737,049,856** kutokana na vyanzo vya ndani. Mapato hayo yatatumika kugharamia uendeshaji wa kituo, mishahara na ununuzi wa vifaa tiba na mradi ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya AICC.

224. Mheshimiwa Spika, Kituo kitaendelea kuvutia mikutano ya kimataifa kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuitangaza nchi kama kitovu cha diplomasia ya mikutano. Ninayo furaha kulijulisha Bunge hili kuwa Kituo kinategemea kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa ikiwemo kikao cha Shirikisho la Soka Barani Afrika (CAF) na African Women in Leadership itakayofanyika ukumbi wa AICC jijini Arusha mwaka wa fedha ujao.

225. Mheshimiwa Spika, Kituo kinakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa Kituo cha mikutano kitakachoitwa Mount Kilimanjaro International Convention Centre jijini Arusha. Kituo hicho kitaimarisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia ya mikutano na maonesho hapa nchini.

Chuo cha Diplomasia

226. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 chuo kimepanga kukusanya **shilingi 3,601,210,000** kutoka katika vyanzo vya ndani. Aidha, chuo kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendelea kutoa mafunzo ya uhusiano wa kimataifa, lugha ya Kiswahili kwa wageni, na mbinu za kidiplomasia;
- ii. Kuendelea kutafiti maeneo ya uhusiano wa kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- iii. Kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundisha na kujifunzia;
- iv. Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa chuo;
- v. Kuendelea kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa Serikali na taasisi zake; na
- vi. Kuendelea kukitangaza chuo kitaifa na kimataifa.

Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM)

227. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, APRM inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendelea kufanya tathmini katika masuala ya demokrasia na siasa, usimamizi wa uchumi, uendeshaji wa mashirika ya biashara na utoaji wa huduma za jamii;
- ii. Kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM, kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti;
- iii. Kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa APRM kwa kushirikiana na wizara, idara na wakala wa Serikali katika kuandaa taarifa ya mwaka na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na
- iv. Kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu mpango wa APRM kwa kuzingatia Mpango wa Mawasiliano wa Miaka Mitano 2021/2022–2025/2026.

9.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

228. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **shilingi 1,559,879,000** ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya

Wizara na Balozi za Tanzania ambavyo ni pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na kuthibitisha nyaraka.

229. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha **shilingi 208,366,964,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 203,666,964,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, zinazojumuisha **shilingi 188,937,219,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 14,729,745,000** kwa ajili ya mishahara. **shilingi 4,700,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

230. Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za bajeti ya matumizi mengineyo ya wizara, **shilingi 500,000,000** ni kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora, **shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia, **shilingi 1,243,661,150** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na **shilingi 170,000,000** ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, **shilingi 2,833,778,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Diplomasia.

231. Mheshimiwa Spika, kati ya **shilingi 4,700,000,000** zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, **shilingi 4,000,000,000** ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyopo jijini Arusha na **shilingi 700,000,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika Ubalizi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini.

10.0 HITIMISHO

232. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **shilingi 208,366,964,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 203,666,964,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 4,700,000,000** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

233. Mheshimiwa Spika, ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

234. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO

**ORODHA YA MIKATABA NA HATI ZA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO
ILIOSAINIWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

31 MEI, 2022

1. Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje na Maendeleo ya Kimataifa ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Mashauriano ya Kisiasa na Kidiplomasia iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi;
2. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Uvuvi, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi;
3. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Madini, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi
4. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Afya, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi;
5. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kufundisha Lugha ya Kiswahili nchini Burundi na Kufundisha Lugha ya Kifaransa nchini Tanzania, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021, Bujumbura, Burundi;
6. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Nishati; iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi
7. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Kilimo, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi;
8. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi Kuhamisha Wafungwa, iliyosainiwa tarehe 16 Julai, 2021 Bujumbura, Burundi;
9. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Habari na TEHAMA, iliyosainiwa tarehe 2 Agosti, 2021 Kigali, Rwanda;
10. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Elimu, iliyosainiwa tarehe 2 Agosti, 2021 Kigali, Rwanda;
11. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Uhamiaji, iliyosainiwa tarehe 2 Agosti, 2021 Kigali, Rwanda;

12. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu Ushirikiano katika Udhhibiti wa Vifaa tiba, iliyosainiwa tarehe 2 Agosti, 2021 Kigali, Rwanda;
13. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ikiwakilishwa na Mamlaka ya Uwekezaji na kanda Huru ya Uwekezaji (GAFI) Kuwezesha Ushirikiano wa Pamoja katika Uwekezaji, iliyosainiwa tarehe 11 Novemba, 2021 Cairo, Misri;
14. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ikiwakilishwa na Wizara ya Sanaa na Michezo kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Michezo, iliyosainiwa tarehe 10 Novemba, 2021, Cairo, Misri;
15. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ikiwakilishwa na Wizara ya Elimu na Elimu ya Ufundi kuhusu ushirikiano katika Sekta ya Elimu, iliyosainiwa tarehe 10 Novemba, 2021 Cairo, Misri;
16. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Elimu ya Juu kwa miaka 2021-2026 iliyosainiwa tarehe 10 Novemba, 2021 Cairo, Misri;
17. Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Falme ya Ubelgiji kuhusu huduma ya Usafiri wa Anga uliosainiwa tarehe 3 Novemba, 2021 Dodoma, Tanzania;
18. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusu ushirikiano katika sekta ya Uhamiaji, iliyosainiwa tarehe 10 Desemba, 2021 Dar es Salaam, Tanzania;
19. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Afya, iliyosainiwa tarehe 10 Desemba, 2021 Dar es Salaam, Tanzania.
20. Hati ya Makubaliano kati ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Mamlaka ya Uwekezaji Kenya, iliyosainiwa, tarehe 10 Desemba, 2021 Dar es Salaam, Tanzania;

21. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusu Ushirikiano wa Pamoja kuzuia na kudhibiti magonjwa ya Wanyama yanayovuka Mipaka na Magonjwa ya Wanyama Yanayoambukiza Binadamu., iliyowekwa saini tarehe 10 Desemba, 2021 jijini Dar es Salaam, Tanzania;
22. Mkataba wa Kubadilishana Wafungwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya uliosainiwa tarehe 10 Desemba, 2021 jijini Dar es Salaam, Tanzania;
23. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusu Ushirikiano katika Makazi na Maendeleo ya Miji, iliyosainiwa tarehe 10 Desemba, 2021 jijini Dar es Salaam, Tanzania;
24. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusu Ushirikiano katika Masuala ya Magereza iliyowekwa saini tarehe 10 Desemba, 2021 Dar es Salaam.
25. Mkataba wa Jumla kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Ufaransa kuhusu ushirikiano katika Sekta za Fedha, Maendeleo na Vipaumbele katika Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati nchini Tanzania uliosainiwa tarehe 12 Februari 2022 Brest, Ufaransa.
26. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Ufaransa kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Uchumi wa Buluu na Usalama wa Bahari iliyosainiwa tarehe 12 Februari 2022 Brest, Ufaransa.
27. Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Ufaransa kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Miundombinu ya Usafiri na Maendeleo Endelevu nchini Tanzania, iliyosainiwa tarehe 12 Februari 2022 Best, Ufaransa.
28. Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kuhusu Ushirikiano katika Kuboresha Upatikanaji wa Fedha za Kilimo uliosainiwa tarehe 12 Februari 2022 Brest, Ufaransa.
29. Mkataba kati ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kuhusu Ushirikiano katika Kuboresha Upatikanaji wa Fedha za Kilimo uliosainiwa tarehe 12 Februari 2022 Brest, Ufaransa.

30. Mkataba kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Ufaransa kuhusu Ushirikiano katika Utekelezaji wa Awamu ya Tano ya Mradi wa Usafiri wa Mabasi yaendayo kasi uliosainiwa we tarehe 12 Februari 2022 Brest, Ufaransa.
31. Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ya Tanzania (TAA) na Kampuni ya Kimataifa ya Bouygues Batiment International ya Ufaransa kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakini na Ukarabati wa *Terminal Two* katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere iliyosainiwa tarehe 14 Februari 2022 jijini Paris, Ufaransa.
32. Hati ya Makubaliano ya kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje ya Umoja wa Falme za Kiarabu kuhusu Ushirikiano katika Mashauriano ya Kiasia na Kidiplomasia iliyosainiwa tarehe 26 Februari 2022 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu.

WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI

1. Ee Mungu twaomba ulinde
Jumuiya Afrika Mashariki
Tuwezeshe kuishi kwa amani
Tutimize na malengo yetu.

Chorus

- Jumuiya Yetu sote tulinde
Tuwajibike tuimarike
Umoja wetu ni nguzo yetu
Idumu Jumuiya yetu.
2. Uzalendo pia mshikamano
Viwe msingi wa Umoja wetu
Uhuru na Amani
Mila zetu na desturi zetu.
 3. Viwandani na hata mashambani
Tufanye kazi sote kwa makini
Tujitoe kwa hali na mali
Tuijenge Jumuiya bora.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa lamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

Sasa kabla sijamuita Mwenyekiti, kuna orodha ya Wabunge wa Tanzania ambao wanawakilisha Bunge letu kwenye Bunge la Afrika Mashariki, wapo hapa ndani naomba niwatambue, wakiongozwa na Mheshimiwa Kimbisa, ahsanteni kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya NUU. Mwakilishi wake, Mheshimiwa Zahor.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Fungu 34 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu sita; sehemu hizo zinahusu maelezo ya jumla, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, mchanganuo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ni miongoni mwa sehemu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati; msingi wa Kamati kuchambua makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni masharti ya Kanuni za Bunge. Ufafanuzi umeelezwa katika taarifa iliyowasilishwa mapema asubuhi ya leo. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge hili liijadili hoja ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya taarifa; taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara hii Fungu 34, mawanda ya uchambuzi yanajumuisha vifungu vya Balozi za Tanzania nje ya nchi. Balozi hizo ni za aina kuu mbili; Balozi katika nchi *(Bilateral)* na Balozi katika Taasisi za Kimataifa *(Multilateral)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utangulizi huo naomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari ili kuendana na muda pasipo na kuathiri mtiririko wa maudhui. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kumbukumbu kamili naomba Taarifa

yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; Kamati ilitembelea Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega uchumi la Ubalizi wa Tanzania Kinshasa, Congo DRC na mradi wa ujenzi wa makazi ya Balozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia. Naomba kutoa muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa. Aidha, nitasoma kwa kifupi sana sehemu ya taarifa inayohusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa. Maelezo kuhusu maeneo yaliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia; Chuo cha Diplomasia kilitengewa fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 utekelezaji wa mradi huo haukuwa umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi na jengo la kitega uchumi wa Ofisi ya Ubalizi wa Tanzania Kinshasa, DRC; Ubalizi wa Tanzania uliopo Kinshasa katika mwaka huu unaoisha ulitengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na jengo la kitega uchumi. Hadi Kamati ilipoutembelea mradi huo haukuwa umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba ya makazi ya Balozi wa Tanzania Adis Ababa, Ethiopia; Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Balozi. Hadi kamati ilipotembelea mradi huo bado ulikuwa haukuanza.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi; baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa ujumla:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Machi, 2022 wakati Kamati inatembelea miradi iliyopangwa kutekelezwa na Wizara hii hakuna mradi wowote kati ya miradi hiyo uliokuwa umeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, udadisi wa Kamati ulibainisha kuwa sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia ni kuwepo changamoto ya kimkataba baina ya chuo na mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huo. Aidha, mradi wa ujenzi wa ofisi na jengo la kitega uchumi wa Ofisi za Ubalizi wa Tanzania Kinshasa,

haujaanza kutokana na kutokamilika kwa taratibu za manunuzi na kutofanyika kwa tathmini za kihandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudadisi zaidi Kamati ilijulishwa kuwa kuwa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Balozi wa Tanzania Jijini Addis Ababa haukuanza kwa sababu ya kunyang'anywa umiliki wa viwanja. Ufafanuzi zaidi unaonesha kwamba baada ya kupewa umiliki wa viwanja hivyo Serikali haikuanza mchakato wa kuviendeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022; kutokana na yaliyobainika wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Utamaduni wa kutenga fedha kwa miradi ya maendeleo bila kuanza na utatuzi wa changamoto zilizopo katika eneo la utekelezaji unavuruga mwenendo wa utekelezaji wa bajeti. Desturi hiyo husababisha kukwama kwa miradi mingi chiniya utaratibu mzuri kwa maoni ya kamati ni kutatua changamoto kabla ya kutenga fedha.

(b) Utengaji wa kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya vitega uchumi katika Balozi zetu unakwamisha azma ya kuwa na vitega uchumi vinavyokusudiwa. Kwa namna hiyo, inaweza kuchukua muda mrefu kukamilisha miradi inayohusika. Kwa mfano mradi wa ujenzi wa ofisi na jengo la kitega uchumi Jijini Kinshasa, nchini DRC unahitaji zaidi ya shilingi bilioni 100. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 6.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo ni dhahiri kuwa kwa mwenendo huu wa utengaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo inaweza kutuchukua zaidi ya miaka 15 kukamilisha mradi wa kitega uchumi nchini DRC jambo ambalo ni tofauti kabisa na inavyoelekeza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Katika ukurasa wa 185 Ilani inaelekeza, naomba kunukuu; "Kujenga na kununua majengo kwa ajili ya Balozi za Tanzania katika nchi ambazo kwa sasa majengo haya yanakodishwa. Kasi hii ya miaka 15 itakiuka azma ya Chama cha Mapinduzi kilichopata ridhaa ya wananchi wa Tanzania." (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilihusu maeneo Makuu matatu; maeneo hayo ni uzingatiaji wa maoni na ushauri wa kamati, mapitio ya bajeti iliyo idhinishwa na Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa maeneo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati; uchambuzi umeonesha kuwa sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati imezingatiwa. Ufafanuzi zaidi wa hali ya uzingatiaji huo umeoneshwa katika kiambatisho Namba 1 cha taarifa hii. Katika kiambatisho hicho upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kuwawezesha wananchi wengi kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa kikanda na ule wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/2022; matokeo ya uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanywaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2021/2022 asilimia mbili ya lengo kuu la ukusanyaji wa maduhuli kwa Fungu 34 ilitegemewa kukusanywa na Makao Makuu ya Wizara na asilimia 98 ilitegemewa kukusanywa na Balozi za Tanzania nje ya nchi. Uchambuzi wa makusanyo hayo umeonesha yafuatayo:-

- (a) Hadi kufikia Februari 2022 Wizara na Balozi ilikusanya asilimia 25 ya lengo lililowekwa.
- (b) Katika kipindi hicho Balozi zilikusanya asilimia 24 za lengo lake na Makao Makuu ya Wizara ilikusanya asilimia 82 ya lengo lake la makusanyo.
- (c) Wakati wa kupanga maduhuli Makao Makuu ya Wizara ilitegemewa kuchangia makusanyo kwa asilimia mbili, lakini katika uhalisia wa ukusanyaji Wizara imechangia kwa asilimia sita.
- (d) Balozi za Tanzania nje ya nchi zilitegemewa kuchangia maduhuli kwa asilimia 98, lakini katika uhalisia Balozi hizo zimechangia kwa asilimia 94.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya matokeo hayo inaashiria mojawapo ya mambo mawili; ama upangaji wa lengo la makusanyo kwa Balozi za Tanzania nje ya nchi haukuzingatia uhalisia au wakati wa utekelezaji wa bajeti ziko changamoto zilizojitokeza kiuendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kwamba uzoefu huu wa mwenendo wa makusanyo usipozingatiwa katika makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kipindi kama hiki Bunge litapokea taarifa ya ukusanyaji wa mapato isiyoendana na matarajio. Hali hiyo, haipendezi katika utekelezaji bora wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi zaidi Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo kati ya mwaka wa fedha 2020/2021 na mwaka 2021/2022 ili kupata uzoefu uliojitokeza. Uchambuzi huo ulionesha kuwa makusanyo yaliyopatikana hadi kufikia Februari, 2022 yameongezeka kwa asilimia 31.5 ikilinganishwa na makusanyo katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha uliokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa pamoja na changamoto iliyobainika katika upangaji wa lengo la maduhuli kuna hatua kubwa iliyofikiwa katika upangaji na usimamizi wa maduhuli. Hata hivyo, bado Kamati ina maoni kwamba uzingatiaji wa uzoefu unaopatikana kwa mwaka unaokwisha unaweza kuwa na mchango mzuri katika upangaji na utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; uchambuzi wa taarifa kuhusu upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 unaonesha mambo yafuatayo:-

- (a) Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 77 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi kwa Fungu 34 - Wizara na Balozi nje ya nchi.
- (b) Ulinganisho wa kiwango cha fedha zilizopokewa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mwaka 2021/2022 unaonesha ongezeko la asilimia 23.1 kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani asubuhi hii.
- (c) Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 hakuna kiasi cha fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hali hiyo ya kuto kutolewa fedha za maendeleo ni sawa na ilivyokuwa kwa mwaka wa 2020/2021.
- (d) Fedha zizotengwa kwa ajili ya matumizi mengine zilipatikana kwa asilimia 82.7 ya kiasi kilichotengwa. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zilipatikana kwa asilimia 84.07 ya fedha zilizoainiashwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo Kamati ina maoni kuwa siyo vizuri kupanga miradi ya maendeleo na kuidhinisha bajeti bila ya kutekeleza inavyotakiwa. Aidha, kutokutolewa fedha za miradi ya maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge kuna athiri utekelezaji wa miradi hiyo na tija iliyokusudiwa kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa majukumu ya Wizara; uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango na majukumu ya

Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umeonesha kuwa kwa sehemu kubwa Wizara imefanikiwa, hata hivyo taarifa inaonesha kuwepo kwa changamoto zinazohitaji ufumbuzi ili kutimiza azma ya Serikali. Kwa mfano changamoto ya upungufu wa watumishi katika idara na vitengo ikilinganishwa na mahitaji ya majukumu ya Wizara hii inakwamisha ufanisi uliokusudiwa katika Ilani ya Uchaguzi kuhusu diplomasia ya siasa na diplomasia ya uchumi kama ilivyofafanuliwa katika ukurasa wa 184 wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango na bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kabla ya kueleza uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa taarifa kuwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele kumi na moja tofauti na ilivyokuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara imeongeza kipaumbele kimoja ambacho ni kusimamia na kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa. Katika vipaumbele vya mwaka wa fedha 2021/2022 jambo hili halikuwa miongoni mwa vipaumbele vyake. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza kipaumbele hicho ni matumaini ya kamati kwamba utekelezaji wa kipaumbele hicho utafanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato; uchambuzi wa makadirio ya ukusanyaji wa mapato mwaka wa fedha 2022/2023 unaonesha mambo yafuatayo:-

Kwanza kiasi kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kimeshuka kwa asilimia 38.3 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha unaoisha. Lengo la makusanyo kwa Wizara na Balozi za Tanzania nje ya nchi linategemea kuchangia katika makusanyo ya kwenye Fungu 34 kwa angalau 7.5%

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha unaoisha Wizara ilikuwa na lengo la kuchangia makusanyo kwenye Fungu 34 kwa asilimia sita kwa uwiano wa kutegemewa katika makusanyo lengo jipya la ukusanyaji wa maduhuli limezingatia uzoefu wa malengo kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio na matumizi; katika uchambuzi wa makadirio na matumizi umefafanuliwa kwa msaada wa jedwali Na. 1 na graph Na. 1 katika taarifa iliyowekwa mezani asubuhi ya leo matokeo yanaonesha ifuatavyo:-

(a) Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha

2021/2022 ongezeko limechangwiwa na kuongezeka kwa bajeti ya matumizi mengineyo kwa asilimia 12.5 na bajeti ya mishahara kwa asilimia 36 ikilinganishwa na fedha zilizo dhinishwa kwa matumizi hayo katika mwaka wa fedha 2021/2022. Asilimia 96.6 ya makadirio ya matumizi kwa Fungu 34 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, asilimia saba kwa ajili ya mishahara na asilimia 2.2 ni kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika chati Na. 1 ya taarifa hii.

(b) Uwiano wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika bajeti kwenye Wizara hii unatofautiana na uwiano wa makadirio ya jumla ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo na jumla kuu ya bajeti kwa Taifa wakati katika makadirio ya jumla ya nchi uwiano ni asilimia 37.8 ya bajeti kuwa kwenye miradi ya maendeleo. Katika bajeti ya Wizara hii makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo ni asilimia 2.2 hali hii. Hali hii inawezekana kuwa imetokana namna yalivyo majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

(c) Wakati bajeti ya maendeleo kwa ujumla katika Serikali yameongezeka kwa asilimia nane ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo imepungua kwa asilimia 65 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inawezekana uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 umetumika kupata makadirio hayo.

(d) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yalilenga miradi minne, lakini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inalenga miradi miwili tu. Hata hivyo kwa uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka unaoisha unaonesha kuwa hakuna kiasi cha fedha kilichopatikana kwa miradi yote minne iliyolengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Pamoja na kuwa miradi iliyopangwa kwa mwaka 2021/2022 haijatekelezwa miradi yote miwili inayotengewa fedha kwa mwaka 2022/2023 ni miradi mipya miradi hiyo ni ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu na ukarabati wa jengo la ubalozi Tanzania Pretoria - Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo si jambo linalokaa vizuri kuanza miradi mipya ilhali miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2021/2022 haikutekelezwa. Kwa mfano Wizara imepanga kufanya ukarabati wa jengo la Ubalozzi Tanzania Pretoria - Afrika Kusini wakati utekelezaji wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa majengo katika balozi mbalimbali haujafanyika kama ilivyopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaotoa. Naomba kubainisha maoni hayo: -

i) Mipango ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 izingatie ipasavyo uzoefu uliopatikana kwa mwaka 2021/2022, inaweza kutekelezeka inavyostahili.

ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu na miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iendelezwe katika utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

iii) Kutokuzingatiwa ipasavyo kwa maelekezo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2020, ni dosari katika uendeshaji, utekelezaji na hatua za kuisaidia Serikali kukidhi matarajio ya wananchi. Kwa msingi huo, mambo yote yanayohusu majukumu ya Wizara hii yaendeleo kutekelezwa kama inavyoelekeza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati; kutokana na mtazamo wa nilioueleza Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Chuo cha Diplomasia kisaidiwe kumaliza changamoto za Kimkataba zilizopo baina ya chuo na mkandarasi ili kiweze kutekeleza miradi iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane na Hazina kuona namna bora ya kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya chuo hicho.

(b) Ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya CCM inayoelekeza uwekezaji katika ujenzi na ununuzi wa majengo nje ya nchi kwa ajili ya Balozi zetu, uandaliwe mpango mkakati wa kufanikisha jambo hili. Mpango huo uoneshe namna ya kuishirikisha sekta binafsi katika uwekezaji kwenye ujenzi na ununuzi wa majengo hayo. Aidha, katika ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye balozi zetu mbalimbali Serikali ihakikishe kuwa: -

(i) Balozi zetu zinapata hati ya kiwanja kinachohusika kabla ya kuendelea na uupangaji na utekelezaji wa mradi;

(ii) Ubalozi unapata ufafanuzi kuhusu mpango wa matumizi ya viwanja katika maeneo yanayohusika kabla ya kuamua kuwekeza katika kiwanja hicho; na

(iii) Ubalozi uwe unaandaa mkakati wa kimasoko kwa ajili ya kulitangaza jengo linalohusika ili mradi utakapokamilika uweze kuwa na tija.

(c) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango iandae mkakati maalumu wa ukarabati majengo ya balozi zetu kwa awamu ili yaendane na hadhi ya Tanzania inayoonekana nje ya nchi.

(d) Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ziandae utaratibu maalum wa kuwa na *database* ya wanafunzi wa Kitanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi, pamoja na Watanzania waishio nje ya nchi.

(e) Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali vilivyomo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.

(f) Wizara ianze mapema michakato ya kukamilisha taratibu zote muhimu ili kuhakikisha miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2022/2023 inatekelezeka.

(g) Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine iandae mkakati unaotekelezeka wa kutoa elimu juu ya diplomasia ya uchumi na namna inavyotekelezwa kwa vitendo. Mkakati huu uende sambamba na kupeleka wataalamu wa diplomasia ya uchumi katika sekta muhimu kwa uwekezaji na biashara.

(h) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara, ziandae mkakati wa kupeleka watumishi wenye fani husika katika Balozi.

(i) Ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji, Serikali ikamilishe Mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje katika Mwaka wa fedha 2022/2023.

(j) Serikali iendeele kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya za Kikanda.

(k) Wizara iendeele kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezeshwa kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Mbarouk Mbarouk, Katibu Mkuu Balozi Joseph Sokoine pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao

wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nanelwa Mwihambi, ndc kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. Aidha, nawashukuru Ndugu Athuman Hussein, ndc Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha ahsante.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya

Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wizara ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 22 Machi, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu:

-

- i) Utangulizi;
- ii) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
- v) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- vi) Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kulinganisha na Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

SURA YA PILI

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega uchumi la Ubalizi wa Tanzania Kinshasa, Congo DRC na ujenzi wa makazi ya Balozi wa Tanzania Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Maeneo yaliyotembelewa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili: -

- a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

2.1 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa;

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu maeneo yaliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

2.1.1 Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Chuo cha Diplomasia kilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu.

2.1.2 Ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega Uchumi wa Ofisi za Ubalizi wa Tanzania Kinshasa, Congo DRC

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi 6,500,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega Uchumi kwenye Ubalizi wa Tanzania nchini Congo DRC katika **Kiwanja Na. 912 Barabara ya Boulevard du Mtaa wa Gombe.**

2.1.3 Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Balozi wa Tanzania Adis Ababa, Ethiopia

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Makazi ya Balozi Jijini Addis Ababa, Ethiopia kwenye viwanja viwili pacha katika eneo la **Bole Kitema Woreda 03 Adis Ababa**. Viwanja hivyo vinapakana; kimoja chenye ukubwa wa Mita za Mraba 2000 Serikali ya Tanzania ilipewa na Serikali ya Ethiopia mwaka 1998 na kingine chenye ukubwa wa **Mita za Mraba 1,414** Serikali ilikinunua mwaka 1999. Lengo lilikuwa ni kuviendeleza kwa pamoja.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kwa kutaja yafuatayo: -

- i) Hadi Mwezi Machi, 2022 wakati Kamati inatembelea Miradi tajwa hapo juu hakukuwa na mradi ulioanza utekelezaji;
- ii) Kamati ilidokezwa kuwa sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia ni kuwepo changamoto ya kimkataba baina ya Chuo na Mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi;
- iii) Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega Uchumi wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, haujaanza kutokana na kutokamilika kwa taratibu za manunuzi na kutofanya tathmini za kihandisi; na
- iv) Kamati ilielezwa kuwa Viwanja ambavyo Nyumba ya Makazi ya Balozi wa Tanzania Jijini Addis Ababa ingejengwa, Serikali ya Tanzania ilinyang'anywa umiliki wa viwanja hivyo na Mamlaka za nchini Ethiopia kutokana kushindwa kuviendeleza kwa wakati.

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

- i) Baadhi ya miradi ya maendeleo imekuwa ikitengeewa fedha ili hali miradi hiyo ina changamoto mbali mbali za utekelezaji ikiwemo; umiliki wa eneo husika. Ni maoni ya Kamati kuwa kabla mradi haujatengewa fedha; Wizara ihakikishe hakuna changamoto zitakazozuia utekelezaji wa mradi husika;

- ii) Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya miradi ya Ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega Uchumi katika Balozi zetu ni kidogo na itachukua muda mrefu kuweza kukamilisha miradi husika. Mfano, mradi wa ujenzi wa Ofisi na Jengo la Kitega Uchumi wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Kinshasa ili ukamilike unahitaji zaidi ya **Shilingi Bilioni 100**. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulitengewa **Shilingi Bilioni 6,500,000,000**. Ikiwa kila mwaka utatengewa kiasi hicho cha fedha, mradi huu utakamilika baada ya **miaka 15**. Hivyo, ili kufikia malengo ni rai ya kamati kuona Wizara ikishirikiana na Sekta Binafsi ili kupata fedha za kujenga majengo hayo kwa masharti ambayo yatazingatia maslahi ya pande zote mbili.

SURA YA TATU

3.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilihusu maeneo Makuu matatu. Maeneo hayo ni:

- i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
- ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na
- iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo:

3.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa ushauri wa kamati uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Balozi zetu. Taarifa iliyotolewa ilieleza kuwa kwa mwaka huu wa fedha Wizara imeshapeleka **watumishi 137** kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzingatiaji wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kuwawezesha wananchi wengi zaidi kunufaika na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusesitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

3.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Februari, 2022 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

3.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 2,550,879,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 47,240,000.00** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara

na **Shilingi 2,503,639,000.00** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 634,480,703.70** sawa na **asilimia 25** ya lengo lililowekwa. Aidha, kati ya fedha zilizokusanywa, **Shilingi 38,875,000.00** zilikuwa ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara ambayo ni **asilimia 82.2** ya lengo la **Shilingi 47,240,000.00** lililowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2021 na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki yameongezeka kwa **asilimia 31.5**. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 2,550,879,000.00** Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 634,480,703.70** sawa na **asilimia 25 tu**.

ii) Wizara kukusanya **asilimia 25** ya lengo lililopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kumetokana na kukosekana kwa Wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi. Hali hiyo imesababishwa na uwepo wa Janga la UVIKO 19 ambao ulisababisha bishara nyingi kufungwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa Mwenendo wa makusanyo ya Wizara kwa Makao Makuu ni wa kuridhisha na inaamini lengo lililowekwa litafikiwa hadi kufikia Mwezi Juni, 2022. Hata hivyo, kwa upande wa Makusanyo katika Balozi za Tanzania nje, ni dhahiri kuwa Janga la UVIKO 19 limechangia makusanyo hayo kutofikia nusu ya lengo lililowekwa hasa kwa kuzingatia kuwa **asilimia 98.1** ya lengo hilo la makusanyo lilikuwa ni makadirio kutoka Balozi za Tanzania nje.

3.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 48,125,303,276.43** sawa na **asilimia 77** ya fedha zote za Bajeti zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha fedha kilichotolewa ni ongezeko la **Shilingi 5,909,126,818.4** sawa na **asilimia 5.4** ikilinganishwa na **Shilingi 107,834,686,039.66** zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2021 ambazo zilikuwa ni **asilimia 53.9** ya fedha zote za Bajeti zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limechangiwa na fedha za matumizi mengineyo zilizotolewa kwa **asilimia 94** ya fedha

zilizopokelewa. Aidha, katika fedha zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 hakukuwa na fedha za maendeleo. Hali hiyo ya kutokutolewa fedha za maendeleo ni sawa na Mwaka 2020/2021 ambapo hadi kufikia Machi, 2021 hakukuwa na fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Shilingi 139,021,573,841.43** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizo ni sawa na **asilimia 82.7** ya **Shilingi 167,937,219,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi 9,103,729,435** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara ikiwa ni sawa na **asilimia 84.07** ya **Shilingi 10,828,219,000** zilizotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa **shilingi Bilioni 13.5** zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hazikuwa zimetolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2022. Fedha hizi zililenga kutekeleza miradi minne (4) inayojumuisha ujenzi wa Ofisi ya ubalozi na makazi¹ pamoja na ujenzi wa makazi ya Balozi² na ujenzi wa ofisi na Kitega Uchumi³ wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi; na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo⁴

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa kutokutolewa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge, kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati. Serikali inapopanga mipango yake ni matarajio ya Kamati na wananchi kuwa utekelezaji wake utakwenda kama ilivyokusudiwa ili kuleta tija kwa Taifa.

3.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

Mheshimiwa Spika, Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake Kumi ikiwemo Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli, Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Itifaki, kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Watanzania waishio ughaibuni, Kuratibu na Kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara; na Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilichambua Taarifa za Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) na Chuo cha Diplomasia na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini (APRM). Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

¹ Mascat- oman,

² Addis Ababa, Ethiopia

³ Kinshasa

⁴ Chuo cha Diplomasia - Kurasini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali zikiwemo za upungufu wa watumishi katika Idara na Vitengo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu ya Wizara, kupeleka watumishi balozini kulingana na fani husika, kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya Kimataifa na idadi ndogo ya Watanzania wanaoelewa kuhusu masuala ya Mtangamano wa Kikanda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika Uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto zote nne (4) zilizotolewa Taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara wa Mwaka 2021/2022, ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua.

SURA YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

4.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa Taarifa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele Kumi na moja (11) tofauti na ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele kumi (10).

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, kamati imebaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara imeongeza kipaumbele kimoja ambacho ni Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa ambacho hakikuwepo katika vipaumbele vya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza kipaimbele hicho na kwa kuwa Wizara hii inahusika na masuala ya kimataifa; ni imani ya kamati kwamba itatekeleza kipaumbele hicho kwa ufanisi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mapitio hayo yalibaini kuwa Wizara imewekewa lengo la kukusanya **Shilingi 1,559,879,000.00**. Kiasi hicho kinachokadiriwa kukusanywa ni pungufu na Makadirio ya Makusanyo yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa **Shilingi 2,550,879,000.00**.


Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, **Shilingi 116,069,000.00** sawa na **asilimia 7.5** ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na Makao Makuu ya Wizara. Aidha kiasi kinachobaki cha Jumla ya **Shilingi 1,443,810,000.00** sawa na **asilimia 92.5** kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania Nje.

Aidha, katika Uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano (5) tu za Tanzania nje ya Nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris, na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la Nyumba za Serikali. Balozi hizo ndizo pia zilitegemewa kukusanya mapato katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 hivyo hakuna Balozi mpya ambazo zinazotarajiwa kuiingizia Serikali mapato kutokana na kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo hilo limezingatia changamoto mbalimbali ambazo zimechangia kutofikia lengo la makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na hivyo kuweka lengo lenye uhalisia.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 208,366,964,000/=**, Kati ya fedha hizo, **Shilingi 188,937,219,000/=** sawa na **asilimia 90.6** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), **Shilingi 14,927,745,000/=** sawa na **asilimia 7** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 4,700,000,000/=** sawa na **asilimia 2.2** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika **Chati Na. 1** ya Taarifa hii.



C
hati Na.
1:
Uwiano
wa
Fedha
zinazoo
mbwa
kwa
Matumi
zi ya
Wizara

Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi Kamati imebaini kuwa, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Mwaka 2022/2023 imeongezeka kwa **asilimia 8.4** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko limechangiwa na kuongezeka kwa Bajeti ya matumizi mengineyo kwa **asilimia 12.5** na Bajeti ya Mishahara kwa **asilimia 36** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi hayo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.


Mheshimiwa Spika, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na ulinganisho wake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 inaonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Grafu Na. 1**.

Jedwali Na. 1: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023

MWAKA	2021/2022		2022/2023		% +/-
	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA	
MISHAHARA (PE)	10,828,219,000.00	5.6	14,729,745,000.00	7	36
MENGINEYO (OC)	167,937,219,000.00	87.34	188,937,219,000.00	90.6	12.5
MAENDELEO	13,500,000,000.00	7	4,700,000,000.00	2.2	-65
JUMLA	192,265,438,000	100	208,366,964,000	100	

Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022 na 2022/2023
Grafu Na. 1: Ulinganisho wa Uwiano wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023

31 MEI, 2022



Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022 na 2022/2023

Mheshimiwa Spika, vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilirejea mapendekezo ya Bajeti Kuu ya Serikali na kubaini kuwa wakati Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ni **asilimia 2.2** tu ya Bajeti yote, **asilimia 37.8** ya bajeti kuu imeelekezwa kwenye matumizi ya maendeleo.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, wakati Bajeti ya Maendeleo ya Bajeti Kuu ya Serikali imeongezeka kwa asilimia **Nane 8** ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imepungua kwa **Shilingi bilioni 8.8** sawa na **asilimia 65** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na kuwa mapendekezo ya Bajeti ya maendeleo imepungua ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 13.5** zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, uhalisia ni kwamba fedha hizo bado hazijatolewa. Kiasi hicho kilipangwa kutekeleza miradi mine (4) ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili ya maendeleo. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa upangaji wa miradi michache ambayo inaweza kutekelezeka ni suala linalotakiwa kupewa umuhimu wa kipekee. Ni rai ya Kamati kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali itoe fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya miradi miwili (2) iliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, hakuna mradi uliokuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni mipya. Miradi hiyo inayojumuisha Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Arusha) na ukarabati wa Ubalozi wa Tanzania Pretoria-Afrika Kusini. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuwa na miradi michache itakayotekelezeka kuliko

31 MEI, 2022

kuwa na miradi mingi isiyotekelezeka kutokana kutokutolewa kwa fedha za maendeleo pamoja na kutokamilisha taratibu za manunuzi kwa wakati.

SURA YA TANO

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1.0 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi kama nilivyoieleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo: -

- i) Mipango ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ikizingatia ipasavyo uzoefu uliopatikana kwa Mwaka 2021/2022, inaweza kutekelezeka inavyostahili.
- ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu na miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 iendelezwe katika utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
- iii) Kutokuzingatiwa ipasavyo kwa maelekezo ya Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2020, ni dosari katika uendeshaji, utekelezaji na hatua za kuisaidia Serikali kukidhi matarajio ya wananchi. Kwa msingi huo, Mambo yote yanayohusu majukumu ya Wizara hii yaendeleo kutekelezwa kama inavyoelekeza Ilani ya CCM;

2.0 Ushauri wa Kamati

Kutokana na mtazamo wa niliyoueleza kutokana na uchambuzi, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Chuo cha Diplomasia kisaidiwe kumaliza changamoto za Kimkataba zilizopo baina ya Chuo na Mkandarasi ili kiweze kutekeleza miradi iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane na Hazina kuona namna bora ya kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya Chuo hicho.

(b) Ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya CCM inayoelekeza uwekezaji katika ujenzi na ununuzi wa majengo nje ya nchi kwa ajili ya balozi zetu, uandaliwe Mpango mkakati wa kufanikisha jambo hilo. Mpango huo, uoneshe namna ya kuishirikisha sekta binafsi katika uwekezaji kwenye ujenzi na ununuzi wa majengo hayo. Aidha, katika ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye balozi zetu mbalimbali Serikali ihakikishe kuwa: -

(i) Balozi zetu zinapata Hati ya kiwanja kinachohusika kabla ya kuendelea na uupangaji na utekelezaji wa mradi;

(ii) Ubalozi unapata ufafanuzi kuhusu mpango wa matumizi ya viwanja katika maeneo yanayohusika kabla ya kuamua kuwekeza katika kiwanja hicho; na

(iii) Ubalozi unaandaa mkakati wa kimasoko kwa ajili ya kulitangaza jengo linalohusika ili mradi utakapokamilika uweze kuwa na tija;

(a) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango iandae mkakati maalumu wa kukarabati majengo ya balozi kwa awamu ili yaendane na hadhi ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi.

(b) Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali ziandae utaratibu maalum wa kuwa na Database ya wanafunzi wa Kitanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi, pamoja na Watanzania waishio nje ya nchi.

(c) Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali zilizopo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.

(d) Wizara ianze mapema michakato ya kukamilisha taratibu zote muhimu ili kuhakikisha miradi ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inatekelezeka kwa ukamilifu.

(e) Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine iandae mkakati unaotekelezeka wa kutoa elimu juu ya Diplomasia ya Uchumi na namna inavyotekelezwa kwa vitendo. Mkakati huu uende sambamba na kupeleka Wataalamu wa Diplomasia ya Uchumi katika sekta muhimu kwa uwekezaji na biashara.

(f) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara, ziandae mkakati wa kupeleka watumishi wenye fani husika katika balozi.

(g) Ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji, Serikali ikamilishe Mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje katika Mwaka wa fedha 2022/2023.

(h) Serikali iendeele kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuya za Kikanda;

(i) Wizara iendeele kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022.

SURA YA SITA

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*): -

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Muharami Shaban Mkenge, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Naibu waziri Mhe. Balozi Mbarouk Mbarouk, Katibu Mkuu Balozi Joseph Sokoine pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwihambi, ndc kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. Aidha, nawashukuru Ndg. Athuman Hussein, ndc Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Gerald Magjili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo na wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashid Kawawa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO
YA NJE, ULINZI NA USALAMA

31 Mei, 2022

KIAMBATISHO NA. 1

UTELEKEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA (NUU) KATIKA MPANGO NA
BAJETI YA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilijadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kutoa maagizo na ushauri wa namna ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ninapenda kujulisha Kamati yako kuwa, maagizo, maoni na ushauri uliotolewa umezingatiwa wakati wa utekelezaji wa mpango na bajeti husika. Maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

(i) Kutokamilika kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje kunasababisha Sera iliyopo kuendelea kutumika ilihali haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi Duniani na kuendelea kutumia Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 kunaathiri utekelezaji wa masuala yanayohitaji muongozo wa kisera ambayo hayajatajwa kwenye Sera ya sasa kama vile; masuala ya Diaspora na Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje baada ya kukusanya maoni ya wadau ambayo pamoja na mambo mengine itajumuisha masuala ya Diaspora, Uchumi wa Buluu, Mazingira, kukuza Kiswahili na Uchumi wa Kidigitali. Ninapenda kujulisha Kamati kuwa, kwa sasa Serikali inatumia miongozo iliyopo katika kutekeleza masuala haya nje ya nchi.

(ii) Changamoto ya umiliki wa Chuo cha Diplomasia imekuwa ya muda mrefu jambo ambalo linasababisha Serikali ya Tanzania pekee kuendelea na jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuwasiliana na Serikali ya Msumbiji ili kupata msimamo wao kuhusu kugharamia shughuli za uendeshaji

wa Chuo cha Diplomasia. Aidha, tunategemea kujadili suala hili katika mkutano ujao wa Tume ya Pamoja (JPC) baina ya Tanzania na Msumbiji utakaofanyika kwa tarehe itakayopangwa. Mkutano wa Tume ya Pamoja haukuweza kufanyika kama ilivyopangwa hapo awali kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Uchaguzi Mkuu wa Msumbiji, mlipuko wa UVIKO 19 na changamoto za kiusalama nchini Msumbiji. Aidha, kutokana na historia ya uanzishwaji wa Chuo hiki tunategemea kujadiliana masuala ya kubadilishana uzoefu na utaalim ikiwemo katika maeneo ya lugha za Kireno na Kiswahili kwa manufaa ya pande zote mbili.

(iii) Ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kunufaika na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki, Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo pamoja na vigezo vya bidhaa zinazohitajika katika masoko nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine ndani ya Serikali katika kutoa elimu kwa umma juu ya fursa za mtangamano wa Jumuiya za Kikanda na hususan Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, i za Serikali kuratibu ushiriki wa sekta binafsi katika maonesho ya Juakali Nguvu Kazi, Maonesho ya Utalii ya Afrika Mashariki na Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba). Vilevile, Serikali iliendesha vipindi maalum katika runinga na redio sambamba na kutumia mitandao ya kijamii kuelezea fursa zitokanazo na Mtangamano.

(iv) Kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa miaka kumi na tano (15) wa ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi kunakwamisha utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukujulisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango iliendelea kuipatia Wizara yangu fedha zilizoidhinishwa na Bunge kulingana na mahitaji yaliyojitokeza katika utekelezaji wa bajeti. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulichelewa kutokana na uhitaji wa kufuata taratibu za manunuzi ambazo hazishahabihiani na baadhi ya taratibu za ujenzi katika nchi ambazo miradi hiyo ilikuwa imepangwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha Wizara imekamilisha kuandaa michoro na makadirio ya gharama (BOQ) kwa ajili ya kutekeleza miradi katika balozi za Nairobi, Kinshasa, Moroni, Washington na Muscat. Aidha, zabuni katika utekelezaji wa miradi hiyo zimetangazwa na zinatarajia kufunguliwa tarehe 25 Machi, 2022. Nimatumaini ya Wizara kuwa baada ya kufunguliwa kwa zabuni hizo, taratibu za manunuzi zitakamilika mwezi Aprili, 2022 ili kuanza utekelezaji wa ujenzi. Katika kipindi hiki, Wizara inaendelea na zoezi la ukarabati na ujenzi katika Balozi za Lusaka, Skockholm, Brussels na Ofisi ya Mambo ya Nje, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Wizara imeanza juhudi za kutafuta Wabia mbadala wa kuendeleza viwanja vyake ikiwemo kushirikisha benki za hapa nchini ambapo majadiliano ya awali yamefanyika baina ya Wizara na Benki ya CRDB. Vile vile Wizara imeanza kufuatilia uwezekano wa kuendeleza viwanja vyake kwa utaratibu wa mikopo ya karadha (*mortgage financing*) yenye riba nafuu. Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina ili kufanikisha adhma yetu.

(v) Pamoja na nia ya dhati ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoielezea katika aya ya 9 na ya 10 ya tarifa hii kuwa Wizara ya Fedha na Mipango iliendelea kuipatia Wizara yangu fedha zilizoidhinishwa na Bunge kulingana na mahitaji yanayojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ikiwemo Miradi ya Maendeleo.

(vi) Kupeleka watumishi zaidi katika Balozi zetu, pamoja na kuongeza magari ya kutoa huduma katika Balozi zetu kunaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kupeleka watumishi katika Balozi zake ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Kwa mwaka huu wa fedha Wizara imeshapeleka watumishi 137 kwa awamu. Wizara inaendelea kuwasiliana na Mamlaka nyingine Serikalini ili kupata watumishi watakaongeza nguvu Makao Makuu, Ofisi ya Mambo ya Nje, Zanzibar na katika Balozi zetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zahor. Sasa tunaingia kwenye kuchangia na tunaanza na Mheshimiwa Ahmed Abdul Wakil, ajiandae Mheshimiwa Taska Mbogo, ajiandae Mheshimiwa Shabiby, ajiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na ajiandae Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. AHMED ABDUL WAKIL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mtu wa kwanza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ambayo inatuunganisha na dunia ya kisasa. (*Makofi*)

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuamka salama na kwa utulivu mkubwa katika Bunge letu na hapo hapo nikimshukuru Rais wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na ya gear kubwa aliyoanza kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Balozi Libarata pamoja na mkongwe Balozi Mbarouk kwa kazi kubwa ya kumsaidia Rais katika diplomasia ya uchumi. Timu yako ya Wizara inafanyakazi kubwa sana kwenda na kasi ya mama katika kuweka diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo nalipongeza kwamba dunia si kijiji au dunia ni Kijiji, mama amekifanya kijiji kiwe chini ya mikono yetu hivi sasa na hakuja na diplomasia ya kuzungumza tu, lakini amekuja na diplomasia ya uchumi ambayo uchumi ni kila kitu katika dunia. Kwa hiyo, uteuzi wa balozi alioufanya karibu nchi 45 na umekiri kwamba hivi karibuni amefungua Balozi mpya ya Indonesia imeleta faraja kubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi hizi tunaziona zinavyofanyakazi katika mitandao mbalimbali kama Italy, USA, China, Korea na Balozi nyingine nyinginezo zinakwenda moja kwa moja katika kutekeleza diplomasia ya uchumi.

Mimi nitazungumzia uchumi tu, kwa hiyo ipo haja na hoja kwamba Balozi hizi Mheshimiwa Waziri zije na mpango kazi ambao tutahakikisha sasa kwa mfano nchi ya Turkey ni mzalishaji wa chuma, mzalishaji wa bati, vifaa vya uvuvi na vifaa vya *marine*. Kwa hiyo, tujikite kutafuta fursa zile pale kwa nchi yetu kusudi tuweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija na balozi nyingine kadhalika wakija na mpango kazi madhubuti tutakuwa tunajua *focus* gani tunaweza tukapata maendeleo na kufaidika katika nchi zetu. Kwa jumla mimi sina mengi sana ya kuzungumza nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwamba ipo haja na hoja Zanzibar tusiishie ukarabati wa Wizara, ipo haja sasa hivi kwa miaka hii karibu 60 ya Uhuru lijengwe jengo la kisasa, wageni wakija tuachane na vichocho vidogo vidogo vililopo ili kusudi Zanzibar nayo kuwe kuna jengo walau lenye hadhi ya kibalozi, *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache ahsante sana na naunga hoja mia *dhul* mia ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante namuita Mheshimiwa Taska Mbogo, ajiandae Mheshimiwa Shabiby, ajiandae Mheshimiwa Mwakagenda na ajiandae Mheshimiwa Salome.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa pili na kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na pia na afya njema.

Napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nje Mheshimiwa Mulamula, Naibu wake Mheshimiwa Mbarouk kwa kazi nzuri ambazo amezifanya na kwa kuonyesha kwamba wamefanyakazi nzuri leo hii tunao mabalozi ndani ya nyumba hii ambao wamekuja kusikiliza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje nafikiri kwa mara ya kwanza ukumbi umejaa mabalozi na wawakilishi wa konseli mbalimbali tunakushukuru sana na tunaomba muendeleo na moyo huo wa ushirikiano kwa nchi za jirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuifungua nchi yetu ya Tanzania na kidhibiti cha mambo haya ni pamoja na Balozi ambazo ziko hapa leo, lakini pamoja na mambo ambayo Serikali ya Tanzania imeyapata kutokana na Mheshimiwa Rais kufungua nchi yetu. Tumeona matokeo mengi sana kwa ziara za Mheshimiwa Rais tumeona ushirikiano jinsi gani Mheshimiwa Rais anashirikiana na Marais wengine lakini pia tumeona ni jinsi gani anakwenda kutafuta pesa za kuweza kuleta kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi sisi kama Wabunge tunatakiwa tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuifungua nchi yetu ya Tanzania, lakini pia tunampongeza kwa tuzo ambazo ameendelea kuzipata hususani tuzo ambayo ameipata hivi karibuni aliyopewa na Benki ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa kutoa mchango wangu mbalimbali kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje. Kwanza kabisa napenda nizungumzie suala la viwanja vilivyopo kwenye Balozi zetu. Katika ripoti ambayo ameisoma Mheshimiwa Waziri nimeifuatilia na nimeisikiliza na kuisoma ameeleza ni jinsi gani Serikali ya Tanzania imeweza kupoteza viwanja vyake ambavyo vipo nje ya nchi, hususani kile kiwanja cha Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia Ethiopia kwa sababu nafahamu Serikali ya Tanzania ilikuwa na kiwanja pale na nilishi pale kwa hiyo naelewa yale mazingira ya pale Ethiopia kiwanja hicho kilikuwepo siku nyingi tangu miaka ya 2000 lakini nafikiri hatukuweza kuwekea mkazo kukijenga. Hivyo basi niombe Serikali ya Tanzania lakini kupitia Wizara hii ya Mambo ya Nje zile mali ambazo zipo nje ya nchi, hususani viwanja Serikali ijitahidi kujenga yale majengo ili watumishi wanaofanya kazi nje ya nchi waweze kukaa kwenye hizo nyumba ni gharama sana Serikali kupanga nyumba nje ya nchi, lakini tukiwa na jengo letu tutaweza kuokoa fedha zile ambazo zinalipwa kwa ajili ya pango la nyumba za wafanyakazi wanaofanya kazi Wizara hiyo. Niombe basi katika bajeti inayokuja Serikali ijaribu kutoa fedha ili majengo hayo yajengwe, *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niombe kutoa msisitizo kwa mabalozi ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais wanapokuwa nje ya nchi yetu ya Tanzania, wao ndio wawakilishi wa Watanzania wote, lakini pia wao ndio wawakilishi wa Mheshimiwa Rais. Niwaombe wanapokuwa kule kwenye zile nchi za nje waweze kutumia nafasi yao kukuza hii diplomasia ya uchumi ambayo Mheshimiwa Rais anapambana nayo sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumuachia Mheshimiwa Rais peke yake kwenda kungea na wadau nje ya nchi wakati kuna Balozi zipo kule ni suala pia ambalo Balozi anatakiwa alifanye, Balozi ni mwakilishi pale kwenye nchi ile, lakini Balozi anauwezo wa kukutana na wadau mbalimbali Wachumi akakutana na wawekezaji. Kwa hiyo Balozi anapokuwa kule kwenye nchi za nje azingatie kukuza diplomasia ya uchumi ambao Mheshimiwa Rais ameianzisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la *diaspora*, katika suala la *diaspora* nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia ni jinsi gani itaweza kuwa-*accommodate* Watanzania ambao wanakaa nje ya nchi. Mara ya mwisho niliweza kuchangia hapa na katika bajeti iliyopita mwaka jana nilizungumza kwamba Serikali inaweza ikawapa uraia pacha wale watanzania wanaokaa nje ya nchi, lakini ikawawekea *condition* ya kutokugombea nafasi za uongozi na hii itasaidia sana kuwawekea ile *limit* ya kuingia Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiacha kizazi cha Watanzania kukaa nje ya nchi bila kuwapa uraia pacha naona kama tunapoteza kizazi chetu ambacho kinakaa ughaibuni. Ukienda kwenye baadhi ya nchi unakuta kuna Watanzania kule wameoa wana watoto wana wajukuu yaani wanafamilia, yaani wana kizazi ambacho unakuta wanakwambia kwamba kizazi hiki asili yake ni Tanzania, wengi wao unakuta wamepoteza ule uraia wa Tanzania kwa sababu nchi yetu ...

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa mzungumzaji taarifa kwamba Serikali tayari inajipanga kutoa hadhi maalum na kupitia hadhi hii maalum Watanzania *diaspora* wataweza kupata haki zote kasoro tu kushiriki kwenye masuala ya kiasiasa pamoja na kufanya kazi kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbogo, Taarifa hiyo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nafikiri kwa sababu Mheshimiwa Waziri atakuja ku-*wind up* atalielezea vizuri suala ambalo Mheshimiwa Neema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele ya pili, ahsante.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja Wizara ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shabiby, ajiandae Mheshimiwa Mwakagenda na Mheshimiwa Salome.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara yetu ya Mambo ya Nje. Kwanza ifahamike kwamba tunapochangia hatuchangii kwamba tunaipinga Serikali au mambo mazuri yanayofanywa na Serikali, kazi ya Mbunge ni kuishauri Serikali, hiyo ndiyo kazi ya Mbunge. Sasa Serikali walichukue au wasilichukue ni juu yao *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataka tusema tu kwamba mimi naunga mkono hoja hii, lakini tunataka tumshauri mama yetu na Waziri wetu, labda kwanza nianze na hili tu ambazo ameliacha mama la uraia pacha. Uraia pacha ni muhimu kwa nchi yote hata kama kuna kuja hilo neno la hadhi maalum au chochote na tunaposema uraia pacha yule mtanzania atakayepata hiyo *passport* labda atakuwa na *passport* mbili, sisi hatuna haja kama mimi sina haja mimi nataka *passport* ya Tanzania tu inanitosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wengi waliokuwa kule ughaibuni ni wale watu ambao wameenda kutafuta maisha hawajaenda kule kutalii, watu lazima wafahamu hicho kitu, ebu tuzungumze je, hawa wanafunzi wanaomaliza vyo vikiu au hao watu wanaomaliza shule hapa Tanzania kuna kazi za kuwapa? Hakuna kitu kama hicho, watu wanakwenda kule kutafuta maisha tuchuke kama nchi ya Philipines, Philipines leo inajengeka lakini inapata fedha nyingi sana kutoka kwa hao watu wake ambao wapo nje. Kwa hiyo mpango wowote na Wizara ya Mambo ya Nje haijawahi kufanya Semina ituambie je, kuna shida gani kwenye uraia pacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida gani kwenye usalama, kuna shida gani kwenye hiki, hatujawahi kufanyiwa semina sisi Wabunge. Kwa hiyo Mbunge akisimama akizungumzia kitu kama hicho haki yetu lazima tukizungumze kitu kama hicho, lakini uraia pacha kwa watu waliokaa kule, waliopo kule sizungumzii kwa waliopo ndani ya nchi, uangaliwe utaratibu wa aina yoyote hawa watu wapewe uraia pacha kwa sababu wanamaliza hata fedha za Tanzania bila kujua. Mimi nina mtoto labda yupo Marekani au

Uingereza raia wakule halafu nimeuza shamba unafiriki mimi simtumii fedha hizo na yeye akapata urithi, kwa hiyo fedha si inakwenda huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuangalie nilitaka kuzungumza kwa kifupi tu kwamba Serikali ijaribu kujipanga vizuri iweke utaratibu kama kwenye vyombo vya usalama, kama kwenye siasa ijue vyote lakini kuwapa uraia ni kitu cha msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la kwangu kubwa la leo Mheshimiwa Waziri amezungumzia habari ya diplomasia pamoja na biashara na kwamba ametuambia anatengeneza sera inayokuja, lakini nataka niseme hii nchi hii sasa hivi Mama yetu Rais yupo katika mpango wa kufungua nchi, lakini ukiangalia sisi tunafungua tu Mawaziri lazima muwe makini sana, sisi tunafungua wapi kuja kufanya biashara Tanzania, lakini hatufungui wafanyabiashara wa Tanzania waende kufanya biashara nchi nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi na nafiriki pale Kariakoo ipo chini ya Jimbo lako, hivyo leo Wachina wanauza hadi vikombe vya plastiki, wanauza karanga, huko ndiko kufungua nchi? Halafu Watanzania tunakatazwa kwenda China, sasa hivi nchi zote mimi sio mfanyabiashara wa kutoka China, sifanyi biashara yoyote kutoka china zaidi ya kuagiza magari naagiza kwa IDC likija baya nawarudishia basi, lakini wapo watu wanaofanya *retail*, wanaofanya *wholesale* hizi kweli ni biashara ya kidiplomasia kweli za kufanya wachina kwenye hii nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Waziri wetu wa Mambo ya Nje pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara lazima waangalie hili suala Watanzania leo Wachina wanakuja kama shamba la bibi kila siku wanaingia, lakini Mtanzania hauruhusiwi kwenda China, unaambia uagize kwa *whatsApp* bidhaa, kwa hiyo aliyekuwa na bidhaa anaweza akaagiza anayetaka kwenda kuanza biashara au anayetaka kupeleka vitu China akauze China haiwezekani kitu kama hicho kwa sababu unajua hivi ni vituko, nchi zote *Europe* kweli China ni rafiki yetu, lakini angalia wa *Europe*, angalia India, angalia Dubai, angalia Marekani ukiwa una chanjo unaingia hiyo nchi bila kufanywa chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini China mpaka leo uchanje usichanje hakuna kitu, ndege yetu ya Tanzania imejaribu kwenda mara ya kwanza wakaambiwa kuna watu wana *corona*, mara ya pili kuna watu wana *corona* Wachina wenyewe hao hao ndege msileta, lakini KLM inaruhusiwa inakwenda kutoka hapa hadi China dola 14,000, kutoka China kuja hapa dola 7,000 na ndege ya Tanzania imezuiliwa na kila Ijumaa ndege ya Tanzania inakwenda China, lakini inakwenda tu kuchukua mzigo hairuhusiwi kupakia hata mtu mmoja. Sasa huu urafiki au diplomasia ipi! Hebu tuulizane hapa swali. (Makofi)

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wao wa China kuja Tanzania wanakuja kwa wingi basi hata wangeturuhusu ndege yetu iwapakie wao tu kwa dola 14,000 maana tukipakia watu 40 ndege imelipa, lakini hata hiyo ndege hawataki kupanda wanaenda kupanda KLM sasa hivi naona Ethiopia imeruhusiwa na Kenya Airways nayo imeruhusiwa diplomasia hii ya kibiashara lazima iwe *fair* wao wafaidike na sisi tufaidike, hiyo ndio diplomasia na lazima pawe na sheria na utaratibu kuhusu mambo ya biashara ya nchi za nje hizo sio biashara ndogo ndogo anazofanya Mtanzania anakwenda kufanya mtu wa nje haiwezekani hicho kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Kariakoo mtu akichukua kontena moja mbili za vitu china ujue ni mara yake moja, mara ya pili mchina anakuja kufungua duka Tanzania, yaani ukionekana tu unafanya biashara pale ya vitu vitu hivi ukileta siku ya pili wanaleta wao. Sasa Watanzania wataendelea kuwa wachuuzi siku zote haiwezekani, mimi ushauri wangu kwa mama yetu aangalie...(Makofi)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nilitaka kumpa taarifa mchangiaji kwamba Watanzania wengi tunafanya biashara na China na hata kukubali kuchanja chanjo za corona tulitegemea nchi zitafunguka kwenye sehemu zetu za biashara kama China na nchi nyingine zimechanjwa madawa kama ya kwetu kutoka Marekani na sehemu nyingine wanaruhusiwa kuingia Marekani, lakini sisi tuliochanjwa za China, sisi tuliochanjwa hizo dawa tunaonekana bado hatujapona.

Kwa hiyo nilitaka kukupa Taarifa Mheshimiwa kwamba tulichanjwa ili tukubali masharti ili tukubali kuingia China kwa sababu ndio mji wa kibiashara kwa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali taarifa yake ipo vizuri kabisa.

Kwa hiyo la mwisho nataka kumshauri mama yetu akae na hawa kama wanataka na wao wawe wanaingia huku na sisi waturuhusu na sisi watu wetu waingie kule, kama hawataki na sisi tuwe hatuna imani na chanjo zao sio wao wanafanya biashara na nataka nikwambie wanatumia akili

sana mwishoni biashara zote za Tanzania, sisi tutakuwa tutabaki tu kuuza mahindi na maharage, watafanya wao, wao Wachina, watu wa *Europe* kama anavyosema Mheshimiwa Musukuma wanaruhusiwa kuingia lakini watu wa Afrika hawaruhusiwi kuingia. Kwa hiyo tusipoamka tutakuwa tunawafanyia wao biashara, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kabla ya mchangiaji Mheshimiwa Mwakagenda napenda kuutambua uingiaji wa Balozi wa Uturuki Balozi Mehment Gulluoglu, *welcome to the Parliament the Ambassador of Turkey*, karibu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwakagenda, ajiandae Mheshimiwa Makamba.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Balozi Mulamula nafahamu sio mwanasiasa ni mtendaji nakumbuka bajeti ya mwaka jana alizungumzia atatekeleza suala la uraia pacha na kuileta kwenye bajeti hii, lakini hata hajazungumzia na wala hajaingiza kwenye bajeti yake. Kwa hiyo nataka tu kumkumbusha aendelee kuwa mtendaji asitufuate sisi wanasiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la viwanja, kiwanja cha Maputo kiwanja namba 157/1 wewe mwenyewe Naibu Spika ukiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje unafahamu ni kiwanja kipo zaidi ya miaka 40 enzi zile la Samora Machel na Julius Nyerere walipeana mpaka leo kiwanja kile hakijaendelezwa, hii imekuwa ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu la Tanzania juu ya Balozi zinakuwa na viwanja vinakuwa vibovu popo wanaota mle kwenye majumba mabovu hii inajumuisha na nyumba kumi katika viwanja vitatu ambavyo vipo Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Mulamula, Mheshimiwa kiongozi Waziri ukienda Zambia viwanja vyetu vipo *prime area* kabisa ambayo sisi kama Taifa tulikuwa tuna uwezo wa kuvijenga viwanja vile, mimi nina uhakika Msechu yule wa *National Housing Cooperation* alikuwa na uwezo mkamwambia akajenga pale na akijenga pale, Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kusaidia *corridor* ya Kusini yote tukaweza zile fedha ambazo zitapatikana pale zikaweza kusaidia Balozi zetu za Kusini mwa Afrika, lakini nashangaa majengo yameoza, majengo ni mabovu mpaka wanafikiria namna ya kutunyang'anya. Hii ni aibu sana kwa Taifa kama la Tanzania lenye uchumi ambao una uwezo wa kujenga balozi zile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Balozi hizo wewe ni shahidi tunazo Balozi nyingi tumeshtakiwa majengo yanakuwa sio... Ufaransa kuna kipindi tulikuwa na jengo sio zuri sina uhakika kama mliendelea nalo na kulitengeneza.

31 MEI, 2022

Sasa Mheshimiwa nimesema wewe ni mtendaji sio mwanasiasa jitahidi kusimamie ile heshima yako uliyonayo ya kuisaidia Tanzania ikapata heshima ambayo tumedharaulika kwa muda mingi. Kiwanja kinakaa miaka 40 umri wa mtu anazaliwa anaoa anazeeka bado hatujaweza kukisaidia hicho kiwanja Mheshimiwa Spika naomba uingilie hilo, Naibu Spika naona na wewe kama kiongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda pale Abuja kuna kiwanja walitupa toka mwaka 1995 hadi leo wenzetu na kibaya zaidi kwa sababu mabalizi mnapopewa viwanja mnakuwa mpo wengi, kwa hiyo inaenda na lami inaenda vizuri, ikija kwenye Tanzania pana msitu unaenda tena sehemu nyingine Indonesia wananchi wamejenga Watanzani hatujajenga hii haiwezekani na wala haikubaliki...

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu..

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji amekuwa anarudia maneno yake kwamba Mheshimiwa Waziri asiwe kama sisi wanasiasa. Sasa *statement* yake anatuchukulia wanasiasa wote hatuna *credibility*, kwani ni *statement* mbaya ya hovyoo nataka nimwambie wana Siasa si kama wanavyojichukulia wenyewe, wengine ni wanasiasa tuna *professionals* zetu na tuna *credibility*, ahsante sana. (Makofi)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee naona ndugu yangu alikuwa ana hamu ya kuchangia sipokei...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia, ngoja basi.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia ngoja nikuite ndio nikwambie. Mheshimiwa Sophia umeipokea taarifa?

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei naomba niendelee, naomba tuendele na suala la watumishi waliopo mabalozini najua kuna sheria ya utumishi unapompa mtu kazi akufanyie ni lazima uhakikishe stahiki zake zinakuwepo. Balozini kuna shida sana ya madai

ya muda mrefu, kuna wafanyakazi wanadai unapowaongezea vyeo hawaendani sawa sawa na kipato wanachokipata, kuna madaai ya nyuma ya safari na vitu kama hivyo tunaomba muwafanyie watu hawa stahiki zao ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la diplomasia ya uchumi, tunashukuru Rais sasa hivi amerudi tena kwenye kuwasiliana na nchi mbalimbali tulikuwa tumepumzika kwa muda wa miaka kama sita, sasa ameamua kufungua upya. Ameenda kwenye *Royal Tour* na kweli tumeanza kuona mambo yakiendelea na wewe mwenyewe Waziri umesema kuna wafanyabiashara kama 100 kutoka Misri walikuja, na sisi hiyo tunaifurahia lakini pia Rais amefanya hiyo *Royal Tour* bado kuna shida kwenye mambo ya utalii ninajua kwamba mambo ya nje ya utalii vinaendana sambamba na hasa kwenye mambo ya hoteli. Kwa sababu utapata wageni sisi bado tupo chini sana kwenye *industry* ya kusaidia wageni tunaomba sasa wizara yako na Wizara ya Utalii kwa pamoja tusaidiane kusaidia wafanyabiashara wa kukaribisha hao watu ambao wanakuja kwa wingi tusipofanya vizuri hatutaweza kuingiza fedha na nguvu kubwa iliyofanyika tayari itakuwa imekwisha kupotea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mabalizi mfanye kazi yenu ya kuhakikisha mnapochukua baadhi ya wafanyabiashara hapa na kuwapeleka nje wakaone wenzao wanafanya biashara vipi hasa za hoteli kwa sababu tunahaja na tunakaribia kupokea wageni wengi sana na bado *industry* yetu ya hoteli haijawa nzuri, watu wameendelea kuwa wavivu, watu hawafanyakazi kwa kujituma. Tayari wageni wanakuja ukipata wageni 100 na wewe unaanda chai saa nne badala ya saa mbili iwe tayari, tayari unakosa wateja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo kwenye suala la hiyo hiyo diplomasia ya uchumi; umesema kuna mtandao wa *jb.com* kule China ambao unaangaliwa na watu takribani milioni mia saba umesema, hawa ni watu wengi sana, lakini bado sisi pamoja na *corona*, lakini bado Tanzania kule Guangzhou ambao ndiyo mji wa kibiashara tulikuwa hatuna Balozi ndogo pale ni mpaka waende kwenye Balozi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji ukishakuwa wakibiashara lazima ujiongeze wewe kama nchi, tunafahamu nji ya jirani zetu sitaki kuwataja, wao hadi kwenye mabasi ya wachina kuna matangazo yao sisi tunashindwa nini! Mimi nimesema hapa kuna mmoja amesema nisikuambie wewe mwanasiasa bado ninakwambia mtu ambaye ni mtendaji haongei lugha mbili, ninaomba usimamie hilo uhakikishe kwamba tunaweka nguvu mpya ya kibiashara Guangzhou na tunapeleka matangazao mengi Guangzhou, tuhakikishe tunafanya biashara ya Guangzhou ili tuweze kukuza diplomasia ya uchumi. (Makofi)

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninaendelea kuomba, ninaomba mama yangu chapa kazi, usimamie yale unayoyaamini kama nilivyosema wanawake wakiamini jambo lao wanalifanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa kuna baadhi ya wageni ambao wapo ndani ya Bunge lakini hawakutangazwa kutokana na sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo.

Naomba kutangaza Mheshimiwa Waziri Mulamula ana wageni 16 wakiongozwa na binti yake Ndugu Tanya Mulamula, kama yupo asimame. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Joseph Kahama - Katibu Mkuu wa *Tanzania China Friendship Association*; Mr. *Kristnn Gunnarsson - Director of Strategic Minerals and Metals Tanzania Limited*. *(Makofi)*

Meja Jenerali Mstaafu Hamis Semfuko - *Board Member Tanzania China Friendship Association*. *(Makofi)*

Balozi Kombo - Balozi wa Tanzania Italy, karibu sana; Balozi Mbelwa Kairuki - Balozi wa Tanzania China; Balozi James Msekela, Balozi Mstaafu; Balozi Bertha Sommi - Balozi Mstaafu, Meja Jenerali Charles Karamba - Balozi wa Rwanda, karibu sana Mheshimiwa Balozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mousa Farhang, Balozi wa Iran; Victoria Emil and Girian Joseph *Representative from Embassy of Uganda*, karibuni sana. *(Makofi)*

Diana Paul Chando - *AU Youth Ambassador for East African Regions*; Eben Mzava - *East Africa Community Youth Ambassador to Tanzania*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Catherine Kilinda - Meneja *JNICC*; Ndugu Chabu Mishwaro - mwakilishi *CRDB*; Ndugu Getrude Mallya - mwakilishi *NMB* na Ndugu Nsolo Mlozi - mwakilishi *NMB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani niwe na neno zuri la kumwambia Mama yangu Balozi Mulamula, lakini labda nianze kwa kusema unahitaji kufanya usafi kwenye nyumba yako, unahitaji kusafisha Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Rais Samia Suluhu Hassan amejipambunua kutangaza Sera ya Mambo ya Nje, amejipambanua kwa kutangaza diplomasia ya uchumi katika nchi yetu. Na kwa kufanya hivyo ameona tofauti na watangulizi wake ana uwezo mkubwa wa kutuletea maendeleo Watanzania kupitia mahusiano na mashirikiano mazuri na mataifa mbalimbali hapa duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, vipo vikwazo vingi ambavyo wewe kama balozi mbobezi ni lazima uviondoe ili kuweza kuifanya dhamira ya Mama Samia Suluhu Hassan iweze kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tulikwenda Dubai, Marekani, tumefanya *Royal Tour*, tumeita wawekezaji, lakini kwa mfano Mkataba wa Kimataifa wa Huduma na Biashara ambao tuliingia mwaka 1994 mkataba ule unaruhusu wawekezaji kutoka nje kwenye maeneo mawili tu; eneo la utalii na usafirishaji kwa maana ya eneo la utalii na eneo hoteli kuanzia ngazi ya nyota nne. Sasa jiulize nguvu tunayotumia kutangaza, lakini kwenye eneo hilo la huduma tumeridhia kwenye maeneo haya mawili tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena mama yangu unakazi kubwa sana ya kufanya *alignment* ya sheria zetu, ya kufanya *alignment* ya mikataba mbalimbali ili wawekezaji waweze kuja kama ambavyo Rais wetu anawaomba na kuwasisitiza waje kuwekeza kwenye nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji yeyote duniani niliwahi kusema hii kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara na leo narudia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nje, mwekezaji yeyote ambaye anatumia pesa zake kuja kuwekeza ndani ya nchi ni lazima afanye kitu kinaitwa *economic intelligence* lazima afanye *intelligence*. Hivi tunavyozungumza tunakwenda kuwatangazia kule lakini wanajua Shinyanga kunapatikana dhabahu na almasi, wanajua Arusha Mererani kunapatikana *Tanzanite* wanajua rasilimali tulizonazo, lakini kitakacho wakwamisha ni sheria zetu, mikataba yetu, tamaduni zetu na namna ambavyo tunakosa msimamo kwenye mazingira ya kibiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutolee mfano, mwaka 2019 tulipitisha sheria mbili humu ndani zinasema sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutakuwa na uwezo wa kuitisha mikataba ya wawekezaji na kuipitia mikataba ile na kama hiyo mikataba itaonekana kwamba haiwanufaishi Watanzania kutokana na rasilimali zao mikataba ile inaweza kufanyiwa marekebisho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa *clause* kama hiyo ni nani anaweka kuja kuweka hela yake hapa, yaani kuna vifungu vya namna hiyo kwamba mtu anaweza akaingia mkataba akijua tumeshasaini *deal*, tumeshafunga

mkataba lakini kesho asubuhi anaibuka Rais mwingine tofauti na Rais ambaye alikuwa labda ana nia njema anasema huu mkataba namna ulivyopitishwa pitishwa huu lazima tuufanyie *review*, tunafanyia *review* mwisho wa siku mkataba unabadilika ni *unstable business environment*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu hiyo ndiyo maana hata unaona Mheshimiwa Waziri hicho kifungu hakitekelezeki, kwani tumeomba mara ngapi ilete mkataba hapa hakitekelezeki kwa sababu yaani haiwezekani ku-*review* mikataba kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini tuna kitu kinaitwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, tena kwa bahati nzuri Mahakama hiyo ipo Arusha hapa hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri unaomba fedha bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa mahakama na bilioni 1.2 kwaajili ya uendeshaji wa mahakama. Hakuna mtanzania au taasisi ya Tanzania inayoruhusiwa kwenda kufungua kesi kwenye ile mahakama na mwaka 2019 ndiyo tulijitoa kwenye haki hiyo.

Sasa mama yangu Mheshimiwa Liberata Mulamula utusaidie hii *foreign policy* na hii *economic diplomacy* anayoitangaza Mheshimiwa Rais inatokana na msimamo mzuri msimamo ambao una tabirika wa kibiashara ndani ya nchi mpaka mtu aje kuwekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema vizuri ndugu zangu hapa kuhusu suala la uraia pacha, tumeenda kuwavutia wawekezaji na baina yao ni Watanzania wanaoishi nchi za nje, tunasema waje kuwekeza, lakini unasema kwasababu anakaa nje nchi hawezi kuja kuwekeza huku ndani na kumiliki ardhi kwa sababu ni *foreigner*. Sasa mmoja ametoa taarifa anasema kuna kitu kinaitwa hadhi maalum, ni nini hiki hadhi maalum ni kitu gani? Kwa nini msiseme tunaposema hadhi maalum tunaamanisha itakuwa moja na mimi nilitegemea hivyo na ndiyo maana sikuhaji Mheshimiwa Rais aliposema kwamba watapewa hadhi maalum kwa sababu nilijua Mheshimiwa Waziri ukija kusoma hotuba yako utafafanua nini maana ya hadhi maalum na hilo ndilo swali la Watanzania wengi, na umesema vizuri wanachangia kwenye Pato la Taifa lakini ninani atakayekubali kwenda kuwekeza kwenye nchi ambayo hana uhakika kama mali anayoenda kuwekeza pale ataendelea kuwa nayo vizazi na vizazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hawa watu wanafanyakazi ngumu *diaspora*, mimi nakuomba unapokuja kuhitimisha hapa uje utuambie hiyo inayoitwa hadhi maalumu ni kitu gani hasa humo ndani kuna vitu vya namna gani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu mwanzoni Waziri wetu wa Mambo ya Nje alipeleka ripoti ya utekelezaji wa haki za binadamu ambayo

ni nzuri sana, mimi nakubaliana nayo, tume-adopt mambo mengi sana na moja kati ya jambo ambalo tulili-adopt tumesema hivi naomba ni quote; *“The State supports the part of recommendation which leads to take all necessary measures to combat discrimination and violence against women including domestic violence”* halafu mkaenda kukiri mkasema; *“The State notes that part of the recommendation of on the family violence are this concept is yet to be define in the state policies”* yaani sera zetu za nchi hazitambui au hazija accommodate suala la unyanyasaji (domestic violence) kwenye ngazi ya familia tumekubaliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wewe unaona kwenye vyombo vya habari, jana kuna mwanamke Mwanza ameuwawa, leo tunaona hapa wamechangia vizuri sana wenzangu kwenye bajeti zao, watu wanauwawa, wanawake wanauliwa kwenye familia zao. Shinyanga asilimia 56 ya watoto wa Shinyanga wanaolewa wakiwa wadogo wanapata mimba za utotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni *UN Report* imepelekwa na Mheshimiwa Waziri anahusika, ndiyo mwenye dhamana ya hii ripoti yetu, ndiyo maana namwambia anatakiwa kusafisha nyumba yake. *We have a lot of International Agreement* ambazo hatuja ratify. Zipo *International Agreement* ambazo hatuja domesticate, hii yote ndiyo msingi, ndiyo tija, ndiyo shibe ya hiyo *foreign policy* ambayo Mama Samia Suluhu Hassan anahangaika kutembea duniani mama wa watu anamiaka sijui sitini na ngapi kuhakikisha kwamba anavutia wawekezaji. Sheria zetu, mipango yetu, mikataba yetu kama haiwalindi wawekezaji ndani ya nchi tutazunguka sana na jambo hili litakuwa ni la muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimalizie fedha tunayoenda kuwekeza kwenye *African Court Peoples and Human Rights* kama nimei-quote vizuri ni fedha nyingi, tufungue, kuna wakati mwingine haya mambo mnayafunga watu wanadhania kwamba mna nia mbaya yaani yanaonesha tu kwamba kuna dhamira ovu kwenye kufunga watu wasiende na taasisi, rhusuni watu waende kwenye hizi mahakama rudisha kile kifungu cha 38 ili *article* tuliyo *withdraw 38(6)* nafikiri, rudusheni twende kwenye mahakama hizo tufungue, sisi ndiyo *host* na *by the way* umeomba fedha kwaajili ya kuendeleza mahakama hii, kwa nini unakataza wanachi wa Tanzania wasiende kushtaki kwenye mahakama ile, naelewa mazingira ya kisiasa yalivyokuwa mwaka 2019 wakati tunajiondoa, lakini mmejinasibu wenyewe kwamba huko tumetoka. Sasa hivi tuna uhuru wa vyombo vya habari, sasa hivi tuna uhuru wa maandishi, sasa hivi tuna uhuru wa watu kusema na mambo kama hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni hivyo na hiyo mahakama ndiyo kazi yake kwenda kusikiliza watu wanaonyanyaswa maandishi wa habari, kwenda kusikiliza watu wanaonyanyaswa kwaajili wameongea na *freedom*

of assembly, fungueni watu waende nchi ifunguke kama mnavyosema lakini tukisema tuna *advocate*, tunatangaza Tanzania ifunguke kiuchumi ilihali tunajua kabisa hapa yaani tunasema nini tunajipiga ngwala wenyewe, Mheshimiwa Liberata safisha nyumba yako, usimkwamishe Mheshimiwa Rais hatutaki kurudi kwenye kukusanya shilingi 20,000 za machinga. Mama analeta matrilioni ya fedha barabara zinajengwa, analeta matrilioni ya fedha vituo vya afya vinajengwa, biashara ya kuchangisha watu masikini tuachane nayo, fedha kwa ajili ya nchi zinaoendelea huko nje zipo kibao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Dennis Londo, ajiandae Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, ajiandae Mheshimiwa Nollo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya mimi pia kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Rais wetu ama kama alivyotajwa mwanadiplomasia namba moja, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya kufungua milango ya nchi lakini pia kuitangaza Tanzania nje ya mipaka ya nchi yetu. Kazi anayofanya ni kubwa na *commitment* ya Serikali tunaiona kwa kupeleka fedha kiasi kikubwa kwenye balozi zetu, kukarabati lakini pia kujenga majengo mapya ambayo nia ni kuboresha makazi, mazingira rafiki ya watumishi wetu ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu, lakini pia ni muhimu sana kwa sera zetu za ndani. Nasema haya kwa sababu moja, sasa hivi tunashuhudia mabadiliko makubwa ambayo yanaendelea huko duniani, changamoto ambayo inaikuta Ulaya ya Mashariki, Ulaya ya kwa ujumla kama Bara, lakini pia Marekani sisi hatuwezi kujitenga nazo. Vikwazo ambavyo makampuni mbalimbali yanawekewa kwa sababu ya vita ambavyo vinaendelea kule Ukraine sisi hatuwezi kujitenga navyo, tunajua tunawashirika wengi ambao wanajenga miradi mikubwa hapa ambao na wenyewe ni sehemu ya mizozo ambayo inaendelea. Pamoja na kwamba sitawataja kwa majina lakini tunafahamu miradi mikubwa ambayo inaendelea hatuna hakika ya kesho kwa sababu kila mmoja anajipanga jinsi gani ya kumdhibiti mwenzie. Ni kwa kiasi gani siasa zao zinaenda kutuathiri hilo ni swali ambalo tunapaswa kulitengenezea mkakati wa majibu yake hasa tunapoenda kutekeleza bajeti yetu ya mwaka huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu jinsi dunia ilivyogawanyika katika makundi ya Mashariki na Magharibi ambayo ilikuwa ni matokeo ya Vita

Vikuu vya Pili vya Dunia, lakini tunafahamu nchi zetu zilivyotengwa kwamba huyu atakuwa niwa Mashariki huyu wa Magharibi kutokana na siasa ambazo zilikuwa zinaendelea duniani. Kwa kiasi kikubwa nchi hizi ambazo zimetengwa Mashariki na Magharibi ni kwa sababu ya mlengo wa kisiasa, lakini moja kubwa ambalo tulikuwa tumetengwa tukifahamu kabisa kwamba tupo wapi ni zile nchi ambazo ni za Kusini na Kaskazini, kwa maana nchi za Kaskazini walikuwa ni matajiri, wameendelea kiviwanda na kiteknolojia na nchi Kusini ni maskini ambao hawajiwezi.

Sasa hapa katikati tumefanya vizuri, baada ya kuvunjika kwa ukuta wa Berlin na *West* na *East* kuungana tumefanyakazi vizuri katika jina la utandawazi na sisi kwa kiasi kikubwa tumeacha ile misingi yetu ya ujamaa na kujitegemea tukiwa sehemu ya hii Sera ya Utandawazi lakini hiki kinachoendelea sasa hivi hatujui kesho tunaenda kurudi kulekule tulikotoka ama dunia inatufungulia ukurasa gani katika historia ya mahusiano duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaishi katika kipindi ambacho tunapaswa kujipanga kwasababu tusipojipanga tutapangwa na katika namna hiyo ni muhimu sasa kurudia ile sera yetu ya kutofungamana na upande wowote ili tujenge uchumi wetu wa ndani lakini mataifa na mahusiano yetu na nchi za nje yajijenge katika namna ya kutusaidia kujibu changamoto zetu za ndani. Na katika hili tunaona dunia inavyonyenyekea inavyohangaika kuhusiana na masuala mazima ya *energy*, masuala ya *gas* na rasilimali zingine ambazo Tanzania tunazo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba wakubwa wanatuangalia kwa hofu kwasababu wenyewe kwa wenyewe hawaaminiani na *move* wanazozifanya kuja Afrika zinawafanya wasilale sasa ni kiasi gani na sisi tunajipanga kutumia migogoro hiyo kama fursa kwetu kwasababu fursa lazima ujiandae nayo usipojiandaa nayo fursa itakupita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sasa wa kuangalia mataifa ambayo tumekuwa na mahusiano nayo ya muda mrefu Taifa kama Iran ambalo tuna mahusiano nayo ya muda mrefu wana ubalozi Dar es Salaam muda mrefu ni sababu zipi ambazo zinatufanya tusifungue ubalozi Iran hawa wenzetu wapo mbali katika teknolojia ya *petrol*, teknolojia ya *gas* kwanini hatuoni kwamba ni muhimu sasa wakati umefika wa kubadilishana nao ujuzi na *skills* katika maeneo ya *petrol* na *gas* kwasababu hawana marafiki wengi lakini sisi wachache ambao tupo kwanini tusitumie hiyo kama fursa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tunapozungumzia Sera ya Nje ni lazima ijibu changamoto za ndoto lazima tuwe na Sera ya Ndani ambayo tunajua inataka kutupeleka wapi. Kwa hiyo, Sera ya Nje lazima itumike kama *tool* ya kujibu changamoto zetu za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilijipa agenda ya kwenda kufanya mapinduzi ya kilimo na tunaona *commitment* ya Serikali kwa kuongeza bajeti ya kilimo tunaenda kufanya *rural transformation*, tunaenda kufanya *rural empowerment* ni kwa kiasi gani mikakati ya Sera ya Mambo ya Nje inaenda kujibu hizi changamoto ambazo sisi tumejipa jukumu kwasababu kama mikakati ya Sera ya Mambo ya Nje haijielekezi kwenda kujibu changamoto zetu vijijini basi kuna walakini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kazi kubwa ya Wizara ya Mambo ya Nje ni kuratibu taasisi za Serikali kwa maana Wizara zote, lakini asasi binafsi na mashirika, jinsi gani na mikakati gani ambayo wamejiwekea ndani, sisi tunatumia sera yetu ya nje kujibu ama ku-*facilitate* malengo ya ndani, na katika hili tuna suala la kilimo, mifugo lakini uvuvi. Huko teknolojia yetu iko nyuma, ni kwa kiasi gani bajeti yetu ya Mambo ya Nje inaenda kuchukua ujuzi ama inaenda kutuunganisha na watu ambao wamefika mbali kwa ajili ya kubadilishana ujuzi na uzoefu ili ku-*transform* sekta hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo wewe ni shahidi katika kipindi kirefu tulikuwa na sera inaitwa *economic diplomacy* ama sera ya kiuchumi. Sera hii ni nzuri, lakini inahitaji maboresho makubwa kwa sababu tunapitia mabadiliko makubwa ambayo hatujawahi kupitia katika kizazi chetu, ni lazima tukae, tutafakari *domestically* tunaenda wapi? Sera zetu zinatuelekeza wapi na kwa namna gani tutumie Sera ya Mambo ya Nje kujibu changamoto zetu za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *short of that* tutaendelea kuwa wasindikizaji wa wenzetu kwa sababu wenzetu wanamalengo, wenzetu wanandoto ambazo kama sisi tutashindwa kupeleka ndoto zetu na kuwatumia wao kama *facilitator* na kama *partner* katika kufikia malengo yetu basi tutakuwa sehemu ya kufanikisha malengo yao ambayo wanakijiji wetu, wananchi wetu hawatafaidika na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo wewe ni shahidi, unafahamu diplomasia yetu wakati wa vita baridi, mashariki na magharibi. Kuna Taifa dogo sana ambalo katikati ya vikwazo vikubwa liliweza kujenga shule nne za kilimo pale Kibiti, Ruvu, Ifakara na Kilosa. Shule hizi zilikuwa *specific* kwa ajili ya kilimo na Taifa hili kwa kweli litaendelea kudumu kwenye fikra na maono ya Watanzania wengi na ndiyo maana Watanzania wengi walimlilia Fidel Castro kwa sababu alisomesha watoto wengi maskini katika familia katika kila kona ya Tanzania kupitia shule hizi nne za kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu alijua kama Taifa tunataka tujikomboa kupitia kilimo, alijua kama Taifa wananchi wengi wameajiriwa kupitia kilimo, alijua ili tutoke ni lazima wananchi wetu wale, washibe na ndio maana akatuletea ujuzi, lakini akatusaidia kutujengea shule ambazo sina

hakika zina hali gani sasa hivi na nini mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha shule hizi ili ziendeleo kuwa alama ya mahusiano kati ya nchi ambazo zinaendelea, nchi ambazo ziko kusini kama zinavyoitwa *south cooperation*, hiki ni kielelezo kikubwa cha nchi ambazo ziko kusini jinsi gani zinaweza zikashirikiana katika kubadilishana ujuzi, uzoefu lakini tukashirikiana katika maeneo ambayo tunaweza kubadilisha maisha ya wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba *economic diplomacy* kwa kiasi kikubwa imetuletea marafiki. Lakini umefika wakati sasa wa ku-*adapt* kitu kinaitwa *innovative diplomacy*, kwa jinsi gani tunatumia ubunifu kama njia ya kufikia mataifa mengine, lakini mataifa mengine kutufikia, kwa sababu tumejikita katika maendeleo vijijini. Ni wazi tunahitaji ubunifu katika viwanda vidogo, tunahitaji ubunifu katika kilimo, tunahitaji ubunifu katika uvuvi, tunahitaji ubunifu katika mazao na hata kupunguza wanaita *prost loss harvesting* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wana teknolojia, wenzetu wana ujuzi, ni kwa kiasi gani sera yetu ya mambo ya nje inaenda kutusaidia kwa kututengenezea *food security*, lakini kututengenezea ajira kwa wananchi wetu vijijini. Kwa sababu tunasema tunaenda kujikita kijijini, ni kwa jinsi gani mahusiano haya tunayaboresha kwa ajili ya kupunguza tatizo la ajira *motivative...* (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa kengele ya pili.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nilishamwita Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Nollo, ajiandae Mheshimiwa Kawawa.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, *Bismillah Rahman Rahim*, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini halikadhalika napenda vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mulamula pamoja na Mheshimiwa Balozi Mbarouk na timu yao ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakifanya katika kuboresha diplomasia ya uchumi pamoja na kuhuisha mahusiano mema ya Tanzania ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika kabla sijaenda mbali naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kitendo cha uungwana alichokifanya ambacho hakuwa amekipangia cha kuweza kuwahudumia vizuri wale wakimbizi wa Ukraine ambao walikuwa wamekwama kule Zanzibar wakati kwao lilipotokea lile tatizo la vita na wakawa hawana jinsi isipokuwa wabakie Zanzibar, na katika hili pia napenda kuishukuru Wizara kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Tanzania ndiyo ilishirikiana na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kuweza kuwahudumia wale wakimbizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo nimpongeze vilevile ndugu yangu Balozi Simbachawene kwa jitihada zake ambazo alizifanya hivi karibuni na kitendo kile kimeonesha mfano wa Mabalizi wetu kwamba wanaweza wakafanya kazi nzuri katika hali ya dharura. Kuna vijana ambao walikuwa wavuvi wetu kule Zanzibar, walipata tatizo baharini na wakaenda wakaokotwa Kenya. Lakini ubalozi wetu wa Kenya ulifanya kazi kwa haraka na vijana wetu wale wakashughulikiwa, wakahudumiwa, wakalazwa na wakasafirishwa mpaka Zanzibar kwa muda muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiki kinatufundisha kitu, kitu gani tunasoma hapa; kwamba ni muhimu Wizara, Mheshimiwa Waziri Mulamula tutenge fungu la fedha za dharura katika Mfuko wetu wa Maafa ambao unaweza ukahudumia majanga kama haya ambayo hatuyategemei kutokea wakati wowote ule. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini halikadhalika naomba sasa niende katika diplomasia ya kiuchumi ambayo wenzangu pia wamezungumzia. Diplomasia ya kiuchumi kabla sijazungumzia hapa nafikiri kwanza nipeleke pongezi zangu kwa Mama Samia kwa sababu yeye ameonesha kivitendo na kihalisia umuhimu wa diplomasia ya kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka kwamba Tanzania ikiwa ni kama nchi inahitaji tuzidi kuifungua. Tayari imefunguka kwa sababu kazi ya kuifungua tofauti na wenzetu wanavyozungumza hapa Tanzania imefunguliwa na toka Rais wa Kwanza Baba Nyerere, akaja Mheshimiwa Mkapa, Ali Hassan Mwinyi, amekuja vilevile Jakaya Mrisho Kikwete, Magufuli na sasa hivi Mama Samia tunaendelea kuifungua nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kwamba labda nchi ilikuwa imekwama haijafunguka, lakini sasa hivi Mama Samia amekuja katika utaratibu ule mpya ambao mwenzangu amegusia hapa, ile *innovative diplomacy* kwamba *issue* ya *royal tour* imekwenda kuifungua na siyo kuitangaza tu Tanzania, lakini imekwenda kuifungua kiuchumi na ku-unlock zile fursa za maendeleo na kiuchumi ambazo zilikuwa kidogo zimekwama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili naomba tu Wizara sasa mama ameanza na mabalozi wetu waichukue hii *royal tour* katika hatua ya pili. Tungetegemea sasa hivi mwakani tukija tukikutana hapa, tuje tutoe taarifa ya ongezeko la makongamano ambayo yamefanyika katika nchi mbalimbali kutokana na wenzetu hawa mabalozi katika maeneo yao ambayo tutakwenda kupima kutokana na ongezeko la wageni ambao wameongezeka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuongelea suala zima la ushauri katika maeneo mbalimbali hasa kwa upande wa Zanzibar kwa sababu *royal tour* bahati nzuri ime-reflect Zanzibar vizuri sana. Sasa wakati *royal tour* inaongea vizuri kuhusu Zanzibar, nafikiri ni muda muafaka sasa tuongeze wigo wa uwakilishi wa ubalozi na watendaji au Maafisa Ubalozi katika balozi zetu mbalimbali duniani ili tuongeze vivutio au tuongeze wigo wa fedha za maendeleo ambazo zinakwenda Zanzibar kupitia balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hivi sasa watalii ambao wanakuja Tanzania ni kama theluthi moja, hata haifiki vizuri ambao wanakwenda Zanzibar. Sasa kwa kutumia balozi zetu hizi twende tukahamasishe balozi ziweze kufanya kazi za kuweza kusaidia wigo wa kuimarisha maendeleo ya Zanzibar. Lakini pia naomba jambo lingine la muhimu tukaongeze wigo wa wawakilishi katika mikutano yetu ya kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwakilishi wa mikutano yetu hii kuna mikutano mingi ambayo Tanzania imeridhia, mfano kuna UNCC-COP yaani Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi, kuna *United Nation Conference on Biodiversity*, kuna *United Nations on Control and Combat Desertification* kuna mikutano ya *trades* ya kibiashara, kuna mikutano mbalimbali ambayo tumeridhia kama Tanzania. Lakini uwakilishi wa Zanzibar hauko vyema na hata tunapokwenda kuwakilisha sijaona kama kuna mkutano ambao *Chief Negotiators* amekuwa ni Mzanzibar, lakini *always Chief Negotiators* wanatoka upande wa pili wa Muungano, sasa na hii wakati mwingine kidogo inaminyama maendeleo au zile fursa za uchumi kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, naomba hili tukalisimamie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika pengine twende mbali zaidi kwenye masuala ya sera, kwa sababu *foreign policy* ya Tanzania ina-reflect vilevile *United Republic of Tanzania*. Sasa iko so *generic* kiasi kwamba haioneshi Zanzibar hasa inakuwa *reflected* vipi katika *policy* ile. Kwa hiyo, naomba Waziri ikiwezekana japokuwa sera yetu ni ya mwaka 2015 lakini tuna uwezo wa kuifanyia marekebisho mapema tukaangalia sasa hivi na Zanzibar ina-fit vipi katika maeneo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye mikutano hii kama kuna *Chief Negotiators* basi kuwe na *Deputy Chief Negotiators* ambaye atatoka

upande wa pili wa Muungano. Kama *Chief Negotiators* atatoka Zanzibar basi msaidizi wake atoke Tanzania Bara, halikadhalika kama atatoka upande wa Bara basi msaidizi wake atoke Zanzibar. Lakini halikadhalika katika mabalozi pia siyo lazima tufate utaratibu ambao upo sasa hivi duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile sisi tuna Muungano na Muungano wetu ni *very unique*, tunaweza tukaamua sasa balozi akawa na msaidizi wake. Kama balozi atatoka Tanzania, msaidizi balozi atoke Zanzibar. Na hii itaisaidia Zanzibar kuweza kujitangaza zaidi na kuweza kutengeneza fursa nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kuna mikataba miwili hii ambayo ina *reflect* kibiashara; kuna mkataba mmoja unaitwa *Basel Convention* ambao ni *International Treaty on Control of Transboundary Hazardous of Waste and their Disposal*; halafu kuna mkataba mwingine wa *sites* ambao ni *Convention on International Trade in Endangered Species*; mikataba hii yote ni mikataba ya kibiashara. Sasa ombi langu kwa sababu ni ya kibiashara hii, sekta ambazo zinatekeleza hii mikataba zote ziko Tanzania Bara kwa upande wa *Basel Conventions* sekta ambayo inahusika ni NEMC kwa Bara na kwa upande wa *sites* ni Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba tu kwa sababu hizi Mzanzibar akitaka kusafirisha vyuma chakavu au akitaka kusafirisha hizi aina za wanyama ambazo ni adimu inabidi aje Dodoma, aje afuatilie vibali. Kwa hiyo, inapoteza muda na inaingiza gharama zaidi. Naomba tu mikataba ya namna hii tuangalie uwezekano wa kuwa na uwakilishi wa zile *institutions* za Zanzibar ambazo zinaweza zikatoa vibali vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama NEMC kuna ZEMA kule Zanzibar inaweza ikafanya kazi hiyo, lakini halikadhalika kwa upande wa Maliasili na Zanzibar vilevile kuna Idara ya Misititu na Maliasili Zisizorejesheka inaweza pia ikafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, naomba tukaangalia uwezekano wa kuweza ku-*reflect* hizi taasisi nazo kwa hii mikataba mbalimbali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nollo, Mheshimiwa Kawawa na ajinadae Mheshimiwa Mhata.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa dhati nianze kuipongeza Serikali kwa namna ilivyoahidi mwaka jana kwenye bajeti iliyopita kuhusu kufungua ubalozi mdogo pale Lubumbashi, ila vilevile niipongeze kwa kufungua sasa ubalozi Indonesia. Indonesia sasa ni nchi ambayo inaelekea kuwa nchi ya nne katika kuwa na uchumi wa kilimo. Kwa hiyo, ni jambo zuri na naipongeza Serikali kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee habari ya sera ya mambo ya nje na wataalam katika masuala ya diplomasia wanasema sera ya mambo ya nje ni kitu kinachoishi yaani sera ya mambo ya nje ni kitu kinachoishi, kwa hiyo, sera zetu katika miaka ya 1980 miaka ile tunafanya ukombozi wa Afrika wakati wenzetu bado hawajapata uhuru haziwezi kulingana na leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mabadiliko yametokea katika nyanja hizo na sera ya mambo ya nje inabadilika kila wakati, inabadilika kutokana na mazingira ya dunia, lakini vilevile inabadilika kutokana na namna ya uongozi unavyokuwa madarakani. Lakini Tanzania nataka niseme tumekuwa vinara wazuri katika sera ya mambo ya nje na kikubwa zaidi ambacho tumeshikilia ni kuhusu suala la kutokufungamana na upande wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe maoni yangu binafsi kwamba kumekuwa na maneno wakati mwingine yanatoka ndani ya Serikali kwamba miaka sita iliyopita nchi yetu kama ilikuwa imejifunga yaani kwamba sasa nchi yetu ilikuwa imefungwa, yaani haina uhusiano na nchi zingine na bahati mbaya niliwahi kunukuu hata balozi mmoja anasema sasa Tanzania inafungua milango yake baada ya kuwa na siasa ambayo ilikuwa imejifunga na *international community*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kama nchi tuwe na msimamo, ni balozi gani tulifunga kwamba tumefunga ubalozi kutokana na ugomvi huo? Ni balozi gani tulimfukuza kwamba sasa kutokana na hili tumekufukuza, tumekuondoa. Kwa hiyo, tumekuwa tunajibebesha maneno kana kwamba nchi yetu iliingia kwenye mgogoro mkubwa wa kimataifa na tukafunga kila kitu, kitu ambacho si kweli. Biashara zimeendeleo kama kawaida, si kwamba sasa ndiyo tumeanza biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme maneno haya, inawezekana tukawa tunabomoa kwa upande mmoja, aidha kwa kutokujua au katika propaganda ambazo zinatoka katika upande mwingine wa dunia. Kwa hiyo, nchi yetu imeendelea na sera madhubuti za kuimarisha hasa hasa uchumi

na tulipofika hapa leo ni muendelezo wa kipindi chote, hakuna sehemu ambapo kama ni behewa lilikatika, tunaendelea hivyo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme wenzangu wamechangia kuhusu diplomasia ya uchumi na kama nilivyosema *foreign policy*, siasa ya mambo ya nje ni siasa inayoishi. Kazi tuliyonayo sasa ni nchi yetu kuamua namna gani inaweza kukuza biashara kati ya mataifa mengine duniani. Mimi nataka niseme kuhusu Pakistan. Pakistan ni Taifa ambalo tumekuwa tunafanya nalo biashara kwa muda mrefu, mwaka 2019/2020 biashara yetu kati ya Pakistan ilikuwa kati ya dola bilioni 69 sisi tuliuzia Pakistan na Pakistan nao waliweza kuuza kwetu bilioni 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bahati mbaya hatuna ubalozi Pakistan. Balozi anayetumika anatoka India lakini na Waziri leo kasema kwamba kati ya India na Pakistan kumekuwa hakuna mahusiano mazuri ya kisiasa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kwamba iongeze, ifungue ubalozi Pakistan. Kenya na Uganda mwaka jana jumla wameuza dola milioni 154 biashara waliyoifanya na Pakistan. Kwa hiyo, kama tulivyofungua Indonesia tufungue na Pakistan. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekuwa na rafiki zetu wa damu katika nyakati mbalimbali, Iran ni mojawapo ya Taifa ambalo tumepita nalo katika nyakati mbalimbali kwa sera ya Mwalimu Nyerere alivyokuwa anatetea haki na unyanyasaji duniani kote. Iran limekuwa ni Taifa ambalo sisi tumesimama nalo katika nyakati mbalimbali, lakini kwa bahati mbaya Iran ni Taifa kubwa japo kama mtu halisemi, haliandiki lakini ukweli unabaki Iran ni Taifa kubwa hapa duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna Ubalozi Iran, tumefungua Ubalozi Israel, sitaki kusema kwamba kufungua Ubalozi Israel basi na Iran ufungue, lakini kwa umuhimu, kwa undugu wetu wa damu na Iran ni lazima tufungue ubalozi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri jambo uliangalie na utumie kwamba sisi hatufungamani na upande wowote na Iran ni sehemu yetu muhimu kwa maana ya biashara na mahusiano yetu ya kindugu kama nilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwenye *economic diplomacy* mambo makubwa yaliyofanyika kwamba ni biashara, sisi tunafanya biashara mbalimbali, tunatoa huduma kwa mfano Tanzania katika bandari yetu ile ni huduma, kuhudumia nchi ambazo hazina bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali ijipange katika suala hili. Tumeichukua Congo katika *East Africa* na bahati nzuri sasa mizigo yetu mingi na nchi nyingine/wenzetu majirani walikuwa wanapata sasa

imelekezwa kwetu. Lakini bado viko vikwazo vya kufanya biashara kwa maana ya kwamba kwenye mizani yetu kuna ucheleweshaji mkubwa, lakini na *efficiency* ya bandari yetu. Nilikuona naomba sana jambo hili Serikali ilianganalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka niongelee habari ya huduma ya matibabu. Nchi nyingi duniani na hata sisi wenyewe tumekuwa wakati mwingine tunaenda sana katika Taifa la India kwa ajili ya matibabu. Nataka nikwambie na nikupe taarifa kwamba Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa sasa inapokea wagonjwa wengi kutoka nchi zinazotuzunguka hasa za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali itangaze kwa makusudi kwamba Benjamin Mkapa sasa ni *center of excellency* katika *East and Central Africa*, na tukifanya hivyo tuweke sasa huduma muhimu zinazopatikana kwenye suala la magonjwa kama ya figo, upasuaji na vitu vingine, sasa hospitali inafanya vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri kupitia pamoja na Wizara ya Afya Hospitali ya Benjamin Mkapa ipewe vifaa vyote na huduma zote stahiki lakini tuitangaze kwamba kwa tangazo maalum sasa hii ni *center of excellency* kwa *East and Central Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niongeze jambo la sisi kuteuliwa na SADC kwamba tuwe ni *supplier* wa dawa na ukiangalia kama Waziri alivyosema kumekuwa na wenzetu wanasuasua kutumia Tanzania kama sasa ndiyo *procurement agency* kwa ajili ya wao kupata dawa. Ni vyema Serikali ikawekeza kwamba badala ya sisi kuwa kama ni dalali basi tuwe na viwanda ili wenzetu wa SADC waweze kununua kwetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo nilikuwa naomba sana na haileti *logic* kwamba mimi nikakununulie halafu nikuletee dawa kwa kuuzia. Ni bora tuweke viwanda vya kutosha hapa vya dawa ili waje wanunue kwetu badala ya sisi kuwa madalali kwa SADC.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri amesema habari ya kwamba sisi sasa ndiyo kitovu cha kupambana na ugaidi katika nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Habari hii ni njema lakini katika hisia si habari njema sana na sijui kwa nini Serikali walilichukua hivi na kutamka lile jambo lile nzito kwamba sisi tumekuwa *excellency*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Mhata.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu mdogo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri Mbarouk Mbarouk, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya na wamefanya kazi nzuri katika kutekeleza majukumu yao katika Wizara hii, katika kusimamia na kuratibu masuala ya uhusiano wa kimataifa kati ya nchi yetu ya Tanzania na nchi nyingine duniani na kwa kumshauri vyema Rais wetu katika kazi anayofanya ya diplomasia ya uchumi na ya siasa duniani na kwa ushauri wao mzuri mpaka wamefanya Rais wetu katika kipindi cha miezi 13 na nusu ameweza kutangazwa na gazeti pia la *Times* kuwa mmoja wa viongozi mashuhuri katika wale 100. Na inaelezwa katika vyombo vya habari kwamba kwa mara ya mwisho Gazeti la *Times* ambalo lina miaka 99 lilianzishwa mwaka 1923 lilimtangaza Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kuwa kiongozi mashuhuri mwaka 1964 miaka 58 iliyopita, mwaka niliozaliwa mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika kipindi cha miezi 13 na nusu Rais wetu amefanya kazi nzuri sana na mpaka ameonekana duniani anafaa kupata nafasi hiyo. Ni jukumu letu sisi kuwa *proud* na Rais wetu na tuendeleo kumpongeza sana Rais wetu katika eneo hilo.

Ushauri wangu naomba muendeleo kama Wizara kusimamia kwa umakini pia jukumu lenu la kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa, lakini pia muendeleo kuratibu biashara ya kimataifa na diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 ukurasa wa 184 imesitiza kuhusu diplomasia ya siasa na ya uchumi. Tumeona Rais wetu amehudhuria mikutano mingi ya kimataifa na kikanda katika kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kuifungua nchi yetu diplomasia ya kiuchumi. Mimi ushauri wangu naomba wananchi wote tuendeleo kumuunga mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan, Chifu Hangaya kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuiunganisha nchi yetu na mataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu siyo kisiwa, nchi yetu inahitaji kujumuika pamoja na nchi za kimataifa na nchi za kimataifa pia zinahitaji nchi yetu. Hivyo ushauri wangu pia kwa kuwa Rais anatekeleza kwa vitendo kazi zilizoainishwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni muhimu kwa Wizara zingine pia katika majukumu yao ya angalio pia mambo ya diplomasia ya uchumi. Tunafahamu diplomasia ya uchumi tumeipa Wizara hii ndiyo jukumu lake, lakini kuna umuhimu wa sekta zinazoambatana na uzalishaji mali kwa mfano za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, utalii na huduma, nishati na madini, Wizara zake pamoja na Kamati zake zinazozishauri na kuzisimamia Wizara hizi

kuwa na mpango mkakati wa pamoja wa kufanikisha mahitaji ya masoko haya ya nje ambayo Wizara hii inayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii tumewapa Mabalazi na ni kweli wanaifanya kazi hii, lakini bila ushirikiano wa sekta zingine wakileta wateja kwa ajili ya masoko yao tunaweza kukawa kuna ugumu.

Mimi nitawapa mfano mmoja tu mfupi, katika Balozi yetu ya Misri mwaka jana ilitafuta soko la viungo vya ndani kama hiliki, mdalasini, pilipili mtama na kadhalika, angalau tani tano ziwe zinasafirishwa kwenda Misri kwa mwezi. Lakini soko lake lilikuwa taabu sana kupata bidhaa zile, maana yake ni kwamba wazalishaji walikuwa hawajaandaliwa, sekta husika ilikuwa bado haijajiandaa.

Sasa tunaomba sana huo ni mfano mmoja, sisi tumesema katika mifugo tuna ng'ombe milioni 36, sasa tuandae wafugaji wetu wasiwe wachungaji tu, wawe pia wanajiandaa kibiashara kwa ajili ya soko la nje. Lakini pia mazao yetu ya kilimo kama mfano niliyoutolea hapa tuwaandae kifikra, tuwape elimu ya soko hili la nje ili tuhakikishe kwamba wanapozalisha wazalishe kwa masoko ya nje, soko la ndani na soko la nje ili waweze kufahamu taratibu ya masoko ya kikanda na masoko ya kimataifa. Kwa hiyo ni muhimu sana sekta hizi zingine tusichoke kutoa elimu na kuwafunza wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uvuvi pia tuna bahari kubwa, nakumbuka miaka ya nyuma kuna meli zilikamatwa zinazokuja kuvua katika eneo letu la bahari kuu. Hivyo hivyo maana yake ni kwamba tuna samaki wa kutosha katika soko la nje. Kwa hiyo, ni muhimu pia tuangalie eneo hili hapa la uvuvi wa bahari kuu yetu na kuweza kuzungumza vizuri na hao wanaohitaji samaki wetu ili tuweze kupata soko na kuweza kuuza katika soko la kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa mdogo huo wa diplomasia ya uchumi, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, naomba uzingatie ushauri uliotolewa na Wabunge katika maeneo mbalimbali ili muende kuyafanyia kazi na tunaomba mzingatie pia ushauri tulioutoa na Kamati. Tutaendelea kushirikiana na ninyi kuhakikisha tunaisogeza mbele nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mhata.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii mchana huu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu yangu Sokoine na wafanyakazi

wote wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki kikamilifu katika maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nijielekeze katika maeneo matatu; kwanza juu ya diplomasia ya kiuchumi na hususan katika Mkoa wangu wa Mtwara ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu. Pale ndani ya Jimbo la Nanyumbu tunalo Daraja la Umoja, daraja lile ndiyo kiungo kati ya Mkoa wa Mtwara na Msumbiji, ndani ya daraja lile Serikali yetu ya Tanzania imejenga barabara kwa kiwango cha lami hadi pale darajani. Sasa ukivuka lile daraja ndiyo unafika Mji unaoitwa Ngomano, ukivuka lile daraja na kutoka pale Ngomano unakwenda kilometa 300 unakutana na mji unaoitwa Silver Makua. Sasa pale ndiyo kuna njia panda ya kwenda Maputo na huku unakwenda mji mmoja unaitwa Pemba hadi Mtwara kwa upande ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutoka pale Silver Makua kuja hapa Ngomano ni kilometa 300; bahati mbaya sana barabara ile mpaka leo ni ya vumbi. Lakini kulikuwa na makubaliano ya kimsingi kabisa kwamba Tanzania inajenga kwa kiwango cha lami hadi pale darajani na wale wenzetu upande wa pili wajenge kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu sana katika kuifungua nchi yetu na hasa kwenda Msumbiji hadi *South Africa*, mfano mwezi Aprili pale Mtambaswala kituo chetu cha TRA kimekusanya shilingi 1,400,000,000; mwezi wa tatu shilingi 1,200,000,000; mwezi wa pili halikadhalika. Kwa hiyo, kuna mapato mengi ambayo Serikali yetu inakusanya kupitia pale.

Sasa rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri naomba uendelee kufanya mazungumzo na Serikali ya Msumbiji, wafanye jitihada za makusudi kuweza kujenga barabara ile ya kiwango cha lami kutoka pale Silver Makua kuja pale Ngomano ni kilometa 300 tu kwa kufanya hivi ninaimani kabisa nchi yetu itafunguka na wananchi wetu watafanya biashara sana. Kwani hivi sasa hivi ninavyoongea mbao zote ngumu zinapita pale, hii shilingi bilioni 1.5 ni usafirishaji wa mbao, uingizaji wa magari, uingizaji wa mitambo na mambo mengine mengine. Kwa hiyo, kuna mambo mengi mazuri yakifanyika tutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili unahusu masuala mazima ya ukusanyaji wa mapato ndani ya Wizara hii. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaeleza hapa ameeleza mapato mbalimbali ambayo Balozi zetu inakusanya kwamba moja ya chanzo kikubwa ni pango, lakini hata Kamati imeleza vyanzo mbalimbali vya mapato kule Ubalozini na changamoto ambazo Balozi zinakumbana nazo.

Sasa Mheshimiwa Waziri naomba nikushauri; tunalo Shirika letu la Nyumba, Kamati imezungumza tutumie sekta binafsi, tutumie mashirika yetu ya Tanzania yaweze kufanya shughuli hizi. Kwa kusema Serikali ijenge nyumba sasa hivi una Balozi 45 hutaweza Mheshimiwa Waziri. Tunalo Shirika letu la Nyumba, tumefanyiwa semina hapa na Ndugu yetu Msechu

tunauona uwezo wao wa lile shirika, kama tatizo ni sera ni suala la kubadilisha ili shirika nalo likawekeze nje ya nchi. (Makofi)

Kwa kufanya hivi Mheshimiwa Waziri utakuwa umefanya mambo matatu makubwa; kwanza utakuwa umeweza ku-save fedha za kigeni. Tunatumia fedha nyingi za kigeni kupeleka nje ya nchi kila mwezi kwa ajili ya kulipia nyumba za wafanyakazi na Ofisi za Kibalozi. Tukitumia Shirika letu la Nyumba fedha za kigeni hazitatumika badala yake tutaweza kutumia fedha zetu za Tanzania kuilipa *National Housing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine Balozi zetu tukijenga kule Ofisi mfano Paris, Mheshimiwa Waziri unaingiza milioni 400 mpaka 600 kwa mwaka kwa sababu Ubalozzi wetu wa pale pia tumewapangisha baadhi ya Balozi. Halikadhalika tukitumia shirika letu hili litaweza kujenga nyumba, ofisi na kuweza kupangisha Balozi zingine.

Kwa hiyo, ni wakati muafaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri uendelee kutumia shirika letu ili liweze kujenga nyumba zetu kwa kufanya hivyo utaokoa sana. Tumeona mwaka jana hapa miradi ya maendeleo umeshindwa kutumia hata senti tano kwa sababu hukupata fedha na Kamati imezungumza haikutumika hata senti moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mwaka huu umeomba shilingi bilioni nne ni hela ndogo sana, huwezi kujenga, una Balozi 45 na tunategemea kufungua Balozi zingine. Kwa hiyo, lazima tushirikishe sekta binafsi na mashirika yetu ambayo yanajihusisha na masuala ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la watumishi; nimemsikiliza sana Waziri kwamba mwaka jana watumishi wengi walikwenda Balozini, hili jambo nimelipenda sana na utaratibu huu Mheshimiwa Waziri uendelee, kila baada ya miaka minne kama sera inavyosema watumishi wanaokwenda waende na wanaorudi warudi. Ila tunazo changamoto, wale wanaorudi mara nyingi hawabakishwi makao makuu, wanaondolewa na kupelekwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndugu zangu ni Wizara muhimu sana watumishi wake wawekwe katika eneo moja. Haiwezekani mtumishi umemtoa Ubalozini umem-*train*, ana *knowledge* kubwa ya Ubalozzi unafika hapa unampeleka kwenye Halmashauri. Unaenda kumuanzisha upya, unapoteza *resource* kubwa ambayo umeiweka. Sasa lazima hawa watumishi wakifika hapa tusiwaone kama maadui, yaani kuna chuki fulani inajengwa kwamba huyu ameula, ameula nini yeye ni *resource*, lazima huyu tumlee, tumlee ili baada ya muda tumpeleke tena. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo mimi ninaimani kabisa hii diplomasia ya kiuchumi tunayoihubiri hapa itakwenda na itatekelezeka. (Makofi)

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge jioni tutaanza na Mheshimiwa Zahor Haji, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Cosato Chumi na wengine tutawatangaza kama vile idadi inavyoonesha. Hawa ndiyo tutaanza nao jioni ili wajandae ndiyo wanatakiwa waanze kuja mapema humu ndani.

Kwa kweli maneno uliyozungumza Mheshimiwa Mhata ni ya kweli, tuna tatizo Tanzania kuwa na *phobia* ya kuogopa wataalam. Tunalo hili tatizo kubwa sana, mtu akishakuwa na uwezo tu anatupwa sehemu nyingine, tunaogopa mabadiliko. Hata kwenye Wizara zingine hizi za teknolojia watu wengi wenye uwezo wanawekwa pembeni sababu watu hawataki kuacha nafasi zao, wanakaa na elimu zilezile za kizamani, hawataki *changes* ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri linakuhusu sana hili na Mheshimiwa Simbachawene uko hapa litizame, kuna vijana wengi wataalam wazuri sana, *opportunities* nyingi wanakosa sababu watu hawataki kuondoka. Lakini Mheshimiwa Mhata si umeukata upo humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.11 mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Tukae.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha, 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilishataja Waheshimiwa kadhaa kabla hatujasitisha Bunge mchana, naanza na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, ajiandae Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi na naomba nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali lakini hasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba yake kwa umahiri mkubwa sana hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya yeye pamoja na wasaidizi wake, hakika nchi imetulia, nchi imeongeza marafiki, lakini diplomasia yetu inaendelea kukua kwa kuongeza marafiki. Kwa sababu Wizara yako ndio Wizara ya marafiki, ni kazi ngumu sana kutunza marafiki, lakini kwa kweli umewatunza, endelea kuwatunza kwa niaba yetu sisi kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kidogo nikupe pole na nikupe pole kwa sababu unafanya kazi kubwa ya kuleta taswira yetu nzuri nje au duniani huko, lakini bahati mbaya sana kazi yako ni ngumu kwa sababu sisi kama Wabunge hatujafanya kazi yetu ya kukusimamia kuhakikisha unapatiwa uwezo wa kufanya kazi zako kama Wizara. Hakika huu ni wajibu wetu na hakika ni sisi ndio wa kujilaumu kwa sababu tunapoanguka huko kwenye mataifa kwamba hatuiwezeshi Wizara ni kosa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulisema hapa kwamba sisi kama Bunge tunakutana, tunapitisha bajeti nani apewe nini, lakini tunaiacha kwenye eneo fulani ili mmoja aamue kwa *discretion* yake, hii haijaka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Bunge linapofanya maamuzi lichukue nafasi yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali tunapopitisha bajeti, maana yake hatuchezi mchezo wa kitoto hapa, tunafanya kazi *serious* kwa ajii ya Taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba nikupe pole kwa sababu ni kazi ngumu lakini fanya kwa sababu wanasema kazi ngumu mpe Mnyamwezi, *I am not sure* kama wewe ni Mnyamwezi au laa, lakini nikupe hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo naomba sana liko jambo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo nimekusikia Waziri, lakini tumesoma hapa hotuba ya Kamati, kwa miaka miwili mfululizo Wizara hii haijapewa hata senti tano ya maendeleo. Sasa hili pia ni tatizo letu sisi kama Bunge kwa sababu wanasema duniani *nothing is constant*, maana yake ni kwamba *changes* ni kila kitu kinabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningomba basi na niishauri sana Serikali kwamba tunapopanga kama Bunge na wenyewe waione kwamba

Wizara hii ni muhimu ndani na nje kwa sababu ndio inayotuletea marafiki, ndio inatuongezea uchumi, inaongeza imani kwa wawekezaji tuwape nafasi na nyenzo za kuweza kutekeleza mipango yao ya maendeleo. Kama hatutaki waendeleo tuwaambie kaeni msituletee mipango ya maendeleo, lakini haiwezekani tunakaa, tunapanga, tunapitisha, tunaamua halafu *nothing is going on*. Haiwezekani hii, ningepomba sana wenzetu hasa wenzetu wa Wizara ya Fedha mtusikilize Wizara ya Mambo ya Nje ndio kioo chetu duniani. Hakikisheni mnaiwezesha, msiiache kwa sababu ni wataalam hawapendi kupiga kelele mkaona hapana tutaiacha tu kama ilivyo, hakikisheni mnaiwezesha Wizara ili iweze kufanya mambo yake ya mipango ya maendeleo, ni lazima sio *choice*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nichukue nafasi hii kuwaomba wenzetu wa Wizara kwamba tuendeleze diplomasia ya uchumi kwa sababu tunayo maeneo yetu mengi duniani. Mimi nilijaaliwa kuishi India kuanzia mwaka 1992 mpaka mwaka 2000 pale Delhi tulikuwa na kiwanja chetu tumepewa miaka ya 1960, lakini mpaka tunaondoka mwaka 2000 kiwanja kile hakijaguswa na bahati mbaya sana kilichukuliwa wakapewa Ubalazi mwingine, sisi tukaishia patupu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetafutiwa eneo lingine dogo, tumejenga, *simply* kwa sababu hatukuona umuhimu wa kujiendeleza au hatukupata nafasi, Wizara haikutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza viwanja hivi. Ningepomba sana kwa viwanja vya aina hii au kwa nafasi za aina hizi tusidharau kwa sababu juzi tumekwenda Addis Ababa pale viwanja vyetu viwili tumenyang'anywa, sio kwa sababu Wizara haitaki, hapana, lakini kwa sababu utaratibu uliotumika lakini na sisi tumepewa hatukuweza kujiendeleza, hatukuona umuhimu huo. Leo tumerudishiwa lakini ninaamini tukizembea watachukua wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningepomba sana hii ni nafasi yetu ya kukuza mahusiano, lakini na kukuza uchumi kama Taifa. Ningepomba sana tukubaliane, tuwawezeshe wenzetu, lakini maana yake wenzangu wamesema hapa kwamba tuhakikishe basi tunawashirikisha na wenzetu wa ndani, yako mashirika kwa mfano mwenzetu amezungumza *National Housing Corporation* wanaweza wakafanya, lakini ziko benki zinaweza zikafanya, lengo letu *asset* hizi zinajengwa na sisi zinatusaidia sisi, lakini zinajenga Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ningepomba niipongeze Serikali pamoja na jitihada kubwa, lakini bado iendeleo kufanya jitihada kwa sababu hatuwezi tukaishi, hatuwezi tukakuza Wizara ya Mambo ya Nje bila ya kuwaendeleza vijana wetu. Lazima tuwaendeleze kwenye mafunzo kwa maana tuanze kwenye *recruitment*, tuwafunze, lakini tuwa-*place* ili kuwe na kitu kinaitwa *continuity*, bila hivyo Wizara hii itaumia,

inazungumza inajipanga, inatumia nguvu nyingi, lakini haipati nyenzo za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Zahor Mjumbe wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kumtambua Balozi Ahmed Djellah, Balozi wa Algeria na kama hayupo basi *Hansard* itatambua kuwa ametambulishwa rasmi kwenye Bunge letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Hassan King hayupo, Mheshimiwa Riziki Lulida, ajiandae Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia nan kutupatia afya njema tukawepo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuitangaza Tanzania katika kuongeza diplomasia ya Kimataifa na sasa hivi naona hali ya Tanzania kutambulika katika Umoja wa Mataifa na duniani inakuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Mheshimiwa Waziri Mama Mulamula, Balozi Mbarouk - Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. Hii timu yote ilikuwa katika Balozi mbalimbali, kufanya kazi kwao hapa ina maana wamekuja kutuongezea uwezo na juhudi walizozipata, maarifa waliyoyapata ili kutuongezea na sisi kuweza kufanya kazi vizuri katika hii Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge ni mhimili kama mihimili mingine ambayo ni Mahakama na Serikali Kuu na sisi tunapenda watambue kama mhimili wa Bunge lazima utambulike katika masuala ya kimataifa. Kunafanyika mikutano mbalimbali na maazimio mbalimbali ya Umoja wa Mataifa, ya *Commonwealth*, kuna *summit* mbalimbali lakini bahati mbaya muda mrefu hatujapata mrejesho. Nitoe mfano katika Umoja wa Mataifa kuna maazimio kila mwaka yanapitiwa iwe maazimio ya usalama, maazimio ya haki za binadamu ikiwemo walemavu, haki za wanawake, haki za watoto, haki za vijana na maazimio mengine ya Umoja wa Mataifa kuhusu *United Nations for Climate Change*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maazimio yale yote hayafiki Bungeni tukayafanyia kazi. Hivyo Wabunge wengi wanapata taarifa zao aidha wasome katika mitandao, lakini je, utaitegemea mitandao wakati saa nyingine katika mitandao kuna taarifa ambazo sio za kawaida, ni *fake news*. Hivyo tunaamini kabisa wao kukaa kule walete yale maazimio yaliyotoka kule

ili yaje katika mhimili wa Bunge, katika kuleta katika mhimili wa Bunge, Bunge itaifanyia kazi na ikiifanyia kazi sheria ile itakuwa inawasaidia kwenda chini. (Makofi)

Mheshiwa Naibu Spika, nataka ni-*declare interest* mimi ni mlemavu, lakini ulemavu wangu sio wa kuzaliwa ni wa kupata ajali ya gari. Tuna maazimio yanapita kila mwaka katika Umoja wa Mataifa, lakini kutokana na Bunge halipati taarifa za watu wenye ulemavu tunapata taabu sana ushiriki wetu katika mikutano ya Umoja wa Mataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano leo ukitaka kwenda kuhudhuria mkutano ule wanaleta mlolongo lazima upitie Wizara ya Sera, Kazi, Ajira na kama Waziri haendi basi ina maana watu wengine hata taasisi zingine iwe SHIVYAWATA, CHAWATA watu ambao inabidi nao wakashiriki katika Mikutano ile jibu wanakuambia kwa vile Waziri haendi na ninyi wengine mnakosa fursa, hii kitu lazima muirekebishe.

Nishukuru jana nilikutana na Naibu Katibu Mkuu kwa kweli inabidi nimpongeze Mama Fatma nafikiri ni mama ambaye ana uelewa mkubwa na kutokana na uzoefu aliokuwa nao, amenifariji sana na amefanya kazi ya ziada kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinafanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Umoja wa Mataifa ndio sisi ni wanachama Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na kama ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, sheria na maazimio yale yakifika huku kwetu yanateremka mpaka chini kwa ajili ya kufanyia kazi na kujua haki zao ni nini. Lakini matokeo yake hivi vitu vinapuuziwa huu ni mwaka wa tano Tanzania hatujashiriki katika Mikutano wa Umoja wa Mataifa wa Watu Wenye Ulemavu. Matokeo yake kama wao hawaendi na huku chini kote watu wanashindwa kufanya kazi. Vyama vya watu wenye ulemavu havihudhuria kwa ajili ya urasimu ambao umewekwa na nataka nitambue tena, Bunge ni mhimili, hatutaki tena mpitie mlolongo mingine pelekeni *direct* katika Bunge, Spika apokee taarifa zetu na azifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo itakuwa tunapata taabu, ndani ya Bunge kuna Kamati hizi Kamati inabidi zitumike kwa kupitia mhimili wa Bunge. Kwa mfano, kunapita Mikutano ya Umoja wa Mataifa kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi (*United Nations for Climate Change*), lakini Wabunge hawahudhuria wala Kamati haijui chochote, sasa matokeo yake unajiuliza sisi tumekaa hapa kufanya kazi gani, tunakuja hapa kufanya kazi na wenzetu duniani wanafanya nini. Mwaka 2007 tumekwenda kuridhia haki za wenye ulemavu katika Umoja wa Mataifa Watanzania tulikuwa watano, Kenya alikuja mtu mmoja lakini nimekwenda tena mwaka 2016 Wakenya wako 80. Hivi vitu msivone kama ni vya kawaida vinaturudisha nyuma kiupeo wa maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapohudhuria Mkutano ule sio unahudhuria kwa ajili ya wale mavu kuna masuala ya uchumi, kuna masuala ya ajira, kuna masuala ya elimu, kuna masuala mbalimbali ya maendeleo ambayo sisi tunayakosa tuko katika kisiwa ambacho kinabidi kisiwa hiki kiongezwe kiweze kufanya kazi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabalozi nimelizungumzia karibu mara mbili kila Balozi ajitathmini katika Balozi zake je, niko hapa kwa kufanya kazi gani? Kazi ya kwanza ya Balozi kuiangalia Tanzania inanufaika vipi na kilimo, inanufaika vipi na uchumi wake na kuitangaza pale na pawepo na ma-desk maalum ya kuitangaza. Nilikuwa nazungumza mimi nakwenda pale New York lakini unakuta desk la utalii halina kazi maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama ameipeleka *royal tour* duniani je, kama *ma-desk* haya hayafanyi kazi hizi *royal tour* hazitakuwa-*sustainable* kabisa, hatutaweza kufanya kazi. Ni lazima wajitambue kama wako pale kuisimamia nchi ya Tanzania iweze kuondokana na umaskini twende katika uchumi na uchumi ni *ku-share resource* baina ya wenzetu na sisi. Kama watakaa pale hawajitathmini basi haina haja yakuwapeleka watu ambao hawana nafasi katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la mjusi narudia tena. Mjusi *Dinosaur* ni haki ambalo lipo Ujerumani sitaliacha hili mpaka ufafanuzi upatikane, ule ni uchumi na kama uchumi ule wa *Dinosaur* ambaye yuko Ujerumani Lindi hatufaidiki na chochote. Si hivyo tu mwanzo nikafikiri ni nchi kumbe ni kikundi/taasisi kimechukua lile *Dinosaur* wanafanya biashara, wanafanya uchumi mkubwa kuhusu *Dinosaur* lile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jiulize mapato yanayopatikana ndani ya Serikali ni yapi; tuna *royalty* gani ndani ya Serikali ni yapi; je, Balozi wetu ambaye yupo Ujerumani anatuambia nini anatupa ripoti gani kuhusu mafanikio ya mjusi wanayoyapata wale vs nchi yangu, mkoa wangu na Lindi yetu nayo ifaidike na mjusi. Haiwezekani, maana yake sasa hivi taarifa tulizokuwa nazo mijusi yote mikubwa sita au *Dinosaur* makubwa sita yanatoka mkoa wa Lindi, ndege wakubwa 13 wanatoka Mkoa wa Lindi, lakini mpaka sasa hivi pamekaa kimya hakuna ripoti hakuna nini tunapeana tu kila mmoja anajiona mimi kama ni Wizara... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, ahsante.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, Maliasili haina miliki ya peke yake ni Wizara ya Elimu na Wizara zingine na Wabunge vilevile tuna haki ya kupambana na mjusi na haki zetu zifanikiwe. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante, sasa namuita Mheshimiwa Chumi.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naunga mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ajiandae Mheshimiwa Fakharia Shomar, ajiandae Mheshimiwa Ighondo.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ambayo pia mimi ni mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema lolote kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake pamoja na maafisa wote ambao kwa namna moja au nyingine wameshiriki katika kufanikisha hotuba hii ya bajeti. Lakini pia wanafanya kazi nzuri sana ya kupokea wageni, ya kuratibu ziara za Mheshimiwa Rais na viongozi mbalimbali katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi niseme jambo moja nimeona katika michango yetu baadhi yetu Wabunge na mimi kama Mbunge, lakini hasa kama Mjumbe wa Kamati ningependa kuliweka sawa kwa sababu wananchi wanatusikia sasa tusije tukaenda nje ya mjadala katika suala zima la uraia pacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana tukaelewa kama Wabunge kwamba suala la uraia pacha pamoja na kuwa ni jambo la Kikatiba, lakini jambo linalokuja kwenye masuala ya uraia Wizara inayohusika ni Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, tusije tukawabebesha mzigo Wizara ya Mambo ya Nje katika jambo hili ambalo kwa kweli tumeshalisema mara nyingi lakini bado linarudi kule kule kwamba ni suala la Kikatiba lakini ni suala la Wizara ya Mambo ya Ndani kama linaamua kufanyiwa kazi katika mifumo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja, nimelisema hili mara kadhaa jinsi ambavyo anakuwa mwanadiplomasia namba moja kwa vitendo na kuitangaza diplomasia yetu ya uchumi. Tunaposema diplomasia ya uchumi maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba vile ambavyo tunaweza, tukatumia mbinu zote za kidiplomasia kama Taifa katika kutafuta maslahi mapana ya Kitaifa kama vile kutafuta wawekezaji, kama vile kufungua fursa za kibiashara, kama vile kutafuta masoko ya bidhaa zetu. Kwa mfano, sisi tunaotoka Iringa na Njombe tumeona kabisa kwamba tumefungua fursa za mazao kama vile mazao ya misitu lakini pia na zao la parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo ni kazi kubwa sana inayofanywa na mwanadiplomasia namba moja ambaye ni Rais wetu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassan, lakini pia kuvutia wawekezaji na mimi ninasema haya ni mmoja wa wanufaika wa diplomasia hii ya uchumi ambao Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja anaitendea haki. Sisi katika Jimbo la Mafinga tuna wawekezaji wengi ambao wamekuja kutokana na Taifa letu kutangazwa kupitia hii diplomasia ya kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu kupitia mwanadiplomasia namba moja kama Taifa pia tunanufaika, tunapata mikopo ya riba nafuu, yako maeneo tunapata misaada au kama *grants* lakini pia tunapata fursa za kimasomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa uniruhusu nitoe mfano, sisi watu wa Iringa tukiongozwa na Mheshimiwa William Lukuvi kwa miaka mingi sana tumesema kuhusu barabara ya kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park*, hivi juzi tumeona Benki ya Dunia imetoa mkopo wa riba nafuu wa triloni 1.2 ambao mkopo huu sio tu kwamba utatunufaisha sisi watu wa Iringa kwa kujenga barabara ile ya kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park*, lakini pia yako maeneo yatakayonufaika na ungeniruhusu niyataje machache kuonesha jinsi ambavyo mwanadiplomasia namba moja kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje kazi inavyofanyika inatuletea manufaa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo huu wa triloni 1.2 kutoka Benki ya Dunia, pamoja na mambo mengine utaenda kujenga barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi ya urefu wa kilometa 201; utajenga barabara ya Rusahunga – Rusumo kilometa 92; utajenga barabara ya Songea – Rutukila kilometa 111; lakini pia utaenda kujenga hiyo barabara ya Iringa kwenda *Ruaha National Park* pamoja na kujenga viwanja vya ndege vya *Lake Manyara*, Iringa na Tanga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ndio maana halisi ya diplomasia ya uchumi kwamba, kupitia ziara hizi mbalimbali, kupitia makubaliano mbalimbali tunafungua fursa za kibiashara, lakini pia fursa za kimikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Mheshimiwa Rais alipoenda *Dubai Expo 2020* kule, tumeona mikataba na hati za makubaliano 37 zilisainiwa ambazo pamoja na mambo mengine zitaendelea kufungua hizo fursa na hapa mimi kama zao la Wizara ya Mambo ya Nje nipate kupata ufafanuzi kidogo kwamba tunaposema hati na makubaliano watu wengine walikuwa wanajaribu kubeza kwamba hayo si ni makubaliano tu, kumbe katika nyanja ya kidiplomasia huwezi kufanya jambo lolote kabla kwanza hujafanya makubaliano yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana nitumie nafasi hii kupongeza Ubalozi wa Abudhabi pamoja na Dubai kwa kushirikiana na watendaji wa

Serikali kufanikisha maonesho hayo ya *Dubai Expo*, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza Balozi Mbelwa Kairuki ambaye kupitia majadiliano na makubaliano mbalimbali Taifa letu limekubaliwa kuingiza muhogo na soya katika soko la China. Huwezi tu ukaingiza hizo bidhaa bila kufanya makubaliano mbalimbali, yote haya yanatokana na kazi nzuri inayofanywa katika dilpomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu pia kupongeza kwa kufunguliwa Ubalozi wa Lubumbashi, nakumbuka toka nimekuwa Mbunge hapa mwaka 2016 na wewe ukiwa Mwenyekiti wetu kuanzia kwenye Kamati, tumeshauri sana na hatimaye Ubalozi mdogo Lubumbashi umefunguliwa. Hii ni manufaa kwetu ikiwemo watu wa Iringa ambao pale Lubumbashi kwenye mpaka wa Mokambo zaidi ya malori 400 kwa siku yanaingia katika nchi ya Congo. Kwa hiyo, tumefungua masoko mbao zetu kutoka Mafinga zimepata soko Lubumbashi. Na sasahivi DRC imekuwa sehemu ya Afrika Mashariki, tuna imani kwamba, tutaendelea kunufaika na soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nitoe ushauri, kazi yetu ni pamoja na kushauri; pamoja na changamoto za kidunia baadhi yetu wamesema iko sasa sababu ya kufikiria kama Serikali na mifumo mingine ya Kiserikali kuona umuhimu wa kufungua ubalozi katika nchi ya Iran. Iran imepiga hatua sana katika suala la *textile industry* na sisi hapa tunalima pamba, tunaweza tukajikuta kwamba tunafungua fursa sio tu za kibiashara, lakini pia fursa za kugawana uzoefu katika eneo kubwa la viwanda, hasa hususan viwanda vya nguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili; niishauri sana Wizara mambo mengi tukitaka tufanikiwe tupitie zile tume za ushirikiano za pamoja kwa maana ya kwamba tume za kudumu kwa maana ya zile *JPC*. Kupitia hizi mambo mengi yatanufaisha nchi yetu na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu; kama Wizara ningeshauri sana Wizara *i-take lead* katika kuhakikisha kwamba kama Taifa tunanufaika na mifuko mbalimbali katika dunia inayotoa fedha katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alishiriki kule Glasgow kwenye mkutano wa mazingira na aliwaambia wakubwa wa dunia ambao kwa sehemu kubwa wanaongoza katika kuchafua mazingira kwamba waheshimu zile ahadi zao na kwa uchache nitaje, kuna mifuko kama *Green Climate Fund*, *Africa Climate Change Fund* ambao uko chini ya Benki ya Maendeleo ya Afrika, kuna *Adaptation Fund*, kuna mifuko kama *Climate Investment Fund*, na kadhalika iko mifuko mingi.

Kwa hiyo, niombe Wizara, Rais wetu ameshiriki kule kikamilifu na kwa kweli alikuwa ni miongoni mwa viongozi waliohutubia. Sasa Wizara itusaidie

katika kuratibu kama Taifa tunaweza tukanufaika vipi na fedha hizi za mifuko ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Iringa, watu wa Mafinga, watu wa Njombe, tunalima, kwa mfano mwaka huu kutokana na matatizo ya mvua tutaelekeza kilimo chetu kwenye kilimo cha mabondeni, kilimo cha vinyungu kwa hiyo, tuginufaika na mifuko hii itakuwa ni fursa kwetu nzuri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chumi kwa mchango mzuri.

MHE. DAVID C. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja na kama kawaida nasema Mungu atubariki sote na Taifa letu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Chumi. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, ajiandae Mheshimiwa Ighondo.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budin kumshukuru Mwenyezi Mungu aza *wajaalah* kwa kunijalia uhai na uzima na leo kuwa mbele ya Bunge hili. Vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wao wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nizungumzie kidogo kuhusu hii Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ishirikiane na Wizara ya Utalii wakati sisi tuna Balozi ambao Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje waweze kufanikisha kuleta watalii kwa wingi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi aliyoifanya Mheshimiwa Mama Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutembelea vivutio vyote vya kiutalii vya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar hii kazi iwe sio ya bure, ametengeneza filamu ya *royal tour* na ile filamu inatakiwa itekelezwe na watekelezaji wetu ni mabalozi wetu kwa kuweza kutuletea watalii kwa wingi, kazi ya mama isiwe ya bure iwe kazi ya mama inafaa, yeye kaona maono kutuanzisha sisi nini tufanye. Sasa suala hili Wizara mlikamate, mshirikiane na mabalozi kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la Sera ya Mambo ya Nchi za Nje. Mheshimiwa Waziri ameeleza uzuri katika ukurasa wake wa saba na tunashukuru kwamba, ilikuwa siku nyingi imekaa kwa sababu, hii sera ndio itazidi kuwa chachu ya diplomasia ya kiuchumi. Kwa sababu sera ikifanya kazi sambamba na diplomasia ya kiuchumi ikaenda pamoja ina maana wakulima, wafanyabiashara, bidhaa zetu zinatoka mashambani, usafirishaji wa bidhaa pamoja na masoko ya nje yataweza kupatikana na tutanufaika

na tutaondokana na umasikini. Nafikiri na hilo mliangalie, lakini kuliangalia vipi, mtoe elimu kwa wafanyabiashara, mtoe elimu kwa wakulima maana maparachichi yanalimwa, tunalima vitu vingi Tanzania na vina soko nje, lakini bila kumpa mtu elimu atalima na kisha yatajaa Kariakoo tele yamerundikwa pale chini, bila ya kufanya kazi hataweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukarabati wa Balozi zetu. Balozi zetu kwa kweli kuzikarabati kama Wizara si rahisi maana yake nyingi chakavu, kwingine hakuna, kwingine hazikaliki, nyumba za mabalozi, nyumba za wafanyakazi na ofisi za ubalozi, lakini jambo lililokuwepo tunaweza tukafanya awamu kwa awamu na tukazishirikisha taasisi za kiuchumi na wanakubali. Kama kuna sheria inapinga leteni Bungeni, tuteeni ushauri ili hizi ofisi, itakuwa kila siku tunaimba, tunasema, tunapiga kelele, utekelezaji hauonekani. Sasa tubuni mbinu, mbuni mbinu, ili hizi balozi ziweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mfano mimi nilikwenda ziara Congo, Kinshasa, tumeona nyumba ya Balozi haina hadhi ya kibalozi. Ofisi yao haina hadhi, ingawa zimekarabatiwa, lakini itakuwa ndio hapo kwa hapo tu, lakini wamejiongeza kwa sababu ule mtaa waliokuwepo Mtaa wa Gombe, *prime area* na nafasi wanayo kubwa ambayo *plot* yao nafikiri namba 912 tatizo lililokuwepo walivyojiongeza, makisio wamefanya tayari, lakini hata wakifanya makisio wakati Wizara hamjawapelekea pesa wafanye nini? Hawawezi kufika kokote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wametuonesha hilo jumba wanalotaka, maana yake la kiuchumi, mtakuwa na ofisi, nyumba, watakodisha watapata wao na itanufaika Tanzania na sifa itakuja Tanzania. Sasa hizi hii awamu kwa awamu lazima hizi ofisi muwe mnaziangalia ili Tanzania nayo iwe katika maajabu katika mabalozi yao. Sio niwe Tanzania Balozi inaonekana ya kizamani, hilo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi jumuiya ya kikanda na masoko; hii Mheshimiwa tulipewa semina sisi hivi juzi tukaelezewa kwa kweli, mafanikio tumeyaona, lakini nawaomba hii semina wapewe na Wabunge wote kwa sababu kila mmoja akipata kwa sababu sasa hivi uzalishaji mzuri tu, masoko yako na isitoshe njia zi wazi, Tanzania tunauza sana, lakini watu hawajui. Elimu itolewe na Wabunge pia wafanyiwe semina ili na wao wawe ni mabalozi watakaotoka nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ighondo, ajiandae Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia na mimi fursa ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini pia kwa usikivu mkubwa sana, Waziri huyu amekuwa msikivu pamoja na Naibu wake, tunapokuwa na changamoto mbalimbali kwa kweli huwa wanatusikiliza kwenye Kamati na hata nje ya Kamati na mimi naendelea kuwaomba kwamba, tabia hiyo waiendeleze wasibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nichukue pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi yake nzuri anayofanya katika kuitangaza nchi yetu kimataifa na lazima tukubali kwamba Tanzania sio kisiwa, nchi yetu sio kisiwa kwa hiyo, lazima tu-*interact*, lazima tujue fursa zinazopatikana nje ya nchi yetu na lazima tuzichangamkie. Kwa hiyo, Rais wetu anapofanya juhudi hizi za kwenda huku na kule lazima tumtie moyo na lazima tumuunge mkono. Na kimsingi kwa yeye ambaye ndio tunasema ndio *first diplomat* yale anayoyafanya kule watendaji lazima wayachukue na wayatafsiri katika maisha na katika mazingira ya nchi yetu na fursa zinazopatikana kule lazima wazitafsiri katika mazingira halisi ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa lazima twende mbali kidogo, mimi nilikuwa nataka nijikite kidogo kuelezea faida tunazozipata ama ambazo tumeshazipata kama nchi kufuatia ziara alizofanya Mheshimiwa Rais wetu nje ya nchi na hapa nilitaka pia niombe jambo moja, Waziri labda atakapo-*wind up* atanisaidia, pale tunaposema mama yetu, tunapomtambua Mheshimiwa Rais kama mama, *yes I real appreciate she is our mother*, ndio mama yetu, ni mlezi wetu, lakini kama kiongozi wa nchi nilikuwa najaribu kujiliza mwenyewe kwa nini tusimuite Mheshimiwa Rais wa nchi au Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuitofautishe na mama; ndio ni mama kwa kuwa ni mama yetu ni mlezi wetu, lakini tumtambue kwamba ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nitaomba hili kidiplomasia ikiwezekana Mheshimiwa Waziri hapa atupe muongozo sahihi. Ni mama yetu, Mheshimiwa Rais wetu anapenda tumtambue kama mama, lakini kimamlaka imekaaje? Kwa nini tusitambue kwamba huyu ni Mheshimiwa Rais kwa *title* yake kama Rais kwa nafasi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli mfano Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje wewe ni mama, tuseme mama yetu Waziri wa Mambo ya Nje? Mimi nadhani tumtambue Mheshimiwa Rais kwa nafasi yake ya Urais. Tuiheshimu ile mamlaka aliyonayo kama mkuu wa taasisi ya Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikizungumzia kwa uchache faida ambazo nchi imepata kufuatia ziara za Mheshimiwa Rais nje ya nchi; kwanza tumepata miradi mingi sana ya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali, kwenye sekta mbalimbali. Tumepata miradi mingi kwenye sekta ya afya, kwenye sekta ya kilimo, kwenye maji, kwenye elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tumeona tumepata vyumba vya madarasa zaidi ya 15,000 nchi nzima. Haya yalikuwa ni matokeo ya ziara za Mheshimiwa Rais alipokwenda kutembelea nje ya nchi yetu ama kutembea nje ya nchi yetu, lakini pia tumepata wawekezaji kwenye sekta mbalimbali waliokuja nchini baada ya Mheshimiwa Rais kwenda wameona fursa ambazo nchi yetu inazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi utalii umeongezeka, watalii wameongezeka na tunafahamu sekta ya utalii inavyoingizia nchi yetu kipato au pato lililotokana na watalii ni fedha nyingi tunazopata kwa hiyo, lazima tuendeleo kuyatafsiri mambo haya katika mazingira halisi sasa ya Kitanzania, ili watu waone umuhimu wa ziara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumepata mikopo ya riba nafuu kutoka nje ya nchi, lakini pia kufungua mahusiano ya kidiplomasia ya nchi yetu na nchi nyingine. Tunafahamu hapa katikati mambo yalikuwa magumu kidogo, lakini sasa hivi tunaona mahusiano yalivyokuwa mazuri, tunapata wageni, tunapata wawekezaji, *diplomatically* nchi yetu sasa hivi iko vizuri kiuchumi na hata kijamii. Kwa hiyo, lazima tuyathamini mambo haya na tuendeleo kuyasema na tuendeleo kumpa moyo Mheshimiwa Rais katika ziara hizi anazozifanya na watendaji sasa wayachukue mambo haya, wayatafsiri katika mazingira yah uku chini ili wananchi waendeleo ku-support na kuelewa haya mambo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na moja ya fedha za miradi ambazo tumezipata, ametangulia kusema Mheshimiwa chumi hapa, kuna fedha ambazo tumezipata zinaelekezwa kwenye miradi mahususi. Mathalani zile ambazo zinakwenda kujenga, kuna fedha hizi ambazo tumepata Euro milioni 450 sawa na shilingi za Kitanzania trilioni 1.17 zinazotoka Umoja wa Ulaya. Fedha hizi zinakwenda kwenye kutekeleza ujenzi wa viwanja mbalimbali vya ndege hapa nchini, kuboresha hata ule uwanja wetu wa ndege wa kimataifa wa *Julius Kambarage Nyerere - Terminal II* pale, uwanja wa Kigoma wa ndege, uwanja wa Shinyanga na vingine nchini. Kwa hiyo, vitu hivi tusipovieleza hapa haya anayoyafanya mama hayawezi kueleweka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hili ambalo ni la hizi barabara, kuna barabara kubwa nne ambazo zinaenda kuboreshwa; kuna barabara hii ya Iringa – Msembe kilometa 104; kuna barabara ya Songea – Rutukila

kilometa 111; barabara ya Rusahunga – Rusumo kilometa 92; kuna barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi kilometa 201. Hizi fedha ni nyingi na hizi barabara ni muhimu kwa uchumi wan chi yetu, hatuwezi kuzungumza uchumi kama hatuna miundombinu mizuri ya barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilifikiri niliseme hili ili hasa watendaji wa Wizara na hata...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ighondo ahsante, kengele ya pili.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, japo muda umekuwa mdogo, lakini na viwanja vyetu vilivyoko nje ya nchi huko viendeleo kujengwa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Askofu Gwajima, ajiandae Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda na ajiandae Mheshimiwa Condester Michael Sichelwe.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa muda ili nichangie na mimi hii hoja ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Kwanza nikushukuru wewe, lakini pia nimshukuru dada yangu Balozi Liberata Lutageruka Mulamula kwa namna alivyo-present hoja yake vizuri kwa ufupi na kwa namna ya kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita hasa kwenye suala la uraia pacha; nimeona suala la uraia pacha limeongelewa na watu wengi sana na limekuwa suala la muda mrefu sana. Kwanza nataka nioneshe kwamba uraia pacha duniani siyo issue ngeni, nazitaja kwa ufupi nchi ambazo zinaruhusu uraia pacha; ya kwanza ni Marekani yenyewe, Pakistan, Nigeria, Brazil, Bangladesh, Russia, Mexico, Egypt, Uturuki, Ujerumani, United Kingdom, Ufaransa naweza kuzitaja ni zaidi ya nchi 70 na kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuna zingine zimeenda mbali zaidi kama Finland pamoja na Ufaransa wenyewe wameruhusu mpaka *multiple* maana yake mtu anakuwa na uraia zaidi ya tatu au nne. Sasa siyo issue ngeni duniani kwa sababu zaidi ya nchi 70 na kitu zinakubali suala la uraia pacha. Pamoja na *presentation* nzuri ya dada yangu Balozi Mulamula, lakini nimekuwa *disappointed* sana kwa jinsi ambavyo kwenye hotuba yake hakutaja kabisa kwa habari ya uraia pacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bunge lililopita tulilizungumza sana kwamba kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zetu walio ughaibuni ni muhimu sana ku-consider uraia pacha, lakini kwenye hotuba yake hakuzungumzia kabisa

kabisa. Kwa hiyo, nataka nimtangulizie dada yangu Balozi Mulamula nisipopata maelezo mazuri kwenye majumuisho yake ninalo kusudio la kukamata shilingi kwenye mshahara wake, nikipata maelekezo mazuri of course nita-withdraw.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nimeona amelikumbuka kwenye hotuba yake ukurasa wa 83 amekubali kwamba kuna *remittances* kwa maana ya walio ughaibuni *diaspora* wame-transfer fedha kuja Tanzania mwaka 2020 *almost* dola milioni 400 na amesema mwaka 2021 wame-transfer fedha dola milioni 569.3; hizi pesa zimetoka ughaibuni au *diaspora* kuja hapa Tanzania zikiletwa na ndugu zetu walio ughaibuni. (Makofi)

Pia kwenye hotuba yake hiyo ukurasa wa 83 amesema kwamba hawa ndugu zetu wa diaspora pia wamenunua nyumba *National Housing* zenye thamani ya bilioni 2.3 na ameongeza pia wame-invest kwenye *Hamidu City Park* kule Kigamboni. Kwa hiyo, ametambua kabisa mchango wa watu wa diaspora na fedha au *remittances* ambazo zimetoka ughaibuni kuja hapa Tanzania, lakini namshangaa kwa nini sasa hajaona umuhimu wa kuwaza uraia pacha kwa hawa mabwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya Uraia Sura Na. 357 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 inatambua uraia wa aina tatu; uraia aina ya kwanza ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia tajinisi. Sasa uraia wa kurithi ni ule ambao mzazi mmoja ni raia wa Tanzania akizaa mtoto anapewa uraia; uraia tajinisi ni uraia wa kuomba *basically* mtu anaomba uraia sawa sawa na *criteria* ya nchi yetu anapewa uraia na uraia wa kuzaliwa ni zawadi ambayo mtu anayoipata kutoka kwa Mungu, hakuna mtu anaweza kuzaliwa nchi mbili kwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza mimi kwa habari ya uraia pacha nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Mulamula pamoja na wenzako wale Watanzania waliokwenda ughaibuni kutafuta Maisha, mtu amekwenda kusoma, amezaliwa Tannzaia ni Mndendeule, ni Mdigo, ni Mgogo, ni Mpare, ni Mnyaturu akaenda kubangaiza maisha kule na kwenye harakati ya kubangaiza maisha kuna baadhi ya nchi zinaweza wa kutambua *brain* za watu wetu, anafanya vizuri *Ph.D* wanaangalia *dissertation* yake wanamuona mtu ubongo wake unafaa kutumikia nchi zao, wanawapa uraia, wanabaki kule siyo kwa sababu wanawapenda ili kusudi ile bongo yao itumike kwa ajili ya kuendeleza nchi zao. (Makofi)

Kwa hiyo, sisi kila mwaka na kila wakati tunakuwa tunawapoteza watu hawa kwa kuweka *restrictions* kwamba hatuwahitaji kuwa raia hawahitaji kuwa raia wa nchi zetu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Askofu Gwajima amesema vizuri kuhusu raia wa kurithi, hao raia wa kurithi wakikutana wakaoana huyu raia wa kurithi na huyu raia wa kurithi, wakizaa watoto wanakuwa ni watoto ambao hawana nchi yaani *stateless individuals*. Kwa hiyo *its even worth* na naungana mkono na hoja yako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hoja ya Mheshimiwa Salome.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo tunakosa mambo ya muhimu sana, kwa mfano Taifa la Israel mwaka 1948 baada ya Wayahudi kuwa wamerudi kutoka kwenye nchi walizokuwa wametawanyika kila Myahudi alirudi na *skills* za nchi aliyokuwa, matokeo yake Taifa hilo limeendelea sana kiteknolojia kwa sababu kila mtu alikuwa alirudi na maarifa au *skill* alizokuwa nazo. Kwa kuwapa watu wetu uraia pacha tunapata faida kadha wa kadha mojawapo ni *skill transfer*, mtu anakuwa kwenye ile nchi aliyokuwa amekaa ame-*acquire skills* fulani, anaporudi nchini kama raia wa Tanzania tunaweza ku-*tap* hiyo *skill* na kuitumia kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo tunapata tunapata *freight capital*, kuna baadhi ya Watanzania wamekaa kwenye nchi za kigeni wamefanya vizuri sana kiuchumi. Mimi nilikuwa kule *North Caroline* nikamkuta Mtanzania mmoja Mnyaturu wa kwetu kule Singida anamiliki *University* kubwa kama ile *University of Dar es Salaam*, ni Mtanzania; nilikuwa kule Canada wakati fulani nilikuta Watanzania watatu ni sehemu ya Baraza la Mawaziri katika Serikali ya Canada. (Makofi)

Sasa watu kama hawa tukiruhusu uraia pacha tunaweza ku-*tap skills* na ku-*transfer capital* kutoka kwao na tukapata hatua ya nchi yetu kuipeleka mbele zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini faida nyingine kwa kuwanyima uraia pacha tumewatenga na familia zao, ni masikitiko sana unapofika kwenye ubalozi zetu mahala pengine unawakuta wamejipanga kuomba *visa* ukimsemesha anaongea kindendeule, mwanamke ni Mndendeule, mwanaume ni Mndendeule, watoto Wandendeule wanaomba *visa* kuja kwenye nchi yao Tanzania, *it doesn't make any sense...*

31 MEI, 2022

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Gwajima, kengele ya pili hiyo.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kidogo, kwa hiyo kwa sababu hiyo, nilikuwa naomba kama itakupendeza tujitahidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni *human resource*; nchi yetu ina *natural resources* nyingi sana, lakini *natural resources* ili uzigeuze ziwe hospitali uzigeuze ziwe shule inahitaji *human resource* ya watu hawa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gwajima mengine unaruhusiwa kuleta kwa maandishi.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini nisipojibiwa vizuri nitaondoa shilingi, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ng'enda, ajiandae Mheshimiwa Sichelwe.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na pia nakushukuru wewe kiongozi wangu kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika Bunge lako kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wengine wote wakiwemo Mabalizi wetu ambao wanatuwakilisha katika nchi mbalimbali. Ninaamua kuwapongeza kwa sababu hivi karibuni kulikuwa na kongamano la biashara la nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika, Mheshimiwa Waziri uliwaruhusu Mabalizi wako wakaja kushiriki katika kongamano lile ambalo kwa sehemu kubwa lilikuwa linazungumza diplomasia ya uchumi, kwa hiyo nakupongeza sana wewe pamoja na Mabalizi wote wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imepita katika vipindi tofauti katika Sera zetu za mambo ya nje mtakumbuka mara baada ya uhuru sera yetu ya mambo ya nje hasa ilijielekeza katika ukombozi wa nchi za Afrika na baada ya hapo sera yetu ikajielekeza katika kuunda Umoja wa Afrika tukaanza na OAU baadaye kuja na AU na katika miaka ya 1990 tulipojielekeza katika sera za uchumi sasa ndiyo tukaanza kutazama diplomasia ya uchumi katika nchi za Afrika na hata nchi za Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba sasa hivi dunia inazungumza uhusiano wa kimataifa ikiweka uchumi mbele

na sisi kama Watanzania na hasa kwa sababu tunazo changamoto nyingi za kiuchumi zinazohitaji maendeleo ya watu wetu ni lazima diplomasia ya uchumi ipewe nafasi ya kwanza kabisa kuliko mambo mengine yote na hili naona Mheshimiwa Rais amelielewa na analisimamia vizuri na ndiyo maana utamuona yuko katika shughuli mbalimbali, anakwenda Dubai huko, zote zile ni kuhangaika na shughuli za diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo ambalo linanisikitisha sana ni kuona kwamba tunakwenda kuhangaika na mambo ya mbali na yaliyo karibu tunayaacha. Hivi karibuni *East African Business Council* (Baraza la Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki) lilitoa ripoti yake, katika ripoti hiyo imeonesha mwaka 2018 nchi jirani yetu DRC ilifanya biashara ya kuingiza bidhaa mbalimbali nchini kwao zenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 7.4; mwaka 2019 wamefanya biashara ya kuingiza nchini mwao bidhaa mbalimbali zenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 6.7; hizi ni fedha nyingi sana, lakini tujjulize sisi tunaohangaika na diplomasia ya uchumi katika kuingiza bidhaa hizo sisi kama Tanzania tumeingiza kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hiyo ya Baraza hili la biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inasema China imekuwa nchi ya kwanza ambayo imeingiza bidhaa kwa 31.9%; *South Africa* imekuwa nchi ya pili 16%; Zambia imekuwa nchi ya tatu 13.32%; Kenya imekuwa nchi ya nne, sisi tuko kama nchi ya saba kwa 6.9% na sisi ndiyo tunaopakana na DRC. Huu kwa kweli lazima tuseme ni msiba mkubwa katika diplomasia ya uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jirani tusihangaika na ya Dubai tusihangaika na ya Ulaya jirani DRC kuna soko kubwa la kila bidhaa ambayo tuliyonayo hapa. Ukipeleka mbuzi wananunua, ukipeleka ng'ombe wananunua, ukipeleka kuku wananunua, ukipeleka cement wananunua, ukipeleka mabati wananunua kila kitu tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazotukuta kutokana na hilo la kwanza mazingira yetu siyo rafiki, hatujatengeneza mazingira rafiki ya kibiashara kuanzia kwenye shughuli za kikodi mpaka za kidola hilo kongamano juzi walikuwa wanalaumiwa watu mbalimbali mpaka idara ya uhamiaji imelaumiwa. Kuna Mkongo mmoja alikuwa anashiriki kwenye kongamano hilo akasema siku moja aliambiwa na Afisa Uhamiaji kwamba na nyinyi kila siku mko huku hamtulii kwenu? Yaani mtu anawaletea fedha za biashara unamwambia hamtulii kwenu wakati dunia watu wa namna hiyo wanawapokea. Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba lazima tuwe na mazingira rafiki yanayoweza kufanya biashara na jirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni urasimu katika nyaraka, vibali na mambo chungu nzima; la tatu ni kuchelewa kufanya maamuzi na hili jambo linai-cost nchi yetu kwa kiasi kikubwa sana, watu wengi wanaogopa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu spika, naweza kutoa mfano mmoja tu leo tuna meli imekaa miaka saba na hiyo meli inatuunganisha na nchi za Zambia, nchi za DRC haitembezi, nyingine ina miaka minne, hatuna meli hata moja watu hawafanyi maamuzi meli zimekaa kukarabatiwa tu tena kwa gharama ndogo zimekaa hapo meli hakuna meli hata moja. Nchi yetu moja ya jambo linalotu-cost ni watu kutokufanya maamuzi kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni miundombinu na katika hili nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Bwana Mwigulu Nchemba na Waziri wa Ujenzi. Mimi nimefurahi sana maamuzi mliyoyachukua ya kumsaidia Rais katika reli inayokwenda DRC badala ya kupita Kigali inapita Uvinza inakwenda Msongati inakwenda mpaka Kindu kule Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, lazima tuangalie miundombinu hii tunayoiweka ili kufanya biashara na wenzetu tunajenga kwa faida ya kiasi gani kwa nchi yetu na kwa gharama nafuu, hapa mimi nakupongeza sana kwa uzalendo wako Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ujenzi. (Makofi)

Kwa hiyo, ninachotaka kusema kwamba tunajielekeza katika diplomasia ya uchumi ili itutoe katika hali hii tuliyonayo na muelewe kwamba kiwango chetu cha kukopa na kukopesheka kinategemea namna sisi tunavyofanya biashara na nchi nyingine na kuingiza *foreign currency*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la Kiswahili; sisi tumekuwa mabalozi wazuri wa kutetea matumizi ya Kiswahili, lakini Kiswahili hiki ni ajira, nikuombe Mheshimiwa Balozi ambaye pia ni Waziri wa Wizara hii utusaidie utakapokuja hapa kufanya majumuisho ni kiasi gani vijana wetu waliosoma Kiswahili wamepata nafasi ya ajira nje ya nchi kwenye vyo mbalimbali kwenda kufundisha lugha ya Kiswahili. Tuiseme tu tunataka watu wazungumze Kiswahili lakini pia tunataka tunufaike na hicho Kiswahili ambacho tunakifundisha na tunakijua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Sichalwe, ajiandae Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, kwanza kabisa nianze kwa kusema naunga hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amejitahidi kuwa mwanadiplomasia namba moja kuhakikisha

anaendelea kuiunganisha nchi yetu na nchi zingine ili kuleta maendeleo kwenye Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye diplomasia ya uchumi na kwenye diplomasia ya uchumi nitaongelea mambo mawili; nitaongelea masoko, lakini pia nitaongelea zile nchi ambazo zina masoko, lakini tunaendelea kupitia vikwazo vingi ambavyo tunatamani kuona Wizara hii iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu spika, lakini kabla ya kuanza kuchangia mchango wangu nataka mchango wangu ujielekeze kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ina Sura 10; kwenye Sura ya Saba inaongelea kwenye Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sura hiyo nataka nisome kwenye ukurasa wa 184 ambao Chama cha Mapinduzi kilielekeza Serikali hii katika kipindi cha miaka mitano inapaswa kufanya nini. Katika kipindi cha miaka mitano Chama cha Mapinduzi kinajielekeza Serikali kwenye diplomasia ya uchumi kufanya mambo kadhaa yafuatayo:-

- (a) Kukuza mahusiano ya kiuchumi na mataifa, Jumuiya za Kikanda na taasisi zingine za kimataifa.
- (b) Kulinda uchumi na maslahi mapana ya Taifa kwa kutumia jiografia na nchi kimkakati una ushawishi wa historia hususan kwenye Ukanda wa Kusini.
- (c) Kuhakikisha kuwa balozi zetu zinakuwa kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji na upatikanaji wa masoko na bidhaa na huduma zetu.
- (d) Kuweka mazingira wezeshi ya kuendelea kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*Diaspora*) ili waweze kuzitangaza fursa zinazopatikana nchini na kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo hususan ya kiuchumi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nataka ku-*quote* kidogo kwenye sera ya diplomasia ya uchumi inasemaje? Inasema hivi; diplomasia ya uchumi katika eneo hili pamoja na mambo mengine inapaswa kuwezesha wafanyabiashara kupata masoko na huduma na bidhaa zinazozalishwa na kutaka kukuza katika masoko ya nje katika jambo hili wanapaswa kuonesha ukubwa wa soko la bidhaa na huduma husika na taratibu za kuingia katika masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko baadhi ya nchi ambazo zinatumiya sana mazao ambayo tunazalisha hapa nchini kwetu ni pamoja labda na mchele ambao unatokana na mpunga, mahindi na mazao mbalimbali ya mikunde

na zipo baadhi nchi nyingi tu kwenye ukanda wa SADC ambazo zinatumia mazao hayo. Lakini cha kusikitisha kwa kuangalia hiki kipengele ambacho kinasema balozi zihusike naweza kusema kwamba mwaka jana kulikuwa na mdororo sana wa bei za mahindi hapa nchini kwetu na ikapelekea Serikali kukopa bilioni 50 ili kununua mahindi yale kwa wakulima wetu, unaweza ukaona kwamba hili lilikuwa ni jukumu la Wizara hii wao kuendelea kuzitumia balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali ili kuendelea kututafutia masoko kwenye nchi mbalimbali zipo nchi nyingi sana ambazo ziko hapa Afrika zinatamani kupata mahindi tukianza hata na nchi ya Congo yenyewe na nitaeleza hapo baadaye vikwazo kwenye *point* yangu namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo nchi nyingine Kenya wanatumia mahindi kutoka kwetu, lakini pamoja na mazao mengine je, Wizara hii mmewajibika namna gani kuhakikisha mnaendelea kututafutia masoko, *imagine* hii bilioni 50 ingeweza kutumika kwenye mambo mengine, Serikali isingeweza kwenda kununua yenyewe kwa sababu mngokuwa mmefungua wigo wa wakulima wetu, wafanya biashara wetu kwenda kuuza mazao huko sehemu nyingine ikiwa Ilani yenyewe ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni chama ambacho kimeweka Serikali madarakani kiliwapa jukumu hili kufanya katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kuongelea vikwazo vya kibiashara ambavyo nchi yetu inapata kuelekea kwenye masoko mengine na hapa nataka kuliongelea sana soko la DRC Congo; sasa hivi Congo amekuwa ni mwanachama katika *East Africa* ni mwanachama wa SADC lakini ni mwanachama wa COMESA, ukiangalia sisi tulijitoa kwenye COMESA kwa hiyo Congo anao wigo mpana sana wa kimasoko sasa sisi zipo baadhi ya vikwazo ambazo tunavipitia kutoka nchi ya Zambia, nataka kurejea kitu kidogo kwenye hi sehemu (b) inayosema; kulinda uchumi na maslahi mapata ya Taifa kwa kutumia jiografia ya nchi kimkakati na ushawishi wa kihistoria hususani kwenye Ukanda wa Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wetu na nchi ya Zambia ni wa kiasili kabisa, ni wa kibaiolojia hatukupaswa sisi Wizara yetu kuupuuza, angalia sasa hivi tumetafuta *option* nyingine ya kuzikwepa vikwazo vya Zambia kwa kupitia Ziwa Tanganyika, tumeziwezesha bandari zetu nyingi kule, tumetumia fedha nyingi sana kuhakikisha namna gani tunaingia kwenye Jimbo la Tanganyika, mimi nasema naunga mkono Serikali kutaka kwenda kufungua hata barabara upande ule kule wa Congo, lakini naweza kusema hii tuitumie kama fursa tu ya kutafuta namna gani tuweze ku-*penetrant* Congo katika Majimbo 26, lakini hatupaswi kuchukua kile kigezo ambacho tunaona kwamba Zambia wametuzingira, tunashindwa kuingia Lubumbashi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kutoka Dar es Salaam upite Tunduma ili uweze kuingia Lubumbashi ni rahisi sana kuliko kutoka Dar es Salaam, upite Tabora, uende ukaingie ufike kwenye zile bandari sijui

Kasanga, Kabwe, Kalema ambayo imejengwa sasa hivi zaidi ya bilioni 49. Tuliitakiwa tukae na nchi ya Zambia tujadiliane tuweke mambo sawa kule yale Majimbo kwa mfano lile Jimbo la Hot Katanga ambalo ndio Lubumbashi, Rwalaba ambapo ni Kolowezi tutumie hiyo njia ya Tunduma kufika kwa sababu ni rahisi sana, na huku tuangalie hayo majimbo kwa ajili ya kuingia kwenye Majimbo mengine ambayo yapo mengi kule Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumechukulia kama jambo hili kwamba tunajaribu kui-escape Zambia hakuna namna tunaweza tukai-escape Zambia kwa sababu bado tutataka kuingia kwenye nchi nyingine hata kama isipokuwa Congo. Tukitaka kuingia Zimbabwe tutaingiaje, tukitaka kuingia Botswana tutaingiaje ni lazima tutapita Zambia. Kwa hiyo ushirikiano wetu na Zambia si jambo la kuepukika si jambo la kupuuza Wizara hii mmechukua jukumu gani kuhakikisha tunaendelea kuji-expand/kujipanua zaidi kuona namna gani ambapo tunafikia soko la Congo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeliona hili jambo kama ni la kupuuza wafanyabiashara, madereva watu mbalimbali wanateseka sana. Sasa hivi imekuwa yaani unapopitisha mahindi Zambia ni kama umepitisha madawa ya kulevya na jambo hili sio kwamba Serikali ya Zambia ndio imelizingatia sana kwamba inaizua Tanzania, wakati mwingine ni vita ya kiuchumi ambayo inafanywa na nchi nyingine, mbona *South Africa* wameanza kujenga reli ambayo inapita Angola, iingie Lubumbashi iende mpaka Kolowezi. Hii ni vita ya kiuchumi ambayo wapo wafanyabiashara wanaendelea kutuchonganisha sisi na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuwezi kugombana na Zambia sisi na Zambia ni ndugu, sisi na Zambia ni washirika wazuri ni washirika wa kihistoria ambao undugu wetu hauwezi kuepukika. Kwa hiyo mimi nilikuwa naona kuna haja kubwa sana Wizara hii itafute namna nzuri ya kwenda kukaa na nchi ya Zambia ili kuondoa vikwazo ambavyo tunavipata, ili wafanyabiashara ambao wanataka kupitisha mizigo yao kuingia Congo kwa kupitia njia ya Lubumbashi wapite kiurahisi na yale maboresha ambayo yamefanyika kwenye bandari zetu ili kuingia Jimbo la Tanganyika na majimbo mengine ambayo yapo Congo tuitumie kama fursa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Sichele nilikuongeza dakika tatu.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

MHE. ALI JUMA MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Awali ya yote napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, lakini vilevile napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Nawapa pongezi hizo kwa kuweza kushirikana kwa pamoja kuipaisha nchi yetu ya Tanzania katika anga ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumza suala hili la namna Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyofanya kazi kwa ajili ya kuipaisha nchi yetu katika anga ya kimataifa na hapa nataka nizungumzie kuhusu hii *Royal Tour* pamoja na *Dubai Expo*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Watanzania wenzetu wachache wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii katika kubeza hili suala la filamu hii ya *Royal Tour*, lakini nafiriki wangekuwa wanaijua faida yake nafikiri wangetulia kwa sababu na wao siku yoyote kama si leo kesho itawagusa katika mzunguko wa uchumi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, filamu hii la *Royal Tour* inaweza ikaongeza idadi kubwa ya wageni ambao wataingia nchini hususani watalii, lakini vilevile tunategemea kupata wawekezaji wengi kutoka mataifa mbalimbali kuja kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania na wanapokuwa wengi maana yake malipo ya viza yatakuwa mengi maana yake tutapata pato kubwa, lakini hoteli zetu zitajaa na zitachukua watalii kwa madaraja yote daraja la juu daraja la chini na madaraja ya kati, lakini vilevile italetaka ongezeko kubwa la fedha za kigeni na hii itasababisha kuwa uchumi wetu wa Tanzania kuwa upo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ukurasa 182 Ilani yetu imeelezea namna fursa ambazo zinatakiwa zifanywe na viongozi wetu kuweza kuhangaika na kuweza kuwatafutia maisha mazuri wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inatuambia muasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitumia nafasi yake ya Urais muda mwingi kwa ajili ya kuweka mahusiano mazuri ya Tanzania na mataifa mbalimbali duniani, kwa hivyo haya ambayo anayafanya Rais wa sasa wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan sio mambo mageni yeye amejielekeza zaidi sasa hivi katika diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa napenda niwapongeze Mabalizi wetu hususani Balozi Mavura ambaye anaiwakilisha Tanzania katika nchi ya *South Korea*, amekuwa na jitihada kubwa katika kuunganisha Watanzania ili kuweza kupata fursa mbalimbali ambazo zipo *South Korea*. Lakini vilevile nimpongeze Balozi Kairuki ambaye analiwakilisha Taifa letu katika nchi ya China naye amekuwa mstari wa mbele katika kuhangaika na kuweza kuleta fursa mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Balozi Mahmoud Thabit Kombo ambaye anaiwakilisha nchi yetu katika nchi ya Italy, naye amekuwa anafanya jitihada kubwa katika kuunganisha Watanzania na hivi karibuni kulikuwa kuna tamasha kubwa kule nchini Italy ambalo linaitwa Macfrut lilifanyika katika mji wa Rimini, Italy tamasha hili liliwapeleka wadau wengi wa kilimo wa nchi yetu ya Tanzania na banda la maonesho ambalo lilitumiwa na Watanzania lilikuwa ni kivutio kikubwa kwa bidhaa mbalimbali ambazo zilioneshwa pale. Hivi sasa tunajionea wazi kwa Taifa letu linaanza kuwabeba wakulima wa kawaida wa Tanzania na kuwapeleka katika soko la kimataifa huko ughaibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili suala sio suala la kubeza kwa hiyo tunaomba tumuunge mkono Rais wetu pamoja na Mawaziri wote ambao wanafanya kazi kwa niaba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha miaka minne iliyopita nchi yetu ya Tanzania iliingia mkataba na nchi ya Qatar na mkataba huu ulionesha wazi kuwa namna ya kuweza kupata ajira kwa Watanzania vijana pamoja na Watanzania ambao wana kada mbalimbali za kitaalam. Sasa hivi ni mwaka wanne lakini inaonekana bado jitihada za kuchukua fursa hizo na kuzifanya kazi bado zimezorota, kwa hiyo nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa malizia sekunde 10.

MHE. ALI JUMA MOHAMED: Mheshimiwa Waziri akatapokuja hapa basi angalau aje kutueleza kuhusu mkataba huu wa Tanzania na nchi ya Qatar.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Musukuma. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ...

NAIBU SPIKA: Jiandae Naibu Waziri.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: ...na mimi niweze kuchangia Wizara ya Mambo ya Nje. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri tunaona bidii ya kazi yake anayoifanya, aendelee kurudisha mahusiano ambayo yalivurugika.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 90 ya Watanzania wa hali ya chini tunategemea sana bidhaa kutoka China na Watanzania wale wa kawaida kabisa na hata humu sisi wenyewe Wabunge asilimia kubwa tunatumia bidhaa ya China. Kwa hiyo, rafiki mkubwa wa Tanzania kiuchumi ni Mchina, sasa na mimi ninazunguka huko China mara nyingi na nimemuona Balozi Kairuki hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeenda hadi ofisini kwake Beijing na labda tuone wapi tumekosea. Kweli kwa Watanzania wa hali ya kawaida ambao ni wafanyabiashara wenye elimu ya kawaida ya darasa la saba kuwapeleka kwenye biashara ya mtandao wewe unakaa Kariakoo wengi sana wamekula hasara, niombe sana Waziri na Balozi mkae na wenzetu kama kuna mahali tuliwakwaza au kuna vigezo hatujafikia waone namna ya kuiachia Tanzania kwa sababu kwanza ni soko lao kubwa kwenye bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi watanzania wengi pale kariakoo wamekula hasara kubwa sana na wenzetu wa China ni wajanja kweli, watu wengi wanaoagiza bidhaa mtandaoni mara nyingi inapokuja Tanzania inakuwa tofauti na kitu ulichokiagiza, ulichoonesha ni kingine na kilichokuja kwenye kontena ni kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata ukirudi kwenye *address* ya kule china unakuta ameshabadilisha na *address* kwa hiyo watu wengi wanakula hasara biashara nyingine kama za Kariakoo za nguo za urembo zinahitaji *choice* ya macho sio ya mtandao, leo ukienda Kariakoo inakufa wewe mwenyewe ni shahidi ukienda Uganda na Kenya wenzetu sasa hivi tunatoka Tanzania kwenda kununua bidhaa Uganda na Kenya tuone namna wapi tulikosea turudishe mahusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima na wao wawe *fair*, leo Wachina wapo kila kata wanachezeshwa kamari yaani kuja kwetu Tanzania hakuna corona, ila sisi tukienda kwao kule kuna tatizo, mahusiano tuyatafute kotekote kwa sababu na wao wenyewe wanafaidika na Tanzania waone namna ya kulegeza. Mimi nadhani kwenye Afrika ni nchi Tanzania pake yake ambayo leo ukienda kila kata asubuhi saa tatu utamkuta Mchina anakusanya fedha kwenye kamari. Sasa sisi kwenda kule ni kwasababu ya yale mahusiano ambayo tumeyajenga pamoja na wao lakini ukienda kwenye biashara za madini wamejaa Wachina, ukienda kwenye *contract* za

miradi wamejaa Wachina, ukienda kila kazi ambayo ina maslahi makubwa wapo Wachina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kwenda huko inakuwa ngumu na mimi mwenyewe ni mfano mzuri na Mheshimiwa Amar hapa tumeagiza mitambo unaoneshwa katapira lakini imekuja mitambo ya Kichina mpaka leo Mheshimiwa Hussein amesimamisha mtambo kwa sababu wataalam hawawezi kuja eti kuna corona ila kuja kucheza kamari wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Balozi mtuelewe, mtusaidie Watanzania wengi waliotajirika wametajirika na China, kulikuwa na maonesha tunakwenda kujifunza maonesho ya teknolojia za kisasa ni vizuri waangalie namna ya kuachia yale mahusiano vizuri kabisa ili tuweze kwenda kama tulivyokuwa tunaenda zamani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni suala ambalo kila mwaka humu Bungeni huwa linazungumzwa la uraia pacha. Hofu yangu mimi najjuliza ni nini, yaani tunaweka kikwazo kwamba mtu aliyekuwa nje, Mtanzania ambaye nikimsomesha mwanangu akimaliza akasema baba nimepata kazi akafanya maarifa yake akapata uraia, kurudi Tanzania anakuwa ni mgeni, hii ni uonevu mkubwa sana, tunapoteza watoto wetu, tunawanyima fursa kwa sababu ya vitu ambavyo mimi nadhani ni hofu ya kisiasa pia, kwa sababu wanasema eti aruhusiwi kugombea kazi za kisiasa kwanini yaani kwa tatizo gani yaani mtu amesoma, amepata *knowledge* kubwa akirudi akiwa Waziri hapa ndio watu ambao tunawataka tubadilisha mawazo tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana hili halikwepeki, hata mkilikwepa jaribu kufanya *analysis* ya wahindi matajiri hapa Tanzania wote wana uraia mbili, utamkuta ni Mtanzania ana *passport*, lakini ana *passport* ya Canada na ana ya Uingereza kwa kwetu sisi tuna hofu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Uingereza juzi nilikuwa naangalia *television* tumepata Diwani Msukuma wa Nzela kule Jimboni kwangu kapata Uingereza, tuna Mawaziri wapo sijui Canada, tunaona wivu gani tunasomesha nje ili tupate mawazo mapya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naiomba Wizara hizi hofu tuziondoe turudishe tu hali halisi kwamba watu wapate uraia wa nchi mbili kama anafanya vizuri akirudi hata Jimbo langu agombee, akinishinda basi, ndio vitu tunavyovitaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama Mbunge unajiamini unafanya kazi vizuri hata ukija na *degree* zako hata ukitoka Marekani unamkuta King kazuia hapo, utapigwa unarudi unajipanga tena. (Makofi)

Kwa hiyo, tuondoe hofu tunapeleka watoto wetu nje ili wapate *knowledge* ya kuja kulisaidia Taifa na tujifunze hata Asia walipeleka kwanza watoto wao Ulaya wakaiga Ulaya wanafanyaje, waliporudi kwao wakafanya mambo mazuri, tuondoe hofu kazi nzuri Mheshimiwa Waziri, lakini nakusisitiza na kukuomba tena Watanzania wengi wanaitegemea China, hata humu ndani ukiangalia suti nyingi humu ndani ni za Kichina, mnaguna nini wengi tu mmekula (mmevaa) Mchina sasa ukiweka masharti mwisho tutavaa *fake* ambayo sio *choice* ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana hata nywele humu nyingi ni za Kichina. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa (*national competitiveness*). Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuimarisha mahusiano ya kimataifa, na pia kwa mafanikio makubwa ya *Royal Tour* ambayo imeanza kuleta matunda makubwa kwa nchi yetu hususani sekta ya kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kuimarisha diplomasi ya uchumi kwa lengo la kuongeza masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo,

madini na utalii. Pamoja na kuongeza mapato kwa Taifa letu, itaisaidia kuongeza fedha za kigeni na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. PARTICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpungeze sana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Liberata Mulamula na Naibu wake Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza utahusiana na umuhimu wa diplomasia ya uchumi katika kipindi hiki hapa Tanzania. Kutokana na hali ya kudorora kwa uchumi wa dunia na Tanzania yetu kunakochangiwa na ugonjwa wa UVIKO-19, mabadiliko ya tabianchi na vita vya Urusi na Ukraine, Tanzania inatakiwa kutumia mbinu za kidiplomasia ili kujinasua na athari hizi. Kwenye hili, nchi yetu inatakiwa kujielekeza katika kujenga uchumi wa kujitegemea na kutafuta fursa za uwekezaji ili kukuza uchumi wetu kupitia diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Rais wetu kwa juhudi zake za kuifungua nchi yetu kimataifa. Kwa kipindi kifupi, Rais wetu amefanikiwa kurejesha heshima ya nchi yetu Barani Afrika na nje ya Afrika kama ilivyokuwa kipindi cha awamu za kwanza, pili, tatu na nne. Rais wetu ametembelea mataifa mbalimbali Barani Afrika na nje ya Bara letu pamoja na kushiriki mikutano ya kimataifa kama njia na mbinu ya kuongeza ushirikiano na mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi zetu waelekeze nguvu kwenye kusaidia juhudi za Rais wetu kuitangaza vyema Tanzania ili tufanikiwe kuipaisha nchi yetu kiuchumi na kisiasa. Juhudi zifanyike kushawishi kupitia diplomasia ya kiuchumi kuvutia uwekezaji, biashara za kimataifa na utalii. Tukiongeza nguvu, Tanzania yetu itakuwa na ushawishi Barani Afrika kama zilizavyo nchi za Nigeria, Afrika Kusini na Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha hili, ninaishauri Serikali itoe mafunzo maalumu kwa Mabalizi wetu pamoja na wasaidizi wao ili wawe na uelewa wa diplomasia ya uchumi pamoja na mbinu na mikakati ya kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu malalamiko niliyopokea kutoka kwa mwanafunzi wa Sudan aliyemaliza Shahada ya Uzamivu (*PhD*) katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyoko Arusha, Tanzania. Msomi huyu ni mwalimu wa chuo kikuu huko Sudan. Alipowasilisha vyeti vyake chuoni Sudan ili abadilishiwe cheo, alielekezwa na uongozi wa chuo apeleke vyeti vyake vikathibitishwe kuwa ni

halali na ubalozi wa Tanzania huko Khartoum. Alipokwenda kwenye ubalozi, alikuwa na nakala halisi za cheti chake cha *PhD*, pasi yake ya kusafiria iliyokuwa na kibali cha kuishi Tanzania, kadi ya kitambulisho cha uanafunzi kutoka Chuoni Mandela, barua iliyomsajili chuoni Mandela, na nakala ya *dissertation* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwasilisha ushahidi wote huu, Ubalozzi wa Tanzania hawajamsaidia na imechukua muda mrefu sana kupata huduma hii na analalamika huenda akachelewa kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mteja huyu analalamika kuwa atajisikia vibaya sana kama itamlazimu kutuma vyeti vyake Tanzania kuthibitishwa ili hali kuna ubalozi unaoiwakilisha nchi yetu Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iwaelekeze mabalozi wetu watekeleze majukumu yao kwa wakati ili kuepuka kero za kulalamikiwa kwani hali kama hizi zinaharibu taswira nzuri ya nchi yetu kwenye uso wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu ni kwenye eneo la umuhimu wa Wizara kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili duniani. Lugha ya Kiswahili imetumika kwa mafanikio makubwa sana kuliunganisha Taifa letu. Kiswahili ni lugha ya Taifa na hutumika katika shughuli zote za Serikali likiwemo Bunge. Hivi karibuni sheria imepitishwa na kuelekeza Kiswahili kitumike mahakamani. Kenya inatumia Kiswahili kama lugha ya Taifa, Uganda wanatumia Kiswahili kama lugha ya Jeshi na Polisi. Kiswahili kinatumika Mashariki mwa Congo, Rwanda, Burundi, Visiwa vya Ngazija, baadhi ya maeneo ya Malawi, Zambia, Msumbiji na Somalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha hii imekuwa inatumiwa katika kusambaza habari katika vituo mbalimbali ulimwenguni kama vile Sauti ya Amerika, BBC, Deutsche Welle, Monte Carlo, RFI na nchi nyinginezo kama vile Uchina, Urusi na Iran. Aidha, imekuwa ni mojawapo ya lugha muhimu zinazofundishwa katika vyuo vikuu nchini Marekani Uingereza, Ulaya bara, Urusi, Uchina na Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini Afrika Kusini Baraza la Mawaziri limeidhinisha Kiswahili kifunzwe katika shule za umma na za kibinafsi. Kwenye hili, Kiswahili imekuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika inayotoka nje ya Afrika Kusini kufunzwa katika nchi hiyo. Vilevile Umoja wa Afrika na Jumuiya ya SADC imeidhinisha Kiswahili kitumike kama mojawapo ya lugha za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki itatekeleza azma hii kwa kushirikiana na wadau wengine, Kiswahili kina nguvu ya kupanuka katika nchi ambazo hazijawahi

kukizungumza na kina nguvu ya kuliunganisha Bara la Afrika na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi ya ukuaji wa Kiswahili, ninaishauri Serikali kupitia kwenye Wizara hii iwe na mkakati mahsusi wa kueneza lugha ya Kiswahili kupitia Balozi zilizo katika nchi mbalimbali duniani ili Kiswahili kiwe moja ya lugha kuu duniani. Naishauri Wizara iendeleze kwa nguvu zote kuendeleza na kutangaza kiswahili pale alipoachia Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze Tanzania ina Mabalazi wangapi na watumishi wangapi katika Balozi zetu nchi za nje, lakini napenda utufamahishe ni Mabalazi wangapi kutoka Zanzibar na wangapi kutoka Tanzania Bara na hivyo hivyo kwa watumishi wa Balozi zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama kuna kasoro katika hili ulete utaratibu utakaotumia kuondoa kasoro ili isiwe kero ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia ulieleze Taifa ni kwa nini taasisi nyingi za Tanzania Bara ambazo sio za Muungano zinatumia jina la Tanzania hadi kufikia Zanzibar taasisi kama hizo kukosa uwakilishi wa kimataifa kwa kuambiwa tayari Tanzania ni mwanachama au vinginevyo, lakini Zanzibar inakuwa haina tena nafasi kwa mfano *Tanzania Football Federation (TFF)* ni mwanachama wa *FIFA* lakini Zanzibar imekataliwa sababu ya *TFF*.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu inayoonesha sura ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu mapato. Wizara hii ni Wizara kama Wizara nyingine, ina malengo na makusudio yake. Moja katika malengo yake ni kujiwekea *target* ya matumizi na mapato ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilijiwekea lengo la kukusanya shilingi

2,550,879,000. Lakini hadi kusomwa kwa hotuba hii ni asilimia 33 tu ya lengo ndio iliyokusanywa. Hii ni rekodi isiyoridhisha kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wangu unaonesha kuwa vyanzo vilivyotarajiwa kutumika haviko imara (*not stable*), hivyo basi kuna haja ya kuangalia vyanzo vingine zaidi ili kutimiza lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika suala hili la makusanyo ya mapato ni kama ifuatavyo; hivi sasa nchi yetu inasifika kwa zoezi zima la *Royal Tour*. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuanzisha *Royal Tour*. Nchi nyingi zinapenda kuja kuona vivutio vyetu. Lakini watu wengi katika baadhi ya nchi hawavijui vilipo na hadhi yake. Ofisi zetu za ubalozi za nje zingetengeneza ramani ya nchi yetu huko kwenye ofisi za mabalozi zinazoonesha vivutio vyetu pamoja na hadhi ya vituo hivyo zikawaonesha watu wa nchi hizo kwa gharama ndogo pamoja na vipeperushi vinavyoonesha vivutio vyetu. Lengo ni kuuza ili kuongeza mapato, lakini pia kuwashawishi kuja nchini kuangalia vivutio vyetu. Hii itaongeza mapato kwa Wizara na kwa nchi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu kwa umma; hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetaja namna ya kuelimisha umma juu ya yanayofanyika nchini mwetu. Hii ni habari nzuri sana kwa umma, lakini kasoro ya zoezi hili ni vyombo vinavyotumika sio sahihi kwa kuwafikia wananchi wa maeneo ya vijijini. Hotuba imetaja vyombo vinavyotumika ni *magazine, television, radio* na vipeperushi. Vyombo hivi si rahisi sana kuwafikia wananchi wa vijijini ambao ni sehenu kubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Wizara na Serikali kuweka kikosi kazi kwa kutumia usafiri wa magari kwenda vijijini kuwaelimisha wanavijiji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Diplomasia; naipongeza Serikali yetu kwa kuweka chuo hiki, kimekuwa ni miongoni mwa vyuo muhimu sana katika nchi yetu. Serikali inapaswa kuchukua juhudi za makusudi kuboresha chuo hiki kwa kukiwekea mazingira mazuri ya kimataifa. Bado kuna hali isiyoridhisha kwenye miundombinu za chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mitaala ya chuo hiki pia ni vyema ikajielekeza kuwafundisha vijana wetu pamoja na mambo mengine namna ya kuweza kujitegemea wenyewe baada ya kumaliza mafunzo yao. Bado mpaka leo mitaala ya chuo hiki inawatengeneza wahitimu wetu kutegemea ajira za Serikali. Hivyo kuna haja ya kuwatengeneza watu wetu katika hali ya kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ajira kwa upande wa Serikali nafasi haziwezi kukidhi kuajiri vijana wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote, kwa jinsi alivyotuvusha kwenye majanga kama vile corona, ukame, mafuriko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini kutoa pongezi za nyingi sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwanza kwa kutunukiwa tuzo na kwa jinsi anavyotuwakilisha na kudumisha mahusiano na mataifa mbalimbali na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa – Waziri Mkuu, Baraza la Mawaziri na watendaji wote Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Balozi Mbaruok Nassor Mbaruok – Naibu Waziri wa Wizara, Mheshimiwa Balozi Edward Sokoine - Katibu Mkuu wa Wizara, Mheshimiwa Fatma Rajabu Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Wizara hii; kwa kuwa suala la kutokujengwa na kuendelezwa limechukua muda mrefu tunaiomba Serikali itafute fedha za kujenga majengo ya ofisi za Balozi zetu na makazi ya watumishi hata kwa awamu, kwani Serikali inatumia gharama kubwa sana katika kupangisha majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuwepo kwa maafisa wachumi wabobezi katika Balozi zetu na kama wapo watumike ipasavyo kwa kutangaza diplomasia ya uchumi na matumizi sahihi ya *blue print* na kutafuta fursa za mazao mbalimbali na bidhaa za nchi yetu katika masoko mataifa ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu ina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa ajira hapa nchini Serikali kupitia Balozi zetu ifanye uhamasishaji mkubwa sana makampuni ya nje kufungua viwanda vingi hapa nchini kwa kuondoa vikwazo na kuweka mazingira rafiki ili vijana wengi wa Kitanzania wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa sana la kusafirisha mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage na kadhalika kwenda nchi za Afrika Mashariki, kuna hatari kubwa sana ya Taifa letu kukumbwa na baa la njaa. Serikali itumie njia za kidiplomasia kuzuia hali hii bila kuathiri mahusiano yetu na mataifa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri, *Attorney General* (Mwanasheria Mkuu).

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kukushukuru kwa nafasi ambayo umenipatia, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri lakini na Kamati yenye dhamana na Mambo ya Ulinzi na Nje na mawasilisho ambayo umewasilisha kwenye Bunge lako tukufu, ninaunga mkono mawasilisho ya Bajeti ya Wizara, lakini nina wiwa walau kuchangia kwa machache kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kwa uelewa wangu Serikali yoyote makini hufanyia kazi mawazo na ushauri inaoupokea kutoka kwa wananchi wake na kupitia kwa wawakilishi wao, lakini pili Serikali yoyote makini huheshimu sana mgawanyo wa madaraka uliowekwa na Katiba yetu. Sasa ningependa kuheshimu sana mawazo ya wachangiaji wengi ambao wameyawasilisha, lakini pia hata mawazo ya wasomi wenzangu wanasheria na nitagusia hili la ushiriki wa Tanzania katika Mahakama ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumbukumbu zetu ziwe sahihi kwamba Tanzania ni nchi mojawapo muasisi wa Umoja wa Afrika lakini ni mwanachama mwaminifu na hai, lakini pia nchi yetu bado ni mwanachama wa Mahakama ya Afrika na hata sasa Rais wa Mahakama hiyo ni Mtanzania. *(Makofi)*

Sasa inapokuja namna ya kupeleka migogoro kwenye mahakama hiyo utaratibu umewekwa na *protocol* zinazoiongoza Mahakama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *protocol* ya tano imeorodhesha namna ya kufika kwenye mahakama ile na kwenye Ibara ya 3 inatoa fursa kwa nchi mwanachama aliyeridhia anaweza akatoa tamko kwa asasi za kiraia yaani NGOs na watu binafsi pia kufikisha mashauri yao kwenye mahakama hiyo. Wote tunafahamu Tanzania kwa sasa iliiondoa tamko lake kwa NGOs pamoja na watu binafsi kupeleka mashauri yao au migogoro kwenye mahakama hiyo, lakini hiyo haimaanishi kwamba migogoro mingine baki

inayohusu Tanzania na watanzania kwa maana ya zile haki zilizotolewa na kipegele cha A – E kufikishwa kwenye mahakama hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi mkubwa ni lazima tutambue kwamba kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 107A(2) (a) mpaka (e) imetaja ile misingi ambayo migogoro yetu inavyotatuliwa. La kwanza; kwa sababu nchi yetu kama nilivyosema inaoongozwa na Katiba, migogoro imepangwa migogoro ya aina ipi ipelekwe wapi na Katiba yetu pamoja na sheria zingine zote inasema kwamba kabla ya kupata nafuu nyingine au kutafuta nafuu nyingine mamlaka zingine za nje ni vizuri kupata nafuu za kisheria kwenye mamlaka ya utatuzi wa migogoro tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa misingi hiyo kwa kuwa tumesema kwenye Katiba yetu Ibara hiyo ya 107 kwamba mahakama ndiyo chombo pekee, lakini kwenye Ibara ya 13(6) namna ambavyo mtu ana haki ya kupeleka shauri lake kwenye ngazi za mahakama na vyombo vingine vilivyopewa dhamana hiyo. Kwa hiyo, ni msingi wa sheria zetu kwamba wananchi na mtu yeyote anayetaka kutetea haki yake apeleke shauri kulingana na jinsi ambavyo zile sheria zilizopo zimeainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kwa mantiki hiyo kwa sasa tutaona kwamba yapo mpaka mashauri ya Kikatiba ambayo yanapalekwa kwenye Mahakama Kuu na yanashughulikiwa. Lakini kwa mujibu kwa mfano kwa Sheria ya Madai na Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai zimeainisha mashauri yapi yapelekwe wapi. Kwa hiyo, kitendo cha Serikali kuondoa lile tamko haimaanishi kwamba Serikali haina nia ya kurejesha haki ambayo kwa sasa hawapeleki, vilevile haimaanishi kwamba hao watu wanazuiwa kuleta mashauri yao kwenye mahakama hizi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ambalo tunawaasa wote ambao wanatafuta haki zao mahakamani; moja, ni kuzingatia mipaka ambayo tunayo na wote tunajua jinsi ambavyo hata hili Bunge lako tukufu lingependa sana migogoro ya Watanzania ishughulikiwe na mahakama kwanza ambazo zimewekwa kwa mujibu wa Katiba yetu na kwa sheria zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ile migogoro ambayo inafikia ile hadhi ya kwenda mamlaka za nchi, mamlaka zingine kama Mahakama ya *East Africa*, Mahakama ya Afrika, ICC basi zitafuata kwa mujibu wa zile nyenzo zilizopo za Kikatiba zinaoongoza namna ya kufikisha mashauri kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kipindi hiki ninaweza nikasema kwamba hakuna yoyote kati ya NGOs pamoja na watu/raia waliokwenda Mahakama ya Afrika ambao walijaribu kuleta mashauri kwenye mahakama za nchi hii na wakanyimwa fursa hiyo, na endapo ikitokea hivyo basi hilo ni

jambo ambalo vilevile linaweza likatapata suluhisho ndani ya mamlaka ya sheria zetu tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo sheria kama nilivyosema kwa mfano, tuna Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu lakini tuna Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai kifungu cha 7 kinaeleza kila shauri lianze kwenye ngazi ya chini. Ukienda kifungu cha 264 Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai imepanga mashauri yapi ya kwenda Mahakama ya Wilaya, ya Mkoa. Sheria ya Mahakama imeeleza mashauri ya kwenda Mahakama za Mwanzo, ukija kwenye mabaraza yetu yote yaliyotungwa vilevile yaliyoanzishwa kisheria yanaainisha migogoro hiyo iende wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa mantiki hii hata *protocol* ya tisa ya Mahakama hii ya Afrika kwa mfano inatambua kwamba shauri hata kama lingekuwa kule linaweza likaenda kwenye mashauri yaani kwenye *amicable settlement* na unaporudi kwenye Katiba yetu Ibara ya 107A(2) (d) utakuta inasisitiza namna ya kukuza usuluhishi. Kwa hiyo, haiji akilini kwa nini ukaanze kutafuta usuluhishi kwenye mahakama ya juu au ya nje ukiacha mamlaka iliyo ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itoshe niseme tu kwamba ninashukuru, lakini tutaendelea kuheshimu nafikiri mawazo ya wananchi kupitia kwa wawakilishi wao na kuendelea kufanya kazi nao na kuona namna ambavyo kila mmoja ataendelea kupata haki zake kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha kujadili hotuba hii siku ya leo. Aidha, nichukue fursa hii kwa kipekee kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sina budi kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushauri na maelekezo yao katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe binafsi kwa namna mnavyoliongoza Bunge letu kwa hekima, busara na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na ushauri wao walioutoa kupitia taarifa iliyowasilishwa asubuhi hii. Hii ni Kamati makini sana, Wajumbe wake wanauielewa mkubwa wa masuala ya kidiplomasia na hivyo wamekuwa wakitoa mchango mkubwa ambao umeendelea kusaidia kuboresha utendaji kazi wa Wizara na diplomasia ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa uongozi wake mahiri ndani ya Wizara na ushirikiano mkubwa anaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninamshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizopo chini yake kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwao bila kuwasahau Mabalizi wote ambao wapo nchi za nje wakituwakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuishukuru familia yangu kwa upendo na uvumilivu wao na kuendelea kuniunga mkono wakati nikitokeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nijielekeze katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini kwanza nitoe shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kutoa maoni yao katika hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana pia kwa pongezi nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamezitoa kwa Wizara yetu na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba pongezi hizi kwetu ni deni ambalo tutalilipa kwa kutekeleza majukumu yetu kwa bidii na ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 20 wamechangia hoja hii na michango ya Waheshimiwa Wabunge wote tumeipokea na tunaahidi kujumuisha katika utekelezaji wa mipango ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kuhusu suala la viwanja, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Balozi zetu. Suala hili

limeongelewa takribani na nusu ya Wabunge ambao wamechangia leo hapa. Wizara tayari imekamilisha taratibu za manunuzi za kuwapata wakandarasi watakaotekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati kwenye Balizi zetu nje ya nchi. Miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi ambapo mkandarasi aliyepatikana ni *SRJE East Africa Limited*, ujenzi wa jengo la ubalozi na kitega uchumi katika ubalozi wetu wa Kinshasa mkandarasi ni *China Railways Construction Engineering Group Limited* na ujenzi wa makazi ya jengo la ubalozi na makazi ya balizi katika ubalozi wetu Muscat mkandarasi aliyepatikana ni *Arab Contractors* na pia ujenzi wa jengo la ubalozi la kitega uchumi katika ubalozi wa Tanzania Comoro mkandarasi aliyepatikana ni *Suma JKT Construction Company Limited*, mradi wa ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi *R Street* katika ubalozi wa Tanzania Washington mkandarasi ni Kampuni ya *M&R Construction Group*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya miradi hii tayari imeridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivi sasa ni Wizara ipo katika hatua za kukabidhi maeneo ya miradi (*site possession*) kwa wakandarasi ili ujenzi uanze mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ubalozi wetu wa Msumbiji ambalo kuna jengo lenye ghorofa tisa tayari limekarabatiwa na lipo katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, kuhusu utekelezaji wa kiwanja cha ubalozi mpango wa kukiendeleza umeanza kufanyika kwa kukamilisha michoro na makabrasha ya jengo linalopendekezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubalozi wetu wa Zambia kesho Wizara yetu ina kikao na Benki Kuu, Shirika la Nyumba la Taifa na Wizara ya Fedha pamoja na Wakala wa Majengo Tanzania kwa ajili ya kujadili namna ya kuviendeleza viwanja hivyo kwenye mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, majengo sita yaliyopo Lusaka tayari yamekarabatiwa na yapo katika hadhi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilielezwa hapa kwamba katika Ubalozi wetu wa Ufaransa tuna jengo bovu. Kwa kweli Ubalozi wetu wa Ufaransa hatuna jengo bovu, Wizara ina majengo mapya ambayo yamenunuliwa mwaka 2015 kinachofanyika ni ukarabati wa mara kwa mara hasa kutokana na vipindi vya joto na baridi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilizungumziwa kuhusu ukarabati wa jengo la Ofisi ya Wizara iliyopo Zanzibar naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar tayari umekamilika na jengo hilo sasa lina muonekano wenye hadhi ya Ofisi ya Mambo ya Nje. Aidha, kuna utaratibu pia saa hizi unaoendelea wa kuanza kujenga jengo jipya la Ofisi ya Mambo ya Nje ambalo tunategemea litakuwa sehemu ya

Tunguu mara tutakapokabidhiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi naomba kukufahamisha kwamba hivi sasa Wizara yetu inaendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujadiliana na taasisi za fedha hapa nchini kwa lengo la kuendeleza viwanja kwa kujenga majengo ya ofisi, vitega uchumi pamoja na makazi ya watumishi wa ubalozini. Hadi sasa kwa kutekeleza maagizo hayo tayari tumeshafanya vikao viwili na Benki ya CRDB kwa nia ya kuwa na utaratibu maalum wa kutekeleza maelekezo hayo. Tunafurahi kwamba hata leo hapa wawakilishi wa CRDB walikuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee kidogo kuhusu suala jingine ambalo limechangiwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wengi hili ni suala la wafanyabiashara wa Watanzania kuzuiwa kwenda China kwa kipindi hiki.

Waheshimiwa Wabunge ni vizuri tukaelewa kwamba ndugu zetu Wachina ugonjwa huu wa UVIKO ulianza kwao na ulileta madhara makubwa ikiwemo zaidi ya watu 4,000 kupoteza maisha yao. Hali hiyo iliwafanya waweke masharti magumu ili kudhibiti maambukizo ikiwemo kuzuia raia wa kigeni kuingia China na kuwataka raia wao wanaorudi kwao kukaa *quarantine* siku 21 hotelini kwa gharama zao na kuyataka mashirika ya ndege ya kimataifa kupunguza safari za ndege hadi kufikia safari moja kwa wiki na katika safari hizo ndege isizidishe ujazo wa abiria kwa asilimia 60 ili kuwepo na *social distance* ndani ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, masharti hayo si tu kwamba yamewaathiri wafanyabiashara wetu bali pia yanawaathiri na raia wao na raia wa mataifa mengine yote ulimwenguni tangu mwezi Machi hadi leo hii tunavyozungumzia jiji la biashara la uchumi la Shanghai lipo kwenye *lockdown* baadhi ya wilaya za Jiji la Beijing nazo pia zipo katika *lockdown* na imeelezwa na ubalozini wetu kwamba kwa zaidi ya siku 60 sasa katika Jimbo la Shanghai wananchi wameambiwa wasitoke ndani ya nyumba zao na maduka yote yamefungwa, usafiri wa ndani umesimama, shughuli za mabanki pia zimesimama, shughuli za bandari, soko la hisa na viwanda vingi navyo vimesimamisha uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inatuonesha dhahiri ni jinsi gani ndugu zetu hawa wanavyochukulia ugonjwa wa UVIKO-19 tofauti na nchi nyingine duniani. Hatua zao si tu zinaumiza wafanyabiashara wetu, bali pia zinawaumiza wananchi wao. Hivyo tuvute subira na tuwe na matumaini kwamba mambo yatafunguka na wenzetu wakiwa tayari watatufungulia.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukisubiria hilo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwawezesha wafanyabiashara wetu kutimiza malengo yao ikiwa ni pamoja na kufungua dawati la viwanda na biashara kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafanyabiashara wanaotaka kuagiza bidhaa China. Aidha, Serikali imefungua Ofisi ya Ubalozi mdogo Guangzhou ambayo itaendelea kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi. Aidha, Serikali imeanzisha safari za ndege za *Air Tanzania* na kusafirisha mizigo ya wafanyabiashara wetu ili kurahisisha upatikanaji wa mahitaji yao kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna habari njema, na habari ambayo tumeipokea wiki hii ni kwamba kuanzia Juni mwaka huu shirika letu la ndege limeruhusiwa kuanza tena safari za kubeba abiria kwenda China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kidogo kuna suala hapa pia lilizungumziwa kuhusu kufungua ubalozi nchini Pakistan na Iran. Kwanza nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba Pakistan na Iran tuna mahusiano nao mazuri sana na tumekuwa tukishirikiana katika mambo mbalimbali, lakini kuhusu mpango wa Serikali kufungua ubalozi wake nchini Pakistan na Iran, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tayari imeanza kufanya utafiti wa kuona namna ya kufungua ubalozi katika nchi hizo kwa kuangalia faida za kiuchumi na maslahi mapana ambayo nchi yetu inaweza kunufaika nazo ikiwa ni pamoja na kuainisha gharama za ufunguzi wa ubalozi na uendeshaji wake, mara zoezi hilo litakapokamilika, basi Wizara itawasilisha mapendekezo na ushauri kwa mamlaka kwa ajili ya maelekezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa hoja hapa kuhusiana na fursa za ajira katika nchi mbalimbali huko nje ikiwemo Qatar. Ni kweli kwamba Tanzania na Qatar zilisaini MOU kwa ajili ya vijana wetu wapate fursa za kwenda kufanya kazi nchini Qatar. Hata hivyo, mara tu baada ya kusaini huko kukatokea ugonjwa wa *Covid* ambao ulizuia kidogo kuendelea na process hiyo. Lakini hivi sasa tayari mazungumzo yameshaanza tena na hivi karibuni tutapata habari njema. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri maliza. Mheshimiwa Waziri maliza sekunde 10.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri umezungumzia jengo la Washington limeshapata mkandarasi, sawa?

31 MEI, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo.

NAIBU SPIKA: Na mara nyingi mnasema hivi, kwa hiyo, Mwenyekiti mstaafu wa NUU na Mheshimiwa Spika itabidi uende ukajiridhishe, utazame kama kweli huyo mkandarasi yuko site. Sawa? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri umeelewa eeh? Mheshimiwa mtoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwanza kwa kunipatia nafasi asubuhi ya leo kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kusimamia kwa umakini mjadala wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Umeonesha unaifahamu sana Wizara hii kutokana na kwamba ulikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru tena kwa dhati Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Mheshimiwa Vincent Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini na Wajumbe wa Kamati kwa ushauri na maoni yao. (Makofi)

Niwahakikishie Wajumbe wa Kamati kuwa Wizara imepokea taarifa ya Kamati, tumepokea ushauri, tumepokea na maoni na tutayazingatia wakati wa kutekeleza majukumu ya Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Balozi Nassor Mbarouk, Mbunge na Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya na kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara, kwa hakika ni jembe. Ninamshukuru kwa majibu yake na ufafanuzi alioutoa kwenye hoja zilizoibuliwa kwenye mjadala huu. (Makofi)

Aidha, nawashukuru tena watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Balozi Joseph Sokoine na Naibu Katibu Mkuu, Balozi Fatma Rajabu kwa kusimamia kikamilifu maandalizi ya bajeti ya Wizara. Nimefarijika sana kwa pongezi ambazo mmezitoa kuhusu uongozi wa Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa ujumla wenu kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi. Nadhani haijawahi kutokea, leo tumepata michango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 21, kwa kawaida huwa hatufiki hata kumi. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge na niwahakikishie kabisa na kwa moyo mkunjufu kwamba michango ambayo mmeitoa tumeipokea na tutaifanyia kazi, maoni na mapendekezo yaliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na ufinyu wa muda, Wizara yangu haitaweza kuzijibu hoja zote kwa hapa, lakini tutazitolea maandishi na tutaweza kuwasilisha kwenu. Nipende pia kuwahakikishia Wabunge kwamba sisi pamoja na kwamba ni Wabunge lakini ni watendaji, ni watendaji ambao tunazingatia yote ambayo tunazingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tunazingatia mpango wa maendeleo, tunazingatia sera yetu ya mambo ya nje, tunazingatia maagizo yanayotolewa na viongozi wa kitaifa lakini tunazingatia maelekezo na maoni na mwongozo kutoka Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba nitoe ufafanuzi kwenye masuala machache yaliyoibuliwa kwenye mjadala wa hotuba ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwamba amepitia hoja ambazo zilikuwa zimechangiwa na Wabunge wengi lakini naomba nimshukuru kwa aina ya pekee Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kutolea maelezo kuhusu jukumu la Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu na jinsi gani ushiriki wa NGOs na watu binafsi wanaweza kupeleka kesi zao huko, umelitolea maelezo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge ambaye ameliongelea hili kwamba tutaendelea na nitaomba kwamba tuendeleo kuweza kuwasiliana maana Serikali imejipanga tunaendelea kuliangalia kwa mapana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na pengine Mheshimiwa Salome nikufahamishe kwamba tumepata heshima kubwa ya kuwa na Jaji ambaye ni Rais wa Mahakama hiyo, Mheshimiwa Iman Aboud ambaye tuko naye. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge napenda baada ya kikao hiki unaweza pia na wewe ukatumia fursa hii ukaweza kuongea na Rais wa Mahakama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zilitolewa lakini naomba nijikite kwenye hoja moja ambayo ilikuwa *specific* kuhusu suala la barabara ya Singomakua kwa upande wa Tanzania kama alivyoeleza Mheshimiwa Yahya

Ally Mhata kwa upande unaohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeshajengwa na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba Serikali ya Msumbiji tayari imetenga fedha za kujenga barabara zake ili kuunganisha na barabara zetu kwa lengo la kurahisisha mawasiliano na biashara kama alivyosisitiza Mheshimiwa Mhata. Leo hii nimeletewa taarifa kutoka Serikali ya Msumbiji kwamba barabara hizo ambazo zinafanyiwa matengenezo ni barabara ya Negomano mpaka Muenda ambayo ni kilometa 200, barabara ya Muenda mpaka Mount Pwezi ambayo ni kilometa 150 nayo inafanyiwa kazi na barabara ya kutoka Mount Pwezi mpaka Singomankua ambayo ni kilometa 90 tayari zimetengewa pesa kwa taarifa niliyoipata kutoka Serikali ya Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wameliongelea vizuri sana au wameliweka vizuri sana diplomasia yetu ya uchumi ambayo ndiyo sera yetu ya mambo ya nje imejikita katika utekekezaji wa diplomasia ya uchumi. Tuliulizwa kuhusu mchango wa Wizara na balozi zetu nje na taasisi hizo chini ya Wizara katika kutekeleza diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako tukufu na kuwahakikishia kwamba tumejipanga vizuri katika kuteleleza hii diplomasia ya uchumi na mifano ipo mingi, lakini kwa uchache wa muda naomba tu kuainisha michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa Mabalozzi wetu wote wameelekezwa kwamba wawe na mpango mkakati unaoonesha jinsi gani wanatekeleza diplomasia yetu ya uchumi ikionesha malengo, ikionesha jinsi gani wakiainisha fursa na kujiwekea kama ninavyosema kipimo kwamba wanafanikisha vipi na sasa hivi tumeanza kupata hiyo mipango na kama Wizara inaifatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mheshimiwa Rais alianzisha Idara Maalum ya Diplomasia ya Uchumi kwenye Wizara yetu ambayo pamoja na mambo mengine inajukumu la kuratibu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Kwa hiyo, idara hii inaratibu na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa fursa za biashara, uwekezaji, utalii na nyinginezo zilizopo ndani na nje ya nchi kwa kushirikia na balozi zetu, taasisi za Serikali na sekta binafsi kwa lengo la kuhakikisha Taifa linanufaika na fursa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na nilifarijika kumsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja akisema kwamba ili kufanikisha diplomasia ya uchumi kwamba Waheshimiwa Wabunge na ninyi muwe mabalozzi wetu, tushirikiane kwa pamoja tuweze kufanikisha hii diplomasia yetu ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia kwamba balozi zetu zinajitahidi sana kutangaza fursa za biashara na fursa za masoko. Na kama mlivyotaja Balozi wetu, Mheshimiwa Kombo alioko Italy hivi majuzi tu ameweza kuwaleta wakulima wa kawaida tu kwenye maonesho ya kilimo na niliwaona wengi wao walikuwa ni kinamama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mazao yale hasa matunda na mboga zili-*attract* watu wengi sana. Kwa hiyo, hiyo ninayosema ni jitihada zinazofanywa na balozi zetu kuhakikisha kwamba mazao yetu, bidhaa zetu zinajulikana huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia katika hotuba yangu nilieleza namna ambavyo nyama na bidhaa za nyama kutoka Tanzania vimepata soko katika nchi za Mashariki ya Kati na hivi karibuni Saudi Arabia imefungua soko la nyama yetu na watakuja kuwekeza kuhakikisha kwamba wanapata nyama ile ambayo inasoko katika nchi ya Saudi Arabia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, soko hilo limepatikana kutokana na jitihada za kutumia diplomasia, kushawishi mamlaka za Serikali na sekta binafsi katika nchi hizo kukubali kununua bidhaa zinazozalishwa nchini. Niseme mwezi uliopita nilienda ziara Saudi Arabia nikifuatana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kwamba tunafanikisha hili. Serikali ni moja, tunakwenda pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kutambua mchango wa kituo chetu cha AICC ambacho kimekuwa mwenyeji wa kongamano la habari, lakini pia kitakuwa mwenyeji wa Shirikisho la Mpira (CAF). Kwa hiyo, nadhani hii itakuwa karibu sana tutashiriki huko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua limeongelewa hili kwa mapana yake suala la *diaspora*, suala la uraia pacha na hadhi maalum. Kuhusu suala la uraia pacha nimemsikia sana sana na nashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Gwajima, Mchungaji wetu nakushukuru kwa kuweza kufanya tuseme tafiti (*research*). Umetueleza kwamba karibu nchi 75 duniani zinaruhusu uraia pacha, lakini pia Mheshimiwa Mbunge na Mchungaji wangu nikueleze kwamba kuna nchi zaidi ya 100 ambazo hazikubali uraia pacha. Kwa hiyo, siyo Tanzania tu na sababu ni nyingi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuhusu suala hili napenda kulialifu Bunge lako tukufu kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 suala hilo linahitaji mjadala mpana wa kitaifa. Tayari Serikali inaendelea na mashauriano ya ndani na wadau mbalimbali wakiwemo wana-*diaspora* wenyewe ili kuweza kufikia uamuzi utakaonufaisha *diaspora* kwa kuwapa hadhi maalum hasa ikizingatiwa kuwa siyo nchi zote duniani zinaruhusu uraia pacha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimfahamishe pia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika nchi za Gulf tukiamua kuwapa Watanzania uraia pacha wanaondolewa uraia wa nchi za Gulf. Sasa ndiyo maana nasema tulifanyie mjadala vizuri tuweze kwamba wengine wasiumie, wengine wakafaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesikia utatoa mshahara, nahitaji mshahara tuendeleo na majadiliano na mashauri ili kusudi tuweze kufikia muafaka kuhusu suala hili muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu suala la hadhi maalum ambayo inalenga kuwatambua *diaspora* na kuondoa baadhi ya changamoto mlizozitaja za kisheria na kisera zinazowakwamisha katika kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaeleze kwamba tumekuwa kwenye mchakato huu baada ya kuonekana suala la uraia pacha kwa kweli kwa sasa hivi tusingepata kutokana na hayo ambayo nimeyaeleza. Lakini tukafanya utafiti kwamba nchi ambazo hazina uraia pacha zina mpango gani? Kwa hiyo ndiyo tukakuta kwamba hii hadhi maalum pengine ndiyo *compromise* kwamba Mheshimiwa Mchungaji wangu umesema umeishi Marekani, hadhi maalum ni kama *green card* ya Marekani ambayo ukipata *green card* unapata haki zote. Unaingia bila viza, unafanya biashara yako, kwa tukasema kwa nini na sisi tusijikite hapo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Wizara inapanga kuwa na Semina kuhusu hili suala lakini suala la mchango wa *diaspora* kwa mapana yake tutaiangalia uraia pacha lakini hadhi maalum kwa kweli ukiangalia India mmetaja hapa Pakistani, Iran wote wana hadhi maalum ikiwemo hata Ethiopia nayo ina hadhi maalum kwa wale ambao na nini. (Makofi)

Kwa hiyo mimi nazani labda tu kama mlivyotoa mapendekezo kwamba kutoa elimu, tutatoa semina. Napenda niwahakikishie kwamba na tutawashirikisha wana *diaspora* wenyewe siku hizi wanatuambia msitusemee tulate tuseme wenyewe, kwa hiyo, tutawaleta na tutakuwa na semina. Naomba nisisitize kwamba hili kwa kweli Wizara inalichukulia kwa umuhimu wake na lipo shirikishi na tutakuwa na hiyo semina ukituruhusu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho pengine Sera ya Mambo ya Nje; napenda kurudia kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Wizara imekamilisha mchakato huu wa Sera ya Mambo ya Nje ambayo inazingatia mabadiliko ya hali ya sasa na tunatarajia katika mwaka ujao wa fedha hii sera itakuwa imepita ianze utekelezaji. Kama nilivyosema sera hii imejumuisha

masuala mapya ambayo ni pamoja na uchumi wa kidigitali kama nilivyosema sasa hivi tunajikita kwenye *digital diplomacy*, lakini pia inazingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, lakini pia uchumi wa bluu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tumepitisha sera yetu ya mwaka 2001 kulikuwa hakuna dhana ya uchumi wa bluu. Kwa hiyo sasa sera yetu nayo itajikita katika uchumi wa bluu, lakini pia kukuza Kiswahili kama lugha ya kidiplomasia na biashara. Pengine kuhusu kukuza Kiswahili, Waheshimiwa Wabunge nasema kubwa zaidi na naomba mtusaidie Watanzania hawachangamkii fursa, nchi za jirani zinachangamkia. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tunawabeba kama juzi nilivyosema nilikuwa na Malabo, Equatorial Guinea tumewabeba kuhakikisha kwamba katika kikao hicho tuna wakalimani, wasije wakapata sababu kwamba hawapo. Lakini tunasema kwa pamoja kwa kweli tuchangamkie fursa, majirani zetu wanaenda mbio na sisi tuende mbio. Balozi zetu zimeanzisha vituo, juzi nimefungua Kituo katika Ubalizi wetu wa Seoul, Jamhuri ya Korea na nimeweza kutoa vyeti kwa wanafunzi 300 wa Korea waliyojifunza Kiswahili. Lakini pia ndiyo nasema kuna mwalimu mmoja, tumekuwa tunatafuta, Balozi wetu anahangaika lakini bado kwa hiyo mimi ninasema tuchangamkie fursa na Afrika ya Kusini kwenye Balozi yetu nao wamefungua kituo cha kuweza kutoa mafundisho ya Kiswahili, kwa hiyo fursa zipo tuzichangamkie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwishoni nimalizie kwa kusema katika masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kuna swali lilitokea kuhusu kulipa mafao yao. Naomba nilihakikishie Bunge hili kwamba mafao yote sasa hivi ambayo yalikuwa yamechelewesha yanalipwa na mengine yanafanyiwa uchakataji kwa hiyo naangalia sasa katika mwaka ujao wa fedha tutakuwa tumemaliza mafao ambayo watumishi walikuwa hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimalizie kwa kusema kuhusu kuridhia mikataba; kuhusiana na Serikali kuridhia mikataba mbalimbali iliyosaini, naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa Wizara itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Wizara na Taasisi nyingine za Serikali ili kuhakikisha kwamba Serikali inaridhia mikataba yenye maslahi ya Taifa na kutokana na Mwongozo wa Kamati yetu tayari tulishakuwa na kikao maalum cha kupitia mikataba yote ambayo tulisaini, hatujaridhia au mikataba ambayo hatujasaini na sasa hivi kwa kukaa na wenzetu wa Wizara za Sheria na wengine kwa hiyo mikataba hii ninapenda kukuhakikishia Bunge lako kwamba inafanyiwa kazi kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuwashukuru tena kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

31 MEI, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kutoa hoja, ahsante sana.
(Makofi)

(Hoja imetolewa lamuliwe)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. MOSSI LUKUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu namba mbili, Fungu 34, ukurasa 191 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kifungu 1001 – *Administration and Human*

Resources Management.....Sh. 14,993,010,984

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuko kwenye mshahara wa Waziri na nishapewa majina, Mheshimiwa Askofu Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyosema Watanzania zaidi ya nusu milioni wanakaa ughaibuni kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2020 na kati ya hao kwa mujibu wa *record* ya *Home Office* kule Marekani Watanzania 2,921 wana uraia wa Marekani yaani ni *Tanzanian Americans*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri wakati anawakilisha kwenye wasilisho lake ukurasa wake wa 83 alionesha waziwazi kwamba mwaka 2020 Watanzania hawa wameingiza ndani ya nchi yetu

fedha taslimu dola milioni 400 ambayo ni sawasawa na bilioni 920 ni hela nzuri hii maana yake *remittance* au fedha imetumwa kutoka ughaibuni kuja Tanzania. Lakini pia kwenye wasilisho lake ukurasa huohuo wa 89 ameonesha mwaka 2021 kuna fedha imeingia ambayo imetumwa na Watanzania waliyo ughaibuni dola milioni 569 ambayo ni sawa na trilioni 1.3.

Sasa basi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutuonesha kama Watanzania kuna baadhi ya nchi ukiwa na *passport* yake unaruhusiwa kwenda nchi mbalimbali kupata ajira kwa mfano *passport* ya Marekani au ya Uingereza. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kama tukiruhusu uraia pacha hawa Watanzania wakawa na *passport* za nchi nyingine, wakafanya kazi maeneo mengine sawasawa na hadhi ya *passport* zile tutaingiza fedha zaidi ya hizi *remittance* ambazo tumezipa?

Mheshimiwa Waziri akinipa maelekezo hayo nitawaza vinginevyo kwa namna ya mshahara wake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima, una hoja ya msingi sana na suala la uraia pacha ni suala ambalo liko Serikalini na Serikalini wanali-*caucus*. Lakini Serikali wameikabidhi *instrument* ya uraia pacha Wizara ya Mambo ya Ndani, haipo *Foreign, Foreign* wanahusika na *diaspora*. (Makofi)

Kwa hiyo, hoja yako ni ya msingi na Serikali ipo itaendelea ku-*caucus* na kama Waziri amejibu vizuri sana wakati anajibu kuwa linafanyiwa mchakato na pindi litakapokuwa tayari watalileta, ahsante sana. Mheshimiwa Makamba. (Makofi)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kila baada ya miaka minne hupokea za haki za binadamu na sisi tumepeleka taarifa mwaka huu, taarifa yetu ambayo katika hoja 252 tumeridhia hoja 187 kwenye hilo nawapongeza. Lakini katika hoja ambazo tumeridhia mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa hakuna utekelezaji wowote ambao umeanza kufanyika na naomba niseme nisipopata majibu yanayoridhisha nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza tumekubaliana kwamba tutatunga sheria ya kuwalinda wazee katika nchi hii; pili tumekubaliana kupitia sheria zote za mirathi ili kuweka haki za usawa kuhakikisha wanawake wote wanapata haki na watoto; tumeweka *commitment* ya kuhakikisha kwamba watoto wa kike hawaolewi chini ya miaka 18; tumekubaliana kwamba tutakamilisha mikataba yote ya kimataifa ambayo tumeridhia na tutaweka kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kusikitika pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais wetu amepata tuzo mbalimbali alisema na namnukuu; "The

burden of expectation to deliver gender equality is heavier on my shoulders.”
(Makofi)

Mheshimiwa Rais ana *commitment* kubwa ya kuwasaidia wanawake, watoto na vijana wanaolawitiwa. Jana Wizara ya Maendeleo ya Jamii tumezungumza sana kuhusiana na wazee, wanawake na Watoto, lakini Wizara ya Mambo ya Nje mpaka leo mikataba haijafanyiwa *ratification*, Sheria hazijafanyiwa marekebisha, Mheshimiwa Waziri anatueleza hapa wapo kwenye mpango wa kwenda kupitiapitia hizi sheria na Wizara ya Katiba na Sheria.

Nini *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kuhakikisha anaunga mkono juhudi za Mama Samia kuweza kuwasaidia wazee, wanawake, vijana na watoto katika nchi hii kwa ku-*ratify* na kubadilisha sheria za nchi yetu? Nisiporidhika nitashika shilingi ya Waziri. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene, *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Makamba kwa maelezo aliyoyatoa, lakini *Universal Periodic Review* kwenye Baraza lile tumetoka juzi na mimi ndiye niliyewakilisha Tanzania na miongoni mwa mambo ambayo tumepongezwa sana kama nchi ni kutokana na kwamba nchi yetu imejitahidi sana ukilinganisha na nchi nyingine nyingi. Kwa hivyo tulipongezwa sana na Rais wetu alipongezwa sana na hata hii kusema Rais wetu amekuwa miongoni mwa Marais wachache wenye mvuto duniani inatokana na vigezo vingi ambavyo tumevikidhi katika masuala ya haki za binadamu. (Makofi)

Sasa haya machache ambayo tulikubalina kule ambayo tunatakiwa tuanze kuyafanyia kazi ndiyo haya sasa tukipitisha bajeti kama hii ndiyo tunaenda kutekeleza kwa sababu kwenye mkutano huo nimetoka mwaka huu mwezi wa pili, wa tatu. Sasa haiwezekani hata bajeti hatujapitisha na haya ndiyo nimetoka juzi kwenye mkutano, tayari *UPR* tayari ndiyo tunaanza kutekeleza, tunatakiwa sasa hivi tuanze kuhojiwa kwa nini hamjatekeleza. Nadhani tunakuwa Serikali hatutendewi haki lakini kimsingi sisi duniani tunapongezwa na hata wanachama kule wengi waliokuwa wanatoa mchango wao nchi karibu 21 zili-*recommend* Tanzania kwamba tumepiga hatua kubwa katika masuala ya haki za binaadam. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umejibu vizuri hata tumejikita kwenye *EPRM* tumekubali sisi, tumeridhia Tanzania ili tuweze tufanyiwe tathmini na nchi za nje. Kwa hiyo jibu lako linaridhisha, Mheshimiwa Salome hoja yako imejibiwa vizuri.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa nimesimama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome sijakupa nafasi ya kuzungumza. Hoja yako imeshajibiwa na hoja yako imeshafungwa. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 – Finance and Accounts Unit.....	Sh. 1,203,323,244
Kifungu 1003 – Foreign Affairs Office Zanzibar.....	Sh. 1,265,322,000
Kifungu 1004 – Policy and Planning Unit.....	Sh. 1,727,508,000
Kifungu 1005 – International Cooperation.....	Sh. 1,296,926,000
Kifungu 1006 – Europe and America.....	Sh. 2,195,022,115
Kifungu 1007 – Asia and Australia	Sh. 1,520,304,000
Kifungu 1008 – Africa.....	Sh. 2,771,244,000
Kifungu 1009 – Regional Cooperation.....	Sh. 1,070,380,000
Kifungu 1010 – Protocol.....	Sh. 4,701,820,000
Kifungu 1011 – Legal Services Unit.....	Sh. 2,257,286,000
Kifungu 1012 – Government Communication Unit.....	Sh. 703,393,016
Kifungu 1013 – Middle East Division.....	Sh. 1,064,300,000
Kifungu 1014 – Internal Audit Unit.....	Sh. 558,240,000
Kifungu 1015 – Procurement Management Unit.....	Sh. 610,342,085
Kifungu 1016 – Information and Communication Technology Unit.....	Sh. 648,004,000
Kifungu 1017 – Diaspora Engagement and Opportunity.....	Sh. 635,691,000
Kifungu 1018 – Economic Infrastructure and Social Support Services Division.....	Sh. 798,508,000
Kifungu 1019 – Political, Defence and Security Affairs.....	Sh. 697,872,000
Kifungu 1020 – Trade, Investment and Productive Sector Division.....	Sh. 958,900,000
Kifungu 1021 – Economic Diplomacy Division.....	Sh. 541,675,000
Kifungu 2001 – Embassy of Tanzania – Addis Ababa.....	Sh.2,832,476,659
Kifungu 2002 – Embassy of Tanzania – Berlin	Sh.4,290,409,069
Kifungu 2003 – Embassy of Tanzania – Cairo.....	Sh.2,490,879,485
Kifungu 2004 – Embassy of Tanzania – Kinshasa.....	Sh.4,069,742,480
Kifungu 2005 – High Commission of Tanzania - Abuja.....	Sh.4,549,692,840
Kifungu 2006 – High Commission of Tanzania - London.....	Sh.5,120,981,865
Kifungu 2007 – High Commission of Tanzania - Lusaka.....	Sh.2,333,076,099
Kifungu 2008 – High Commission of Tanzania - Maputo.....	Sh.2,286,865,035
Kifungu 2009 – Embassy of Tanzania - Moscow.....	Sh.4,022,847,955
Kifungu 2010 – High Commission of Tanzania - New Delhi.....	Sh.3,494,067,465
Kifungu 2011 – Permanent Mission to The UN - New York.....	Sh.5,203,308,180
Kifungu 2012 – High Commission of Tanzania - Ottawa.....	Sh.3,115,525,245
Kifungu 2013 – Embassy of Tanzania - Paris.....	Sh.3,559,634,660
Kifungu 2014 – Embassy of Tanzania - Beijing.....	Sh.5,844,419,793

31 MEI, 2022

Kifungu 2015 – Embassy of Tanzania - Rome.....	Sh.4,375,773,678
Kifungu 2016 – Embassy of Tanzania - Stockholm.....	Sh.4,752,251,586
Kifungu 2017 – Embassy of Tanzania - Tokyo.....	Sh.4,437,071,973
Kifungu 2018 – Embassy of Tanzania - Washington.....	Sh.4,473,445,850
Kifungu 2019 – Embassy of Tanzania - Brussels.....	Sh.4,749,591,000
Kifungu 2020 – Permanent Mission to The UN - Geneva.....	Sh. 5,925,330,460
Kifungu 2021 – High Commission of Tanzania – Kampala.....	Sh.2,326,093,770
Kifungu 2022 – High Commission of Tanzania – Harare.....	Sh.2,175,643,365
Kifungu 2023 – High Commission of Tanzania – Nairobi.....	Sh.4,591,387,010
Kifungu 2024 – High Commission of Tanzania – Rivadh.....	Sh.3,235,562,190
Kifungu 2025 – High Commission of Tanzania – Pretoria.....	Sh.3,461,159,135
Kifungu 2026 – Embassy of Tanzania – Kigali.....	Sh.2,076,896,300
Kifungu 2027 – Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi.....	Sh.5,340,797,843
Kifungu 2028 – Embassy of Tanzania – Bujumbura.....	Sh.2,032,578,310
Kifungu 2029 – Embassy of Tanzania – Muscat.....	Sh.2,750,430,760
Kifungu 2030 – High Commission of Tanzania – Lilongwe.....	Sh.2,289,090,975
Kifungu 2031 – Embassy of Tanzania Brasilia.....	Sh.3,572,388,925
Kifungu 2032 – Embassy of Tanzania Kuala Lumpa.....	Sh.2,642,878,315
Kifungu 2033 – Embassy of Tanzania - The Hague.....	Sh.3,602,653,153
Kifungu 2034 – Embassy of Tanzania - Moroni.....	Sh.2,713,563,431
Kifungu 2035 – Embassy of Tanzania – Kuwait.....	Sh.2,316,918,370
Kifungu 2036 – Embassy of Tanzania – Algiers.....	Sh.2,780,369,200
Kifungu 2037 – Embassy of Tanzania – Ankara.....	Sh.3,639,755,490
Kifungu 2038 – Embassy of Tanzania – Khartoum.....	Sh.2,379,341,685
Kifungu 2039 – Embassy of Tanzania – Seoul.....	Sh.5,965,306,276
Kifungu 2040 – Embassy of Tanzania - Tel-Aviv.....	Sh.3,721,404,120
Kifungu 2041 – Embassy of Tanzania – Doha.....	Sh.3,186,364,125
Kifungu 2042 – Embassy of Tanzania – Havana.....	Sh.3,121,342,210
Kifungu 2043 – Embassy of Tanzania – Windhoek.....	Sh.2,988,394,465
Kifungu 2044 – Embassy of Tanzania – Jarkata.....	Sh.2,507,690,825
Kifungu 2045 – Permanent Mission to The UN – Vienna.....	Sh.4,102,490,931

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kifungu 1004 – Policy and Planning Unit.....	Sh. 4,700,000,000
--	-------------------

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hapa mmeandika *Acquisition, Expansion and Reha*

31 MEI, 2022

Mmeweka tu *figure* lakini hamku-mention Mabalazi yetu mlivyotengeneza, maana k
(Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSI LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake. (Makofi)

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki kwa mwaka wa fedha 2022/2022. (Makofi)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2022/2023 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri kwa kupitisha bajeti yake. Bajeti yako imepita kwa kishindo kwa sababu wewe mwenyewe ni mtu wa vishindo na unayaweza mambo ya vishindo, kwa hiyo, ndio maana mambo yako yamekwenda vizuri.

31 MEI, 2022

Nakupongeza Naibu Waziri kwa kazi nzuri uliyofanya pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara, pamoja na michango mizuri ya Wabunge kukamilisha zoezi leo kwa ufanisi, ili muweze kufanya kazi na kutimiza majukumu yenu kama mlivyoagizwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo, Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara kuwa wanakaribishwa kuhudhuria uzinduzi wa Programu ya Upandaji Miti katika Mji wa Serikali Mtumba tarehe 1 Juni, 2022 siku ya Jumatano kuanzia saa 12.30 asubuhi. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni Wajumbe wa Kamati hiyo wanaombwa wahudhurie kwenye programu hiyo muhimu ya upandaji miti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 1 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*